

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA TISA

---

Kikao cha Arobaini na Nne- Tarehe 12 Juni, 2020

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Kamili Asubuhi)*

#### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa naomba tukae.

Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

#### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. SHALLY J. RAYMOND - K.n.y. MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya uchumi wa Taifa kwa mwaka 2019 na Mpango wa mandeleo wa Taifa kwa mwaka 2020/2021 pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**MHE. CECILIA D. PARESSO - K.n.y. MSEMADI MKUU WA  
KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WA WIZARA YA FEDHA  
NA MIPANGO:**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2019, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2020/2021 pamoja na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**MASWALI NA MAJIBU**

*(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibisha kwa njia ya mtandao)*

Na. 416

**TAMISEMI Kupangia Watumishi Vituo vya Kazi  
Moja kwa Moja**

**MHE. OMARY A. BADWEL** aliuliza:-

Kumekuwa na utaratibu wa kuleta watumishi wa kada mbalimbali katika Halmashauri za Wilaya zetu na kupangiwa vituo vya kazi moja kwa moja kutoka TAMISEMI na kutakiwa kuripoti katika vituo hivyo hali ambayo imeanza kuwa kero kwa Ofisi za Wakurugenzi kwani wakati mwingine watumishi hupelekwa sehemu ambazo hazina uhitaji na kuacha sehemu zenye uhitaji.

(a) Je, kwa nini TAMISEMI imekuwa ikiwapangia watumishi vituo moja kwa moja badala ya kuwaachia Wakurugenzi?

(b) Je, kwa nini TAMISEMI isiache kazi hiyo ya kupanga vituo kufanya na Wakurugenzi ambao ndiyo wanajua mahitaji sahihi ya watumishi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA  
NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omary Ahmed Badwel, Mbunge wa Bahi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inayo mifumo inayoiwezesha kuwa na taarifa za miundombinu, vitendea kazi na watumishi wa vituo vya kutolea huduma hivyo inafahamu mahitaji ya watumishi na vitendea kazi kwa vituo vyote vya kutolea huduma vinavyosimamiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Takwimu hizo hukusanywa kutoka kwenye Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kupanga watumishi moja kwa moja ulianza kutekelezwa mwaka 2015 baada ya kubaini changamoto kadhaa ikiwemo watumishi kupata usumbufu kwenye Halmashauri wanazopelekwa wakisubiri kupangiwa vituo vya kazi, wanasiasa kuwashinikiza Wakurugenzi kuwapanga watumishi kwenye maeneo ya mjini hivyo watumishi kurundikana kwenye maeneo ya mjini. Utaratibu wa sasa unaondoa changamoto hizo na kuhakikisha watumishi wanapelekwa kwenye vituo vyenye uhitaji.

Na. 417

**Ubadhirifu Katika Fedha za Mapato ya Ndani  
Kwenye Halmashauri**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA** aliuliza:-

Kumekuwa na tatizo kubwa la matumizi mabaya na ubadhirifu wa fedha za mapato ya ndani pamoja na ruzuku katika Halmashauri nyingi nchini.

Je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na tatizo hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA  
NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalil la Mheshimiwa Goodluck Asaph Mlinga, Mbunge wa Ulanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na ubadhirifu wa fedha kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kuboresha mfumo wa ukusanyaji mapato na mifumo ya matumizi (*Epicor 10.02 na FFARS*) ili kudhibiti ubadhirifu wakati wa makusanyo na wakati wa matumizi. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imezipatia Halmashauri nchini mashine bora na za kisasa za kukusanya mapato (*POS*) 7,227 ambazo zimetengenezwa kwa lengo la kuondoa changamoto zote zilizojitokeza wakati wa matumizi ya mashine za awali.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeimarisha mfumo wa ukaguzi wa ndani kuanzia ngazi ya Halmashauri na inatoa ushirikiano wa kutosha kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) ili kumuwezesha kufanya kazi yake kikamilifu. Serikali pia imekuwa ikichukua hatua za kinidhamu na kisheria kwa watumishi wote wanaobainika kuhusika kwenye ubadhirifu wa fedha za umma.

Na. 418

**Barabara ya Ununio – Mbweni Teta – Mpiji - Bunju**

**MHE. HALIMA J. MDEE aliuliza:-**

Barabara ya Ununio – Mbweni (Ubungo) - Teta - Mpiji - Bunju ni mionganini mwa barabara za ndani muhimu sana kwa kupunguza foleni kwa watumiaji wa barabara ya *New Bagamoyo*. Licha ya kwamba barabara hii imekuwa kwenye mpango wa ujenzi wa kiwango cha lami kwa muda mrefu sana, utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua sana.

Je, ni lini barabara hii itakamilika?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ununio – Mbweni (Ubungo) – Teta – Bunju yenyeye urefu wa kilometri 15.71 ni barabara ya Wilaya ambayo ni moja ya barabara zilizokasimiwa kwa Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) kwa ajili ya kuifanya ukarabati na matengenezo kutokana na umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni mionganini mwa barabara za ndani ambazo zinapunguza msongamano wa magari kwenye barabara kuu ya Tegeta – Bagamoyo na ipo kwenye mpango wa ujenzi kwa kiwango cha lami kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018. Hadi kufikia Aprili, 2020 jumla ya kilometri 2.1 za lami zimekamilika na kazi za mwaka wa fedha 2019/2020 zinaendelea. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 zimetengwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kilometri moja ambapo kilometri 5.0 zitakuwa zimekamilika. Lengo la Serikali ni kukamilisha ujenzi kwa barabara yote kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa barabara hii inaendelea kupitika majira yote ya mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya shilingi milioni 1,500 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara hii.

Na. 419

**Tozo ya Ukaguzi Inayotozwa na SUMATRA**

**MHE. DKT. PRUDENCIA W. KIKWEMBE** aliuliza:-

Je, ni kwa nini *SUMATRA* hutoza tozo ya ukaguzi wa chombo cha usafiri kinapokaguliwa na taasisi hiyo ni ya umma?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Kavuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (*SUMATRA*) ilifanyiwa marekebisho na Bunge la Jamhuri la Muungano kwa kutenganisha shughuli za usafiri wa nchi kavu na majini. Usafiri wa nchi kavu husimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (*LATRA*) kwa Sheria Namba 3 ya mwaka 2019. Aidha, usafiri wa majini husimamiwa na Sheria Namba 14 ya mwaka 2017 ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (*TASAC*).

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia shughuli za usafiri wa ardhini, *LATRA* haina tozo ya ukaguzi. Aidha, Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (*TASAC*) hutoza tozo ya ukaguzi wa vyombo vya usafiri majini kwa mujibu wa Kanuni za Ada ya Ukaguzi na Marekebisho yake (*Merchant Shipping (Fees) Regulations, 2005 as Amended*) zilizoandalishi chini ya Sheria ya Usafiri wa Majini (*Merchant Shipping Act, 2003 as amended*).

Mheshimiwa Spika, ni jukumu la msingi la *TASAC* kuhakikisha kuwa vyombo vya usafiri majini ni salama kabla havijaanza kutoa huduma. *TASAC* hufanya ukaguzi wa lazima (*statutory survey/inspection*) kwa vyombo hivyo kila baada ya muda muafaka ili kubaini kama vyombo hivyo vinaendelea kukidhi viwango vya ubora na usalama viliviyokusudiwa ili kuendelea kutoa huduma ya usafiri majini. Kufuatia ukaguzi huo, *TASAC* hutoa yeti stahiki ikiwa ni pamoja na Cheti cha Usajili (*Registration Certificate*), Cheti cha Ubora (*Seaworthiness Certificate*) na vinginevyo kama kielelezo cha chombo kukidhi viwango vya ubora kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri Majini na kanuni zake.

Aidha, *TASAC* kama zilivyo mamlaka zingine za udhibiti nchini, hujiendesha kwa mapato yatokanayo na kazi za

udhibiti ikiwa ni pamoja na kutoza ada za ukaguzi zinazotokana na kaguzi mbalimbali inazozifanya kwa vyombo vya usafiri majini.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo wamiliki wa vyombo vya usafiri majini hupaswa kulipa tozo za ukaguzi kwa mujibu wa sheria ili kuwezesha *TASAC* kufanya majukumu yake kisheria.

Na. 420

**Safari za Ndege Dodoma – Mwanza – Dodoma**

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali kuititia *ATCL* itaanzisha safari ya ndege ya Dodoma - Mwanza - Dodoma ili kusaidia usafiri Kanda ya Ziwa?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mbunge wa Magu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upangaji wa safari za ndege huzingatia mambo mengi kama vile uhitaji wa safari za ndege za sehemu husika (soko) na uwezo wa kampuni kuhudumia sehemu hizo ambapo huhushisha idadi ya ndege, aina ya ndege, idadi ya marubani na uwezo wa viwanja vya ndege. Kutokana na Makao Makuu ya Serikali kuhamishiwa Dodoma, kumekuwepo na hitaji kubwa la mikoa mbalimbali kuunganishwa na Dodoma kwa kutumia usafiri wa ndege. Serikali imeliona hili na Wizara yangu tayari imeagiza Kampuni ya Ndege Tanzania (*Air Tanzania Company Limited – ATCL*) kufanya utafiti wa kuanzisha safari za ndege kutoka mikoa mingine kwenda na kurudi Dodoma au kwa kuunganisha na mikoa mingine, kwa mfano Dar es Salaam – Mwanza – Dodoma na kurudi hivyo kusaidia usafiri wa kutoka mikoani

kwenda na kurudi Dodoma. Utaratibu wa kuunganisha na mikoa mingine unasaidia *ATCL* kuwa na idadi ya abiria wa kutosha na hivyo kutoa huduma kwa ufanisi na tija.

Mheshimiwa Spika, kutokana na nia ya Serikali kudhibiti kuenea kwa maambukizi ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya Covid-19, kwa sasa safari za abiria kwa ndege za kimataifa zimesitishwa. Aidha, safari za ndege za ndani ya nchi nazo zimeathiriwa ambapo abiria wamepungua kwa kiasi kikubwa, maana watu wengi wameacha kusafiri kuepuka maambukizi ya virusi vya Covid-19. Baada ya kuondolewa kwa zuio la ndege za kimataifa kuingia nchini na biashara ya usafiri wa anga itakaporejea kwenye hali yake ya ushindani, njia ya Dodoma – Mwanza – Dodoma itapewa kipaumbele mara baada ya kufanya uchambuzi wa kibiashara na kubainika kwamba safari zake zitakuwa na tija kwa Kampuni.

Na. 421

### **Mali Zilizokuwa za Mbinga Cooperative Union**

**MHE. MARTIN A. M. MSUHA** aliuliza:-

Chama Kikuu cha Ushirika *Mbinga Cooperative Union (MBICU)* kilishindwa kuendesha shughuli zake kibiashara na hatimaye kukabidhiwa kwa Mfilisi mwaka 1994/1995 kutokana na madeni pamoja na kuyumba kwa soko la kahawa.

Je, kwa nini Mfilisi bado anashikilia mali za chama hicho badala ya kukabidhi kwa chama kipyaa cha *Mbinga Farmers' Cooperative Union (MBIFACU)* kwa muda mrefu kiasi hicho.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Martin Alexander Mtonda Msuha, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Vijijiini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Chama Kikuu cha Ushirika Mbinga (*MBICU*) kilifutwa katika daftari la Serikali mwaka 1994 kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kushindwa kuijidesha, uwepo wa madeni mengi pamoja na kutokidhi matakwa ya Sheria ya Vyama vya Ushirika. Kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika, mali na madeni ya chama hicho yalikabidhiwa kwa Mfilisi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufutwa chama hicho, kilianzishwa Chama Kikuu cha *MBIFACU Ltd.* ambacho wanachama walio wengi walitokana na kilichokuwa Chama Kikuu cha Ushirika cha *MBICU Ltd.* kilichofutwa na Serikali. Mnamo tarehe 27 Aprili, 2016 chama kipyaa cha *MBIFACU Ltd.* kilifanya kikao cha pamoja kati ya Mfilisi, Ofisi ya Mrajis na Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa ajili ya kutafuta makubaliano ya uwezekano wa kumiliki mali na madeni ya *MBICU Ltd.* Baada ya kikao hicho, Mfilisi alikabidhi baadhi ya mali za *MBICU Ltd.* kwa *MBIFACU Ltd.* ambazo ni maghala, hoteli, jengo la ofisi, nyumba za kuishi, mashamba pamoja na samani zote.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mali hazijamilikishwa kisheria kwa *MBIFACU Ltd.* na zimeendelea kuwa chini ya Mfilisi kutokana na deni la kiasi cha shilingi 1,000,000,000 lilitotokana na mkopo wa pembejeo kutoka *NBC Holding Ltd.* Hati za mali zinaendelea kushikiliwa ni zile za mali lilitowekwa rehani ambazo ni maghala, hoteli na ofisi ya *MBICU Ltd.*

Mheshimiwa Spika, aidha, kupitia kikao yalifikiwa makubaliano kuwa riba na adhabu zote zisamehewe na kuwezesha deni kushuka kutoka shilingi 1,000,000,000 mpaka kufikia shilingi 723,352,833. Mfilisi amekabidhi deni hilo kwa Chama Kikuu cha *MBIFACU Ltd.* kwa ajili ya kuanza kulipwa na baada ya kumaliza kulipa deni hilo hati za mali zilitowekwa rehani zitakabidhiwa kwa *MBIFACU* ili kuzimiliki kisheria. Aidha, Wizara itasimamia zoezi la kurejeshwa kwa mali hizo haraka kutoka kwa mfilisi.

Na. 422

### **Vituo vya Polisi na Nyumba – Mkoa wa Kaskazini Pemba**

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD** aliuliza:-

Mkoa wa Kaskazini Pemba unakabiliwa na ukosefu na uchakavu wa vituo na nyumba za makazi ya askari.

(a) Je, ni lini Serikali itawapatia askari hao nyumba za makazi?

(b) Je, ni lini Vituo vya Jeshi la Polisi vya Micheweni, Konde na Wete vitafanyiwa ukarabati kwani nyakati za mvua majengo yake yanavuja sana?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibuu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Mbunge wa Wingwi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kujenga na kuyaboresha makazi ya askari wake ili kuhakikisha wanaishi kwenye nyumba bora ili waweze kutimiza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa. Serikali imekuwa ikifanya hivyo kwa nchi nzima inapopata fedha na Mkoa wa Kaskazini Pemba ukiwemo.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutoa shilingi bilioni kumi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za askari nchi nzima ambapo Mkoa wa Kaskazini Pemba nyumba hizo zimejengwa eneo la Limbani, Wilaya ya Wete. Nyumba zote zilizojengwa kutokana na fedha alizotoa Mheshimiwa Rais kwa sasa zinakaliwa na askari.

Mheshimiwa Spika, aidha Serikali inaendelea kujenga majengo mengine ya kuishi askari katika kambi ya kikosi cha

kuzuia ghasia (FFU) Finya Mkao wa Kaskazini Pemba. Hivyo Serikali itaendelea kuboresha makazi ya askari kadri inavyopata fedha. Serikali itaendelea kuboresha na kukarabati vituo vyote vya polisi nchini nzima kwa awamu kadri ya upatikanaji wa fedha utakavyokuwa unaimarika.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Vituo vya Polisi vya Micheweni, Konde na Wete Mkao wa Kaskazini Pemba vinahitaji ukarabati. Kutokana na changamoto ya kukosekana rasilimali fedha, vituo hivyo bado havijafanyiwa ukarabati. Pindi fedha zitakapopatikana vitafanyiwa ukarabati kwa wakati.

Na.423

### **Tatizo la Maji Momba**

**MHE. DAVID E. SILINDE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza kabisa tatizo sugu la maji katika Jimbo la Momba?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Jimbo la Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wananchi wa Jimbo la Momba wanapata huduma ya majisafi, Serikali imekamilisha mradi katika Kijiji cha Ndalambo na miradi katika vijiji vya Chitete na Tindingombwa ipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo Chitete ni asilimia 40 na Tindingombwa asilimia 80. Miradi hii ikikamilika itahudumia jumla ya watu 23,397 na kuongeza asilimia 13.86 ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Programu ya Matokeo (*P4R*) inatekeleza miradi mitano katika Vijiji vya Mkulwe, Chiwanda, Kasinde, Ikana na Namsinde il kwa

gharama ya shilingi milioni 737.5. Mpaka sasa vifaa vya ujenzi kama vile saruji na nondo zimenunuliwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa matenki matano, vituo 55 vya kuchotea maji na *pump house* sita. Kukamilika kwa miradi hii kutahudumia jumla ya watu 42,864 na kuongeza asilimia 25.40 ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama.

Na. 424

### **Hitaji la Maji – Kijiji cha Chonga**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Wananchi wa kijiji cha Chonga wana ukosefu wa majisafi na salama na hii ni kutokana na ubovu wa miundombinu.

Je, Serikali ipo tayari kujenga miundombinu ya maji katika kijiji hicho?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Chonga ni miongoni mwa vijiji vinne vilivokuwa vikihudumiwa na Mradi wa Maji wa Pamoja wa Kate uliokuwa ukihudumia Vijiji vya Kate, Ntalamila, Nchenje na Chonga (*Kate Group Water Supply*). Kutokana na uharibifu wa miundombinu ya maji ilipelekea Kijiji cha Chonga kukosa huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha huduma ya maji inarejea katika Kijiji cha Chonga, Serikali kupitia Wizara ya Maji inatekeleza Mpango wa Malipo Kulingana na Matokeo (*PforR*). Kupitia mpango huo, Serikali tayari imetoa fedha kiasi cha shilingi milioni 273.998 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa kurudisha huduma ya maji katika Kijiji cha Chonga ambapo hadi sasa utekelezaji wa mradi huo upo kwenye

hatua za manunuzi ya vifaa vya ujenzi na mafundi. Mradi huu utatekelezwa na RUWASA, Mkoa wa Rukwa na Wilaya ya Nkasi kupitia mfumo wa *force account*. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2020.

Na. 425

### **Usambazaji wa Umeme - Jimbo la Kibaha Mjini**

**MHE. SLYVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Jimbo la Kibaha Mjini ni mojawapo ya mitaa/vijiji vilivyokuwa katika Mpango wa REA, lakini kwa kuwa ni Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani Serikali imeuweka katika mpango maalum wa kusambaza umeme maarufu umeme wa ujazilisho (*Peri Urban*).

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha usambazaji wa umeme katika mitaa iliyobaki?

**WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Slyvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Pwani umepangwa katika mradi wa kusambaza umeme katika maeneo yaliyo pembezoni mwa miji (*Peri-Urban*) ambapo katika hatua ya awali mradi unatekelezwa katika Wilaya nne za Mkoa wa Pwani ikiwemo Wilaya ya Kibaha. Mradi huu kwa ujumla wake unatekelezwa kwa gharama ya shilingi bilioni 65 na umeanza kutekelezwa mwezi Agosti, 2019 na utakamilika mwezi Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kibaha, Mkandarasi Kampuni ya *Sengerema Engineering Group Limited* inatekeleza mradi huu kwa gharama ya shilingi bilioni 14.97. Kazi za mradi zinajumuisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometra 157.9;

ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometra 275; ufungaji wa transfoma 62; pamoja na kuwaunganishia huduma ya umeme wateja wa awali 6,145. Maeneo ya Halmashauri ya Mji wa Kibaha yanayonufaika na utekelezaji wa mradi wa *Peri-urban* ni pamoja na Kata ya Pangani; Mitaa ya Kosovo, *Fabian Farm*, Viwanja vya REA, *Mpingo Farm*, Kidimu, *Kidimu Water Pump*, Lumumba, Mkombozi, Mtakuja na Machinjio Mapya.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yanayopelekewa umeme katika Wilaya ya Kibaha kuitia mradi huu ni pamoja na Kata ya Mbwawa: Mitaa ya Miswe, Miswe Mabwawa ya Samaki, na Mbwawa Tondo; Kata ya Maili Moja: Vitongoji vyote vya Muheza; Kata ya Kibaha: Mtaa wa Chang'ombe; Kata ya Picha ya Ndege: Vitongoji vyote vya Lulanzi; Kata ya Sofu: Vitongoji vyote vya Sofu; Kata ya Misugusugu: Mitaa ya Vitendo; Miomboni, Zahanati ya Misugusugu na Kata ya Visiga: Vitongoji vyote vya Visiga B.

**SPIKA:** Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2020 (*The Finance Bill, 2020*)**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Muswada huo wa *Finance Bill, 2020* umeshasomwa Mara ya Kwanza, Kamati ya Bajeti muanze kufanyia kazi *immediately* kwa ratiba mtakayojipangia, siku ya Jumatatu asubuhi tunaushughulikia hapa ndani. Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

## **HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2019 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 – Wizara ya Fedha na Mipango**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea baada ya Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango kuwasilisha hoja yake siku ya jana vizuri kabisa wote tukiwepo na naamini tumeshapata nafasi nzuri ya kuweza kulpitia tena na kutafakari, sasa naamini tuko tayari kabisa kuweza kuingia katika hatua inayofuata.

Kutokana na zoezi letu lile la kuanza saa nane mchana na zoezi hili la kuanza saa tatu asubuhi nafikiri mnaona kabisa kwa Bunge la Kumi na Mbili kipi kitakuwa ndio kinachofaa zaidi, ushahidi unaonesha lakini muda mfupi ujao tutakuwa tumeshajaa kwa ukamilifu wake haituzuii kuanza shughuli zetu.

Sasa tunaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa muda wa nusu saa hapo hapo ulipo ama mwakilishi wako, tuanze kupitia Mheshimiwa Waziri wa Fedha yuko tayari hapa kutusikiliza na baada ya hapo Msemaji wa Kambi ya Upinzani na yeye ana nusu saa na wachangiaji wote kadri mlivyoleta majina nitawapa nafasi. Sehemu kubwa sana ya wachangiaji watachangia leo na wengine watachangia kesho.

Mheshimiwa Mashimba Ndaki au mwakilishi karibu.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Taarifa ya Hali ya Uchumi

wa Taifa mwaka 2019, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2020/2021; Tathmini ya Utekeleaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2019/2020 pamoja na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 105(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo Januari, 2016 naomba kutumia fursa hii kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2019; Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2020/2021 pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2019/2020 pamoja na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia taarifa yangu hii iweze kuwekwa katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge kwa sababu sitawenza kusoma maeneo yote ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeendelea kutekeleza ipasavyo majukumu yake kikanuni na kisheria kama yalivyoainishwa kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2016, pamoja na Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015. Aidha, Kamati imeendelea kushauri na kuisimamia Serikali katika kutekeleza bajeti yake kwa ufanisi kwa nia ya kujenga na kuimarisha uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali imekuwa ikitoa ushirikiano wake wa kutosha kwa Kamati katika kipindi chote na hivyo kuwa na uhusiano mzuri wa kikazi baina ya Kamati na Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati inapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa namna ambavyo ameliongoza Taifa kwa umahiri mkubwa hasa katika janga la Corona na mapambano dhidi yake. Mheshimiwa Rais ameonesha utashi, utayari, umahiri na weledi mkubwa katika kupambana na janga hili. (*Makofii*)

Vilevile Kamati inapenda kuwapongeza Makamu wa Rais - Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake. Pia kipekee sana tunakupongeza wewe kwa namna ambavyo umeliongoza Bunge hili la Kumi na Moja vizuri kwa weledi, utulivu na uzoefu mkubwa wa kutosha kiasi kwamba sisi kama Kamati tuliweza kufanya kazi yetu vizuri kwa kukushirikisha mambo mengine, lakini kwa kweli kila kitu tulichokihitaji kutoka kwenye ofisi yako tulikipata ili tuweze kufanya zetu vizuri. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha tunapenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango - Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji - Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa kushirikiana vyema na Kamati wakati wote tulipowahitaji waliitikia wito wetu na hivyo tukafanya nao kazi vizuri. Tunapenda pia kumshukuru Katibu Mkuu wa Fedha Ndugu Doto James na Naibu Makatibu wake, pia tunamshukuru Gavana wa Benki Kuu Profesa Frolens Luoga, pia tunamshukuru Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania Dkt. Edwin Muhede na Wakuu wa Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali kwa ushirikiano wao na mshikamano walilouonesha kwa Kamati.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye kipengele cha sura ya bajeti; Kamati ya Bajeti ilipata fursa ya kupitia na kuchambua utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2019/2020 pamoja na Ulinganisho wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa 2020/2021.

Uchambuzi huu ultoa hali halisi wa mwelekeo wa Bajeti ya Serikali pamoja na utekelezaji wa malengo ya bajeti yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Pia tumetoa hali halisi ya utekelezaji wa sera za kodi kwenye maeneo husika hasa maeneo yanayohusu mapato ya ndani, mapato ya Halmashauri, misaada na mikopo ya kibiasara ya ndani na kutoka nje na matumizi ya kawaida kwa maendeleo.

Aidha, kumekuwepo na ongezeko au punguzo katika baadhi ya maeneo ya mapato na matumizi kwa asilimia kadhaa kama ambavyo inaonyeshwa katika jedwali namba 1.

Mheshimiwa Spika, sura ya bajeti kwa mwaka 2020/2021 ikilinganshwa na bajeti ya mwaka 2019/2020 inaonesha kuwa tutakuwepo na ongezeko la kiasi cha shilingi bilioni 1,774,383.2 sawa na asilimia 5.36 ya jumla ya bajeti yote. Pamoja na ongezeko hili bado kutakuwa na nakisi ya bajeti ya asilimia 2.6 ya Pato la Taifa sawa na shilingi triliuni 3.7.

Aidha, mapato ya ndani yataongezeka kwa asilimia 4.36 sawa na ongezeko la kiasi cha shilingi bilioni 970.727. Mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yataongezeka kwa asilimia 6.4 sawa na ongezeko la kiasi cha shilingi billioni 49.477. Misaada na mikopo kutoka nje itaongezeka kwa asilimia 3.2 sawa na ongezeko la kiasi cha shilingi bilioni 90.69.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya ndani na nje yenye masharti ya kibiashara itaongezeka kwa asilimia 9.12 sawa na ongezeko la kiasi cha shilingi bilioni 663.481. Aidha, matumizi ya kawaida yataongezeka kwa asilimia 5.39 sawa na ongezeko la kiasi cha shilingi triliuni 1.123 na matumizi ya maendeleo yataongezeka kwa asilimia 5.31 sawa na ongezeko la kiasi cha shilingi bilioni 650.381. kielelezo tumeweka hapo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa taarifa yangu ni ndefu kama nilivyosema, nijielekeze zaidi kwenye maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusiana na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imefanya uchambuzi wa mabadiliko ya sheria mbalimbali yenye marekebisho mbalimbali yaliyozingatia dhamira ya Serikali ya kuendelea kuwa na mfumo wa kodi ambao ni tulivu na wa kutabirika. Aidha, marekebisho yalilenga kuchochea

kasi ya ukuaji wa uchumi hususan katika sekta ya kilimo na viwanda, kuongeza kipato kwa waajiriwa na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na Serikali kwa uamuzi wake wa busara wa kutokufanya mabadiliko ya viwango katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, uamuzi huu unaondoa dhana potofu iliyokuwa imejengeka kwamba Serikali inajienda kodi za sigara, bia na soda tu. Kamati baada ya kupitia mabadiliko ya sheria yaliyopendekezwa ina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148; Serikali kwa kufanya mabadiliko katika eneo hili kwa sababu itasaidia mazao yetu ya kilimo kuwa na bei shindani katika masoko ya nje. Aidha, hatua hili itawezesha wawekezaji katika sekta ya kilimo na madini kuongeza mitaji na kupanua uwekezaji. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifungashio vya mazao ya maua na mboga mboga ili vifungashio hivyo vipatikane kwa bei nafuu na kwa wingi. Vilevile Kamati inashauri Serikali kufanya marejesho ya kodi hiyo kwa sababu kwa kufanya marejesho hayo yatasaidia makampuni husika kuongeza mitaji na uendeshaji na kuongeza tija kwenye uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332; Kamati inaikubaliana Serikali kwa uamuzi wake wa kufanya marejeo ya Jedwali la Kwanza la Kodi ya Mapato kwa sababu kwanza jedwali hilo limekuwa la muda mrefu bila kufanyiwa marekebisho na upangaji wa makundi haukuzingatia hali ya sasa.

Kitendo cha kuongeza kiwango cha mapato ambacho hakitozwi kodi kutoka shilingi 170,000 ya sasa hadi shilingi 270,000 inaonyesha kwa namna gani Serikali hii inawajali wanyonge hasa wale wa kipato kidogo wanaofanya kazi viwandani na mashambani. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kufanya mabadiliko zaidi

katika *Tax Band* ili ziendane na wakati na vipato kadri hali itakavyokuwa inaruhusu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 438; Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kumruhusu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kutatua mapingamizi yanayoletwa kwake. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha mamlaka hayo yanatumika kwa nia iliyokusudiwa na kwa kuzisaidia biashara ziendelee kuzalisha mapato mengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Sheria ya Fedha za Mamalaka za Serikali za Mitaa, Sura 290; mabadiliko yaliyopendekezwa imekuwa ni kilio cha muda mrefu cha wadau katika sekta ya mawasiliano ambao walikuwa wanalaazimika kufanya malipo ya tozo za Huduma kwa Halmashauri 186 ambazo ama wana minara au wana maduka ya kutolea huduma. Pamoja na pendekezo hili jema la mapato haya kuwasilishwa katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa niaba ya Halmashauri jambo la kuzingatia ni kuwa fedha hizi zirudishwe kwa usahihi na kwa wakati katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, aidha Kamati inashauri masuala yafuatayo yazingatiwe wakati utekelezaji wa suala hili; kwanza, kupata idadi kamili ya minara iliyopo nchini; pili uwezo wa kutambua mawasiliano yanayofanywa na kila mnara katika kila Halmashauri na mwisho kuhakikisha kuwa mtawanyo wa mapato unafanywa bila kujali eneo minara hiyo ilipo au ofisi zake zilipo. Vilevile utungaji wa kanuni zitakazotungwa zishirikishe wadau wote ikiwemo Serikali za Mitaa, *TCRA* na wadau wa mawasiliano nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 na Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370; sheria hizi mbili zina lengo la kupanua mawanda ya ukusanyaji wa asilimia 15 ya mapato kutoka taasisi za *TIC*, *TFRA*, *NIDA* na *GPSA* pamoja na kumruhusu Msajili wa Hazina kukusanya asilimia 70 ya fedha za ziada kwa makampuni ambayo yanapata fedha za matumizi kutoka

bajeti ya Serikali. Kamati inaishauri Serikali hatua hizi zisiwe na lengo la kuongeza mapato ya Serikali tu bali na kuhakikisha kwamba taasisi hizi zinaendeleza shughuli zake kama awali.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Sheria ya Usajili wa Magari, Suraya 124; Sheria ya Ardhi, Na. 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Madini 123; mabadiliko yanayopendekezwa katika sheria hizi yana lengo la kuanzisha vyanzo vipyta vya mapato na kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato. Kamati inakubaliana na mapendekezo haya na inaunga Serikali mkono.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004; Kamati imepitia na kuchambua hatua zote ambazo zimechukuliwa na kubaini kwamba hatua hizo zina malengo yafuatayo; kulinda viwanda vya ndani ya Jumuiya, kupunguza ghamara za vifungashio na malighafi zinazotumika katika viwanda vya Jumuiya, kuwezesha sekta ya kilimo na mifugo na kuendeleza usindikaji wa mazao.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imekuwa ikipendekeza mara kwa mara kwa Serikali kwamba hatua hizi za mabadiliko Sheria ya Forodha ya mwaka 2004 yawe yanawasilishwa kwa Kamati ya Bajeti kwa niaba ya Bunge lako tukufu ili kuishauri Serikali kabla hayajapitishwa na Mawaziri wa Fedha, Uwekezaji, Biashara na Uchumi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ileleweke wazi kwamba utaratibu wa kurejesha mabadiliko hayo katika Jumuiya endapo Bunge lako tukufu halikubaliani na mapendekezo yaliyopitishwa ni mrefu na hautaleta taswira nzuri kwa Taifa letu. Kamati inaiomba Serikali ilifikirie suala hili kwa undani ili Bunge ijalo lisikutane na changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango wa kuboresha mazingira ya kufanya biashara (*blue print*); Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania kwa uamuzi wa kusimamia, kufuta na kupunguza tozo, ushuru na ada mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, uamuzi huu ulisubiriwa na sekta binafsi kwa muda mrefu na kwa hatua hii sekta inafsi itatumia fursa hii kukuza na kuendeleza biashara. Kamati inatoa angalizo kwamba Serikali iangalie utaratibu wa kuanzisha ada, ushuru na tozo mbalimbali kupitia kanuni zisiwe kikwazo kwa maendeleo ya sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha janga la Covid-19; janga la Covid-19 limetokea katika kipindi cha robo ya tatu ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020. Kwa ujumla bajeti za Wizara, Taasisi na Idara za Serikali zilikuwa hazijajikita kukabiliana na janga hili. Aidha, Kamati inalpongeza Serikali kwa juhudhi kubwa ya kusimamia na kuimarisha huduma ya afya na usalama wa watu pamoja na kutoa maelekezo mbalimbali ya kujikinga na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, janga la Covid-19 lina athari kubwa katika utekelezaji wa bajeti hii tunayoimalizia sasa na pia kwa Bajeti inayokuja ya mwaka 2020/2021 kwa kuzingatia kuwa wakati Bunge likipitisha mpango na ukomo wa bajeti mwezi Desemba, 2019 ugonjwa huu haukuwepo. Hivyo, baada ya Covid-19 kuna haja ya kufanya tathmini na mapitio ya mafungu ya bajeti tuliyoyapitisha (*internal reallocation*) ili kuakisi uhalsia huu mpya kwa kuzingatia uimarishaji wa huduma ya afya, usalama wa watu na maendeleo ya uchumi. Hatua hii itasaidia kuwa na uhalsia wa bajeti itakayotatua matatizo ya wananchi kama yalivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Uchaguzi Mkuu; bajeti tunayoipitisha sasa imehusisha pia fedha kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa 2020 wa Rais, Wabunge pamoja na Madiwani. Kamati ya Bajeti inapenda kulijulisha Bunge lako kuwa Serikali imejiandaa ipasavyo katika kutekeleza suala hili. Hivyo, ni muhimu vyombo vyote vinavyohusikia na

Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 vijiandae ipasavyo ili kuhakikisha kuwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 unaimarisha misingi ya kidemokrasia ambayo nchi yetu imejiwekeea.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2020/21; katika kutekeleza Mpango wa Pili wa Taifa wa Miaka Mitano jumla ya shilingi triliioni 107 zilitakiwa kugharamia mpango huo. Mpango huo ulitegemea Serikali kutoa jumla ya shilingi triliioni 59 na sekta binafsi shilingi triliioni 48. Kamati imebaini kwamba kuna changamoto kubwa katika upatikanaji wa takwimu za uchangiaji wa fedha za miradi ya maendeleo kutoka kwa sekta binafsi kwa sababu mbalimbali.

Kamati inaishauri Serikali kutumia utaratibu wa wawekezaji wenyewe kutoa taarifa zao kwa hiari (*self-declaration*) za uchangiaji wa miradi ya maendeleo ili kupata takwimu za uwekezaji uliofanywa na sekta binafsi kwenye miradi ya maendeleo. Baada ya takwimu hizo kupokelewa zinaweza kutumika na Serikali kwa kuziangalia uhalsia wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na ukarabati wa miundombinu ya barabara vijijini; mabadiliko ya hali ya hewa yamesababisha kuwepo na mvua kubwa iliyosababisha mafuriko na uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara hasa kwa upande wa maeneo ya vijijini. Kamati ya Bajeti ilikutana na *TARURA* na kubaini kwamba kiwango cha fedha kilichokuwa kinahitajika kurejesha miundombinu ya barabara ni shilingi bilioni 132.6. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 fedha zote zinazohitajika katika kurejesha miundombinu ya barabara iliyo chini ya *TARURA* zinatolewa ili kukarabati miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na matumizi ya Mfumo wa Stempu za Kodi za Kielektroniki (*ETS*); moja ya matatizo makubwa ambayo yanaikabili nchi yetu ni uwepo wa bidhaa ambazo ama si halisi na zisizo na ubora au zilizoingizwa nchini

kwa njia zisizo rasmi kwa magendo. Bidhaa hizi mara nyingine zinakuwa na madhara makubwa sana kwa wazalishaji wa ndani, afya za wananchi na Wakulima. Mfano sukari ya magendo, mafuta ya kula, pembejeo, madawa ya binadamu na mifugo pamoja na vipodozi.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Mamlaka ya Mapato inatumia mfumo wa Stempu wa Kodi za Kieletroniki ili kujua bidhaa halisi na bidhaa zisizo halisi katika soko pamoja na kuangalia uzalishaji wake ili kodi stahiki ikusanywe. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kutumia mfumo huo katika utambuzi wa bidhaa za ndani kama vile sukari, mafuta ya kula na kujipaka, vipodozi, madawa ya mifugo na pembejeo za ndani na nje ili kwanza kulinda viwanda vya ndani na pili kuwalinda Watazania dhidi ya matumizi ya bidhaa zisizo na ubora. Aidha, Mamlaka ya Mapato Tanzania inatakiwa kuhakikisha inakuwa na mpango wa kurithi mfumo huo na kuendesha mara baada ya mkandarasi aliyepo kumaliza muda wake.

Mheshimiwa Spika, ahueni ya ulipaji wa kodi iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania; hivi karibuni Mamlaka ya Mapato Tanzania imetoa *GN* Na. 351 ambayo imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha 70(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 432. Tangazo hilo lina nia ya kutoa ahueni ya ulipaji wa kodi (*remission*) kama mkakati mmojawapo wa kukabiliana na m dororo wa uchumi unaotokana na janga la Covid-19.

Kamati ya Bajeti ilipata fursa ya kupitia Tangazo hilo na kubaini mambo mbalimbali ambayo kimsingi yana nia njema ya kuisaidia sekta binafsi katika wakati huu mgumu. Hata hivyo, Kamati haijavutiwa na masharti yaliyowekwa. Kanuni ya 5 inatoa masharti ya mnufaika, sharti ambalo linatoa mashaka ni sharti la 5(d) ambalo linamtaka mlipa kodi kulipa kodi yote itakayoahirishwa katika tarehe ambayo Kamishna Mkuu wa *TRA* ameibanisha katika uamuzi wake.

Mheshimiwa Spika, nankuu; "(d) agreed to pay the whole of his principal tax liability on the due date to be

*prescribed by the Commissioner General in his".* Mwisho wa kunukuu.

Kamati inaishauri Serikali kulifirkiria upya sharti hili kwa sababu itakuwa vigumu kwa biashara inayotoka katika msukosuko kulipa kodi yote iliyoahirishwa kwa mkupuo. Ni vyema utaratibu ukabainishwa mathalani ulipaji wa awamu walau tatu baada ya tarehe iliyoamriwa na Kamishna Mkuu kuwadia.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na vitambulisho nya wajasiriamali wadogo; suala la vitambulisho nya wajasiriamali lilikuwa na mkanganyiko mkubwa wakati wa utekelezaji wake. Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alikuwa na nia njema sana ya kusajili wafanyabiashara wote nchini ili watambulike na wachangie kwenye Pato la Taifa. Hata hivyo, utolewaji wake kwa baadhi ya maeneo haukuwa na msingi na dhamira ile ya Mheshimiwa Rais. Tunashukuru sasa Serikali imeandaa kanuni chini ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi ambayo inaweka msingi wa nani anahusika na majukumu kati ya Mamlaka ya Mapato ya Tanzania na Serikali, muda ambao kitambulisho kitakuwa halali na kiwango kinachotakiwa kulipwa kwa ajili ya kupata kitambulisho hicho.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia utaratibu huo na inashauri mambo yafuatayo; kwanza Kitambulisho kuwa na picha ya mfanyakibashara na mahali anapofanya biashara ili kuepusha kitambulisho kimoja kutumika na watu tofauti; pili, kubainisha muda wa miezi 12 uliobanishwa kwenye kanuni haujataja wazi kama ni mwaka wa fedha wa Serikali au mwaka wa kalenda na tatu Serikali za Mitaa hazijajipanga vizuri katika kuainisha maeneo ya wafanyabiashara wadogo kama kanuni inavyowataka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini endapo masuala hayo yatafanyiwa kazi basi yataongeza ufanisi katika kuwatambua wajasiriamali wadogo pamoja na kupata takwimu sahihi za ukusanyaji wa mapato kutoka kwa wafanyabiashara wadogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na utunzaji wa mazingira; utunzaji wa mazingira pamoja na kudhibiti na kujenga uwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ni masuala ya msingi katika kuhakikisha ukuaji endelevu wa uchumi. Katika kutambua hili, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza la Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) zimeweza kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira pamoja na kuratibu na kusimamia programu mbalimbali za mazingira kama vile Mradi wa Kuhimili Athari ya Mabadiliko ya Tabia nchi Kupitia Mifumo ya Ikolojia, kufanya kaguzi za uharibifu wa mazingira katika maeneo ya uwekezaji, upandaji wa miti na kuzuia uharibifu wa misitu na vyanzo vya maji. Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali ikamilishe Mradi wa Kuwezesha Mfuko wa Mazingira kwa kuainisha na kupendekeza vyanzo vya mapato kwa ajili ya uendeshaji wa mfuko na hivyo kutimiza malengo yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, njia za kuchochi ukuaji wa uchumi; hotuba ya Hali ya Uchumi imebainisha shughuli za kiuchumi ambazo zimechangia kwa kiasi kikubwa kwenye ukuaji wa Pato la Taifa. Shughuli hizo ni uchimbaji wa madini, ujenzi, sanaa, burudani, usafirishaji na uhifadhi mizigo. Aidha, shughuli hizi zote isipokuwa sanaa na burudani zimetokana na uwekezaji mkubwa wa Serikali katika sekta husika. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwa na mipango na mikakati itakayosalidia shughuli nydingine za kiuchumi zinazoendeshwa na sekta binafisi mfano sekta za huduma, kilimo na mifugo ili na zenyewe zikue kwa kasi na kuweza kusaidia kukua kwa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na uvuvi wa bahari kuu, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua yake ya kuondoa tozo ya dola 0.4 kwa kilo moja ya samaki aina ya jodari anayevuliwa katika bahari kuu. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuharakisha mchakato wa ujenzi wa bandari ili Serikali iweze kupata mapato ya leseni peke yake. Bandari ya uvuvi itawezesha uwepo wa viwanda vya kuchakata minofu ya samaki nchini, ajira kwa Watanzania,

kodi na tozo kutoka mamlaka mbalimbali, udhibiti wa uvuvi haramu na ushushaji wa samaki wasiolengwa kwa matumizi ya soko la ndani.

Mheshimiwa Spika, gharama za *ETS* kwenye sigara; pamoja na hatua nzuri ya Serikali kuanzisha Mfumo wa Kodi za Kielektroniki ambao umeonesha matokea mazuri hasa katika kuhakikisha kuwa Serikali inapata kodi stahiki, mfumo huu umekuwa sio rafiki kwa sekta ya sigara katika gharama za stempu za bidhaa husika. Sigara zinatozwa kiasi cha dola 20 kwa stempu 1000, gharama ambazo zipo juu ukilinganisha na viwango vinavyotozwa kwa bidhaa kama vile bia dola nane kwa stempu 1000. Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kubadilisha kiwango hiki kilingane na kiwango kinachotozwa kwenye bidhaa nydingine.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la mapato ya *TAWA*, *TANAPA* na *NCCA* kukusanya na Mamlaka ya Mapato Tanzania; Serikali imekusudia kuanzisha utaratibu mpya wa kukusanya mapato yote yanayotokana na shughuli za utalii, wanyamapor na uhifadhi yaliyokuwa yakikusanya awali na *TANAPA*, *NCCA* na *TAWA*. Hatua hii imekuja kipindi ambacho mamlaka hizi zimeathiriwa kwa kiwango kikubwa na gonywa la Covid, hivyo mapato yake kushuka kwa kasi na kuna wasiwasi zingeweza kushindwa kuijendesha.

Mheshimiwa Spika, Serikali hajjaweza kufafanua nia hasa ya uamuzi huu kwa sababu mamlaka hizi zimekuwa na ufanisi mkubwa katika ukusanyaji wa mapato yake na utekelezaji wa majukumu yake na Serikali imekuwa ikikusanya kodi, mchango wa asilimia 15 na michango mingine mbalimbali. Kamati ingependa kujua lengo hasa la Serikali katika uamuzi huu ni lipi ukizingatia kuna mashirika mengi ya Serikali ambayo yanatoa huduma na mapato yake hayakusanywi na *TRA*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ufanyaji wa tathmini ya utekelezaji wa mpango na miradi ya maendeleo; Serikali iko katika mchakato wa kutafuta mshauri mwelekezi kwa ajili ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo

wa Taifa wa Pili kwa kipindi cha miaka minne wa utekelezaji pamoja na tathmini ya miradi ya maendeleo. Kimsingi, tathmini ya mpango huu ulipaswa kuweka misingi ya uandaji wa mpango unaofuata. Kamati ilibaini kwamba tathmini hiyo itakapo kamilika haitwakuwa na mantiki kwa sababu Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa utakuwa umeanza kutekelezwa. Hivyo, Kamati inashauri tathmini hiyo iwe inafanyika walau katika nusu ya muda wa utekelezaji wa mpango wa miaka mitano husika.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango imeonesha kuwa zoezi la tathmini ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Serikali za Mitaa limekasimiwa TAMISEMI.

Aidha, Kamati inaona changamoto ya utekelezaji wa suala hili, hasa ikizingatiwa kuwa kuna miradi inayotekelizwa katika Serikali za Mitaa lakini inasimamiwa moja kwa moja na Wizara za Kisekta. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kwamba Wizara ya Fedha na Mipango ikishirikiana na TAMISEMI kuwa Wizara zinazoratibu ufuatiliaji na tathmini na kuachia zoezi hilo kufanywa na Wizara, Idara, Wakala na Taasisi mbalimbali za Serikalii ili waweze kutekeleza zoezi hilo kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya *Business Facilitation Act 2020*na Sheria ya Kujilinda Dhidi ya Athari za Biashara (*Trade Remedies Act, 2020*). Kamati pia inaitaka Serikali kukamilisha na kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya *Business Facilitation Act, 2020* pamoja na Sheria ya Kujilinda Dhidi ya Athari za Biashara (*Trade Remedies Act, 2020*) kwa lengo la kuzuia uingizaji wa bidhaa kwa wingi pamoja na kuzuia kuingiza bidhaa zisizo na ubora. Hatua hii ni muhimu sana kwani itasaidia kulinda viwanda vyetu vya ndani na kuvifanya viwe shindani zaidi. Aidha, Serikali iweke msisitizo wa kutumia zaidi bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu nchini kabla ya kutumia bidhaa za nje.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii tena kukushukuru wewe kwa kunipa fursa mimi binafsi na kuniamini

kuwa kiongozi wa Kamati hii ya Bajeti wakati Mheshimiwa Simbachawene alipopata kazi nydingine. Ninakushukuru sana kwa kuniamini na ninaamini ya kwamba sikukuangusha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumshukuru sana tena Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango - Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji - Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nawashukuru Katibu Mkuu na wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili mapendekezo ya mpango huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii ya Bajeti kwa umakini wao na utayari wao kufanya kazi tangu asubuhi mpaka jioni na wakati mwingine mpaka usiku; jana tumefanya kazi mpaka saa sita usiku. Nawashukuru sana kwa kujitolea kwa namna hiyo. Sijui kama ulikuwa unaulizia wametokea wapi lakini naamini kwamba wao wanamoyo wa kujitolea na kwa kweli walionekana kama wanatoka familia moja, maana hakuna aliyekuwa mbishi, tukisema tukutane saa mbili usiku tunakutana. Kwa hiyo, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii ya Bajeti. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia fursa hii pia kumshukuru Ndugu Stephen Kagaigai, tumekuwa tukiwasiliana naye tunapopata matatizo au tukihitaji miongozo mbalimbali. Huyu Katibu wa Bunge ameiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, natambua mchango mkubwa wa Sekretarieti ya Kamati kwa kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makof*)

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI  
KUHUSU TAARIFA YA HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA  
2019, MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA  
2020/21, TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI  
KWA MWAKA 2019/20 PAMOJA NA MAPENDEKEZO YA  
SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA  
MWAKA WA FEDHA 2020/21 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 105 (8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo Januari 2016 naomba kutumia fursa hii kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2019, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2020/21 pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2019/20 pamoja na Mapendekoz ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/21.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeendelea kutekeleza ipasavyo majukumu yake kikanuni na kisheria kama yaliyoainishwa kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la 2016, pamoja na Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015. Aidha, Kamati imeendelea kushauri na kuisimamia Serikali katika kutekeleza bajeti yake kwa ufanisi kwa nia ya kujenga na kuimarisha uchumi wa Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali imekuwa ikitoa ushirikiano wake wa kutosha kwa Kamati katika kipindi chote na hivyo kuwa na uhusiano mzuri wa kikazi baina ya Kamati na Serikali. Kamati inapenda kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa namna ambavyo ameliongoza Taifa kwa umahiri mkubwa katika kuhakikisha kwamba Tanzania inasonga mbele hasa katika mapambano dhidi ya janga la COVID 19. **Mheshimiwa Rais** ameonyesha Utashi, Utayari, umahiri na weledi mkubwa katika kupambana na janga hili. Vilevile Kamati inapenda kuwapongeza Makamu wa Rais

Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, Kamati inakupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa uongozi wako mahiri uliojaa weledi na uzoefu wa kutosha katika kuliendesha Bunge hili la Kumi na Moja (11) la Jamhuri la Muungano la Tanzania. Sisi kama Kamati tunakushukuru kwa miongozo yako na ushirikiano uliotupa katika kutekeleza majukumu yetu.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Philip Mpango Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Ashatu Kachwamba Kijaji Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa kushirikiana vyema na Kamati wakati wote tulipowahitaji kwenye Kamati ili kuhakikisha Kamati inafanya kazi zake kwa ufanisi. Aidha, Kamati inawashukuru Katibu Mkuu wa Fedha Ndg. Doto James na Manaibu wake, Gavana wa Benki Kuu Prof. Frolence Luoga, Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania Dkt. Edwin Muhede na Wakuu wa Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali kwa ushirikiano wao na mshikamano waliouonyesha kwa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii inatoa taswira ya mwelekeo wa nchi kwa kuangalia viashiria mbalimbali vyta uchumi, miradi ya kimkakati inayotekelawa na Serikali, mwenendo wa mapato na matumizi. Pia, imemainisha maeneo mbalimbali ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Aidha, taarifa hii pia imegusia juu ya janga hili la ugonjwa wa COVID-19 ulioukumba nchi yetu na dunia kwa ujumla ambayo kimsingi utapelekea kuwepo na mabadiliko katika uchumi.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu saba (7). Sehemu ya kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya pili ni Tathmini ya Mwenendo wa viashiria vyta uchumi jumla; Sehemu ya tatu ni Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/20; Sehemu ya nne ni Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Pili (2016/17-2019/20) pamoja na Mpango wa Mendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2020/21; Sehemu ya tano inahusu Sura ya Bajeti ya Serikali

kwa mwaka wa fedha 2020/21, Maoni na Mapendekezo ya Kamati na mwisho ni Hitimisho.

## TATHMINI YA MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI KWA MWAKA 2019

### Hali ya uchumi wa Dunia


**Mheshimiwa Spika**, kufuatia Janga la homa kali ya mapafu yaani COVID 19 umesababisha athari kubwa katika mtazamo na mwelekeo wa ukuaji wa uchumi wa nchi mbalimbali Duniani. Kwa mujibu wa Taarifa ya World Economic Outlook inayoandaliwa na Shirika la fedha Duniani IMF inaonyesha kwamba ukuaji wa uchumi wa Dunia kwa mwaka 2021 kwa nchi zilizoendelea utashuka hadi kufikia **asilimia 2.4** tofauti na **asilimia 5.8** iliyokuwa imetarajiwa hapo awali. Aidha, kwa upande wa nchi zinazoendelea uchumi unatarajiwa kushuka kutoka matarajio ya **asilimia 6.6** mwaka 2021 hadi kufikia **asilimia 2.0**. Taarifa hiyo imetoa rai kwa mataifa yote Duniani kuwa na mkakati wa kupambana na m dororo wa uchumi katika muda wa kati na muda mrefu na kuwa na mbinu za kuchochaea ukwasi katika sekta za uchumi na mkakati wa kuinua uchumi utakapokuwa unarejea katika hali yake ya kwaida. Jedwali Namba 1, hapa chini linaonyesha mwenendo wa Uchumi wa Dunia kuanzia kipindi cha 2015 hadi Mwezi Aprili 2021. Kamati inaishauri Serikali kuzingatia ushauri huo ili iweze kusaldia Taifa kujikwamua katika m dororo wa uchumi uliopo na unaotarajiwa katika mwaka 2021.

### Jedwali Namba 1: Mwenendo wa Uchumi wa Dunia kwa Kutumia kuanzia Mwaka 2015 hadi Aprili 2021:

MWAKA	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Uchumi wa Dunia	3.2	3.7	3.9	3.6	2.9	-3	2.4
Uchumi Nchi zilizoendelea	1.9	1.7	2.4	2.2	1.7	-6.1	2.9
Uchumi Nchi zinazoendelea	4	4.1	4.4	4.5	4.7	-5.4	2.0

**Chanzo:** *World Economic Outlook report za Mwezi Aprili kuanzia 2015 hadi 2020*

### Kielelezo Namba 2 .Ukuaji wa Uchumi Duniani:




Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

### Hali ya ukuaji wa Uchumi kwa Mwaka 2019

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2019 Pato la Taifa kwa bei ya mwaka husika ilikuwa na thamani ya **Shilingi Bilioni 129,043,901** ukilinganisha na **Shilingi bilioni 108,362,329** mwezi Desemba 2019. Ongezeko hilo ni sawa na ukuaji wa **asilimia 6.9** ambao ni sawa na ule wa mwaka 2018. Ukuaji huu umechangiwa zaidi na shughuli za uchimbaji madini na mawe (**asilimia 17.7**), ujenzi (**asilimia 14.8**), sanaa na burudani (**asilimia 11.2**), na usafirishaji na uhifadhi mizigo (**asilimia 8.7**).

### Kielelezo Namba. 3: Pato la Taifa kwa Bei za Mwaka Husika

#### Pato la Taifa kwa Bei za Mwaka Husika



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

## Mfumuko wa Bei

**Mheshimiwa Spika**, Kiwango cha mfumuko wa bei katika mwaka 2019 ilikuwa **asilimia 3.4** ukilinganisha na **asilimia 3.5** mwaka 2018 ambacho kiko ndani ya wigo wa lengo la Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki la **asilimia 5**. Mfumuko wa bei wa Chakula ulikuwa kwa **asilimia 4.3** kutokana na kuimarike kwa bei ya mazao ya bidhaa kwa nchi jirani hivyo kupelekea chakula kingi kuuzwa nje. Hivyo kiwango cha Mfumuko wa Bei kuimarike kimesababishwa na kupungua kwa bei ya mafuta katika soko la Dunia pamoja na upatikanaji wa chakula cha kutosha nchini. Kutokana na hali hii, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba kunakuwa na hifadhi ya kutosha ya chakula kuepuka Mfumuko wa Bai unaosababishwa na upungufu wa chakula.

## Mwenendo wa Thamani ya Shilingi

**Mheshimiwa Spika**, Thamani ya Shilingi dhidi ya dola ya Marekani imeendelea kuwa imara kwa kipindi cha miaka mitatu. Uimara wake unatokana na kuongezeka kwa mazao ya asili ya biashara (Traditional Crops) kama vile Korosho katika kipindi cha kuanzia mwezi Desemba mwaka 2017 hadi mwezi Desemba 2019. Dola ya marekani imekuwa ikibadilishwa kwa wastani wa shilingi za kitanzania **2,267.3** mwaka 2017, **Shilling 2,275.9** mwaka 2018 na **Shilingi 2,289.1** mwaka 2019. Kamati inaishauri Serikali kuongeza mauzo nje ya nchi ili kuimarisha shilingi dhidi ya dola ya marekani.

## Mwenendo wa Sekta ya Benki

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Desemba 2019 uwiano wa mitaji ya Taasisi za Kibenki ukilinganisha na rasilimali ulikuwa **asilimia 17.08** kiwango ambacho ni zaidi ya ukomo wa chini wa **asilimia 10**. Vilevile kiwango cha mali zinazowenza kubadilishwa kuwa rasilimali fedha kilikuwa **asilimia 31.61**, kiwango ambacho ni juu ya ukomo wa **asilimia 20**. Aidha mwenendo wa riba za mikopo binafsi ulishuka kutoka **asilimia 16.97** mwaka 2018 hadi **asilimia 16.87** mwaka 2019. Mikopo chechefu ilipungua kutoka **asilimia 10.7** mwezi Desemba 2019

hadi **asilimia 9.7**. Hata hivyo, pamoja na mabenki kuwa na hali hiyo nzuri ushukaji wa viwango vyta riba umekuwa sio kwa kiwango kilichotarajiwa. Kamati inaitaka Serikali kuangalia ghamama za mabenki na vihatarishi vinavyosabaisha riba zisishuke kama inavyotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua zilizochukuliwa na Serikali kupitia Benki Kuu (BOT) katika kurekebisha na kudhibiti sekta ya fedha na upatikanaji wa huduma ya fedha katika shughuli za kiuchumi, Kamati bado inasisitiza kuwa hatua hizi zilenge kuwanufaisha walengwa na sio Taasisi za fedha. Aidha, taasisi za fedha ziangalie uwezekano wa kufanya marejeo ya mikopo pamoja na ulipaji unaozingatia hali halisi ya uchumi ili wakopaji wasiweze kupoteza mali walizoziweka kama dhamana.

### **Sekta ya Biashara ya Nje**

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Biashara ya Nje imekuwa ikifanya vizuri kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2019/20. Takwimu zinaonyesha katika kipindi hiki, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ilikuwa Dola za marekani **milioni 5,554.4** na thamani ya bidhaa na huduma ilyoagizwa nje ilikuwa dola za marekani **milioni 5,648.1** hivyo ni wazi kwamba nakisi ya urari wa jumla ilikuwa ikipungua kwa kasi kutokana na uuzaaji wa zao la korosho na mazao mengine ya kiasili pamoja na dhahabu. Kamati inasisitiza Serikali kuendelea kufanya mapitio ya sera za fedha na kibajeti ili kuimarisha uchumi ili kupunguza athari zilizoanza kujitokeza na zinazoweza kujitokeza baadae.

### **Akiba ya Fedha za Kigeni**

**Mheshimiwa Spika**, moja ya kigezo muhimu Duniani cha kupima uwezo wa nchi kukabiliana na majanga au msukosuko wa uchumi ni akiba ya fedha za Kigeni. Hadi kufikia mwezi Desemba 2019 Tanzania ilikuwa na akiba ya fedha za kigeni ya jumla ya Dola za marekani **Bilioni 5,554.4** ambayo ni sawa na ongezeko la **asilimia 9.1**. ukilinganisha na jumla ya Dola za marekani **Bilioni 5,044.6** katika kipindi

kama hicho mwaka 2018. Kiwango hichi kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa miezi 6.4, kiwango hiki ni zaidi ya lengo la miezi 4 kwa nchi za Afrika Mashariki na Miezi 6 kwa nchi za SADC. Kamati inaamini kiasi hiki cha fedha kinawezeka kabisa kulivusha Taifa katika kipindi hiki kigumu.

### **Deni la Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Marchi 2020 Deni la Serikali lilikuwa jumla ya **Shilingi Bilioni 54,976.2** sawa na ongezeko la **asilimia 8.3 ukilinganisha** na **shilingi Bilioni 50.772.3** katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Ongezeko hilo la Deni limetokana na upatikanaji wa mikopo mipyka kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati imejiridhisha pasipo shaka kwamba Deni la Serikali ni himilivu kwa viwango vyote vya kimataifa vya kupima uhimillivu wa deni. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba mikopo yote inayochukuliwa inaelekezwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo tu. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kutumia fursa iliyotangazwa na Shirika la Fedha Duniani (IMF), Benki ya Dunia (WB) na Nchi za G20 kwa uangalifu ili fursa hizo zisijekuwa mzigo kwa Taifa huko baadae kwa kuliongezea taifa deni la Serikali.


### **Tathmini ya Hali ya Umasikini Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, tafsiri ya Umasikini ni hali ya kaya au mtu binafsi kutojitosheleza mahitaji ya msingi ya kila siku ikiwa ni pamoa na chakula na mahitaji mengine ya msingi kama huduma ya jamii, kinga ya jamii, huduma za kifedha, mavazi na malazi kwa kiwango kinachokubalika. Kamati ya Bajeti inatambua kuwa mojawapo ya hatua kubwa ya kupiga maendeleo sio tu kukua kiuchumi lakini pia kuhakikisha umaskini wa mahitaji ya msingi na umaskini wa chakula unapungua. Kwa mujibu wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi (Household Budget Survey (HBS-2017/18)) uliofanywa na Ofisi ya Takwimu (NBS), unaonyesha kuwa **asilimia 26.4** (13,910,507) ya watu wa Tanzania Bara wanaishi katika umaskini wa mahitaji (**matumizi chini ya TZS 1,644.0** kwa

siku na ni mkubwa vijijini (31.3%) kuliko mijini (15.8%). Na **Asilimia 8.0** (4,215,305) ya watu wa Tanzania Bara wanaishi katika umaskini wa mahitaji ya chakula (**matumizi chini ya TZS 1,109.53 kwa siku**) na ni mkubwa vijijini (9.7%) kuliko mijini (4.4%).

#### Kielelezo Namba. 4: Viashiria vya Umaskini katika Ngazi ya Taifa

##### Viashiria vya Umaskini katika Ngazi ya Taifa




Chanzo: Ofisi ya Takwimu ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, ukifuatilia na kulinganisha takwimu hizi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, utaona kuwa Serikali imejitahidi kupunguza umaskini wa mahitaji na umaskini wa chakula kwa kiwango cha kuridhisha. Kwa Tanzania Bara, takwimu zinaonyesha kutoka mwaka 2011/12 hadi 2017/18 umaskini wa mahitaji ya msingi umepungua kwa **asilimia 1.8** (kutoka 28.2 hadi 26.4) na umaskini wa chakula umepungua kwa **asilimia 1.7** (kutoka **asilimia 9.7** hadi **asilimia 8.0**). Pia kumekuwepo na ongezeko la tofauti ya kipato kutoka **asilimia 0.34** mwaka 2011-12 hadi **asilimia 0.38** mwaka 2017-18. Ongezeko hili unaliona zaidi katika maeneo ya mijini (**kutoka 0.37 hadi 0.38**), Dar es Salaam (**kutoka 0.35 hadi 0.42**) na katika maeneo ya vijijini kutoka 0.29 hadi 0.32. Aidha, kuna uhusiano wa moja kwa moja kwa kuongezeka kwa idadi ya watu katika kaya na kuongezeka umaskini. Umaskini

unaongezeka kulingana na ongezeko la idadi ya wanakaya. Takwimu zinaonyesha kuwa umaskini wa mahitaji ya msingi ni mdogo kwenye kaya za mtu mmoja mmoja (**1.7%**) kuliko kwenye kaya zenye watu7 au Zaidi (**38.7%**). Pia, Karibu ya nusu (**47.8%**) ya idadi ya watu nchini ni wategemezi, ikiwa na maana kwamba wenye umri chini ya miaka 15 au wenye umri zaidi ya miaka 65 au zaidi. Uwiano wa utegemezi ni mkubwa mkoa wa Simiyu (**55.2%**) na mdogo mkoa wa Dar es salaam (**35.0%**).

#### Kielelezo Namba. 5: Mwenendo wa Umaskini 2011/12 Hadi 2017/18

##### Mwenendo wa Umaskini 2011/12-2017/18



**Chanzo:** Ofisi ya Takwimu ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu hizi zinaonyesha wazi kwamba juhudii zaidi zinahitajika kufanyika na Serikali ili kupunguza kiwango cha umasikini kwa Watanzania kwa kasi zaidi.

#### 3.0. MAPAMBANO DHIDI YA JANGA NA ATHARI COVID -19 KATIKA UCHUMI WA NCHI.

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kuwa Tarehe 16, Machi 2020, Serikali kuititia kwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu (MB) ilitangaza Kisa cha kwanza cha kuwepo kwa Mgonjwa wa COVID-19 nchini. Tangu kutangazwa kwa Ugonjwa Mheshimiwa **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** aliushangaza ulimwengu kwa kufanya uamuzi thabiti, mahiri na kuliongoza taifa katika namna bora ya kupambana nalo.

Alimuweka mwenyezi Mungu mbele na Watanzani wote tulikuwa nyuma yake. Japo kuna baadhi ya sekta zimeathirika kwa kiasi kikubwa kama ile ya utalii, ukarimu na usafirishaji. Katika kipindi hichi Mheshimiwa Rais ameliwezesha Taifa kuendelea na shughuli nyingine ambazo ni za msingi kwa maendeleo ya nchi kama kilimo, uzalishaji wa Viwandani, bishara, usafiri na usafirishaji wa ndani.

**Mheshimiwa Spika**, ugonjwa huu unaweza kuleta katika upatikanaji wa mapato kutohana na kupungua kwa ajira, kushuka kwa biashara ya kimataifa na sekta nyingine ambazo uendeshaji wake unategemea mataifa mengine. Aidha, Ugonjwa huu kwa kiasi flani umeathiri Bajeti ya Mwaka 2019/20 kwasababu ilibidi kiasi cha fedha kihamishiwe katika Wizara ya Afya ili kupambana na ugonjwa huu. Haitakuwa jambo la busara endapo sitatambua juhudzi za Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu katika kupambana na janga hilli kweli amethibitisha kwa umma kwamba Wanawake wanaweza. Vilevile napenda kuipongeza Serikali kwa kupokea jumla ya **dola za marekani milioni 14.3** kutoka mfuko wa Catastrophic Containment Relief Fund ili kusaidia katika mapambano dhidi ya ugonjwa huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwepo kwa jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali katika kushughulikia Janga la **COVID- 19** pamoja na Athari zake mathalani Benki Kuu ya Tanzania (BOT), kuanza kuchukua hatua za udhibiti wa sekta ya fedha (Monetary Policy) na upatikanaji wa huduma ya fedha katika shughuli za kiuchumi. Hatua za kushusha kiwango cha amana kutoka **asilimia 7** hadi **asilimia 6**, kushusha kiwango cha riba kutoka **asilimia 7** hadi **5** pamoja na kuongeza unafuu kwenye dhamana na hati fungani za serikali; zitasaidia mabenki na taasisi za fedha kuweza kujadiliana na wateja namna ya kurejesha mikopo kwa kuzingatia unafuu na hali ya mteja ilivyo kwa sasa. Hatua kama hii ifanyike pia katika Sera za Kibajeti (Fiscal Policy) na Sera za Kisekta (mfano Sera ya Elimu, kilimo, biashara na viwanda) kwa lengo la kuhakikisha kunakuwepo na mazingira wezeshi ya maendeleo ya jamii na hivyo kupunguza atahari za janga hili.

**Mheshimiwa Spika**, masuala mengine muhimu ambayo lazima yaendelee kutekelezwa ni kuimarisha huduma ya afya na usalama wa watu; Kulinda na kuimarisha Uchumi ili shughuli ziendelee (To keep the economy afloat); Kuimarisha ajira na kipato; Kuimarisha usalama wa chakula na utoaji wa huduma; Kufanya mabadiliko ya muda kwa kodi, tozo, ushuru na ada kwa baadhi ya bidhaa na huduma zilizoathiriwa. Kamati inaamini juhudhi hizi zitatuvusha salama.

#### **UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20**

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2019/20 Serikali ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya **Shilingi triliuni 33.11**, ikijumuisha **shilingi triliuni 20.86** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi triliuni 12.25** kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 Serikali ilikuwa imekusanya jumla ya **shilingi triliuni 26.13** sawa na **asilimia 93.2** ya lengo la robo tatu ya mwaka. Kati ya fedha hizo jumla ya **shilingi triliuni 17.22** zilitumika kwa matumizi ya kawaida ambazo zinajumuisha **shilingi triliuni 8.48** kwa ajili ya kugharlamia Deni la Serikali, **shilingi triliuni 2.91** zilitumika kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi triliuni 5.83 kwa ajili ya mishahara. Aidha, **shilingi triliuni 7.63** zilitumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapenda kuipongeza sana Serikali kwa ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ambayo imefikia **asilimia 93.2** ya lengo la robo tatu ya 8/19mwaka ikilinganishwa na ufanisi wa kipindi kama hiki mwaka 2019. Ufanisi huu umeweka historia katika nchi yetu chini ya uongozi wa **Mheshimiwa Rais John Joseph Pombe Magufuli**.

#### **Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2019/20**

**Mwenendo wa Mapato.**

##### **a) Mapato ya Kodi**

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha robo tatu ya mwaka, Serikali imepata mafanikio makubwa sana katika ukusanyaji

wa mapato. Ni kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi hii Serikali ilikusanya jumla ya **shilingi trillioni 1.3** katika mwezi Septemba, 2019. Hatua hii inaonyesha hali na muamko wa wananchi kulipa kodi. Idara inayoongoza kwa kuingiza mapato ya kodi ni idara ya forodha, ikifuatiwa na Idara ya Walipa kodi wakubwa na ya mwisho ni idara ya walipa kodi wa ndani. Kutokana na m dororo wa biashara za kimataifa kuna uwezekano wa mapato katika idara ya forodha kushuka. Hivyo ni muhimu kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani na kusimamia ulipaji wa kodi kikamilifu ili fedha za kuendesha Serikali zipatikane na utekelezaji wa miradi ya maendeleo uweze kuendelea.

**b) Mapato yasiyo ya Kodi**

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 mapato yasiyo ya Kodi yalkuwa jumla ya **shilingi trillioni 2.25** sawa na **asilimia 87.2** ya lengo. Ni ukweli usiopingika kuwa ufanisi huu umechangiwa na mapato yasiyo ya kodi yanayotokana na michango na gawio la Mashirika na Taasisi za Umma. Kuna kila sababu ya kuipongeza Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kazi kubwa inayofanya katika kusimamia Mashirika na Taasisi ya Umma. Kamati inasitiza Ofisi ya Msajili wa Hazina kutengewa fedha za kutoka ili kutekeleza kikamilifu majukumu yaliyoanishwa katika Sheria ya Madaraka na Majukumu ya Msajili wa Hazina Sura ya 418.

**c) Mapato ya Serikali za Mitaa**

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha robo tatu ya mwaka wa fedha 2019/20 Serikali za Mitaa zimeweza kukusanya jumla ya **shilingi bilioni 561.49** kati ya **shilingi bilioni 765.5** zilizokusudiwa kukusanywa ikiwa ni sawa na **asilimia 73.3** ya lengo. Kwa mwenendo huu inakadiriwa kuwa Serikali za mitaa zitaweza kukusanywa mapato yake kati ya **asilimia 80** na **90** hadi mwaka huu wa fedha utakapoisha. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutekeleza Miradi ya kuingizia Mapato Serikali za Mitaa ambayo ilikuwa imesimamishwa ili kuzisaidia Halmashauri ziweze kujitegemea kimapato.

**d) Misaada na Mikopo ya Masharti Nafuu kutoka Nje**

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2019/20 Serikali ilitarajia kupokea jumla ya **Shilingi bilion 2,783.3** ambapo kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 1,208.1** ilikuwa ni Misaada na **Shilingi Bilioni 1,575.2** ilikuwa ni Mikopo ya masharti nafuu. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2019 Serikali ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi Bilioni 1,318.10** ambazo ni sawa na **asilimia 47** ya mapato yote yaliyokusudiwa. Kwa kiasi kikubwa mafanikio yameonekana kwenye upande wa mikopo yenyе masharti nafuu ambapo jumla ya **shilingi Bilioni 1,085.9** sawa na **asilimia 68.9** ya lengo zilipokelewa ukilinganisha na misaada ambapo zilipokelewa jumla ya **shilingi Bilioni 232.2** tu. Hii inatuonyesha kwamba wahisani sasa hivi wanahama kutoka kwenye misaada na kwenda kwenye mikopo nafuu. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutekeleza Mkakati wake wa DCF (Development Cooperation Framework) ambao umeonyesha matumaini makubwa katika kipindi kifupi.

**e) Mikopo ya ndani**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20 ilikusudia kukopa jumla ya **Shilingi Bilioni 4,959,992** kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 1,499,774** ilikuwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na **Shilingi bilioni 3,460,218** ilikuwa kwa ajili ya kulipia riba za kudumisha Deni (Rollover). Hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 jumla ya **Shilingi Bilioni 4,45 0,000** zilikuwa zimekopwa katika soko la ndani sawa na **asilimia 103** ya kiwango kilichokusudiwa katika kipindi hicho. Pamoja na kwamba kukopa katika soko la ndani si jambo baya ila Serikali lazima iangalie uwiano wa kiasi inachokopa ndani na nje ili kuhakikisha kwamba sekta binafsi ya ndani nayo inapata mikopo kutoka kwenye Taasisi za fedha za ndani.

**Mwenendo wa Matumizi**

**Mheshimiwa spika**, Uchambuzi wa Kamati katika mwenendo matumizi umebainisha masuala yafuatayo: -

### a) Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi kwa mafungu 67 ya Wizara na Taasisi za mbalimbali za Umma zenyet mafungu na kubaini kwamba matumizi ya kawaida yalitolewa kwa mchanganua ufuatao. **Mafungu 20** yalipokea fedha za matumizi ya kawaida kwa **asilimia 100** ya fedha zilizotarajiwa kutolewa hadi mwezi Desemba, 2019; mafungu 34 yalipokea **asilimia 90**; mafungu 10 yalipokea **asilimia 80**; Mafungu 3 **asilimia 70**; Fungu moja **asilimia 60** na Fungu lilopokea fedha ndogo kuliko yote ni **Msajili wa Hazina ambalo lilipokea asilimia 37 tu**. Kwa upande wa Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa fedha zilizopekelewa kwa ujumla wake ni **asilimia zaidi ya 90**.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inapaswa kupongezwa kwa hatua hili kwa sababu imeonyesha uwezo wa kugharamia shughuli zake za uendeshaji za Serikali kwa wastani wa **asilimia 95**. Hata hivyo, pamoja na Ofisi ya Msajili wa Hazina kukusanya mapato ya Serikali kwa kiwango cha kuridhisha bado utolewaji wa fedha kwa matumizi mengineyo kwa Ofisi hii umekuwa sio wa kuridhisha kwa miaka mitatu mfululizo. Kamati inaitaka Serikali kuiwezesha Ofisi hii ili ifanye majukumu yake kikamilifu.

### b) Matumizi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20 Serikali ilipanga kutumia jumla ya **shilingi trilioni 12.25** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Aprilii, 2020 kiasi **shilingi trilioni 7.63** kilikuwa kimetolewa sawa na **asilimia 62.8**. Kati ya fedha zote za maendeleo zilizotolewa, fedha za ndani ni **shilingi trilioni 6.65** sawa na **asilimia 87.2** na fedha za nje ni **shilingi bilioni 976** sawa na **asilimia 12.8**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa upande wa utoaji wa fedha za ndani za maendeleo. Aidha, bado Kamati inasisitiza juu ya suala la kutegemea fedha za nje ambapo mwenendo wa utolewaji wake wa fedha sio wa kuridhisha.

## **TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2019/20 NA MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kuwa tangu tulivyopata uhuru mwaka 1961, ajenda ya maendeleo imekuwa ikiwekewa msukumo mkubwa hasa katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Katika kipindi chote hicho Serikali imekuwa ikiandaa na kutekeleza mipango ya maendeleo ya muda wa kati na mrefu kwa lengo la kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na hivyo kufikia hadhi ya nchi zenyenye uchumi wa kipato cha kati (Middle income country). Katika kufanikisha hili Serikali iliandaa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wamu Tatu katika kipindi cha miaka mitano mitano.

**Mheshimiwa Spika**, mwaka 2011, Serikali ilifanya maamuzi ya kuwa na Mpango Elekezi wa Miaka 15 (roadmap) kwa ajili ya kutekeleza **Dira ya Taifa ya Maendeleo, 2025** kwa utaratibu wa kuwa na vipindi vitatu vya utekelezaji vyenye dhima mahususi yaani; **Mpango wa Kwanza** wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16) uliolenga ‘**kutanzua vikwazo vya kiuchumi, kupunguza umaskini na kuimarishe upatikanaji wa huduma za jamii**’; **Mpango wa Pili** wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) unaolenga ‘**kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu**’; Na mwisho tunatarajia **Mpango wa Tatu** wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) utakaolenga ‘**kujenga ushindani wa kibiashara**’ utakaojikita katika kuongeza mauzo nje na uwezo wa ushindani kikanda na kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, Mipango ya maendeleo ya muda wa kati wa miaka mitano imekuwa ikitekelezwa kuititia mipango ya maendeleo ya muda mfupi ya mwaka mmoja mmoja ambayo imekuwa ikiandaliwa na kutekelezwa kila mwaka. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kipindi hiki cha miaka minne (4) kwa kuweza kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika maeneo ya vipaumbele ambavyo ni **Miundombinu** (Reli, barabara, bandari, usafiri wa anga na nishati); **Kilimo** (Mazao, Mifugo, Uwindaji, Misitu na Uvuu);

**Viwanda; Madini; maendeleo ya rasilimali watu na huduma za jamii** (Afya, Elimu na Maji) na **miradi maalum ya kimkakati** (Flagship Projects).

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka minne (2016/17 – 2019/20) Serikali imetumia kiasi **Shilingi 37,813,207,053,357.70** kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 24,629,849,730,363.80**, (sawa na **asilimia 65.14**) ni fedha za ndani na **Shilingi 13,183,357,322,993.90**, (sawa na **asilimia 34.86** ni fedha za nje). Hii ni sawa na wastani wa utoaji wa **Shilingi 9,453,301,763,339.43** kila mwaka. Hatua hii imewezesha kukamilisha miradi mikubwa 553 inayohusu sekta ya uchukuzi, ujenzi, nishati, afya na elimu. Aidha, ukirejea Taarifa ya Serikali kuhusu tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) imetoa picha halisi '**nini kimefanyika**', '**wapi bado**' na '**tunahitaji nini kifanyike**' ili tuweze kufanikisha Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa (2021/22-2025/26) wenyewe dhima ya '**Kujenga ushindani wa kibashara**'

**Tathmini ya Jumla ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2019/20.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti imechambua kwa kina utekelezaji wa miradi hii ya maendeleo kwa kuzingatia vipaumbele kwa kila sekta kwa kuangalia upatikanaji wa fedha kwa kila kipaumbele; muda wa kati na mrefu wa utekelezaji wa kila kipaumbele; na uwajibikaji wa wataalamu wa sekta husika katika kila kipaumbele. Hivyo, Kamati inatoa tathmini yake ya utekelezaji wa vipaumbele vya kisekta kama ifuatavyo: -

**Sekta ya Miundombinu (Reli, Nishati, Bandari, Barabara na Usafiri wa anga)**

a) Reli

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kutekeleza kwa awamu Mpango wake kujenga kwa SGR mtandao mzima wa Reli ya Kati wenyewe jumla ya km 2,651.

Hadi sasa, Serikali imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kujenga reli ya standard gauge ambapo ujenzi kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro (300km) umefikia asilimia 76.63 na kipande cha Morogoro hadi Makutupora (422 Km) umefikia asilimia 28. Katika ujenzi huu, fedha za ndani kiasi cha **shilingi 2,798,349,295,766.55** kimetumika. Ni matumaini ya Kamati kuwa Serikali itafanikiwa kupata fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vipande vya Reli kutoka Makutupora – Tabora (Km 294); Tabora – Isaka (km 133); Isaka – Mwanza (Km 249); Isaka – Rusumo (Km 371); Tabora – Kigoma (Km 411); Keza - Ruvubu (Km 36); Kaliua – Mpanda hadi Karema (Km 321).

**Mhesimiwa Spika**, Aidha, tumeona jitihada za Serikali katika kukarabati reli ya kat, kufufua reli ya Dar es salam-Tanga-Moshi pamoja na kununua vifaa mbalimbali vikiwemo vichwa vya treni, mabehewa na mabehewa ya breki. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutafuta vyanzo vingine vya fedha pamoja na kutumia utaratibu wa kutumia mfumo wa PPP ili iweze kupata fedha za kugharamia reli ya katiliyobaki pamoja na matawi yake pamoja na ile ya ujenzi wa Reli ya Mtwara – Mbamba Bay na Mchuchuma & Liganga na Ujenzi wa reli ya Tanga – Arusha - Musoma pamoja na matawi ya Engaruka na Minjingu kwa kiwango standard gauge. Utaratibu wa PPP unapunguza mzigo kwa Serikali kugharamia ujenzi wa reli kwa kutumia fedha za ndani. Pia kukamilika kwa reli hizi kutarahisisha usafirishaji wa mizigo ndani na nje ya nchi na hivyo kusaidia kurudisha gharama ya ujenzi kwa haraka na kusaidia ukuaji wa haraka wa uchumi wetu.

## b) Nishati

**Mhesimiwa Spika**, Katika miaka ya nyuma kulikuwa na tatizo kubwa la mgao wa umeme hasa katika kipindi cha kiangazi. Kama kuna uamuza wa Kijasiri na wa Busara alioufanya **Mhesimiwa Rais Dkt John Pombe Joseph Magufuli** ni ujenzi wa bwawa a kuzalisha umeme wa Maji la Julius Nyerere litakalokuwa na uwezo wa kuzalisha **MW 2,115** na ujenzi wake umekwisha gharimu Serikali kiasi cha **shilingi 1,248,221,921,361.14** ambazo ni fedha za ndani hatua hii si ya

kubeza hata kidogo kwa Mtanzania yeoyote anaeitakia nchi hii mema katika ustawi wa jamii na uchumi wa Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, miradi mingine katika sekta ya nishati ni Mradi wa ujenzi wa Njia ya Msongo wa KV 220 kutoka Makambako hadi Songea (umegharimu kiasi cha **shilingi 160,185,181,494.8**); Mradi wa Kupeleka Umeme Vijijini (REA) Njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa Kv 400, kutoka Singida –Arusha – Namanga (umegharimu fedha kiasi cha **shilingi 71,096,244,024.18** na fedha za nje kiasi cha dola za kimarekani (**USD**): **70,926,854.55** na Fedha za ulaya (**EUR**): **2,613,962.59**); Mradi wa Bomba la mafuta ghafi kutoka uganda hadi Tanzania (umegharimu kiasi cha **shilingi 1,205,654,061**); Mradi wa kinyerezi I,II na III pamoja na miradi mbalimbali ya kuboresha miundombinu ya umeme inayohusu usafirishaji, usambazaji na kupozea umeme katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Arusha, Kilimnaro, Iringa, Singida, Shinyanga, Lindi, Mtwara,

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua hii nzuri bado miradi inayohusu gesi katika upande wa Kuchakata na Kusindika gesi (LNG) pamoja na usambazaji kasi yake ya utekelezaji imekuwa ndogo kuliko iliyotarajiwa. Aidha, bado changamoto kubwa iliyopo ni kuwa mpango huu haujaweza kufafanua mikakati pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya malengo ya kutekeleza miradi ya umeme kwa kutumia nishati mbadala kama vile Joto ardhii, makaa ya mawe, upepo na juu.

### c) Bandari

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **bandari** malengo yalikuwa ni kupanua bandari ya Dar Es Salaam, Tanga na Mtwara kwa lengo la kuongeza huduma ya usafirishaji wa mizigo ndani na nje ya nchi; Kuimarisha huduma za usafiri katika Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa kwa kununua Meli mpya na kukarabati meli zilizopo na kuboresha huduma.Malengo haya yanajumuisha pia kupitia upya mifumo ya uendashaji wa bandari ili kuuwianisha na mifumo mingine ya usafirishaji na uchukuzi wa mizigo pamoja na kuongeza vina vya bandari husika. Hata hivyo changamoto

iliyopo sasa ni Serikali kuweza kufikia malengo ya Mpango wa Maendeleo wa kuhudumia tani milioni 84 kwa mwaka, hadi sasa Serikali imeweza kuhudumia tani milioni 18. tu kwa mwaka na hivyo kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**d) Viwanja vya Ndege**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilisha mradi wa Ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere ambao umegharimu kiasi cha fedha za ndani **shilingi 379,496,949,988.61** na fedha za nje **shilingi 342,961,131,267.14**. Aidha, miradi mingine iliyotekelizwa ni pamoja uboreshaji wa na Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Kilimanjaro, Mwanza, Dodoma, Songwe, Bukoba, Tabora, Geita , Mtwara, shinyanga, Sumbawanga, Kigoma.

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi na uboreshaji huu wa viwanja umeenda sambamba na uboreshaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) kwa kununua ndege mpya nane (8), kulipa madeni muhimu ikiwa pamoja kulipa gharama za kuanzia ili kuiwezesha ATCL kujitegemea na kuendesha shughuli zake kwa ufanisi. Aidha, Kamati inaipongea Serikali kwa kuanza mchakato wa kununua ndege mpya ya mizigo. Mafanikio haya ni ya kiwango cha juu kwa kipindi cha muda mfupi wa miaka mitano.

**e) Kilimo (Mazao, Misitu, Mifugo na Uvuvi)**

**Mheshimiwa Spika**, sekta ya kilimo ikijumuisha kilimo cha mazao, misitu, mifugo na uvuvi imeendelea kufanya vizuri katika uchangiaji wa ukuaji wa uchumi kutoka **asilimia 5.3** mwaka 2018 hadi **asilimia 4.4** mwaka 2019. Pamoja na mafanikio hayo bado Lengo la Mpango wa Pili wa ukuaji wa Sekta ya Kilimo kwa mwaka kutoka **asilimia 2.7** ya mwaka 2010 na kufikia **asilimia 8** mwaka 2020/21 halijafikiwa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja ya Serikali kuelekeza fedha nyingi kwenye program za kilimo kama zile za Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II), Kuongeza Uzalishaji wa zao la

Mpunga (Expanding Rice Production Project – ERPP); Mpango wa kuendeleza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (Southern Agriculture Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT)); Mradi wa Kuongeza Uhifadi wa Nafaka) (Storage Capacity Expansion Project) na nyingine bado sekta hii haijaleta manufaa makubwa yaliyotarajiwa. Wananchi wengi vijiji ambao wanategemea kilimo wameendelea kutumia zana na mbinu duni za kale, wakilima kwa kutegemea hali ya hewa na wakiwa hawana mitaji na huduma ya ugani. Aidha, bado kuna changamoto kubwa katika kukamilisha skimu zote za umwagiliaji nchini pamoja na kuweka mazingira wezeshi katika sekta ya kilimo ili iweze kuvutia Sekta Binafsi kuwekeza katika Sekta hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, sekta ya Kilimo ina mahusiano na mshikamano na sekta nyingine kama viwanda, usafirishaji, utalii na biashara. Hivyo, maendeleo ya kilimo yatachochea maendeleo ya sekta nyingine. Kwa mantiki hii, Kilimo si tu kina athari kubwa katika ukuaji wa Uchumi wa Nchi lakini pia kina mchango mkubwa sana katika kuamua hatma ya maisha ya kila siku na maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja pamoja na kuondoa umasikini. Kamati inaendelea kushauri Serikali ihakkishe: -

- i. Inatenga maeneo zaidi ya kilimo pamoja na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji;
- ii. Inaweka mikakati mathubuti ya kuwezesha upatikanaji wa masoko ya uhakika ya mazao ya chakula na ya biashara ndani na nje ya nchi;
- iii. Inaboresha utaratibu wa uuzaaji wa mazao ikiwa pamoja na kutumia Soko la Bidhaa (Tanzania Merchantile Exchange), kuanzisha minada ya mazao kama vile chai hapa hapa nchini;
- iv. Kurahisisha upatikanaji na kuongeza matumizi ya pembejeo na teknolojia za kisasa na kilimo cha kutumia mashine;
- v. Kuendeleza shughuli za usindikaji wa mazao na uongezaji wa thamani

vi. Kuendelea kuweka mazingira mazuri kwa wakulima hasa katika upatikanaji wa ardhi, marekebisho ya sera za kodi, mabadiliko ya kimta zamo kuhusiana na kilimo hasa katika upande wa upatikanaji wa mikopo;

vii. Kuweka mikataba na nchi nyingine kwa ajili ya kuwezesha uuzaji baadhi ya mazao yetu yanayozalishwa kwa wingi hapa nchini kama vile Korosho, mahindi, Mbazi, Soya, matunda, mboga, nyama, samaki na maua. Hatua hii itasaidia kuwa na masoko ya uhakika.

**Mhesimiwa Spika**, hatua hizi zote zitafanikiwa zaidi kama Serikali itasimamia vizuri utekelezaji wa miradi yake inayohusu kilimo na umwagiliaji pamoja na kutenga asilimia 10 ya Bajeti kwa ajili ya shughuli za Kilimo.

**Mhesimiwa Spika**, bado kuna uwekezaji mdogo katika Sekta ya Mifugo hali inayofanya sekta hii kushindwa kuchangia kikamilifu kwenye Pato la Taifa licha ya idadi kubwa ya mifugo iliyopo nchini. Mpango wa miaka mitano uliweka lengo la kufikia ukuaji wa wastani wa **asilimia 5** kwa mwaka. Hata hivyo, wastani wa ukuaji wa sekta hii katika kipindi husika ulikuwa ni **asilimia 1.5**. Aidha, Sekta hii haifanyi vizuri ukizingatia kuwa; **Moja**, haipati Fedha za Nje kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo; **Pili**, haipati Fedha za Ndani za kutosha kwa ajili ya utekelzaji wa miradi ya maendeleo kama zinazoidhinishwa na Bunge (**lmepokea asilimia 7 tu**). Hivyo, pamoja na kuwepo kwa program mbalimbali za miradi ya maendeleo; kuna hatari kubwa kwa sekta hii kuendelea kudumaa katika ukuaji wake licha ya kuwa Tanzania ni nchi ya tatu kwa wingi wa mifugo Barani Afrika

**Mhesimiwa Spika**, Sekta ya uvuvi, pamoja na kufanya vizuri katika ukusanyaji wa maduhuli na kufikia **Tshs. 2,239,585,000.57** sawa na **asilimia 67.75** ya lengo kwa kipindi cha hadi mwezi Machi 2020; takwimu zinaonyesha kwamba ukuaji wa sekta ya uvuvi kwa Mwaka 2020 ulikua kwa **asilimia 4.9** Hivyo, ni dhahiri programu za maendeleo zilizopo hazijaweza kukidhi lengo la kuu la Mpango wa Maendeleo la kufanya uvuvi wa kisasa na kibashara kwa kuongeza tija

kwenye mapato ya Serikali. Kamati inaendelea kushauri Serikali kuharakisha ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ili Kuwezesha meli zinazovua katika Bahari Kuu kutia nanga na kuhaulisha samaki, kuuza samaki, kutoa takwimu sahihi na huduma nyingine. Pia Serikali ihamasishe ufugaji wa samaki katika mabwawa ili kuongeza kipato kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, aidha Kamati inapongeza kwa hatua ya Serikali kuongeza bajeti ya maendeleo kwa fedha za ndani kwa takribani ya asilimia 70 ili kuhakikisha inatekeleza miradi ya Uvuvi. Hatua, hii imefikiwa baada ya kushuka kwa bajeti ya maendeleo kwa Fedha za Nje kutokana na sababu kuu mbili; **kwanza** kuyumba kwa uchumi wa dunia hususan nchi za Ulaya Mashariki kutokana na ugonjwa wa **COVID 19**, na **Pili** wahisani wameshindwa kutoa fedha za kuchangia maendeleo ya Sekta ya Uvuvi kama walivyoahidi. Ni matumaini ya kamati kuwa ongezeko la bajeti ya maendeleo kwa upande wa fedha za maendeleo kutaleta chachu ya utekelezaji wa miradi wa uvuvi na hivyo kuongeza mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa shughuli za misitu, kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kuboresha shughuli za misitu ikiwa pamoja na kuongeza uzalishaji katika kilimo cha misitu, kuboresha mifumo ya kuhifadhi taarifa za misitu pamoja na kufanya biashara za misitu kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizopo. Hatua hizi zitasaidia kuongeza shughuli za kiuchumi za misitu ili kufikia lengo la kukua na kufikia **asilimia 5.9** tulijiwekea hapo awali. Hadi sasa shughuli za misitu zimekuwa kwa **asilimia 4.9** kwa mwaka 2019/20

**f) Maendeleo ya Rasilimali watu na utoaji wa Huduma za Jamii (Afya, Maji, Elimu na Mazingira)**

**Mheshimiwa Spika**, ubora wa Rasilimali watu na huduma ndio hazina muhimu katika kujenga maendeleo ya Taifa. Nchi yetu inamahitaji makubwa ya nguvu kazi yenye weledi, ujuzi na taaluma mbalimbali inayokidhi mahitaji ya soko na itakayokuwa chachu ya kuleta matokeo thabiti katika sekta husika. Kamati inapongeza Serikali kwa kuendelea kusimamia

utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya rasilimali watu na utoaji wa huduma kwa jamii na kufikia zaidi ya asilimia 80 ya Lengo la Mpango.

**Mhesimiwa Spika**, Kwa upande wa **Huduma za Afya**, Serikali imepiga hatua kubwa katika kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya nchini kwa kuwa na jumla na vituo vya huduma za afya **8,743**. Hadi kufikia Machi, 2020 kuna jumla ya vituo vya huduma za afya **8,446** ikiwa ni ufanisi wa **asilimia 96.6**. Aidha, Serikali imefanikiwa kujenga hospitali 3 za kanda ya Kusini - Mtwara, Magharibi - Tabora, Kanda ya Ziwa – Burigi. Vilevile, Serikali imeendelea kuongeza huduma ya Bima ya Afya na Kuboresha huduma za uchunguzi wa magonjwa ya mifupa (MOI), Moyo (JKCI), saratani (Ocean Road) pamoja na kuwezesha upatikanaji wa mashine za kisasa kupima ugonjwa wa kifua kikuu (TB) (GeneXpert) kutoka 65 mwaka 2015/16 hadi mashine 239 mwaka 2020 (Machi, 2020). Serikali imeongeza idadi ya Watoa huduma za afya pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Hatua hizi zimeweza kupunguza vifo vinavyosababishwa na magonjwa mbalimbali pamoja na kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano kutoka **67** kila vizazi **1,000** mwaka 2015/16 hadi vifo **11** katika kila vizazi **1,000** mwaka 2019/20; vifo vya malaria vimepungua kutoka watu **6,311** mwaka 2015 hadi **2,079** mwaka 2020.

**Mhesimiwa Spika**, pamoja na mafanikio haya, bado kuna changamoto za kukamilisha ujenzi wa maboma ya zahanati, vituo vya afya pamoja na usambazaji wa dawa na vifaa tiba katika maeneo mbalimbali nchini. Pia, kuna upungufu mkubwa wa watoa huduma wa afya katika kila kituo cha kutoa huduma za afya hapa nchini.

### **g) Sekta ya Maji**

**Mhesimiwa Spika**, kwa upande wa **Sekta ya Maji**, malengo ya Serikali ni kuhakikisha inaboresha huduma za maji vijijini kufikia **asilimia 95** ifikapo Mwaka 2025 (Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025) na Malengo ya katni kuboresha huduma ya maji vijijini kufikia **asilimia 85** mwaka 2020. Ili kufikia malengo

haya Serikali imefanikiwa kuanzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijiijini (**Rural Water Supply and Sanitation Agency – RUWASA**) ulioanza kutekeleza majukumu yake rasmi mwezi Julai, 2019.

Kupitia RUWASA inaendelea kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu ya maji, kujenga visima na kujenga mabwawa katika maeneo mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonyesha kuwa, tangu Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ianze kutekelezwa mwaka 2007 na hadi kufikia Desemba 2019, jumla ya miradi **2,450** imetekelizwa mijini na vijiijini. Kati ya hiyo, miradi **1,423** imetekelizwa katika mwaka 2015 na mwaka 2019, ambapo miradi **1,268** imetekelizwa vijiijini na miradi **155** imetekelizwa mijini. Takwimu zinaonyesha kuwa wastani wa idadi ya watu wanaopata huduma ya maji ya safi na salama vijiijini imeongezeka kutoka **asilimia 47** mwaka 2015 hadi kufikia **asilimia 70.1** mwezi Machi mwaka 2020. Kwa upande wa mijini, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji imeongezeka kutoka **asilimia 74** mwaka 2015 hadi kufikia **asilimia 84** mwaka 2020. Kamati ya Bajeti inaipongeza Serikali kwa hatua hii nzuri na inaendelea kusisitiza Serikali ihakikishe inakamilisha kutatua changamoto za upatikanaji wa maji katika maeneo mbalimbali yaliyojadiliwa na Bunge wakati wa kuitisha Bajeti ya Wizara ya Maji.

#### **h) Sekta ya Elimu**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **Sekta ya Elimu**; Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweza kutekeleza na kuboresha utolewaji wa elimu nchini hasa katika ujenzi wa miundombinu ya elimu kama vile vyumba vya madarasa, bmaabara, nyumba za walimu, ununuzi wa vitabu pamoja na kufanya ukarabati na ujenzi wa miundombinu katika shule za msingi, Sekondari na vuyo vya ualimu katika mikoa 26 ya Tanzania Bara. Pia Serikali imeweza kuongeza kwa idadi kubwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu; Jumla ya **Shilingi 1,354,791,502,797** zimelipwa kama mikopo kwa wanafunzi wenye uhitaji na vigezo, kati ya kiasi hicho, **Shilingi**

**454,951,614,829.00** kimetokana na marejesho ya mikopo ilioiva. Hatua hii imewezesha wanafunzi 484,297 wenyewe uhitaji na vigezo kunufaika na mikopo na wanafunzi 2,009 wamenufaika na ruzuku.

**i) Shughuli za Uzalishaji bidhaa viwandani na biashara.**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kupata mafanikio katika utekelezaji wa miradi ya viwanda na biashara kwa lengo la kufanikisha Dhima yake iliyojiwekea katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2017/17 – 2020/21 inayosema **Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu**. Serikali imeendelea kukamilisha Mradi wa Magadi Soda katika Bonde la Engaruka. Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Vanadium, Titanium na Chuma Liganga, Programu ya Maendeleo Unganishi ya Viwanda (Integrated Industrial Development Programmes), Mradi wa Uwezeshaji Biashara wa TMEA, Mradi wa Jumuiya ya SADC (SADC Trade Protocol) pamoja na Kutunisha mtaji wa Mfuko wa Wafanyabiashara na Wananchi (NEDF). Miradi hii pamoja na mingine imeweza kusaidia kuongeza shughuli za uzalishaji pamoja na ufanyaji biashara na hatimaye kuendelea kujitosheleza katika bidhaa muhimu kama vile saruji, marumaru, nondo, vifaa vya umeme, mabomba ya plastiki, unga wa ngano na mahindi, mchele na vyandarua. Hata hivyo, Pamoja na mafanikio ya kuanzishwa kwa viwanda vingi nchini, kuna umuhimu kwa Serikali uendelea kuweka msisitizo zaidi katika kuwezesha uanzishwaji wa viwanda vya kimkakati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia, inaitaka Serikali kukamirisha na kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Business Facilitation Act, 2020 pamoja na Sheria ya Kujilinda Dhidi ya Athari za Biashara (Trade Remedies Act, 2020) kwa lengo la kuzuia uingizaji wa bidhaa kwa wingi pamoja na kuzuia kuingiza bidhaa zisizo na ubora. Hatua hii ni muhimu sana kwani itasaidia kulinda viwanda vyetu vya ndani na kuvifanya viwe shindani zaidi. Aidha, Serikali iweke msisitizo wa kutumia zaidi bidhaa zinazosalishwa na viwanda vyetu nchini kabla ya kutumia bidhaa za nje. Pia taasisi zetu zenye viwanda kama

vile Jeshi la Wananchi, Polisi, Idara ya Uhamiaji na magereza ziwezeshwe ili kuleta ushindani katika uzalishaji wa bidhaa na biashara. Hatua hizi zitasaidia kufikia lengo la ukuaji wa asilimia 11 na zaidi kama liliivoanishwa katika Mpango wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kutilia mkazo sana masuala yafuatayo;

i. Kuanzisha viwanda vidogo, vyatiki na vikubwa vyakuchakata mazao

ya mifugo na mazao ya kilimo ili kuyaongezea thamani na kuyatafutia masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi yetu;

ii. Serikali ikamilishe haraka uanzishwaji wa masoko ya mipakani ukiwemo mpaka wa Tanzania na Msumbiji kwa upande wa Mkoa wa Ruvuma – Mkenda/Congress. (Mpaka huu umesahaulika);

iii. Serikali ianzishe Viwanda vyatiki Dawa na Vifaa Tiba kwa ajili ya matumizi yetu na kuza katika nchi cha SADC, Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla; na

iv. Serikali ikiwezeshe Kiwanda cha Biotech Production Limited kilichopo Kibaha ili kiendelee kuzalisha viluilui wa kuua vijidudu wa mbu wanaoeneza malaria na magonjwa mengine ili kutokomeza kabisa malaria nchini.

#### **j) Utekelezaji wa Miradi ya Kielelezo (Flagship Projects)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kundelea kutekeleza kikamilifu baadhi ya miradi ya Kielelezo kama vile Mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere; Mradi wa ujenzi wa reli ya katika kwa kiwango cha Standard Gauge; Mradi wa kuboresha Shirika la ndege la ATCL; Mradi wa Magadi Soda Engaluka wa ziwa Natron; Ujenzi wa mitambo ya kusindika Gesi ya kimiminika, Lindi (LNG) na Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari Mkulazi. Utekelezaji wa miradi hii na mingine itasaidia ukuaji wa uchumi pamoja na maendeleo ya watu.

**k) Ugharamiaji wa miradi ya vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo 2020/21**


**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2020/21 Serikali imepanga kutumia jumla ya **shilingi bilioni 12,699.4** ikiwa ni sawa ya ongezeko la **asilimia 1.2** kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati imefanya uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti ya maendeleo kwa miaka mitatu tangu mwaka 2016/17 hadi mwaka 2018/19 na kubaini kwamba Serikali hukusanya na kutumia katika **shilingi billioni 7,000** hadi **shilingi billioni 8,000** **katika miradi ya maendeleo**. Hivyo, kwa mwenendo wa takwimu hizi, ni wazi lengo la kutumia wastani wa **bilioni 11,800** kwenye Miradi ya Maendeleo kwa mwaka lililokuwa limewekwa kwenye mpango halijafikiwa. Kamati inaishauri Serikali kutafuta njia ya kutatua changamoto hii tunavyojiandaa kutekeleza awamu ya Tatu ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa (2021/22 – 2025/26) wenye dhima ya '**kuongeza mauzo ya nje na uwezo wa ushindani kikanda na kimataifa**'. Msisitizo uwekwe kwenye kutafuta vyanzo vya vipyta vya mapato kwa kuangalia maeneo mbalimbali ikiwa pamoja na kuangalia maeneo oevu ya mapato kama uvuvi wa bahari kuu na urasimishaji wa biashara.

**SURA YA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti ilipata fursa ya kuititia na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2019/20 pamoja na ulinganisho wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/21. Uchambuzi huu unatoa hali halisi ya mwelekeo wa Bajeti ya Serikali pamoja na utekelezaji wa malengo ya Bajeti yaliyowekwa kwa mwaka wa feda 2020/21. Pia, unatoa hali halisi ya utekelezaji wa sera za kodi kwenye maeneo husika hasa maeneo yanayohusu Mapato ya Ndani (Mapato ya Kodi na yasiyo na kodi), Mapato ya Halmashauri, Misaada na Mikopo ya kibashara ya ndani na kutoka nje na Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Aidha, kumekuwepo na ongezeko au punguzo katika baadhi ya maeneo ya mapato na matumizi kwa asilimia kadhaa kama ilivyooneshwa katika **Jedwali namba 1**.

**Mheshimiwa Spika**, Sura ya Bajeti kwa mwaka 2020/21 ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka 2019/20; inaonesha kuwa kutakuwepo na ongezeko la kiasi cha **shilingi bilioni 1,774,383.20** (**sawa na asilimia 5.36**) ya jumla ya bajeti yote. Pamoja na ongezeko hili bado kutakuwa na nakisi ya bajeti ya **asilimia 2.6** ya **Pato la Taifa** (**sawa na shilingi trilioni 3.7**) Aidha, Mapato ya ndani yataongezeka kwa **asilimia 4.36** (**sawa na ongezeko la kiasi cha shilingi bilioni 970.727**); mapato ya mamlaka za Serikali za Mitaa yataongezeka kwa **asilimia 6.4** (**sawa na ongezeko la kiasi cha shilingi bilioni 49.477**); Misaada na mikopo toka nje itaongezeka kwa **asilimia 3.2** (**sawa na ongezeko la kiasi cha shilingi bilioni 90.69**); mikopo ya ndani na nje yenye masharti ya kibashara itaongezeka kwa **asilimia 9.12** (**sawa na ongezeko la kiasi cha shilingi bilioni 663.481**). Aidha, Matumizi ya Kawaida yataongezeka kwa asilimia **5.39** (**sawa na ongezeko la kiasi cha shilingi trilioni 1.123**) na Matumizi ya Maendeleo yataongezeka kwa asilimia **5.31** (**sawa na ongezeko la kiasi cha shilingi bilioni 650.831**).

#### Kielelezo Na 6: Ulinganisho wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2019/20 na 2020/21(Bilioni).



**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

### a) Sera za Mapato

**Mheshimiwa Spika**, hotuba ya Bajeti kwa mwaka 2020/21, imeainisha hatua mbalimbali zitakazochukuliwa na Serikali katika kuboresha ukusanyaji wa mapato yatakayofikia jumla ya kiasi cha **shilingi trilioni 34.87**. Kwa upande wa mapato ya ndani Serikali inalenga kukusanya kiasi cha **shilingi trilioni 23.25**; kati ya fedha hizo, Mapato ya kodi (TRA) ni **shilingi trilioni 20.32.00** sawa na ongezeko la **asilimia 6.4**; Mapato yasiyo ya kodi **shilingi trilioni 2.92** sawa na punguzo la **asilimia 7.99** na Mapato ya Halmashauri **shilingi bilioni 814.96** sawa na ongezeko la **asilimia 6.4**.

**Mheshimiwa Spika**, ukirejea takwimu hizi utaona kuwa katika bajeti hii Serikali itategemea zaidi kupata mapato kutoka vyanzo vya ndani vya kodi. Hata hivyo bado tuna changamoto kubwa ya kuongeza Mapato Yasiyo ya Kodi ambayo yameendelea kushuka kwa **asilimia 7.99** punguzo ya **shilingi Bilioni 254.11** ukilinganisha na mwaka 2019/20. Kamati inaona kuwa Serikali itabidi ijizatiti kikamilifu ili kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ikiwa ni pamoja na kuboresha taratibu za kiutawala ili kuziba pengo litakalosababishwa na kushuka kwa mapato kutoka sekta ya utalii kutokana na **COVID-19**.


**Mheshimiwa Spika**, Serikali inategemea kupata kiasi cha **shilingi trilioni 2.87** kutoka kwenye misaada na mikopo ya kutoka nje. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la **asilimia 3.2** ukilinganisha na Bajeti ya Serikali mwaka wa fedha 2019/20 (**Bilioni 90.69**). Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa Misaada na Mikopo ya Miradi ya Maendeleo (**asilimia 6.4**) na Misaada na Mikopo ya Kiseka (**Asilimia 38.14**). Aidha, Misaada ya kibajeti (GBS) imepungua kwa **asilimia 49.30**. kwa upande wa mikopo ya masharti ya kibashara kutoka nje, Serikali imepanga kukopa kiasi cha **shilingi trilioni 3.03** sawa na ongezeko la **asilimia 31.05** ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2019/20.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na malengo haya mazuri ya Serikali, Kamati inaijuliza kuwa kwa kiwango gani Serikali

itaweza kufanikiwa katika kupata Misaada na Mikopo ya Kisekta (**shilingi bilioni 275.54**) na mikopo ya masharti ya kibashara (**shilingi trillioni 3.03**) ukizingatia kuwa, kutohana na janga hili la ugonjwa wa **CORONA** hali ya uchumi ya Nchi za wahisani zimetetereka na hivyo kuna uwezekano mkubwa wa nchi hizo kushindwa kutoa fedha kwa Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali kama ilivyotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imepanga kupata fedha za ndani kiasi cha **shilingi trillioni 10.16** sawa na ongezeko la **asilimia 4.3** na fedha za nje kiasi cha **shilingi trillioni 2.73** sawa na ongezeko la **asilimia 8.9** kwa ajili ya kutekeleza wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2020/21. Kamati inatambua nia njema ya Serikali ya kuweza kupata fedha za kutekeleza miradi ya Maendeleo. Hata hivyo, ni vigumu kwa Serikali kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani na yale ya nje kutokana na athari na ugonjwa wa **CORONA**.

#### Kielelezo Na 7: ulinganisho wa mapato ya serikali kwa mwaka 2019/20 na 2020/21 (Bilionti)




**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

**b) Sera za Matumizi.**

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2020/21 Serikali imepanga kutumia kiasi cha **shilingi triliioni 34.87** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kati ya fedha hizi kiasi cha **shilingi triliioni 21.98** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 63** ya bajeti yote na shilingi triliioni **12.89** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo sawa na **asilimia 37**. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa mapato ya ndani yanazidi matumizi ya kawaida kwa kiasi cha **shilingi triliioni 1.27** sawa na **asilimia 3.64** ya bajeti yote. Hii maana yake ni kwamba mapato yote ya ndani yanaweza kugharamia matumizi ya kawaida peke yake. Kutokana na hali hii ni vema Serikali ikasimamia vizuri mapato ili kuhakikisha malengo ya matumizi ya kawaida yanafikiwa.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imetenga kiasi cha **shilingi triliioni 12.89** kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo sawa na asilimia 37 ya bajeti. Kati ya fedha hizo kiasi cha **shilingi triliioni 10.16** ni fedha za ndani ongezeko la **asilimia 4.37** ukilinganisha na Bajeti ya Mwaka 2019/20 na **shilingi triliioni 2.73** ni fedha za nje ongezeko la **asilimia 8.97** ukilinganisha na Bajeti ya mwaka 2019/20. Kwa ujumla ikillinganishwa na Mwaka wa fedha 2019/20, fedha za maendeleo kwa mwaka ujao wa fedha zimeongezeka kwa takribani **shilingi bilioni 650** sawa na ongezeko la **asilimia 5**. Kutokana na changamoto zinazoweza kujitokeza kutokana na uchumi wa Dunia kuyumba, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa, Serikali izingatia hali halisi ya sasa pamoja na upatikanaji wa uhakika wa fedha za ndani na zile za nje katika kuchagua miradi ipi ianze nayo katika utekelezaji wake kwa mwaka huu wa fedha 2020/21.

## Kielelezo na 8: Ulinganisho wa Matumizi ya Bajeti ya serikali kwa mwaka 2019/2020 na 2020/21(Bilioni).



**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango.

### MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI YA BUNGUE YA BAJETI KUHUSU BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2020/21

#### Hatua za Kodi zinazopendekezwa na Serikali

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti imefanya uchambuzi wa mabadiliko ya Sheria mbalimbali yenyе Marekebishо haya yamezingatia dhamira ya Serikali ya kuendelea kuwa na mfumo wa kodi ambao ni tulivu na wa kutabirika. Aidha, marekebishо yanalenga kuchochеa kasi ya ukuaji wa uchumi hususan katika sekta ya kilimo na viwanda, kuongeza kipato kwa waajiriwa na kuongeza mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na Serikali kwa uamuzi wake wa Busara wa kuto kufanya mabadiliko ya Viwango katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, uamuzi huu unaondoa dhana potofu iliyokuwa imejenjeka kwamba Serikali inaijiendesha kwa kodi za sigara, bia na soda tu.

Kamati baada ya kupitia mabadiliko ya Sheria yaliyopendekezwa ina maoni yafuatayo juu ya Sheria mbalimbali:-

### **Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kufanya mabadiliko katika eneo hili kwa sababu itasaidia mazao yetu ya Kilimo kuwa na bei shindani katika masoko ya nje. Aidha hatua hii itawezesha wawekezaji katika Sekta ya Kilimo na madini kuongeza mitaji na kupanua uwekezaji. Kamati inaendelea Kuishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuondoaa kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifungashio vya mazao ya maua na mboga mboga ili vifungashio hivyo vipatikane kwa bei nafuu na kwa wingi. Vilevile kamati inashauri Serikali kufanya marejesho ya Kodi hiyo kwa sababu kwa kufanya marejesho hayo yatasaidla makampuni husika kuongeza mitaji na uendeshaji na kuongeza tija kwenye uendeshaji.

### **Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana Serikali kwa uamuzi wake wa Kufanya marejeo ya Jedwali la kwanza la Kodi ya Mapato kwa sababu kwanza jedwali hilo limekuwa la muda mrefu bila kufanyiwa marekebisho na upangaji wa makundi (Tax Bands) haukuzingatia hali ya sasa. Kitendo cha kuongeza kiwango cha mapato ambacho hakitozwi kodi kutoka **Shilingi 170,000/=** ya sasa hadi **shilingi 270,000/=** inaonyesha kwa namna gani Serikali hii inawajali wanyonge hasa wale wa kipato kidogo wanaofanya kazi viwandani na mashambani. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kufanya mabadiliko zaidi katika Tax Band ili ziendane na wakati na vipato kadri hali itakavyokuwa inaruhusu.

### **Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 438**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kumruhusu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kutatua mapingamizi yanayoletwa kwake. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha mamlaka hayo

yanatumika kwa nia iliyokusudiwa na kwa kuzisaidia biashara ziendelee kuzalisha mapato mengi zadi.

**Sheria ya Fedha za Mamalaka za Serikali za Mitaa, SURA 290;**

**Mheshimiwa Spika**, mabadiliko yaliyopendekezwa imekuwa ni kilio cha Muda mrefu cha wadau katika Sekta ya Mawasiliano ambao walikuwa wanalaazimika kufanya malipo ya tozo za Huduma (Service Levy) kwa halmashauri 186 ambazo ama wana minara au wana maduka ya kutolea huduma. Pamoja na pendekezo hili jema la mapato haya kuwasilishwa katika Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa niaba ya Hamashaurijambo la kuzingatia ni kuwa fedha hizi zirudishwe kwa usahihi na kwa wakati katika halmashauri.

**Mheshimiwa Spika**, aidha Kamati inashauri masuala yafuatayo yazingatiwe wakati utekelezaji wa suala hili. **Kwanza**, kupata idadi kamili ya minara iliyopo nchini; **Pili** uwezo wa kutambua mawasiliano yanayofanywa na kila mnara katika kila halmashauri na **mwisho** kuhakikisha kuwa mtawanyo wa mapato unafanywa bila kujali eneo minara hiyo ilipo au ofisi zake zilipo. Vilevile, utungaji wa Kanuni hizi zishirikishe wadau wote ikiwemo Serikali za Mitaa, TCRA na Wadau wa Mawasiliano nchini.

**Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 na Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370.**

**Mheshimiwa spika**, Sheria hizi mbili zina lengo la kupanua mawanda ya ukusanyaji wa asilimia 15 ya mapato kutoka Taasisi za TIC, TFRA, NIDA na GPSA pamoja na kumruhusu msajili wa hazina kukusanya asilimia 70 ya fedha za ziada kwa makampuni ambayo yanapata fedha za matumizi kutoka Bajeti ya Serikali. Kamati inaishauri Serikali hatua hizi zisiwe na lengo la kuongeza mapato Serikali tu bali na kuhakikisha kwamba Taasisi hizi zinaendeleza shughuli zake kama awali

**Sheria ya Usajili wa Magari, Suraya 124; Sheria ya Ardhi, Na.4 ya Mwaka 1999 na Sheria ya Madini 123.**

**Mheshimiwa Spika**, Mabadiliko yanayopendekezwa katika Sheria hizi yana lengo la kuanzisha vyanzo vipyta ya mapato na kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato. Kamati inakubaliana na mapendekezo haya na inaunga Serikali mkono.

**Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imepitia na kuchambua hatua zote ambazo zimechukuliwa na kubaini kwamba hatua hizo zina malengo yafuatayo. Kulinda viwanda vya ndani ya jumuiya, kupunguza gharama za vifungashio na malighafi zinazotumika katika viwanda vya jumuiya, kuwezesha sekta ya kilimo na mifugo na kuendeleza usindikaji wa mazao.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti imekuwa ikipendekeza mara kwa mara kwa Serikali kwamba hatua hizi za Mabadiliko Sheria ya Forodha ya Mwaka 2004 yawe yanawasilishwa kwa Kamati ya Bajeti kwa Niaba ya Bunge ili kuishauri Serikali kabla hayajapitishwa na Mawaziri wa Fedha, Uwekezaji, Biashara na Uchumi wa Jumuiya. Ileweke wazi kwamba utaratibu wa kurejesha mabadiliko hayo katika jumuiya endapo Bunge lako tukufu halikubaliani na mapendekezo yaliyopitishwa ni mrefu na hautaleta taswira nzuri kwa Taifa letu. Kamati inaiomba Serikali ilifikirie swala hili kwa undani ili Bunge ijalo lisikutane na Changamoto hii.

**Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira Kufanya Biashara (Blue Print)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inampongeza **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Josef Magufuli Rais** wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wa kusimamia kufuta na kupunguza tozo, ushuru na ada mbalimbali. Uamuzi huu ulisubiriwa na Sekta Binafsi kwa muda mrefu na kwa hatua hii sekta binafsi itatumia fursa hii kukuza na kuendeleza bisahara. Kamati

inatoa angalizo kwamba Serikali iangalie utaratibu wa kuanzisha ada, ushuru na tozo mbalimbali kupitia kanuni hauwi kikwazo kwa maendeleo ya Sekta Binafsi.

### **MAONI NA USHAURI WA JUMLA.**

**Mwelekeo wa utekelezaji wa Bajeti katika kipindi cha janga la COVID-19 .**

**Mheshimiwa Spika**, Janga la **COVID -19** limetokea katika kipindi cha Robo ya Tatu ya utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/20 Kwa ujumla bajeti za Wizara, Taasisi na Idara za Serikali zilikuwa hazijajikita kukabiliana na Janga hili. Aidha Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudu kubwa ya kusimamia na kuimarisha huduma ya afya na usalama wa watu pamoja na kutoa maelekezo mbalimbali ya kujikinga na ugonjwa huu.

**Mheshimiwa Spika**, Janga la COVID -19 lina athari kubwa katika utekelezaji wa Bajeti hii tunayoimalizia sasa na pia kwa Bajeti inayokuja ya Mwaka 2020/21 kwa kuzingatia kuwa wakati Bunge likipitisha Mpango na Ukomo wa Bajeti mwezi Desemba 2019, Ugonjwa huu haukuwepo. Hivyo baada ya **COVID-19** kuna haja ya kufanya tathmini na mapitio ya mafungu ya bajeti tuliyoyapitisha (**Internal Reallocation**) ili kuakisi uhalisia huu mpya kwa kuzingatia uimarishaji wa huduma ya afya, usalama wa watu na maendeleo ya uchumi. Hatua hii itasaidia kuwa na uhalisia wa Bajeti itakayotatua matatizo ya wananchi kama yalivyopangwa.

### **Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu**

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti tunayoipitisha sasa imehusisha pia fedha kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu 2020 wa Rais, Wabunge pamoja na Madiwani. Kamati ya Bajeti inapenda kulijulisha Bunge lako kuwa, Serikali imejiandaa ipasavyo katika kutekeleza suala hili. Hivyo, ni muhimu vyombo vyote vinavyohusikia na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 vijiandae ipasavyo ili kuhakikisha kuwa uchaguzi mkuu 2020 unaimarisha misingi ya kidemokrasia ambayo nchi imejiwekea.

## **Mabadiliko katika mifumo ya TEHAMA katika Ununuzi wa Umma**

**Mheshimiwa Spika**, katika Bajeti ya Serikali kati ya shilingi **trilioni 12 hadi 16** zinategemewa kutumika katika manunuzi ya Serikali. Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kuanzisha mfumo wa ununuzi kwa njia ya mtandao ujulikanao kama **TANePS** ambao kimsingi unajumuisha kwa pamoja mifumo ya awali ya "Portal" ya zabuni, **PMIS** na **Tender Alert services**. Uanzishwaji wa Mfumo huu umeweza kukidhi matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura Namba 410, pamoja na Kanuni za Ununuzi chini ya Tangazo la Serikali Namba 446.

**Mheshimiwa Spika**, Mfumo wa **TANePS** utasaidia katika kupunguza gharama mbalimbali zikiwemo zile za kudurufu na kusambaza nyaraka, usafiri na shughuli nyingine za ununuzi. Aidha, Mfumo huu utsungeza ushindani, uwazi, haki pamoja na kupunguza rushwa katika michakato ya zabuni kwa kuwa mawasiliano ya moja kwa moja kati ya wazabuni na maafisa manunuzi yatakuwa hayapo au kupungua sana. Aidha, kwa kuwa mfumo huu ni mpya, Kamati inashauri Serikali iendelee kutoa elimu ya mfumo huu kwa maafisa ugavi na wazabuni.

## **Ushiriki wa Sekta Binafsi katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2020/21.**

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Mpango wa Pili wa Taifa wa miaka mitano; jumla ya **Shilingi trilioni 107** zilitakiwa kugaramia mpango huo. Mpango huo ulitegemea Serikali kutoa jumla ya shilingi **Trilioni 59** na Sekta Binafsi **Shilingi trilioni 48**. Kamati imebaini kwamba kuna changamoto kubwa katika upatikanaji wa takwimu za uchangiaji wa fedha za miradi ya maendeleo kutoka kwa Sekta Binafsi kwa sababu mbalimbali. Kamati inaishauri Serikali kutumia utaratibu wa wawekezaji wenyewe kutoa taarifa zao kwa hiari (Self declaration) za uchangiaji wa miradi ya maendeleo ili kupata takwimu za uwekezaji uliofanywa na Sekta Binafsi kwenye Miradi ya Maendeleo. Baada ya takwimu hizo kupokelewa zinaweza kutumika na Serikali kwa kuziangalia uhalisia wake.

**Ukarabati wa Miundombinu ya Barabara Vijijini (TARURA)**

**Mheshimiwa Spika**, mabadiliko ya hali ya hewa yamesababisha kuwepo na mvua kubwa iliyosababisha mafuriko na uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara hasa kwa upande wa maeneo ya vijijini. Kamati ya Bajeti ilikutana na TARURA na kubaini kwamba kiwango cha fedha kilichokuwa kinahitajika kurejesha miundombinu ya barabara ni **Shilingi bilioni 132.6**. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/21 fedha zote zinazohitajika katika kurejesha miundombinu ya Barabara ilio chini ya TARURA zinatolewa ili kukarabati miundombinu hiyo.

**Mazao ya misitu yatokanayo na usafishaji wa eneo la Bonde la Mto Rufiji kwa ajili ya Bwawa la Uzalishaji wa Umeme la Mwl. Nyerere.**

**Mheshimiwa Spika**, moja ya jambo ambalo Kamati ya Bajeti imelifanya kazi kwa muda bila kupata majibu stahiki ni swala la mazao ya misitu yanayotokana na shughuli ya kusafisha eneo la Pori tengefu la Selou litakalotumika kwa ajili ya kujenga Bwawa na kuhifadhi maji ya Mradi wa kufua umeme wa Mwalimu nyerere katika bonde la mto Rufiji. Serikali kupitia Wakala wa Misitu (TFS) ilitoa kandarasi kwa makampuni ya watanzania yapatayo 30 kwa ajili ya kufanya shughuli hiyo. Kulingana na Tathmini ya TFS ilionekana kwamba **asilimia 80** ya msitu ulifaa kwa magogo na mbao na **asilimia 20** ingefaa kwa matumizi mengine. Wakandarasi walipoenda kuanza kufanya kazi ilibainia ni **asilimia 35** tu ya msitu unafaa kwa ajili ya magogo na mbao na **asilimia 65** kwa matumizi mengine. Baada ya kugundua hali hiyo wadau walitafuta soko la mkaa nje ya nchi ambao ungetokana na **asilimia 65** ya miti ambayo haifai kwa magogo wala mbao. Waliomba kibali cha kuuza mkaa nje ya nchi ambapo walipata barua ya kuruhusu kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na barua ya kutokuwa na pingamizi kutoka TFS.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupata vibali hivyo na kufikisha makasha yenye mkaa bandarini ndipo ilipogundulika kwamba kulikuwa na Tangazo la Serikali namba 664 la mwaka 1986 la kupiga marufuku uuza ji wa mkaa nje ya nchi. Hivi sasa mikataba ya wadau hao imekwisha muda wake ilihali wengi

waliopewa walishindwa kutekeleza shughuli zao kutokana na wingi wa mvua za Mwaka huu. Hivyo suala la kusafisha linafanya na jeshi la JWTZ. Kamati inaishauri Serikali kufanya mambo yafuatayo kwa kuwa biashara ya mkaa inatarajiwa kuingiza jumla ya **shilingi triliuni 2.7** ikiwa ni mapato kwa wavunaji, kodi, tozo, ushuru na ada mbalimbali: -

- i. Serikali kuangalia uwezekano wa kufanya mabadiliko GN namba 664 Export Prohibition na ya mwaka 1986 ili itoe ahueni ya kuza mkaa nje unaotokana na miti iliyovunwa pori la Selou kwenye mradi wa Bwawa la Mwalimu nyerere kwa kipindi maalumu;
- ii. Kwa kuwa hivi sasa Jeshi la Wananchi Tanzania JWTZ ndilo linafanya kazi ya kusafisha eneo na kwa kuwa JWTZ wana kampuni ya Mzinga na SUMA JKT waangalie uwezekano wa kufanya biashara hilo kuliko kuchoma na kuharibu miti hilo na kuendelea kutumia fedha za Serikali kulisafisha bila manufaa yoyote; na
- iii. Kuangalia uwezekano wa kuihusisha Sekta Binafsi ili watumie mitaji yao katika kufanya kazi yao na Serikali ipate pato lake stahiki.

### **Matumizi ya Mfumo wa Stempu za Kodi za Kielektronic ETS.**

**Mhesimiwa Spika**, moja ya tatizo kubwa ambalo linaikabili nchi yetu ni uwepo wa bidhaa ambazo ama si halisi na zisizo na ubora au zilizoingizwa nchini kwa njia zisizo rasmi kwa magendo. Bidhaa hizi mara nyingine zinakuwa na madhara makubwa sana kwa wazalishaji wa ndani, afya za Wananchi na Wakulima. Mfano sukari ya magendo, mafuta ya kula, pembejeo, madawa ya Binadamu na mifugo pamoja na vipodozi. Hivi sasa Mamlaka ya Mapato inatumia mfumo wa Stempu wa Kodi za Kieletroniki ili kujua bidhaa halisi na bidhaa zisizo halisi katika soko pamoja na kuangalia uzalishaji wake ili kodi stahiki ikusanywe. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kutumia mfumo huo katika utambuzi wa Bidhaa za ndani kama vile sukari, mafuta ya kula na kujipaka, vipodozi, madawa ya mifugo na pembejeo za ndani na je ili

kwanza kulinda viwanda vya ndani na pili kuwalinda watazania dhidi ya matumizi ya bidhaa zisizo na ubora. Aidha, Mamlaka ya Mapato Tanzania inatakiwa kuhakikisha inaKuwa na mpango wa kurithi mfumo huo na kuuendesha mara baada ya mkandarasi aliepo kumaliza kazi yake.

### **Ahueni ya ulipaji wa Kodi iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.**

**Mheshimiwa Spika**, hivi karibuni Mamlaka ya Mapato Tanzania imetoa **GN Na.351** ambayo imetolewa kwa mujibu wa Kifungu cha 70(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 432. Tangazo hilo lina nia ya kutoa ahueni ya ulipaji wa kodi (Remission) kama mkakati mmojawapo wa kukabiliana na m dororo wa uchumi unaotokana na janga la **COVID-19**. Kamati ya Bajeti ilipata fursa ya kupitia Tangazo hilo na kubaini mambo mbalimbali ambayo kimsingi yana nia njema ya kuisaidia sekta Binafsi katika wakati huu mgumu. Hata hivyo, kamati hajavutiwa na masharti yaliyowekwa. Kanuni ya 5 inatoa masharti ya mnufaika, sharti ambalo linatoa mashaka ni sharti la 5(d) ambalo linamtaka mlipa kodi kulipa kodi yote itakayoahirishwa katika tarehe ambayo Kamishna Mkuu wa TRA ameibanisha katika uamuzi wake.

Nanukuu “**(d) agreed to pay the whole of his principal tax liability on the due date to be prescribed by the Commissioner General in his**”. Kamati inaishauri Serikali kulifikria upya sharti hili kwa sababu itakuwa vigumu kwa biashara inayotoka katika msukosuko kulipa kodi yote iliyohairishwa kwa mkupuo. Ni vyema utaratibu ukabainishwa mathalani ulipaji wa awamu walau tatu baada ya tarehe ilioamriwa na Kamishna Mkuu kuwadia.

### **Vitambulisho vya Wajasiliamali Wadogo**

**Mheshimiwa Spika**, suala la Vitambulisho vya Wajasiliamali lilikuwa na mkanganyiko mkubwa wakati wa utekelezaji wake. Mhe. Rais John Pombe Joseph Magufuli alikuwa na nia njema sana ya kusajili wafanyabiashara wote nchini ili watambulike na wachangie kwenye Pato la Taifa. Hata

hivyo, utolewaji wake kwa baadhi ya maeneo haukuwa na msingi na dhamira ile ya Mhe. Rais. Tunashukuru sasa Serikali imeandaa kanuni chini ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi ambayo inaweka msingi wa nani anahusika na majukumu kati ya Mamlaka ya Mapato na Serikali, muda ambao kitambulisho kitakuwa halali na kiwango kinachotakiwa kulipwa kwa ajili ya kupata kitambulisho hicho.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imepitia utaratibu huo na inashauri mambo yafuatayo: -

- i. Kitambulisho kuwa na picha ya mfanyabiashara na mahali anapofanya bishara ili kupusha kitambulisho kimoja kutumika na watu tofauti;
- ii. Kubainisha muda wa miezi 12 uliobanishwa kwenye kanuni haujataja wazi kama ni Mwaka wa fedha wa Serikali au mwaka wa Kalenda; na
- iii. Serikali za Mitaa hajjjajipanga vizuri katika kuanisha maeneo ya wafanyabishara wadogo kama kanuni inavyowataka;

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini endapo masuala hayo yatafanyiwa kazi basi yataongeza ufanisi katika kuwatambua wajasiliamali wadogo pamoja na kupata takwimu sahihi za ukusanyaji wa mapato kutoka kwa wafanyabiashara wadogo.

### **Utunzaji wa Mazingira**

**Mheshimiwa Spika**, utunzaji wa mazingira pamoja na kudhibiti na kujenga uwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia-nchi ni masuala ya msingi katika kuhakikisha ukuaji endelevu wa uchumi. Katika kutambua hili, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) zimeweza kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira pamoja na kuratibu na kusimamia programu mbalimbali za mazingira kama vile Mradi wa Kuhimili Athari ya Mabadiliko ya Tabia nchi Kupitia Mifumo ya Ikolojia, kufanya kaguzi za uharibufi wa mazingira katika maeneo ya

uwekezaji, upandaji wa miti na kuzuia uharibifu wa misitu (Deforestation) na vyanzo vya maji. Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali ikamilishe Mradi wa Kuwezesha Mfuko wa Mazingira kwa kuainisha na kupendekeza vyanzo vya mapato kwa ajili ya uendeshaji wa Mfuko na hivyo kutimiza malengo yake.

### **Njia za Kuchochche Ukuaji wa Uchumi (Stimulus Package)**

**Mheshimiwa Spika**, Hotuba ya Hali ya Uchumi imeaninsha shughuli za kiuchumi ambazo zimechangia kwa kiasi kikubwa kwenye ukuaji wa Pato la Taifa. Shughuli hizo ni uchimbaji wa madini, ujenzi, sanaa, burudani, usafirishaji na uhifadhi mizigo. Aidha, shughuli hizi zote isipokuwa sanaa na burudani zimetokana na uwekezaji mkubwa Serikali katika sekta husika. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwa na mipango na mikakati itakayosaidia shughuli nyingine za kiuchumi zinazoendeshwa na sekta binafisi mfano sekta ya huduma, kilimo, mifugo ili na zenyewe zikue kwa kasi na kuweza kusaidia kukua kwa uchumia wa Taifa.

### **Athari za Covid-19 kwenye Sekta ya Elimu**

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ina shule binafsi zaidi ya 2750, shule hizo zizmeajiri walimu takribani 90,000. Mtikisiko wa Covid-19 umedhihirisha umuhimu wa Serikali kuchukua hatua mahsusii kunusuru shule hizo kwa kuahirisha malipo ya kodi na kuhimiza benki kutoa mikopo ya bei nafuu kwa shule hizo ili kuzijengea uwezo kulipa mishahara ya walimu wao. Aidha, Sheria ya Elimu inayozonyima shule hizo uwezekano wa kuweka akiba ya kutumia kulipa mishahara wakati wa dharura iangaliwe upya.

### **Uvubi wa Bahari Kuu**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua yake ya kuondoa tozo ya dola 0.4 kwa kilo moja ya samaki aina ya jodari anaevuliwa katika bahari kuu. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuharakisha mchakato wa ujenzi wa Bandari ili Serikali iweze kupata mapato ya leseni peke yake. Bandari ya uvui itawezesha uwepo wa viwanda vya kuchakata minofu ya samaki nchini, ajira kwa

Watanzania, kodi na tozo kutoka mamlaka mbalimbali, udhibiti wa uvuvi haramau na ushushaji wa samaki wasiolengwa (by catch) kwa matumizi ya soko la ndani

### **Gharama za ETS kwenye Sigara**

**Mhesimiwa Spika**, pamoja na hatua nzuri ya Serikali kuanzisha Mfumo wa Kodi za Kielektroniki ambao umeonyesha matokea mazuri hasa katika kuhakikisha kuwa Serikali inapata kodi stahiki. Mfumo huu umekuwa sio rafiki kwa sekta ya sigara katika gharama za stempu za bidhaa husika. Sigara zinatozwu kiasi cha **Dola 20 kwa stempu 1000**, gharama ambazo zipo juu ukilinganisha na viwango vinavyotozwa kwa bidhaa kama vile bia usd 8. Kwa stempu 1000. Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kubadilisha kiwango hiki kilingane na kiwango kinachotozwa kwenye bidhaa nyingine.

**Suala la Mapato ya TAWA, TANAPA na NCCA kukusanya na Mamlaka ya Mapato Tanzania na kupelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali.**

**Mhesimiwa Spika**, Serikali imekusudia kuanzisha utaratibu mpya wa kukusanya mapato yote yanayotokana na Shughuli za Utalii, Wanayapor na uhifadhi yaliyokuwa yakikusanya awali na TANAPA, NCCA na TAWA. Hatua hii imekuja kipindi ambacho Mamlaka hizi zimeathiriwa kwa kiwango kikubwa na gonywa la COVID hivyo mapato yake kushuka kwa kasi na kuna wasi wasi zingeweza kushindwa kujidesha. Serikali hajjaweza kufafanua nia hasa ya uamuzi huu kwasababu Mamlaka hizi zimekuwa na ufanisi mkubwa katika ukusanyaji wa mapato yake na utekelezaji wa majukumu yake na Serikali imekuwa ikikusanya kodi, mchango wa asilimia 15 na michango mingine mbalimbali. Kamati ingependa kujua lengo hasa la Serikali katika uamuzi huu ni lipi ukizingatia kuna mashirika mengi ya Serikali ambayo yanatoa huduma na mapato yake hayakusanyi na TRA.

**Mhesimiwa Spika**, ili utaratibu unaopendekezwa uweze kutekelezeza tulitakiwa kwanza kupitisha Bajeti ya TANAPA,

TAWA, NCCA kwenye Bajeti ya Wizara ya Maliasiri na Utalii ili fedha hizo zinapokuwa zinatoka mfuko mkuu wa Serikali ziweze kupitia. Aidha, miradi ya maendeleo ambayo ilikuwa itekelezwe na TANAPA, TAWA na NCCA fedha zake zimetengwa kupitia kifungu kipi. Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya uamuzi wake na kuhakikisha kwanza katika kipindi hiki kigumu Mamlaka hizi zinatekeleza majukumu yake kikamilifu na uamuzi wa kuyachukua mapato au la ufanyike pindi hali ya sekta ya utalii itakapo tengemaa.

### **Ufanyaji wa Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango na Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali iko katika mchakato wa kutafuta mshauri mwelekezi kwa ajili ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Pili (FYDP II) kwa kipindi cha miaka 4 wa utekelezaji pamoja na tathmini ya miradi ya maendeleo. Kimsingi, tathmini ya Mpango huu ulipaswa kuweka misingi ya uandaji wa Mpango unaofuata. Kamati ilibaini kwamba tathmini hiyo itakapo kamilika haitwakuwa na mantiki yoyote kwa sababu Mpango wa Tatwa Maendeleo wa Taifa utakuwa umeanza kutekelezwa. Hivyo, Kamati inashauri tathmini hiyo iwe inafanyika walau katika nusu ya muda wa utekelezaji wa Mpango husika.

**Mheshimiwa Spika**, Hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango imeonyesha kuwa zoezi la tathmini ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Serikali za Mitaa limekasimiwa TAMISEMI. Aidha, Kamati inaona changamoto ya utekelezaji wa suala hili hasa ikizingatiwa kuwa kuna Miradi inayotekelawa katika Serikali za Mitaa lakini inasimamiwa moja kwa moja na Wizara za Kisekta. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kwamba Wizara ya Fedha na Mipango ikishirikiana na TAMISEMI kuwa Wizara zinazoratibu ufuatiliaji na tathmini na kuachia zoezi hilo kufanywa na Wizara, Idara, Wakala na Taasisi mbalimbali za Serikalii ili waweze kutekeleza zoezi hilo kwa ufanisi.

**Maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa:** -

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na maoni na ushauri huu uliojikita katika maeneo mahsus, Kamati ingependa kutoa maoni ya jumla kuhusu Mpango wa Maendeleo kama ifuatavyo: -

- i. Serikali iainishe Mkakati wa kutafuta masoko ya mazao nje ya nchi kwa kuingia mikataba na wanunuzi au nchi ili ziweze kununua mazao yetu. Aidha moja ya jukumu la balozi zetu ziongeze kasi katika utafutaji wa masoko ya mazao hayo;
- ii. Mpango uonyeshe dhana, malengo na nia ya Diplomasia ya Uchumi na majukumu ya kila mdau katika kuhakikisha Tanzania inanufaika nayo;
- iii. Serikali iainishe katika Mapendekezo ya Mradi Program zitakazowezesha Digital Economy kuleta manufaa zaidi nchini;
- iv. Serikali iongeze katika Mapendekezo Mradi wa uanzishwaji wa Mnada/Masoko ya Chai na Kahawa nchini ili kuacha kutumia mnada unaofanyika nje ya nchi yetu;
- v. Serikali iongeze katika Mapendekezo ya Mpango Mradi wa kuboresha zao la Zabibu na mnyororo wa thamani (Value Chain) yake;
- vi. Serikali ihakikishe kuwa utaratibu wa uuzaaji mazao ya kimkakati nje ya nchi kupitia Soko la Bidhaa la TMX hauathiri uuzaaji wa mazao nje ya nchi moja kwa moja (niche market);
- vii. Serikali iweke mazingira bora yatakayowezesha wananchi kuchangia katika kutekeleza baadhi ya miradi katika maeneo yao kwa mfano ujenzi wa madaraja, shule, vituo vya huduma za afya.

## **8.0. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe kwanza kwa kunipa fursa na kuniами kuwa Makamu

mwenyekiti wa Kamati wa Bajeti kwa miaka miwili sasa. Aidha, napenda kumshukuru, Mhe. Dkt. Philip Mpango, Mb, Waziri wa Fedha na Mipango na Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji, Mb, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nawashukuru Katibu Mkuu na wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango amba walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili Mapendelekezo ya Mpango huu.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendelekezo mbalimbali. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo;

1. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb Makamu Mwenyekiti
2. Mhe. David Ernest Silinde, Mb Mjumbe
3. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb Mjumbe
4. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb Mjumbe
5. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb Mjumbe
6. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb Mjumbe
7. Mhe. Ali Hassan Omar, Mb Mjumbe
8. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb Mjumbe
9. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb Mjumbe
10. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb Mjumbe
11. Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb Mjumbe
12. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb Mjumbe
13. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb Mjumbe
14. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb Mjumbe
15. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb Mjumbe
16. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mb Mjumbe
17. Mhe. Abdallah M. Bulembo, Mb Mjumbe
18. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb Mjumbe
19. Mhe. Stephen Julius Masele, Mb Mjumbe
20. Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb Mjumbe
21. Mhe. Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mb Mjumbe
22. Mhe. Andrew John Chenge, Mb Mjumbe
23. Mhe. Suleiman A. Sadiq, Mb Mjumbe
24. Mhe. Shally J. Raymond, Mb Mjumbe
25. Mhe. Joseph Kakunda, Mb Mjumbe
26. Mhe. Jummane Kibera Kishimba, Mb Mjumbe

27. Mhe. Dkt. Raphael Chegeni, Mb Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, ninapenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, natambua mchango mkubwa wa Sekretariati ya Kamati kwa kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha, na naunga mkono hoja.

Mashimba M. Ndaki, Mb  
**M/MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**

12 Juni, 2020

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Mashimba Ndaki na wenzako wote katika Kamati ya Bajeti. Kwa kweli mmefanya kazi kubwa kwa masaa mengi, mmetuwakilisha vyema kama Bunge, niwapongeze sana na kuwashukuru saa kwa kazi nzuri ambayo mmefanya. (*Makofii*)

Lakini pia Waziri wa Fedha na wasaidizi wake wote kwa jinsi ambavyo wametoa ushirikiano wa hali ya juu kwenye Kamati ya Bajeti, na hii imeturahisishia sana kazi zetu kama Bunge, tunawashukuru mno, ahsante sana. (*Makofii*)

Sasa nimkaribishe Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani na nimruhusu kutumia chombo hapa mbele, karibu sana. (*Makofii*)

**MHE. HALIMA J. MDEE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa, Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa, Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021, naomba kutumia fursa hii kumpa pole Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe (Mbunge) kwa tukio la shambulio dhidi yake ambao lilimjeruhi na kupelekea kuvunjika mguu wake wa kulia. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalaani kitendo hicho na inaitaka Serikali kuititia vyombo vyake vya dola kufanya uchunguzi wa haraka na kuwachukulia hatua wale wote watakaobainika kuhusika na uhalifu huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninapohitimisha kipindi changu cha tatu cha miaka mitano mfululizo cha kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ninapohitimisha kipindi cha miaka mitano cha kuwa Msemajii Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Fedha na Mipango, nina kila sababu ya kumshukuru Mungu kwa kila jambo nililotenda au nililotendewa katika kuitumikia nafasi yangu. Nitumie nafasi hii kwa heshima kubwa sana kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kawe wa vyama vyote na wasio na vyama walionipa heshima mtoto wa mwalimu kuwawakilisha hapa Bungeni kwa miaka kumi mfululizo, ninawapenda sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uhai wa Bunge hili la Kumi na Moja unaelekea ukingoni na kwa maana hiyo kuifanya hotuba hii kuwa hotuba yangu ya mwisho na huko nyuma tulishaari mambo mengi sana, leo nitajielekeza zaidi kwenye kutoa tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano sambamba na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kuutekeleza mpango huo kwa kipindi cha miaka mitano. Aidha, nitazungumzia kwa kifupi sana majanga yanayolikabili Taifa kwa sasa, na namna majanga hayo yaliivoathiri uchumi kwa ujumla na hususani makisio na upangaji wa bajeti ya mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo; katika kufanya tathmini

hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itaonesha hali ilivyokuwa mwaka 2015 wakati Mpango unaandaliwa, malengo yaliyokusudiwa kufikiwa hadi mwaka 2021 na hali halisi iliyofikiwa kwa utekelezaji hadi mwaka 2020. Tathmini hii itahusu maeneo yanayohusu ustawi wa wananchi wanyonge ambao kimsingi yanabeba uwakilishi mkubwa wa mpango mzima.

Mheshimiwa Spika, wastani wa ukuaji uchumi; wakati Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano unamaliza muda wake mwaka 2015, wastani wa ukuaji wa uchumi ulikuwa ni asilimia saba. Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao ndio huu tulionao sasa hivi ukaweka malengo ya ukuaji uchumi kwa wastani wa asilimia 10. Mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wastani wa ukuaji uchumi ukashuka kwa asilimia 0.2 hadi kufikia ukuaji wa asilimia 6.8 mwaka 2017. Miaka miwili iliyofuata yaani 2018 na 2019 ukuaji wa uchumi ulirejea kwa wastani wa kawaida wa asilimia saba, lakini haukuweza kuvuka hapo.

Mheshimiwa Spika, tafsiri ya uchambuzi huo mdogo ni kwamba Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano umeshindwa kabisa yaani zero kufikia lengo la wastani wa asilimia 10 la ukuaji wa uchumi. Maelezo ya Waziri Mpango jana aliyowasilisha kwa mbwembwe nyingi sana yamebainisha vilevile kwamba ukuaji utapungua tena kutoka asilimia 6.9 mpaka asilimia 5.5.

Mheshimiwa Spika, pato la wastani kwa kila mtu; Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao tunautekeleza hivi sasa ulikusudia kupandisha pato la wastani kwa kila mtu kutoka dola za Kimarekni 1,043 sawa na shilingi za Kitanzania milioni 2.4 mwaka 2015 hadi kufikia dola za Kimarekani 1,500 sawa na shilingi za Kitanzania milioni 3.4 ifikapo mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, kinyume na matarajio hayo mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango huo yaani 2017 pato la wastani kwa kila mtu liliweza kuongezeka kwa

dola moja tu kufikia dola za Kimarekani 1,044 kutoka dola za Kimarekani 1,043. Mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mpango yaani 2018, pato la wastani kwa kila mtu liliongezeka kwa dola za Kimarekani 46 na kufikia dola za Kimarekani 1,090 kutoka dola za Kimarekani 1,044 zilizorekodiwa mwaka 2017. Kwa mujibu wa hotuba ya Waziri wa Fedha jana mpaka sasa 2020 pato la wastani la kila mtu kwa mwaka ni dola 1,121 zimeongezeka dola nyingine 31 toka dola 1,090 zilizoripotiwa mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, ukitazama mwenendo wa ukuaji wa pato la wastani kwa kila mtu kwa mwaka utagundua kwamba hakukuwa na ongezeko la maana la pato la wastani kwa kila mtu ambalo Serikali hii inaweza kujivunia kwamba ilipiga hatua. Kwa mfano, tukichukulia kwamba ongezeko kubwa la dola za Kimarekani 46 liliotokea mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mpango yaani 2018 ndilo ongezeko litakalotokea kila mwaka ina maana kwamba ili kufikia lengo la Mpango la kuwa na pato la dola za Kimarekani 1,500 kwa mwaka kwa kila mwananchi kutoka dola 1,043 zilizorekodiwa mwaka 2015 itachukua miaka takribani tisa kuweza kufikia lengo.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha umaskini; kiwango cha umaskini kilichorekodiwa katika mwaka wa fedha 2011/2012 kilikuwa ni asilimia 28.2 ya Watanzania wote. Hata hivyo, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 - 2020/2021) ulikusudia kupunguza kiwango hicho hadi kufikia asilimia 16.7. Ili kufikia lengo la kupunguza kiwango cha umaskini hadi kufikia asilimia 16.7 kutoka asilimia 28 ilitakiwa umaskini upungue kwa asilimia 11.5 ndani ya kipindi chote cha miaka mitano ya utekelezaji wa Mpango. Hii ina maana kwamba kila mwaka ilitakiwa kupunguza umaskini kwa asilimia 2.3.

Mheshimiwa Spika, kinyume na matarajio hayo, kiwango cha umaskini kimepungua hadi kufikia asilimia 26.4 tu mwaka 2020 ikiwa ni sawa na punguzo la asilimia 1.8. Ikiwa punguzo la asilimia 11.5 ndio kiwango cha asilimia 100 cha kufikia lengo la kupunguza kiwango cha umaskini, ina maana

kwamba punguzo la asilimia 1.8 ambalo Serikali ya CCM imefanikiwa ni sawa na kiwango cha asilimia 15.6 tu cha utekelezaji wa mpango kufikia lengo la kupunguza kiwango cha umaskini hadi kufikia asilimia 16.7. Kwa maneno mengine Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano umeshindwa kwa asilimia 84.4 kufikia lengo lake la kupunguza kiwango cha umaskini kutoka asilimia 28.2 mwaka 2015 mpaka kufikia asilimia 16.7 mwaka huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa umeme; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ulikusudia kupandisha kiwango cha uzalishaji wa umeme kutoka *megawatt* 1,501 zilizokuwepo mwaka 2015 hadi kufikia *megawatt* 4,915 ifikapo 2020. Hata hivyo, hadi kufikia mwaka 2020 ikiwa ni mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa Mpango, Serikali imeweza kuongeza kiwango cha uzalishaji wa umeme hadi kufikia *megawatt* 1,603. Kiwango hiki ni sawa na ongezeko la *megawatt* 102.3 tu kutoka *megawatt* 1,501 zilizorekodiwa mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia lengo la kuzalisha *megawatt* 4,915 ilitakiwa katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Mpango kuwe na uzalishaji wa *megawatt* 3,414. Kwa hiyo, uzalishaji wa *megawatt* 102 uliofanywa ni sawa na asilimia 2.9 tu ya lengo. Hii maana yake ni kwamba Mpango umeshindwa kufikia lengo lake la uzalishaji wa *megawatt* 4,915 kwa asilimia 97.1. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasikitishwa sana na utekelezaji duni kiasi hiki wa Mpango katika kipengele cha uzalishaji wa umeme hasa ukizingatia kwamba Serikali hii imekuwa ikiwaaminisha wananchi kuwa uzalishaji wa umeme unaridhisha na kwamba Serikali ina mpango wa kuanza kuuza umeme nchi jirani kutokana utoshelevu wa umeme nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vifo vyta mama wajawazito wakati wa kujifungua; Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano ulikusudia kupunguza vifo vyta mama wajawazito wakati wa kujifungua hadi kufikia vifo 250 kati ya mama

wajawazito 100,000 wanaojifungua kutoka vifo 432 vilivyokuwepo wakati huo. Badala ya vifo vyaa kinamama wajawazito waliojifungua kupungua kadri ya malengo ya mpango, vifo hivyo vimikuwa vikiongezeka kila mwaka.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani vifo vyaa akinamama wajawazito wakati wa kujifungua vilifikia 556 kati ya akinamama 100,000 mwaka 2016/2017; 524 kati ya akinamama 100,000 mwaka 2017; 578 kati ya akinamama 100,000 mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi zinaonesha kwamba kumekuwa na ongezeko la vifo 124, vifo 92 na vifo 146 kati ya akina mama 100,000 waliojifungua kwa mtiririko wa miaka tajwa hapo juu. Na vifo 432 vilivyorekodiwa mwaka 2014/2015 ikilinganishwa na vifo 432 vilivyorekodiwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatafsiri ongezeko hili la vifo vyaa akinamama wajawazito wakati wa kujifungua kama taswira halisi ya Serikali hii ya CCM kupuuza na kutokuchukulia kwa uzito stahili suala la afya ya mama na mtoto. (*Makofii*)

Kwa kuwa eneo hili la kupunguza vifo vyaa mama wajawazito wakati wa kujifungua Serikali imeshindwa kupunguza hata kifo kimoja kutokana na vifo hivyo vilivyorekodiwa mwaka 2014/2015 na hivyo kupata alama ya asilimia sifuri katika utekelezaji wa mpango kuhusiana na jambo hili.

Mheshimiwa Spika, huduma ya maji safi na salama vijijini; eneo hili ni muhimu sana kwa maisha ya wananchi kwa kuwa maji ni mojawapo ya mahitaji msingi ya binadamu ili aweze kuishi. Kutokana na umuhimu wa maji katika maisha ya wananchi na kwa kutambua changamoto nydingi zinazowakabili wananchi waishio vijijini ikiwemo ya upungufu wa huduma za maji, Mpango ulikusudia kuongeza kiwango cha huduma ya maji safi na salama vijijini hadi kufikia zaidi ya asilimia 80 ifikapo mwaka 2021 kutoka asilimia 70 iliyorekodiwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kinyume na malengo hayo ya Mpango kiwango cha huduma ya maji safi na salama vijiji ni kilipungua hadi kufikia asilimia 64.8 kutoka asilimia 72 iliyorekodiwa mwaka 2014/2015 ikiwa ni sawa na anguko la asilimia 7.2.

Mheshimiwa Spika, unakumbuka hata wewe wakati wa hotuba ya Wizara ya Maji ulilalamika sana jinsi ambavyo Jimbo lako la Kongwa limekuwa halitendewi haki katika eneo hili, kwa hiyo, tunazungumza lugha moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sio nia yangu kufanya tathmini ya kila lengo isipokuwa nataka kuonesha kwamba hiki kitu kinachoitwa mafanikio ya kishindo, kama ambavyo jana kimewasilishwa na Mheshimiwa Mpango kina walakini mkubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kutotekeleza bajeti ya miradi ya maendeleo kikamilifu; hoja nyingine ya msingi ambayo imekuwa kikwazo kikubwa katika utekelezaji bora wa Mpango ya Maendeleo hapa nchini ni tabia sugu ya Serikali ya kutotekeleza bajeti ya miradi ya maendeleo kama ilivyopitishwa na Bunge. Hii ni hoja ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiipigia kelele tangu wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Taifa wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, si jambo la kubishaniwa kwamba ili Mpango wowote uweze kutekelezwa unahitaji bajeti, kwa maana ya fedha za kuutekeleza mpango huo. Ukweli ni kwamba fedha hazipelekwi kama ilivyopangwa, hata jana Waziri Mpango ametuthibitishia kwamba katika mwaka wa fedha 2019/2020 Mpango wa Taifa wa Maendeleo ultenga shilingi triliioni 12.25 sawa na asilimia 37 ya bajeti nzima ya Serikali, lakini fedha iliyopelekwa mpaka jana ni shilingi triliioni 7.63 tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa nitafanya uchambuzi wa sekta chache ambazo tunadhani ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo; ukichukulia sekta ya kilimo ambayo inakadirisha kuajiri takribani asilimia 80 ya Watanzania, bajeti ya maendeleo imetekelezwa kwa wastani wa asilimia 17.55 kwa miaka yote minne ya utawala wa Serikali hii. Ikiwa Serikali imetekeleza bajeti ya maendeleo kwenye kilimo kwa wastani wa asilimia 17.55 hii ina maana kwamba, asilimia 82.45 ya bajeti ya maendeleo kwenye sekta ya kilimo haikutekelezwa; kwa maneno mengine asilimia 82.45 ya miradi ya maendeleo ya kilimo haikutekelezwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukisoma hotuba yangu nimeelekeza kwa kina jinsi sekta inavyogusa Watanzania wengi. Kwa hiyo, naomba mrejee hotuba kwa maeleo zaidi, muda hautoshi kuchambua. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya afya; ukienda kwenye sekta ya afya ambayo ndiyo sekta inayoshikilia sekta nyingine kwa maana kutoa hakikisho la nguvu kazi yenye afya (*healthy labour force*) hali ni mbaya zaidi. Kwa mfano, bajeti nzima ya afya ilipungua shilingi trillioni 1.7 mwaka 2017/2018 mpaka kufikia shilingi bilioni 866 mwaka 2018/2019 ikiwa ni anguko la shilingi bilioni 211. Ukiachilia mbali kuperomoka kwa bajeti ya afya bado utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwenye sekta ya afya umekuwa kizungumkuti. Kwa mujibu wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Sekta ya Afya ni kwamba, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 fedha za miradi ya maendeleo kwenye sekta ya afya zilizokuwa zimetolewa hadi kufikia Machi, 2019 zilikuwa ni asilimia 16 tu. Hii ni sawa na kusema kwamba bajeti ya maendeleo katika sekta ya afya haikutekelezwa kwa asilimia 84 kwa mwaka husika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ya Afya ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 544.1 kwa miradi ya maendeleo, lakini hadi kufikia mwezi Machi, 2020 kiasi cha fedha kilichokuwa kimetolewa ni shilingi bilioni 83.6 sawa na asilimia 15.3 tu ya bajeti ya maendeleo. Aidha, kati ya fedha zilizotolewa fedha za ndani ni asilimia 9.2 na za nje ni asilimia 21. Zile mbwembwe za jana zinatokana na mambo gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya viwanda na biashara; mgawo wa fedha za maendeleo katika sekta ya viwanda na biashara kwa miaka mitatu iliyopita ilikuwa kama ifuatavyo; mwaka 2016/2017 fedha iliyotolewa ilikuwa ni asilimia 44; mwaka 2017/2018 asilimia 9.51; mwaka 2018/2019 asilimia 6.5. Ukitafuta wastani wa utekelezaji wa bajeti katika sekta hii kwa miaka tajwa utagundua kwamba bajeti ya maendeleo katika sekta ya viwanda na biashara imetekelvezwa kwa wastani wa asilimia 20 tu kwa miaka yote minne ya utekelezaji. Mbwembwe za jana ni za nini? (*Makof/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maji; kwenye sekta ya maji mgawo wa bajeti ya maendeleo ulikuwa kama ifuatavyo; mwaka 2016/17 asilimia 25; mwaka 2017/2018 asilimia 22; mwaka 2018/2019 asilimia 15; mwaka 2019/2020 asilimia 61. Wastani wa bajeti iliyotengwa ni asilimia 30 kwa miaka hiyo minne. Hali kadhalika eneo hili la maji ni kat i ya maeneo ambayo kulikuwa na upotevu mkubwa wa fedha za umma kwa uanzishaji wa miradi hewa ulioingizia nchi hasara ya matrillioni ya shilingi ambayo kama yangetumika vyema leo ajenda ya maji safi na salama tungekuwa tumeifunga. Rejea hotuba yangu kwa maelezo ya kina. Mbwembwe za jana zimetoka wapi? (*Makof/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Wizara hizi nne muhimu ambazo tunazitumia kama mfano, lakini ukifanya tathmini ya utoaji wa fedha za maendeleo kwa Wizara nyingine, ukiacha Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ambazo zina nafuu kubwa, hali ni hiyo hiyo. Serikali ifanye mapitio ya makisio ya bajeti dhidi ya vyanzo halisi na uwezo wa makusanyo wa mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka minne mfululizo Serikali imekuwa ikifanya makisio makubwa ya bajeti bila kuoanisha makisio hayo na vyanzo halisi vya mapato na pia uwezo wake wa kukusanya mapato. Jambo ambalo limesababisha Serikali kushindwa kufikia lengo la makusanyo kwa miaka yote.

Mheshimiwa Spika, ukifanya tathmini ya miaka minne iliyopita, utaona kwamba, kuna tatizo kubwa kwenye

ukusanyaji wa mapato. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali ilipanga kukusanya kiasi cha shilingi trillioni 29.54 lakini iliweza kukusanya mapato kutoka vyanzo vyote yaliyofikia shilingi trillioni 20.7 sawa na asilimia 70 ya lengo. Hii ina maana kwamba asilimia takribani 30 iliyobaki sawa na shilingi trillioni 8.3 ilikuwa ni nakisi ya bajeti husika na kwa maana hiyo bajeti ya mwaka husika haikutekelezwa kwa asilimia 30.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali ilipanga kukusanya jumla ya shilingi trillioni 31.7 lakini iliweza kukusanya kiasi cha shilingi trillioni 21.8 tu sawa na asilimia 69 ya lengo. Hii ina maana kwamba asilimia 31 iliyobaki sawa na trillioni 9.8 ilikuwa ni nakisi ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika muktadha huo huo katika mwaka 2018/2019 Serikali ilipanga kukusanya shilingi trillioni 32; hata hivyo iliweza kukusanya shilingi trillioni 28.8 sawa na asilimia 79 ya lengo. Hivyo kiasi cha shilingi trillioni 6.6 hakikukusanya ikiwa ni sawa na asilimia 20. Mwaka 2019/2020 Serikali ilipanga kukusanya shilingi trillioni 33.1 na kufanikiwa kukusanya trillioni 26.3 mpaka bajeti inavyosomwa kama ilivyowasilishwa jana na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mchanganuo huo, ni dhahiri kuwa mwelekeo wa makusanyo wa mapato kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kwa wastani ulikuwa chini ya makadirio yaliyoidhinishwa hali inayoleta athari katika utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Taifa. Kwa hiyo, ni rai ya upinzani kuitaka Serikali ifanye marekebisho ya bajeti kutokana na uwezo wetu wa kukusanya.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Mpango wa Bajeti kukabiliana na madhara ya janga la Corona; ni ukweli usiopingika kwamba wakati Serikali inapanga bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 kulikuwa hakuna janga la Corona hapa nchini na kwa sababu hiyo bajeti hii haikuzingatia kwa mapana yake madhara ya Corona katika uchumi jumla wa Taifa na uchumi wa kila mwananchi na uchumi wa dunia. Hata hivyo, baada ya Corona kubisha hodi

hana nchini hakuna ubishi tena kuwa janga hilo limeathiri kwa kiwango kikubwa uchumi wa nchi mbalimbali duniani na chi yetu vilivile yetu na maisha ya mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira kama hayo ambayo uchumi umetikisika na katika mazingira ambayo Taifa halikuwa na maandalizi ya mtikisiko huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba Serikali ifanye *budget adjustment* ili iendane na mazingira ya sasa ya janga la Corona ambayo mapato ya Serikali yameshuka na yataendelea kuendelea kushuka ikiwa gonjwa hili litaendelea. Hotuba ya Waziri wa Fedha jana pia imainisha maeneo nane muhimu sana ya shughuli za kiuchumi yaliyoathirika na yanayotarajiwa kuendelea kuathirika kutokana na janga hili.

Mheshimiwa Spika, hatua za ziada ya kuchukua kunusuru kuporomoka kwa uchumi kufuatia athari za janga la Corona; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua na inaheshimu hatua zilizochukuliwa na *BOT*na hatua zilizotajwa na Waziri wa Fedha jana wakati akisoma hotuba yake baadhi zikiwa ni mapendekezo ya Kambi katika hotuba zake mbalimbali katika kipindi hiki. Pamoja na hatua hizo kama sehemu ya kunusuru sekta binafsi, tunashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja, Serikali irejeshe madai ya kodi kwa wafanyabiashara. Kumekuwa na malalamiko mengi sana kutoka kwa jamii ya wafanyabiashara kuhusiana na kutorejeshewa kwa fedha zao za kodi na hususan ongezeko la asilimia 15 ya ushuru wa forodha ambaa hulipwa kabla kwa ajili ya kuagiza sukari viwandani toka nje. Utafiti uliofanywa na Shirika la Wamiliki wa Viwanda (*CTI*) kwa viwanda na makampuni mbalimbali ya kibashara nchini umebaini uwepo wa tatizo kubwa na uhaba wa fedha unavyovikabili viwanda na makampuni mengi ya bishara kutokana na waagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi na pia uuzaji wa bidhaa nje ya nchi kutokana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kutorejesha madai ya kodi hivyo

viwanda na makampuni yanayofanya biashara kimataifa kupata taabu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, biashara nyingi ambazo zilikuwa zimeathirika ni zile ambazo zimesajiliwa katika mfumo wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) kama vile sekta ya madini, ujenzi, kilimo na kampuni nyingine za biashara zinazomilikiwa na wazawa na zile zinazotoka nje, lakini zikifanya shughuli zake hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa viwanda na biashara na kampuni nyingine za biashara hazikuwa zimerejeshewa fedha za kodi kwa Kipindi cha miaka miwili hadi mitatu iliyopita. Taarifa hiyo inaonesha kuwa marejesho ya kodi yaliyofanyika kwa kipindi cha miaka minne ya fedha yalikuwa ni shilingi trilioni 1.52 wakati madai halisi *hayajalipwa* (*outstanding refunds*) yalikuwa shilingi trilioni 2.3; hii ni kwa mujibu wa Taarifa ya *CTI*, hii maana yake ni kwamba kiasi kikubwa cha madai ya kodi kilikuwa hakijalipwa kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, deni la Taifa; kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikiwepa kuonesha takwimu za deni la Taifa kwa ujumla wake kwa maana Deni la Serikali na deni la sekta binafsi, badala yake Serikali imekuwa ikitoa takwimu za deni la Serikali pekee. Kwa mujibu wa Ripoti ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwezi Aprili, 2020 jumla ya deni la nje kwa maana ya deni la Serikali na deni la sekta binafsi ilifikia dola za Kimarekani milioni 22.386 kwa hela za Kitanzania ni trilioni 51.8 deni la nje kwa kiwango cha kubadilisha fedha cha jana.

Mheshimiwa Spika, ili kupata takwimu halisi za deni la Taifa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imechukua jumla ya deni la Serikali la nje na ndani ambalo kwa sasa ni shilingi trilioni 53.1 na kujumlisha na deni la sekta binafsi la nje ambalo limefikia trilioni 13.5 na kupata jumla ya deni la Taifa kuwa shilingi trilioni 66.6. Ili kujua kwa namna gani Serikali hii inakopa, bila kuwa na nukta mwaka 2015/2016 deni la Taifa liliikuwa shilingi trilioni 41 mwaka 2020 deni la Taifa limefikia shilingi trilioni 66.6 wakati huku mnajitapa mnatekeleza na fedha za

ndani kumbe mnakopa na hamuwaambii Watanzania ukweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uhimilivu wa deni la Taifa; ukifanya tathmini ya wastani wa makusanyo halisi ya mapato kwa miaka minne iliyopita na fedha iliyotengwa kila mwaka kulipa deni la Taifa na mishahara ya wafanyakazi utagundua kuwa deni la Taifa linaweza likawa himilivu kichumi, lakini ni mzigo kwa Taifa. Hii ni kwa sababu wastani wa makusanyo ya *TRA* kwa miaka minne iliyopita ni shilingi trillioni 15 mpaka 16, zikizidi sana 17. Makusanyo yetu yote ya kodi, Halmashauri na maduhuli ilhali fedha inayokwenda kulipa deni la Taifa ni wastani wa shilingi trillioni tisa mpaka kumi kila mwaka na fedha za mshahara ni wastani wa shilingi trillioni saba.

Mheshimiwa Spika, tafsiri ya takwimu hizo ni kwamba...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. HALIMA J. MDEE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia sentensi hii.

Mheshimiwa Spika, tafsiri ya takwimu hizo ni kwamba nchi inaendeshwa kwa mikopo na misaada toka kwa wahisani ambao ninyi mnawaita mabeberu na sio mapato ya ndano jambo ambalo ni hatari sana kwa ustawi wa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kwa sababu ya muda ninaomba hotuba yote iingizwe kama ilivyo na nimalizie kumuambia Mheshimiwa Mpango, mbwembwe za jana zilitokana na nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee ameamua kuchokoza nyuki. Amemalizia kwa swali zuri sana la

mwembwe za jana zilitokana na nini? Mimi naamini mjadala wa siku hizi mbili utajibu hilo swalii la mbwembwe za jana zilitokana na jambo gani. Tunashukuru sana.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO,  
MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (MB), AKIWASILISHA  
BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU  
HALI YA UCHUMI WA TAIFA, MPANGO WA MAENDELEO WA  
TAIFA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA  
SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za  
Bunge, Toleo la Januari, 2016*

---

**A. UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika**, kabla sijatoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu hali ya uchumi wa Taifa, Mpango wa Taifa wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021; napenda kutumia fursa hii kumpa pole Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe (Mb) kwa tukio la shambulio dhidi yake ambao lilimjeruhi na kupelekea kuvunjika mguu wake wa kulia. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalaani kitendo hicho; na inaitaka Serikali kuititia vyombo vyake vya dola, kufanya uchunguzi wa haraka na kuwachukulia hatua wale wote watakaobainika kuhusika na uhalifu huo.

**2. Mheshimiwa Spika**, ninapohitimisha kipindi changu cha tatu cha miaka mitano mfululizo cha kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na ninapohitimisha kipindi cha miaka mitano cha kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Fedha na Mipango; nina kila sababu ya kumshukuru Mungu kwa kila jambo nililotenda au nililotendewa katika kuitumikia nafasi yangu. Hii ni kwa sababu ninaamini kuwa yote yalifanyika kwa mpango wake; na ni katika mpango wake huo huo,

nimefanya yale niliyoweza kufanya na sikufanya yale ambayo sikuweza kufanya.

**3. Mheshimiwa Spika**, safari yangu hiyo ya utumishi na uwakilishi wa wananchi haikuwa rahisi; ilikuwa na vikwazo na changamoto nydingi. Lakini ninaendelea kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuvishinda vikwazo na changamoto zilizonikabili na hatimaye kuyaweza yote katika yeche anitiaye nguvu. Ninapenda kutumia nafasi hii kipekee kuwakumbuka wale wote tulioanza nao safari pamoja lakini leo hawapo nasi kwa kuwa wametangulia mbele ya haki. Mungu awape pumziko la milele. Haina maana kwamba sisi ambao Mungu ametuacha hai mpaka sasa ni wema kuliko hao waliotangulia; la hasha! bali ametupa muda zaidi ili tuyatimize mapenzi yake kupitia wajibu wetu; na zaidi sana ametupa nafasi ya upendeleo ili tujirekebishe kwa kutubu na kutenda mema ili tustahilli kuurithi ufalme wa mbinguni. Ni namna gani tunautumia muda huo wa upendeleo ili kutimiza malengo hayo; kila mmoja atajibu kwa muda wake na kwa kadiri ya wajibu na nafasi yake.

**4. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa uhai wa Bunge hili la Kumi na Moja unaelekea ukingoni na kwa maana hiyo kuifanya hotuba hii kuwa hotuba yangu ya mwisho kwa Bunge hili kama Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Fedha na Mipango; nitajielekeza zaidi kwenye kutoa tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano sambamba na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kuutekeleza Mpango huo kwa kipindi cha muhula wa miaka mitano wa Serikali hii ya awamu ya tano. Aidha, nitazungumzia kwa kifupi sana majanga yanayolikabili Taifa kwa sasa, na namna majanga hayo yalivyoathiri uchumi kwa ujumla na hususan makisio na upangaji wa Bajeti ya mwaka 2020/2021.

## **B. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA TAIFA WA MAENDELEO WA MIAKA MITANO 2016/17 – 2020/21**

**5. Mheshimiwa Spika**, hii ni bajeti ya tano na ya mwisho kwa Serikali hii ya awamu ya tano inayotarajiwa kuondoka

madarakani mapema mwezi Oktoba mwaka 2020 baada ya kumaliza muhula wake wa miaka mitano ya uongozi. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeona ni wakati muafaka kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ili kuona ni kwa kiwango gani Serikali hii ya CCM imeweza kutekeleza ahadi zake kwa wananchi.

**6. Mheshimiwa Spika**, katika kufanya tathmini hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itaonesha hali ilivyokuwa mwaka 2015 wakati Mpango unaandaliwa; malengo yaliyokusudiwa kufikiwa hadi kufikia mwaka 2021 na hali halisi iliyofikiwa kwa utekelezaji hadi kufikia mwaka 2019. Hata hiyo, tathmini hii itahusu baadhi ya maeneo ya kipaumbele ambayo kimsingi yanabeba uwakilishi mkubwa wa Mpango mzima. Vyanzo vya taarifa katika tathmini hii ni Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21; Taarifa ya Hali ya Uchumi 2018 na Hotuba za Bajeti Kuu za Serikali kwa miaka ya fedha 2016/17; 2017/18; 2018/19 na 2019/2020.

#### i. Wastani wa Ukuaji wa Uchumi

**7. Mheshimiwa Spika**, wakati Mpango wa Kwanza wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano unamaliza muda wake mwaka 2015, wastani wa ukuaji wa uchumi ulikuwa ni asilimia 7. Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambaa ndio huu tulio nao sasa hivi ukaweka malengo ya ukuaji wa uchumi kwa wastani wa asilimia 10. Mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wasatani wa ukuaji wa uchumi ukashuka kwa asilimia 0.2 hadi kufikia ukuaji wa asilimia 6.8 mwaka 2017. Miaka miwili iliyofuata, yaani 2018 na 2019 ukuaji wa uchumi ulirejea kwenye wastani wa kawada wa asilimia 7 lakini haukuweza kuvuka hapo!

**8. Mheshimiwa Spika**, tafsiri ya uchambuzi huo mdogo ni kwamba Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano umeshindwa kabisa (0%) kufikia lengo la wastani wa asilimia 10 la ukuaji wa uchumi. Kwa hiyo; Serikali ijue, inaposema uchumi wetu ni mionganoni mwa chumi zinazokua kwa kasi katika Afrika ya Mashariki na Kati; ikumbuke pia kwamba imeshindwa kusogeza ukuaji wa uchumi wetu hata kwa nukta

moja (0.1%) kwa kipindi chote cha miaka mitano iliyokaa madarakani na badala yake iliushusha ukuaji huo kwa nukta mbili (0.2%) katika mwaka wake wa kwanza wa kuwa madarakani.

*ii. Pato la Wastani kwa Kila Mtu*

**9. Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (huu unaotekelozwa sasa hivi) ulikusudia kupandisha pato la wastani kwa kila mta kutoka Dola za Kimarekni 1,043 sawa na Shilingi za Kitanzania 2,412,459 mwaka 2015 hadi kufikia Dola za Kimarekani 1,500 sawa na shilingi za Kitanzania 3,469,500 itakapofika mwaka 2021.

**10. Mheshimiwa Spika,** Kinyume na matarajio hayo; mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango huo; yaani mwaka 2017; Pato la Wastani kwa kila mta liliweza kuongezeka kwa Dola moja tu ya Kimarekani sawa na Shilingi 2,313 kwa kiwango cha ubadilishaji fedha (exchange rate) cha sasa na kufanya pato jumla la wastani kwa kila mta kufikia Dola za Kimarekani 1,044 kutoka Dola 1,043 zilizokuwepo.

**11. Mheshimiwa Spika,** mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mpango yaani 2018; pato la wastani kwa kila mta liliongezeka kwa Dola za Kimarekani 46 sawa na Shilingi za Kitanzania 60,398 (kwa kiwango cha ubadilishaji fedha cha sasa cha dola moja kwa shilingi 2,313) na kufikia Dola za Kimarekani 1,090 kutoka Dola 1,044 zilizorekodiwa mwaka 2017. Hata hivyo, mpaka naandaa hotuba hii, hakukuwa na taarifa za ukuaji wa pato la wastani kwa kila mta kwa mwaka 2019 na 2020.

**12. Mheshimiwa Spika,** ukitazama mwenendo wa ukuaji wa pato la wastani kwa kila mta kwa miaka hiyo miwili ambayo taarifa zake zipo; utagundua kwamba hakukuwa na ongezeko la maana la pato la wastani kwa kila mta ambalo Serikali hii inaweza kujivunia kwamba ilipiga hatua. Kwa mfano, tukichukulia kwamba ongezeko kubwa la Dola za Kimarekani 46 lilitotokea mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mpango yaani 2018 ndilo ongezeko litakalotokea kila mwaka; ina maana kwamba ili kufikia lengo la Mpango la kuwa na

Pato la Dola za Kimarekani 1,500 kutoka Dola 1,043 zilizorekodiwa mwaka 2015; itatakiwa kuwe na ongezeko la wastani wa pato la kila mtu la jumla ya Dola za Kimarekani 457 kwa kipindi chote cha miaka mitano ya utekelezaji wa Mpango. Hii ina maana kwamba, itachukua miaka takribani tisa (9) ili kufikia lengo hilo (kwa maana ya kugawanya Dola 457 dhidi ya ongezeko la kila mwaka la Dola 46).

**13. Mheshimiwa Spika**, ikizingatiwa kwamba huu ndio mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa mpango; na kuna nakisi kubwa namna hiyo ya kufikia lengo; Kambi Rasmi ya Upinzani inashawishika kuamini kwamba ama uandaaji wa Mpango huo ulikosewa (miscalculated) kwa kuweka makisio makubwa kuliko uwezo wa utekelezaji au Serikali imeshindwa kabisa kuijendesha kwa kushindwa kutekeleza Mpango yake (Failed State).

### **iii. Kiwango cha Umaskini**

**14. Mheshimiwa Spika**, kiwango cha umaskini kilichorekodiwa katika mwaka wa fedha 2011/12 kilikuwa ni asilimia 28.2. Hata hivyo, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21) ulikusudia kupunguza kiwango hicho hadi kufikia asilimia 16.7 ifikapo mwaka 2021. Ili kufikia lengo la kupunguza kiwango cha umaskini hadi kufikia asilimia 16.7 kutoka asilimia 28.2 ilitakiwa umaskini upungue kwa asilimia 11.5 ndani ya kipindi chote cha miaka mitano ya utekelezaji wa Mpango. Hii ina maana kwamba kila mwaka ilitakiwa tuweze kupunguza umaskini kwa asilimia 2.3.

**15. Mheshimiwa Spika**, kinyume na matarajio hayo, kiwango cha umaskini kilipungua hadi kufikia asilimia 26.4 mwaka 2018 ikiwa ni sawa na punguzo la asilimia 1.8 na hii ikiwa ni mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mpango. Ikiwa punguzo la asilimia 11.5 ndio kiwango cha asilimia 100 cha kufikia lengo la kupunguza kiwango cha umaskini, ina maana kwamba punguzo la asilimia 1.8 ni sawa na kiwango cha asilimia 15.6 tu cha utekelezaji wa Mpango katika kufikia lengo la kupunguza kiwango cha umaskini hadi kufikia asilimia 16.7. Kwa maneno mengine Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano umeshindwa kwa asilimia 84.4

kufikia lengo lake la kupunguza kiwango cha umaskini kutoka asilimia 28.2 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 16.7 ifikapo 2021.

**iv. Uwekezaji wa Mitaji Kutoka Nje**

**16. Mheshimiwa Spika**, mwaka 2014, uwekezaji wa mitaji kutoka nje hapa nchini ulikuwa ni wa jumla ya Dola za Kimarekani bilioni 2.4 sawa na Shilingi za Kitanzania takribani trillioni 5.5. Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo uliweka malengo ya kuongeza uwekezaji huo hadi kufikia Dola za Kimarekani bilioni 9 sawa na Shilingi Trillioni 20.8 (kwa kiwango cha ubadilishaji fedha (exchange rate) cha Shilingi 2,313 kwa Dola moja ya Kimarekani).

**17. Mheshimiwa Spika**, ili kufikia lengo hilo ilitakiwa ndani ya kipindi cha miaka mitano ambacho Serikali hii ya awamu ya tano imekaa madarakani uwekezaji wa mitaji ya nje uwe umeongezeka kwa jumla ya Dola za Kimarekani bilioni 6.6 sawa na Shilingi Trillioni 14.8 (kwa maana ya kutoka Dola bilioni 2.4 hadi Dola bilioni 9 kama mpango ulivyokusudia).

**18. Mheshimiwa Spika**, tofauti na malengo hayo ya Mpango, uwekezaji wa mitaji kutoka nje ulifikia Dola za Kimarekani bilioni 4.634 mwaka 2016, ikiwa ni ongezeko la Dola bilioni 2.234 kutoka dola bilioni 2.4 zilizorekodiwa mwaka 2014. Mwaka 2018 uwekezaji ulifikia Dola za Kimarekani bilioni 5.393, ikiwa ni ongezeko la Dola milioni 759 kutoka dola bilioni 4.634 zilizorekodiwa mwaka 2016.

**19. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa hakuna taarifa za uwekezaji wa mitaji kutoka nje kwa mwaka 2019 na 2020; Kambi Rasmi ya Upinzani inachukulia kwamba kwa kipindi chote cha miaka mitano cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo, uwekezaji wa mitaji kutoka nje uliongezeka kwa wastani wa Dola za Kimarekani bilioni 1.4965 kutoka dola bilioni 2.4 zilizorekodwa mwaka 2914 na kutoka dola bilioni 4.634 zilizorekodiwa mwaka 2016.

**20. Mheshimiwa Spika**, Ongezeko hilo la uwekezaji wa mitaji toka nje la wastani wa Dola bilioni 1.4965 ni sawa na asilimia 16.6 tu ya malengo ya Mpango ya kufikia uwekezaji wa mitaji

kutoka nje wa Dola za Kimarekani bilioni 9 ifikapo 2021. Hii ina maana kwamba Serikali imeshindwa kwa kiwango cha asilimia 84.4 kuutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Na kwa kuwa kuna janga la Corona ambalo bado hajulikani litakwisha lini; upo uwezekano mkubwa wa kuendelea kuporomoka kwa uwekezaji wa mitaji kutoka nje.

**v. Uzalishaji wa Umeme**

**21. Mheshimwa Spika**, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ulikusudia kupandisha kiwango cha uzalishaji wa umeme kutoka MW 1,501 zilizokuwepo mwaka 2015 hadi kufikia MW 4,915 ifikapo mwaka 2020. Hata hivyo, hadi kufikia mwaka 2020; ikiwa ni mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa Mpango, Serikali imeweza kuongeza kiwango cha uzalishaji wa umeme hadi kufikia MW 1,603.38. Kiwango hiki ni sawa na ongezeko la MW 102.38 kutoka MW 1,501 zilizorekodiwa mwaka 2015.

**22. Mheshimiwa Spika**, ili kufikia lengo la kuzalisha MW 4,915, ilitakiwa katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Mpango kuwe na uzalishaji wa MW 3,414. Kwa hiyo, uzalishaji wa MW 102.38 uliofanywa ni sawa na asilimia 2.9 tu ya lengo. Hii maana yake ni kwamba Mpango umeshindwa kufikia lengo la uzalishaji wa MW 4,915 kwa asilimia 97.1.

**23. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasikitishwa sana na utekelezaji duni kiasi hiki wa Mpango katika kipengele cha uzalishaji wa umeme hasa ukizingatia kwamba Serikali hii imekuwa ikiwaaminisha wananchi kuwa uzalishaji wa umeme unaridhisha na kwamba Serikali ina mpango wa kuanza kuza umeme kwa nchi jirani kutokana utoshelevu wa umeme nchini.

**vi. Vifo vya Mama Wajawazito wakati wa Kujifungua**

**24. Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ulikusudia kupunguza vifo vya mama wajawazito wakati wa kujifungua hadi kufikia vifo 250 kati ya mama wajawazito 100,000 wanaojifungua kutoka vifo 432 kati ya mama wajawazito 100,000 wanajifungua vilivyorekodiwa mwaka 2014/15.

**25. Mheshimiwa Spika**, badala ya vifo vya mama wajawazito wanaojifungua kupungua kadiri ya malengo ya Mpango; vifo hivyo vimeduwa vikiongezeka kila mwaka. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO); vifo vya akina mama wajawazito wakati wa kujifungua vilififikia 556/100,000 mwaka 2016/17; 524/100,000 mwaka 2017 na 578/100,000 mwaka 2018. Takwimu hizi zinaonesha kwamba kumeduwa na ongezeko la vifo 124, 92 na 146 kati ya akina mama 100,000 wanaojifungua kwa mtiririko wa miaka tajwa ikilinganishwa na vifo 432 vilivyorekodiwa mwaka 2014/15.

**26. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatafsiri ongezeko hili la vifo vya mama wajawazito wakati wa kujifungua kama taswira halisi ya Serikali hii ya CCM kupuuzia na kutolichukulia kwa uzito stahili suala la afya ya mama na mtoto. Kwa kuwa katika eneo hili la kupunguza vifo vya mama wajawazito wakati wa kujifungua Serikali imeshindwa kupunguza kifo hata kimoja kutoka vifo 432/1000 vilivyorekodiwa mwaka 2014/15 na hivyo kupata alama chini ya asilimia sifuri katika utekelezaji wa mpango kuhusu jambo hilo; Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kujibu maswali yafuatayo; Je, hakukuwa na bajeti ya kutosha kutekeleza mpango wa kupunguza vifo vya mama wajawazito wakati wa kujifungua ndio maana vifo vimeongezeka au vifo hivyo vilitokana na uzembe wa watendaji katika Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais (TAMISEMI). Kwa majibu yoyote yale; Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha kuwa vifo vya akina mama wajawazito wakati wa kujifungua vinapungua?

#### **vii. Huduma ya Maji Safi na Salama Vijijini**

**27. Mheshimiwa Spika**, hili ni eneo muhimu sana kwa maisha ya wananchi kwa kuwa maji ni mojawapo ya mahitaji msingi ya binadamu ili aweze kuishi. Kutoptaka na umuhimu wa maji katika maisha ya wananchi; na kwa kutambua changamoto nyingi zinazowakabili wananchi waishio vijijini ikiwemo ya upungufu wa huduma za maji, Mpango ulikusudia kuongeza kiwango cha huduma ya maji safi na salama vijijini hadi kufikia zaidi ya asilimia 80 ifikapo 2021 kutoka asilimia 72 iliyorekodiwa mwaka 2014/15.

**28. Mheshimiwa Spika**, kinyume na malengo hayo ya Mpango; kiwango cha huduma ya maji safi na salama vijijini kilipungua hadi kufikia asilimia 64.8 kutoka asilimia 72 iliyorekodiwa mwaka 2014/15 ikiwa ni sawa na anguko la asilimia 7.2

**29. Mheshimiwa Spika**, kushindwa kufikiwa kwa malengo ya Mpango kunatokana na mapungufu yafuatayo:-

i. **Kukosekana kwa Sheria ya Kusimamia Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo:-**

**30. Mheshimiwa Spika**, tangu wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/12-2015/16); na kwa miaka yote minne ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo 2016/17 – 2020/2021; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikilisisitiza Serikali kuleta Muswada wa Sheria Bungeni ili kukidhi matakwa ya ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya nchi ya kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mpango wowote unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano.

**31. Mheshimiwa Spika**, hili halikuwa pendekezo la Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na wala halikuwa ombi; bali ni sharti la Kikatiba; na kazi ya Upinzani ilikuwa ni kuikumbusha Serikali kutimiza wajibu huo wa Kikatiba. Na lengo la kufanya hivyo lilikuwa ni kuisaidia Serikali kuweka utaratibu mzuri wa kisheria wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ili kudhibiti vikwazo vinavyoweza kukwamisha utekelezaji wa mipango hiyo na hivyo kuifanya Serikali iweze kufikia malengo iliyokusudia kuyafikia katika mipango hiyo.

**32. Mheshimiwa Spika**, pamoja na nia hiyo njema ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Serikali, Serikali hii ya CCM haijawahi hata mara moja kutekeleza wajibu huo wa Kikatiba; ikiwa tunaingia mwaka wa kumi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Kumi na Mitano, uliogawanywa katika vipindi vitatu vyaa miaka mitano mitano (yaani mpango wa kwanza 2011/12 -2015/16; mpango wa pili 2016/17 – 2020/21 na mpango wa tatu 2021/22 – 2025/26.

**33. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ilieleza jinsi Mpango wa Kwanza wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16) ulivyoshindwa kufikia malengo yake kwa takribani asilimia 50, kutokana na kukosekana kwa sheria ya kusimamia utekelezaji wake ambapo mambo yalikuwa yakifanyika kiholela.

**34. Mheshimiwa Spika**, hatari ya kushindwa kufikia malengo ya Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) imekuwa kubwa zaidi kwa kuwa Serikali hii ya awamu ya tano imeacha utamaduni wa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, na badala yake utashi na maelekezo ya viongozi; na hasa kiongozi mmoja; ndiyo yanachukuliwa kama dira ya kuiongoza nchi.

**35. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inathubutu kusema kwamba; Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo umefeli kwa kuwa tuko kwenye mwaka wa mwisho wa utekelezaji wake ikiwa malengo yake makubwa hayajafikiwa kwa hata robo. Lengo kuu la Mpango wa Pili lilikuwa ni kuhakikisha kwamba Tanzania inaingia katika uchumi wa kipato cha kati. Serikali iwaambie wananchi, ni viashiria gani vyta uchumi wa kipato cha kati vimeanza kuonekana ikiwa ajira na fursa za kiuchumi kwa wafanyakiaresha na wakulima zimebanwa na vipato kwa wananchi vimeporomoka? Na hali imekuwa mbaya zadi hasa kwa kipindi hiki ambacho Taifa linakumbwa na janga la Corona!

**36. Mheshimiwa Spika**, lengo lingine la Mpango wa Pili lilikuwa kuziimarisha Serikali za Mitaa katika kupanga na kutekeleza mipango yao. Serikali ijipime imefikia lengo hilo kwa kiwango gani ikiwa imezifilisi mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuzinyang'anya vyanzo vyta mapato na kuzifanya kuwa ombaomba kwa Serikali Kuu? Lengo lingine lilikuwa ni kuboresha viwango vyta maisha ya watu. Serikali ijipime imefikia lengo hilo kwa kiwango gani ikiwa kila mwananchi analia ukata na ugumu wa maisha kiasi cha kushindwa kumudu gharama za milo mitatu kwa siku. Bado wapo

wananchi wanaoishi chini ya dola moja kwa siku!! Je, hayo ndiyo maisha bora kwa Watanzania?

**37. Mheshimiwa Spika**, si nia yangu kufanya tathmini ya kila lengo, isipokuwa nataka kusisitiza kwamba tunashindwa kufikia malengo hayo kwa kuwa utekelezaji wa malengo hayo hauna mwongozo wa kisheria; na pia watekelezaji wanajua kwamba hata wasipofikia hayo malengo hawawajibiki kisheria. Ndio maana bado Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza kwamba; kama Serikali itaendelea kupuuzia matakwa ya Katiba ya nchi ya kutaka kuwe na sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mpango yetu ya Maendeleo; tutakuwa tukipanga mipango ambayo haitekelezeki na hivyo kuendelea kutumia vibaya fedha za umma kutekeleza mipango ambayo haifiki malengo yake.

## **ii. Kutoteketeza Bajeti ya Miradi ya Maendeleo Kikamilifu**

**38. Mheshimiwa Spika**, hoja nyiningine ya msingi ambayo imekuwa kikwazo kikubwa katika utekelezaji bora wa Mpango ya Maendeleo hapa nchini ni tabia sugu ya Serikali ya kutoteketeza Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kama ilivyopitishwa na Bunge. Hii ni hoja ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiipigia kelele tangu wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Taifa wa Maendeleo mpaka kipindi hiki cha utekelezaji wa Mpango wa Pili.

**39. Mheshimiwa Spika**, si jambo la kubishaniwa kwamba ili Mpango wowote uweze kutekelezwa unahitaji bajeti (kwa maana ya fedha za kuutekeleza mpango huo). Hata hivyo, pamoja na ukweli na uhalsia huo; Serikali yetu kwa muda mrefu imekuwa ikitoa fedha pungufu ya zile zilizoidhinishwa na Bunge kutekeleza miradi ya maendeleo inayokuwa imepangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha husika. Mbaya zaidi, fedha hizo hutolewa kwa kuchelewa na hivyo kushindwa kutekeleza kazi zilizokwuwa zimepangwa kwa wakati au muda husika.

**40. Mheshimiwa Spika**, ili kuthibitisha hoja hii ni kwamba katika mwaka wa fedha wa 2019/2020 Mpango wa Taifa wa

Maendeleo ulitengewa shilingi trilioni 12.25 sawa na 37 ya bajeti nzima ya Serikali. Hata hivyo, kwa mujibu wa Taarifa ya Hali Uchumi iliyosomwa hapa Bungeni na Waziri wa Fedha na Mipango jana tarehe 11 Juni, 2020; fedha iliyopelekwa ni shilingi trilioni 7.63 tu sawa na asilimia 62.04 ya fedha iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge.

**41. Mheshimiwa Spika**, upungufu huo wa utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa ujumla wake umeathiri pia utekelezaji wa bajeti za maendeleo katika sekta mbalimbali. Si nia yangu kutoa mifano mingi ya namna Serikali inavyofanya utekelezaji duni wa bajeti ya maendeleo; lakini kwa ajili ya kuipa nguvu hoja hii nitatoa mifano ya sekta kadhaa hususan zile zinazogusa maisha ya wananchi wengi moja kwa moja:-

**(a) Sekta ya Kilimo**

**42. Mheshimiwa Spika**, ukichukua sekta ya kilimo ambayo inakadiriwa kuajiri takribani asilimia 80 ya Watanzania, bajeti ya maendeleo imetekelezwa kwa wastani wa asilimia 17.55 kwa miaka yote minne ya utawala wa Serikali hii. Hii ni kwa mujibu wa Randama za Wizara ya Kilimo ambapo mwaka 2016/17 bajeti ya maendeleo kwenye Kilimo ilitekelezwa kwa asilimia 2.22; mwaka 2017/18 asilimia 11, mwaka 2018/19 asilimia 42, na mwaka 2019/2020 asilimia 15.

**43. Mheshimiwa Spika**, ikiwa Serikali imetekeleza bajeti ya maendeleo kwenye kilimo kwa wastani wa asilimia 17.55; hii ina maana kwamba asilimia 82.45 ya bajeti ya maendeleo kwenye sekta ya kilimo haikutekelezwa! Kwa maneno mengine, asilimia 82.45 ya miradi ya maendeleo ya kilimo haikutekelezwa! Hapa utajua ni kiasi gani cha ajira kwa wananchi wanaotegemea kilimo zilipotea. Aidha, unaweza pia kufanya hesabu ni kiasi gani cha hasara kilichopatikana kutokana na kutotekeliza miradi hiyo kwa kuzingatia myororo wa thamani ya mazao ya kilimo (Value chain in Agro Economy)

**44. Mheshimiwa Spika**, licha ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, kuitambua sekta ya kilimo kama eneo

muhimu ambapo mpango - mkakati wa kiuchumi utatekelezwa ili kuchangia kujenga msingi imara wa uchumi wenyе ushidhani na wenyе nguvu; na licha ya Mpango Mkakati kuweka malengo ya kubadilisha kilimo kutoka kwenye uzalishaji mdogo kwenda kwenyе uzalishaji mkubwa na hivyo kuchangia ukuaji wa viwanda; Ukaguzi wa Ufanisi uliofanywa na CAG umebaini kwamba Serikali imeshindwa kubadili kilimo na kukifanya kuwa cha kisasa ili kichangie katika ukuaji wa uchumi wa viwanda.

**45. Mheshimiwa Spika**, mionganoni mwa changamoto zilizobainika katika sekta ya kilimo tofauti na utekelezaji duni wa bajeti ya maendeleo katika sekta hiyo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

- i. Katika kipindi cha miaka minne iliyopita, ni wastani wa 39% tu ya ugavi wa pembejeo za kilimo uliofanyika lkiwa ni pamoja na mbegu,mbolea na viuatilifu.
- ii. Usambazaji wa pembejeo zisizo na ubora kutokana na udhibiti dhaifu.
- iii. Uwepo wa wauzaji na mawakala wa pembejeo za kilimo ambao hawakusajiliwa pamoja na pembejeo za kilimo zisizosajiliwa katika soko.
- iv.Ukaguzi ulibaini 33% ya mawakala wa kilimo hawakusajiliwa kuuza mbegu na mbolea kwenye soko.
- v. Ukaguzi ulibaini kwamba hadi kufikia mwaka 2018 Wizara ya Kilimo ilishindwa kufanya utafiti wa msingi ili kujua mahitaji halisi ya pembejeo kwa wakulima walioko nchini kwa kuzingatia ikolojia na idadi ya wakulima. Wizara ya Kilimo inatumia makadirio tu ili kuweza kupata mahitaji ya wakulima. Maelezo ya Wizara ni kwamba kufanya utafiti wa msingi kwenye pembejeo za kilimo ni gharama!! Kwa sasa mbolea inayosambazwa nchini haizingatii hali ya uhitaji wa udongo katika maeneo mbalimbali nchini. Ukaguzi ulibaini kutoshirikishwa kwa wakulima wakati wa mchakato wa kutambua mahitaji ya pembejeo nchini hivyo kupelekea

mahitaji kutojumuisha aina ya pembejeo zinazokidhi mahitaji ya kanda mbalimbali za kilimo.

vi. Asilimia 90 ya viuwatilifu vinavyotumika nchini vinaingizwa toka nje ya nchi. Na hakuna utafiti wa msingi uliofanywa na Wizara ya Kilimo ili kuweza kusaidia uingizaji wa viuwatilifu nchini.

vii. Tathmini ya ujuzi na ufahamu wa pembejea za Kilimo ilionyesha kuwa wakulima hawakuwa na ujuzi wa matumizi mazuri ya mbegu , viuatilifu na mbolea. Maafisa ugani hawakuwa na ujuzi wa utoaji wa huduma za utaalam wa kilimo kwa wakulima ambazo ni pamoja na matumizi sahihi ya mbegu,viuwatilifu na mbolea.

viii. Ugazi ulibaini kwamba ni 3% tu ya miradi ya umwagiliaji ndiyo ilifanyiwa upembuzi yakinifu kati ya miradi iliyopangwa kufanyiwa , kinyume na sheria ya umwagiliaji . Kati ya pembuzi yakinifu 360 zilizopangwa kufanywa, zilizotekelawa ni 11 tu.  
ix. Ugazi ulibaini kuwepo kwa utegemezi wa fedha za wafadhili zilizofikia 90% ya fedha zote zilizotolewa kwa ajili ya kugharamia miradi ya umwagiliaji kuanzia mwaka 2014/15 hadi 2017/18.

x. Ugazi ulibaini Maafisa Ugani hawakuwezeshwa na nyenzo na maarifa ya kisasa kuhusu utoaji wa huduma za ugani ili kuwapa ujuzi wa mbinu mpya.

xi. Ugazi ulibaini udhaifu katika mchakato wa bajeti. Shughuli za ugani zilitengewa kiasi kidogo cha fedha na baadhi ya fedha zilizotengwa zilitumika kwenye shughuli nyingine. Utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima ni muhimu kwa ajili ya uzalishaji wa kilimo kwa sababu ina uwezo wa kubadilisha changamoto zingine zote ili kuboresha maisha na ustawi wa wananchi. Huduma za ugani, utafiti na mafunzo zina umuhimu katika kuunganisha wakulima kupata teknolojia mpya, taarifa na ujuzi ambao ni muhimu katika kuimarisha uzalishaji wa Kilimo.

xii. Ilibainika pia kwamba ni asilimia 1 tu ya wakulima ndio walipewa mafunzo ya mbinu bora za kilimo.

xiii. Ilibainika kuwa Maafisa Ugani hawakuwa wanapatiwa mafunzo vizuri, wengi walikuwa wanategemea elimu walizopata vyuoni.

xiv. Ukaguzi ulibaini kwamba ni 9% tu ya wajasiriamali wakiwemo wasindikaji wa mazao ya kilimo na wenye viwanda vidogo waliosajiliwa na shirika la maendeleo la viwanda vidogo walipatiwa mafunzo huku 37% hawakupata Mikopo licha ya kukidhi vigezo.

xv. Kwenye Mbegu na Mbolea imebainika kwamba kutosambazwa kwa wakati kwa pembejeo husababishwa na uwezo mdogo wa wazalishaji wa ndani kuzalisha pembejeo za kilimo hapa nchini. Uzalishaji wa ndani husaldia upatikanaji kwa wakati wa pembejeo ikilinganishwa na uingizaji wa pembejeo kutoka nje ambao huchukua muda mrefu kwa sababu inajumuisha mchakato wa manunuizi, usafirishaji na usambazaji mikoani kutokea kwenye mipaka iingayo nchini.

xvi. Uzalishaji mdogo wa Mbegu bora wa wakala wa Mbegu ni matokeo ya kukosekana kwa mashamba ya Mbegu yenye tija. Ilibainika kwamba ni shamba 1 tu la Mbegu kati ya mashamba 9 yanayozalisha mbegu ndio lina uwezo wa kuzalisha mbegu katika kipindi cha mwaka mmoja. Shamba hilo pekee ndio limewekewa mifumo ya umwagiliaji wakati mashamba mengine 8 yanategemea mvua kuzalisha mbegu.

xvii. Kwa kipindi cha mwaka 2015-2018, Wakala wa Mbegu uliweza kuzalisha kwa kiwango cha juu cha msimu ambacho ulizalisha asilimia 2.2 ya malengo waliojiwekea wa kuzalisha tani 36,000.

xviii. Bei za pembejeo ziko juu sana, hali iliyosababishwa na Serikali kushindwa kutekeleza makubaliano ya utoaji ruzuku kwa wakulima. Ilibainika makubaliano yalikuwa ni kulipia

asilimia 50 ya gharama za pembejeo (Sh. 200,000) kama ruzuku. Hata hivyo ilibainika kwamba Serikali ilitoa kiasi cha shilingi 78,500 kama mchango wake ambao ni sawa na 39% ya gharama za pembejeo. Hivyo wakulima kutakiwa kuchangia 61% badala ya 50% ya bei ya soko. Gharama za kununua pembejeo zilikuwa zikaribiana na kipato ambacho mkulima hukipata baada ya kuuza mazao yake.

**46. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili itawezaje kufikia malengo yake ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kipato cha katikupitia mageuzi ya viwanda ikiwa imeshindwa kuihudumia Sekta ya Kilimo ambayo ndiyo mzalishaji mkubwa wa malighafi za viwanda? Aidha, Serikali ilieleze Bunge, ni kwanamna gani kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa ikiwa bajeti yake ya maendeleo na hususan kilimo cha umwagiliaji ni tegemezi kwa fedha za nje kwa asilimia 90?

#### **(b) Sekta ya Afya**

**47. Mheshimiwa Spika**, ukienda kwenye Sekta ya Afya – ambayo ndiyo sekta inayoshikilia sekta nyingine kwa maana kutoa hakikisho la nguvu kazi yenye afya (healthy labourforce); hali ni mbaya zaidi. Kwa mfano, Bajeti nzima ya Afya ilipungua kutoka shilingi trillioni 1.07 mwaka 2017/18 mpaka kufikia shilingi billioni 866.233 mwaka 2018/19 ikiwa ni anguko la shilingi billioni 211.468 sawa na asilimia 19.622.

**48. Mheshimiwa Spika**, ukiachilia mbali kuporomoka kwa bajeti ya afya; bado utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwenye sekta ya afya umekuwa kizungumkuti! Kwa mujibu wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Sekta ya Afya ni kwamba kwa mwaka wa fedha 2018/2019 fedha za miradi ya maendeleo kwenye sekta ya afya zilizokuwa zimetolewa hadi kufikia Machi, 2019 zilikuwa ni asilimia 16 tu! Hii ni sawa na kusema kwamba bajeti ya maendeleo katika sekta ya afya haikutekelezwa kwa asilimia 84 kwa mwaka husika.

**49. Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2019/20 wizara ya Afya ilitengewa jumla ya shilingi billioni 544.137; lakini hadi

kufikia mwezi Machi, 2020 kiasi cha fedha kilichokuwa kimetolewa ni shilingi bilioni 83.066 sawa na asilimia 15.3 tu ya bajeti ya maendeleo. Aidha katì ya fedha zilizotolewa, fedha za ndani ni asilimia 9.2 na za nje ni asilimia 21.

**50. Mheshimiwa Spika**, sambamba na utekelezaji duni wa bajeti ya afya, bado lipo tatizo la muda mrefu la Serikali mosi, kutopeleka kikamilifu fedha za MSD ziliyoidhinishwa na Bunge na pili kutolipa madeni ya Bohari Kuu ya Dawa (MSD) jambo ambalo limekuwa na athari kubwa katika ufanisi wa Bohari hiyo. Kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabau za Serikali ya 2018/19 deni la Serikali limeongezeka kwa kiasi cha shilingi bilioni 16.18 kutoka shilingi bilioni 37.45 za mwaka uliopita na hivyo kufanya jumla ya deni kuwa shilingi bilioni 53.63. Hali hii imesababisha ukwasi wa Bohari Kuu ya Dawa kuzidi kudidimia hali inayoweza kuathiri utekelezaji wa mipango mbalimbali ikiwamo usambazaji wa dawa na vifaatiba kwa jamii pamoja na utekelezaji wa mipango yake mbalimbali. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaungana na CAG kuitaka Serikali ilipe madeni yake kwa Bohari Kuu ya Dawa kikamilifu na kwa wakati, ili kuleta tija katika utendaji na kuongeza wigo wa usambazaji wa dawa na vifaatiba kwa jamii na hasa katika kipindi hiki ambacho taifa linakabiliwa na mlipuko wa ugonjwa wa COVID - 19.

**(c) Sekta ya Viwanda na Biashara**

**51. Mheshimiwa Spika**, mgawo wa fedha za maendeleo katika Sekta ya Viwanda na Biashara kwa miaka mitatu iliyopita ilikuwa kama ifuatavyo; Mwaka 2016/17 fedha iliyotolewa ilikuwa ni asilimia 44; 2017/18 asilimia 9.51; na 2018/19 asilimia 6.5. Ukitafuta wastani wa utekelezaji wa bajeti katika sekta hii kwa miaka tajwa utagundua kwamba bajeti ya maendeleo katika sekta ya viwanda na biashara imetekelezwa kwa kwa asilimia 20 tu kwa miaka yote minne ya utekelezaji.

**(d) Sekta ya Maji**

**52. Mheshimiwa Spika**, kwenye sekta ya maji mgawo wa bajeti ya maendeleo ulikuwa kama ifuatavyo; Mwaka 2016/

17 asilimia 25; mwaka 2017/18 asilimia 22, mwaka 2018/19 asilimia 15 na 2019/2020 asilimia 61.9

**53. Mheshimiwa Spika**, mbali na utekelezaji duni wa bajeti ya maendeleo katika sekta ya maji; ukaguzi wa ufanisi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika mwaka wa fedha 2018/19 ulibaini kuwa sekta ya maji inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- i. zaidi ya 30% ya skimu za maji vijijini hazikufanya kazi vizuri (uk.5 ripoti)
- ii. 9% ya idadi ya watu nchini ndio wamefikiwa na maji taka. Kati ya 72% ya watu wanaopata maji mijini 9% wako kwenye mfumo wa maji taka. 91% wanategemea magari au maji ya vyoo kuririka mtaani
- iii. Ni asilimia 58.7 tu ya watu wanaoishi vijijini wanapata maji safi na salama
- iv. Miundombinu ya maji ilijengwa bila ya kuwa na vyanzo vya uhakika
- v. Kati ya sampuli 6615. Sampuli 709 (10%) hazikuwa na viwango vya kutumiwa na binadamu (Sampuli hizo zilibainika kuwa na chuma, madini ya manganizi, fluoride, nitrate, vimelea vya magonjwa nk)
- vi. Kulikuwa na Makandarasi wasiokuwa na sifa na uwezo wa kutekeleza miradi ya maji na pia hakukuwa na uhakiki wala tathmini ya uwezo wa makandarasi.
- vii. TAMISEMI na Wizara ya Maji haina mikakati endelevu ya kutenga bajeti kwa ajili ya miradi ya maji. Aidha Wizara ya Maji inapokea chini ya 41% (wastani kwa mwaka) wa bajeti ya maendeleo.
- viii. Kutokukamilika kwa miradi ya maji iliyoanzishwa na pia kuongezeka kwa riba kutohana na kucheleweshwa kwa malipo kwa wakandarsi.

ix. Serikali bado haijafikia malengo ya kuhakikisha kuwa wananchi wanapata maji safi na huduma bora za usafi wa mazingira ili kuboresha maisha yao

x. Kwa miaka mitatu mfululizo (2010/11-2013/14) miradi ya maji iligharimu 27% ya bajeti ya manunuzi ya nchi. Takribani trillioni 2.8 zilitumika kwenye miradi ya maji. Hata hivyo 46% ya miradi iliyotekelawa haikufanya kazi kama ilivyokusudiwa.

**54. Mheshimiwa Spika**, hizi ni Wizara mbili tu kama mfano, lakini ukifanya tathmini ya utoaji wa fedha za maendeleo kwa Wizara nydingine hali ni hiyo hiyo. Hakuna Wizara inayopata fedha zote za maendeleo kwa asilimia 100. Kwa mwenendo huo, hakuna muujiza wowote unaweza kutendeka ili mipango yetu ya maendeleo iweze kutekelezwa kwa ufanisi, ikiwa Serikali haitoi fedha zote za maendeleo kama zilivyoldhinishwa na Bunge na kwa wakati.

**xix. Matumizi ya Fedha nje ya Mpango wa Bajeti (Budget Reallocation):-**

**55. Mheshimiwa Spika**, kama nilivyosema hapo awali, ili mpango wowote wa maendeleo uweze kutekelezwa unahitaji bajeti; lakini hilo halitoshi; inahitajika pia nidhamu ya matumizi ya bajeti hiyo. Kama mpango umeainisha mambo kumi ya kutekeleza na ikatengwa bajeti ya kutosha kutekeleza mambo hayo kumi; kutumia fedha yoyote katika bajeti hiyo kwa ajili ya kutekeleza mambo mengine ambayo hayakuwa yameainishwa katika Mpango husika; huko ni kuuvuruga Mpango; na huko ni kukosa nidhamu ya matumizi ya bajeti iliyokuwa imepangwa kwa ajili ya kuutekeleza mpango husika.

**56. Mheshimiwa Spika**, hali kama hiyo inapotokea; inakuwa vigumu sana kufikia malengo ya Mpango uliokusudiwa kwa kuwa unakuwa umeshavurugwa tayari kwa kuingiza mambo mengine ambayo hayakuwepo awali.

**xx. Kukosekana kwa Uwajibikaji katika Masuala ya Fedha**

**57. Mheshimiwa Spika**, pamoja na mambo mengine yote, uwajibikaji ni sifa ya msingi kabisa inayopelekea ufanisi katika

utekelezaji wa Mpango wowote wa Maendeleo. Wanazuoni wa mausala ya utawala bora wanasema kwamba; naomba kunukuu "**Accountability is the obligation of power holders to take responsibility for their actions**". Hii maana yake ni kwamba, uwajibikaji ni ile hali ya wenye madaraka kutambua kwamba wamekosea na kuchukua hatua ya kuwajibika kwa makosa waliyoyafanya.

**58. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikipigia sana kelele suala hili la uwajibikaji katika masuala ya fedha kutokana na kitendo cha Serikali kuonekana dhahiri ikikwepa kuwajibika katika mchakato mzima wa usimamizi wa Mipango ya Maendeleo.

**59. Mheshimiwa Spika**, kwa miaka yote mitano ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo na kwa miaka yote minne ya utekelezaji wa Mpango wa Pili; Kambi Rasmi ya Upinzani ilionyesha jinsi Serikali inavyokwepa uwajibikaji katika kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo; Mosi, kwa kushindwa kuleta Muswada Bungeni kwa ajili ya kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo kama Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba inavyoelekeza; lakini pili, kwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Bajeti ili kuondoa vipengele vilivyokuwa vinaibana Serikali kuwajibika katika masuala ya fedha.

**60. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani ilieleza kwamba; *kitendo cha Serikali kuifanya marekebisho sheria ya bajeti ambayo inatoa mwongozo wa uwajibikaji wa kifedha/kibajeti (financial accountability) katika kutekeleza miradi ya maendeleo ni uthibitisho tosha wa Serikali kukwepa uwajibikaji.*

**61. Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kwamba, mwaka 2018, Serikali ililetu mapendekezo ya kuvifanya marekebisho vifungu vya 41, 53, 56, 57 na 63 vya sheria ya bajeti ya 2017 kwa kuondoa wajibu wa Serikali wa kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Bungeni ripoti ya matumizi ya fedha kwa kila robo mwaka ya mzunguko wa bajeti (yaani kila baada ya miezi mitatu) ambapo sasa ripoti

hiyo itakuwa ya nusu mwaka wa mzunguko wa bajeti (yaani kila baada ya miezi sita).

**62. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani ilieleza kwamba; athari za marekebisho hayo ya sheria ya bajeti ilikuwa ni kudumaza ufuatiliaji thabiti (tight follow-up) wa utekelezaji wa bajeti ya Serikali; na jambo hilo linaweza kupelekea utekelezaji mbovu wa bajeti kutokana na matumizi yasiyofaa au hata ubadhirifu wa fedha za umma. Sababu ya kueleza hivyo ilitokana na ukweli kwamba; ikiwa ripoti ya matumizi ya Serikali itatolewa kwa kila nusu mwaka wa utekelezaji wa bajeti, maana yake ni kwamba, ripoti hiyo itatoka wakati mchakato wa maandalizi ya mpango wa maendeleo na bajeti ya mwaka wa fedha unaofuata ukiwa umeshaanza. Kwa hiyo, ripoti hiyo inakuwa haisaidii katika kufanya tathmini ya utekelezaji wa bajeti katika mwaka wa fedha unaoendelea (current financial year) ili hatimaye kuweza kufanya makisio na maoteo ya bajeti inayofuata.

**63. Mheshimiwa Spika**, Kwa minajili ya kuwa na tija katika Mapendekazo ya Mpango wa Maendeleo; Kambi Rasmi ya Upinzani ilishauri na kupendekeza kwamba; Serikali ilete muswada wa marekebisho ya sheria ya bajeti ili kurejesha vile vifungu vilivyokuwa vinaelekeza ripoti za matumizi ya fedha ziwe zinaletwa kila baada ya miezi mitatu (robo mwaka). Kwa kufanya hivyo, kwanza kutakuwa na ufuatiliaji madhubuti wa matumizi ya Serikali, lakini pia ripoti za robo mwaka, zitawezesha kufanya tathmini ya mwenendo wa utekelezaji wa bajeti na hivyo kuisadia Serikali kujipanga vizuri zaidi kwa bajeti zinazofuata”.

#### **C. SERIKALI IFANYE MAPITIO YA MAKISIO YA BAJETI DHIDI YA VYANZO HALISI VYA MAPATO NA UWEZO WA MAKUSANYO YA MAPATO**

**64. Mheshimiwa Spika**, kwa miaka minne mfululizo; Serikali imekuwa ikifanya makisio makubwa ya bajeti bila kuoanisha makisio hayo na vyanzo halisi vya mapato na pia uwezo wake wa kukusanya mapato; jambo ambalo limesababisha Serikali kushindwa kufikia lengo la makusanyo kwa miaka yote.

**65. Mheshimiwa Spika**, ukifanya tathmini ya miaka minne iliyopita, utaona kwamba kuna tatizo kubwa kwenye ukusanyaji wa mapato. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2016/17 Serikali ilipanga kukusanya kiasi cha shilingi trillioni 29.54<sup>1</sup> lakini iliweza kukusanya mapato kutoka vyanzo vyote yaliyofikia shilingi trillioni 20.7<sup>2</sup> sawa na asilimia 70.1 ya lengo. Hii ina maana kwamba, asilimia takriban 30 iliyobaki (sawa na shilingi trillioni 8.83) ilikuwa ni nakisi ya bajeti husika na kwa maana hiyo bajeti ya mwaka husika haikutekelezwa kwa asilimia 30. Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/18 Serikali ilipanga kukusanya jumla ya shilingi trillioni 31.71<sup>3</sup> lakini iliweza kukusanya kiasi cha shilingi trillioni 21.89<sup>4</sup> sawa na asilimia 69 ya lengo. Hii ina maana kwamba, asilimia 31 iliyobaki (sawa na shilingi trillioni 9.82) ilikuwa ni nakisi ya bajeti na kwa maana hiyo, bajeti ya mwaka husika haikutekelezwa kwa asilimia 31.

**66. Mheshimiwa Spika**, katika muktadha huohuo, katika mwaka wa Fedha 2018/19 Serikali ilipanga kukusanya shilingi trillioni 32.47 hata hivyo iliweza kukusanya shilingi trillioni 28.8 sawa na asilimia 79.1 ya lengo. Hivyo kiasi cha shillingi trillioni 6.65 hakikukusanya ikiwa ni sawa na asilimia 20.1 ya

**67. Mheshimiwa Spika**, ukiachilia mbali tatizo la kufanya makisio makubwa kuliko vyanzo halisi vya mapato; uwezo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) nao umekuwa ni changamoto. Kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali uwezo wa TRA kukusanya mapato ya kodi umekuwa na mserereko wa kushuka. Mathalani kwa mwaka fedha 2018/19, Mamlaka ya Mapato ilikadiria kukusanya mapato ya kodi jumla ya shilingi trillioni 18.297 lakini iliweza kukusanya shilingi trillioni 15.744 tu ikiwa ni pungufu ya shilingi trillioni 2.552 ambazo ni sawa na asilimia 14 ya malengo.

---

<sup>1</sup> Rejea Hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango wakati akiwasilisha Bajeti Kuu ya Seriakali kwa Mwaka wa Fedha 2016/17

<sup>2</sup> Ibid.

<sup>3</sup> Hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango akiwashilisha Bungeni Bajeti Kuu ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/18

<sup>4</sup> Ibid.

**68. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka uliotangulia 2017/18; hali ilikuwa hivyo hivyo. Kwa mwaka huo, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilikusanya jumla ya **shilingi trilioni 15.386** ikiwa ni pungufu ya **shilingi trilioni 1.929** ya lengo la kukusanya **shilingi trilioni 17.315**. Upungufu huo ni sawa na **asmilimia 11** ya lengo<sup>5</sup>.

**69. Mheshimiwa Spika**, taarifa ya CAG ya mwaka 2017/18 inaonyesha kwamba; idara zote tatu za mapato zilishindwa kufikia malengo kwa mwaka wa fedha 2017/18. Taarifa hiyo inaonesha kwamba Idara ya walipa kodi wakubwa ilikusanya **asilimia 41** ya makusanyo yote ambayo ndiyo sehemu kubwa kuliko idara zote; ikifuatiwa na Idara ya Forodha yenye **asilimia 40** na idara ya kodi za Ndani yenye **asilimia 19** ambayo ndiyo ya mwisho kwa mwaka wa fedha 2017/2018, makusanyo haya hayahusishi vocha ya misamaha ya kodi kutoka Hazina.

**70. Mheshimiwa Spika**, kwa masikitiko makubwa, taarifa ya CAG ya mwaka 2018/19 imeendelea kuonyesha udhaifu huo wa idara kushindwa kufikia malengo yake ya makusanyo. Taarifa hiyo inaonyesha kwamba, kwa mwaka wa fedha 2018/19 Idara ya Forodha na Ushuru wa bidhaa iliongoza kwa kukusanya asilimia 40.2 ya mapato yote; ikifuatiwa na Idara ya Walipakodi wakubwa iliyokusanya asilimia 39.8 na Idara ya Kodi za Ndani iliyokusanya asilimia 20. Makusanyo haya hayahusishi vocha za misamaha ya kodi kutoka Hazina.

**71. Mheshimiwa Spika**, Kutokana na mchanganuo huo, ni dhahiri kuwa mchango wa makusanyo kutoka Idara ya Mapato ya Ndani umekuwa nyuma ikilinganishwa na idara nyingine. Aidha, taarifa hiyo inaonyesha kuwa mwelekeo wa makusanyo ya mapato kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kwa wastani, ulikuwa chini ya makadirio yaliyoidhinishwa, isipokuwa kwa mwaka wa fedha 2015/16 wakati wa Serikali ya awamu ya nne ndipo makusanyo halisi yalikuwa juu ya makadirio kwa **asilimia 0.13. Kwa hiyo**,

---

<sup>5</sup> Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/18

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Taarifa hiyo ya CAG, ni dhahiri kwamba Serikali ya awamu ya tano imeshindwa kufikia malengo ya makusanyo ya mapato kadiri ya mpango iliyojivekea jambo linalotoa picha kwamba Mpango wa Taifa wa Maendeleo haujatekelezwa kikamilifu kutokana na upungufu wa fedha unaotokana na makusanyo kidogo.

**72. Mheshimiwa Spika**, uwezo mdogo wa TRA kukusanya kodi unafahamika pia kimataifa. Ripoti ya CAG inasema kwamba; Mchanganuo linganifu wa ufanisi wa kodi kwa nchi za Afrika Mashariki unaonesha kwamba, Tanzania ilishika nafasi ya mwisho katika ukusanyaji mapato kwa mwaka wa fedha 2017/18. Kambi Rasmi ya Upinzani inaionya Serikali kuacha kujitapa kuwa ina uwezo mkubwa wa kukusanya mapato wakati tafiti zimeonyesha kuwa ina uwezo mdogo na badala yake ijielekeze kutekeleza mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tuliyoyatoa siku nyingi.

**73. Mheshimiwa Spika**, mapendekezo hayo ni pamoja na kuongeza wigo wa vyanzo vya kodi, kudhibiti mianya ya upotevu wa kodi na kuwapa motisha walipa kodi, ili kuongeza ulipaji kodi kwa hiari.

#### **D. MAREKEBISHO YA MPANGO WA BAJETI KUKABILIANA NA MADHARA YA JANGA LA CORONA (BUDGET ADJUSTMENT TO MITIGATE THE EFFECTS OF COVID 19 PANDEMIC)**

**74. Mheshimiwa Spika**, ni ukweli usiopingika kwamba; wakati Serikali inapanga bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021; kulikuwa hakuna janga la Corona hapa nchini; na kwa sababu hiyo, bajeti hii haikuzingatia kwa mapana yake, madhara ya Corona katika uchumi jumla wa Taifa na uchumi wa kila mwananchi. Hata hivyo, baada ya Corona kubisha hodi hapa nchini; hakuna ubishi tena kuwa janga hilo limeathiri kwa kiwango kikubwa uchumi wa nchi yetu na maisha ya mwananchi mmoja mmoja. Hii ni kwa sababu ya kupungua kwa mapato ya Serikali kutokana na kupungua au kusimama kwa biashara nyingi hususan katika sekta ya utalii, usafiri wa anga na uwekezaji wa mitaji kutoka nje. Mtikisiko huo wa kiuchumi umesababisha pia kupungua kwa

ajira za moja kwa moja na zile ambazo si za moja kwa moja na hivyo kuathiri kipato cha mtu mmoja mmoja (per capita income)

**75. Mheshimiwa Spika**, katika mazingira kama hayo ambapo uchumi umetikisika na katika mazingira ambayo Taifa halikuwa na maandalizi ya mtikisiko huo; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba Serikali ifanye marekebisho ya bajeti (adjustment) ili iendane na mazingira ya sasa ya janga la corona ambapo mapato ya Serikali yameshuka na yanategemewa kuendelea kushuka ikiwa gonjwa hili litaendelea. Kwa mujibu wa Hotuba ya Waziri wa Fedha wakati anasoma taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ni kwamba ukuaji wa Pato la Taifa unatarajiwa kupungua kidogo kutoka maoteo ya awali ya asilimia 6.9 hadi 5.5.

**76. Mheshimiwa Spika**, ili Serikali iweze kuendelea kugharamia huduma za kijamii kwa kiwango cha kuridhisha na wakati huo huo kuweza kupambana na gonjwa la corona; Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba miradi yote ya maendeleo ambayo haina masharti ya mkataba na ambayo kutotekelzwa kwake kwa mwaka wa fedha 2020/21 hakutakuwa na madhara yoyote ya kiuchumi au kijamii isimame kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuelekeza nguvu kwenye sekta za huduma za jamii ambazo zimeathiriwa na janga la corona na ambazo zina uhusiano wa moja kwa moja na maisha ya wananchi ya kila siku. Aidha, Serikali ifanye mapitio ya Bajeti ya Matumizi Mengineyo katika idara na vitengo mbalimbali vya Serikali ili kupunguza fedha katika matumizi ambayo si ya lazima ili fedha hizo zielekezwe kwenye sekta ya huduma za jamii ambazo zimetikiswa na COVID – 19.

#### **E. HATUA ZA ZIADA ZA KUCHUKUA KUNUSURU KUPOROMOKA KWA UCHUMI KUFUATIA ATHARI ZA JANGA LA CORONA**

**77. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua na inaheshimu hatua zilizochukuliwa na Benki Kuu kupunguza Kiwango cha Kisheria cha Hifadhi ya Fedha katika mabenki kutoka asilimia 7 mpaka 6 ili kuongeza uwepo wa

fedha katika benki; kushusha punguzo la riba kutoka asilimia 7 mpaka 5 ili kutoa unafuu kwa mabenki ya biashara kukopa Benki Kuu kwa gharama nafuu na kwa sababu hiyo mabenki hayo kukopesha kwa riba nafuu zaidi kwa wateja wao; Kushusha viwango vya amana za Serikali kupitia hati fungani ili kuongeza uwezo wa mabenki kukopa katika Benki Kuu kwa kuweka amana kidogo kuliko ilivyokuwa hapo kabla na pia kuzielekeza taasisi za fedha kufanya marekebisho ya mifumo ya utoaji mikopo, riba na urejeshaji wa mikopo ili kuendana na mazingira ya sasa ambapo COVID 19 imeathiri shughuli nyingi za kiuchumi.

**78. Mheshimiwa Spika**, hatua hizo ni njema kwa kuwa zinalenga kunusuru mabenki kuanguka. Hatua hivyo zimelenga zaidi kunusuru taasisi za fedha zisishindwe kuijidesha; lakini kwa upande wa wajasiriamali wadogo, wafanyabiashara na mwananchi mmoja mmoja hatua hizo zinaweza zisiwe na tija sana. Hii ni kwa sababu baada ya mtikisiko wa uchumi, wengi wa wajasiriamali na wafanyabiashara wanaogopa kwenda kukopa benki kwa kuwa biashara hazitabiriki na hivyo kuna hofu ya kushindwa kufanya marejesho na amana zao kuchukuliwa.

**79. Mheshimiwa Spika**, kutohana na tishio la Virusi vya Corona katika uchumi; nchi nyingi duniani zimechukua hatua madhubuti kuzuia chumi zao zisianguke. Mathalani nchi jirani ya Rwanda katika kukabiliana na hali hiyo, mamlaka ya nchi hiyo imetangaza hatua kadhaa kukabiliana na kupanda kwa bei kiholela. Kwa mujibu wa tovuti ya Rfi<sup>6</sup> Benki Kuu ya Rwanda imetangaza kupunguza masharti ya ulipaji wa mikopo ya benki kwa kampuni na watu walioathirika na ugonjwa wa Covid-19. Ili kufanikisha mpango huo, karibu Euro milioni 50 zimetolewa kwa benki za biashara, ambazo zitahitaji ukwasi zaidi. Aidha, ili kuzuia maambukizi ya virusi kupitia biashara ya fedha (kutoa na kupokea fedha), mamlaka pia imesitisha ada ambayo ilikuwa ikitozwa kwa kutoa fedha kupitia mfumo wa kidijitali ili kuwavutia watu wengi zaidi kutumia mifumo ya

---

<sup>6</sup><http://www.rfi.fr/sw/afya-mazingira/20200320-rwanda-yachukua-hatua-za-kiuchumi-kukabiliana-na-ugonjwa-wa-covid-19>

kielekroniki zaidi katika miamala ya kifedha kuliko fedha taslimu. Hatua hizo zinalenga kupunguza athari za Covid-19 kwenye uchumi wa Rwanda. Kwa mujibu wa Mamlaka ya Mapato ya Rwanda, sekta ya utalii imeathiriwa zaidi na mlipuko wa COVID 19, ambapo matukio takribani 20 ya kitalii yaliyokuwa yamepangwa kufanyika mwezi Machi na Aprili, 2020 yamesogezwa mbele, na hivyo kusababisha nchi hiyo kupoteza Euro milioni 7.

**80. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Kenya nayo imetangaza hatua za kunusuru uchumi kipindi hiki cha janga la Corona. Kwa mujibu wa taarifa ya Rais Kenyatta kwa wananchi wa Kenya ni kwamba, ili kulinda ajira kwa wananchi na kuwapa waajiri uhakika wa kutopata hasara; Serikali ya Kenya imetoa nafuu ya kodi ya mapato kwa asilimia 100 kwa wafanyakazi wote wenye pato ghafi lisilozidi shillingi za Kenya 24,000/= kwa mwezi (kwa hapa kwetu ingekuwa takribani shilingi za kitanzania 524,000/=. Hii imekwenda sambamba na kupunguza kodi ya mapato (Kulingana na mtu anavyopata – Pay As You Earn) kutoka ukomo wa kiwango cha juu cha asilimia 30 hadi asilimia 25 na kodi nyingine za mapato.

**81. Mheshimiwa Spika**, hatua nyine kubwa iliyochukuliwa na Serikali ya Kenya ni kupunguza Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kutoka asilimia 16 hadi asilimia 14 kuanzia mwezi Aprili, 2020. Hatua hii imekwenda sambamba na Mamlaka ya Mapato ya Nchi hiyo (KRA) kutakiwa kuharakisha kulipa kiasi kilichohakikiwa cha shilingi za Kenya Bilioni 10 za madai ya marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT refund claims) kwa wafanyakabiashara ili kuhakikisha kwamba kuna mzunguko wa fedha wa kutosha katika biashara.

**82. Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua nyine nyangi za kiuchumi ambazo Kenya imechukua kukabiliana na janga la Corona, Rais Kenyatta amependekeza punguzo la mishahara kwa hiari kwa viongozi wakuu wa Serikali kama ifuatavyo:- Rais na Makamu wa Rais asilimia 80, Mawaziri asilimia 30 na Makatibu Wakuu wa Wizara asilimia 20.

**83. Mheshimiwa Spika**, si nia yangu kuishawishi Serikali yetu kuiga hatua walizochukua wenzetu, lakini ni Wajibu wa Serikali kuhakikisha Taifa usalama wa uchumi hasa kipindi cha janga hili. Serikali inatakiwa kuwa na '*interest*' kwenye jambo hili zaidi kuliko hata jumuiya ya wafanyabiashara; kwa kuwa endapo kutatokea anguko la kiuchumi, Serikali ndiyo itakayokuwa ya kwanza kushindwa kuendesha nchi.

**84. Mheshimiwa Spika**, katika mazingira kama hayo; Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza hatua za ziada kuchukuliwa ili kunusuru biashara na mitaji ya wajasiriamali na wafanyabiashara pamoja na kipato cha wafanyakazi kwenye taasisi za umma na binafsi visiyumbe na kuhakikisha kwamba kunakuwa na ukwasi wa kutosha katika mzunguko wa fedha.

**i. Serikali Irejeshe Madai ya Kodi kwa Wafanyabiashara (Tax Refunds)**

**85. Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na malalamiko mengi sana kutoka kwa jamii ya wafanyabiashara kuhusiana na kutorejeshewa fedha zao za kodi na hususan ongezeko la asilimia 15 ya ushuru wa forodha ambao hulipwa kabla kwa ajili ya kuagiza sukari ya viwandani toka nje ya nchi. Utafiti uliofanywa na Shirikisho la Wamiliki wa Viwanda - CTI kwa viwanda na makampuni mbalimbali ya biashara ulibaini uwepo wa tatizo kubwa la uhaba wa fedha unaovikabili viwanda na makampuni mengi ya biashara kutokana na uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi na pia uuzaaji wa bidhaa nje ya nchi kutokana na Mamlaka ya Mapato Tanzania - TRA kutorejesha madai ya kodi hiyo kwa viwanda na makampuni yanayofanya biashara ya kimataifa.

**86. Meshimiwa Spika**, biashara nyingi ambazo zilitokuwa zimeathirika ni zile ambazo zimesajiliwa katika mfumo wa Kodi ya Ongezeko la Thamani-VAT, kama vile sekta ya madini, ujenzi, kilimo na kampuni nyingine za biashara zinazomilikiwa na wazawa na zile zinazotoka nje lakini zikifanya shughuli zake hapa nchini. Utafiti ulilenga kuangalia madhara ya kutokurejeshwa kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani-VAT, Ushuru wa Forodha - Import Duty na madai mengine ya

marejesho ya kodi kwa mfano asilimia 15 ya nyongeza ya Ushuru wa Forodha. Aidha, utafiti ulilenga kuainisha athari za kiuchumi za ucheleweshaji wa marejesho hayo ya kodi sambamba na kuangalia kiasi halisi kinachodaiwa na viwanda na wafanyabiashara mbalimbali ambao ni wanachama wa CTI.

**87. Mheshimiwa Spika**, matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa viwanda na biashara kampuni nyingine za biashara hazikuwa zimerejeshwa fedha za kodi kwa kipindi cha miaka miwili hadi mitatu iliyopita; na sekta zilizoongoza kwa madai ni sekta za ujenzi, madini, biashara ya huduma na bidhaa, na makampuni ya uagizaji na uuzaaji wa bidhaa za viwandani nje ya nchi pamoja na sekta ya Kilimo.

**88. Mheshimiwa Spika**, taarifa hiyo inaonesha kuwa marejesho ya kodi yaliyofanyika kwa kipindi cha miaka minne ya fedha yalikuwa ni shilingi trilioni 1.52 wakati madai halisi ambayo yalikuwa hayajalipwa (outstanding refunds) yalikuwa ni shilingi trilioni 2.3. Hii maana yake ni kwamba kiasi kikubwa cha madai ya kodi kilikuwa hakijalipwa kwa wafanyabiashara. Utafiti huo ulibaini pia kwamba, kiasi hicho cha madai ya kodi hakikingizwa kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2018/19 ili kilipwe jambo ambalo linaashiria kwamba deni hilo lipo na litaendelea kuwepo.

**89. Mheshimiwa Spika**, utafiti wa CTI, ulibaini pia kwamba ulipaji wa madai ya marejesho ya kodi una mwelekeo wa kushuka na pia fedha zinazotengwa kwa ajili kulipa marejesho ya kodi zimekuwa zikipungua kwa miaka mitatu mfululizo iliyopita. Mwenendo huu wa kupungua kwa ulipaji wa marejesho ya kodi sambamba na kutotenga fedha za kutosha kulipa marejesho hayo umetajwa kama sababu mojawapo ya kuendelea kuongezeka kwa malimbikizo ya madai ya marejesho ya kodi ambayo yalifikia kiwango cha asilimia 7.2 ya bajeti yote ya mwaka wa fedha 2018/19<sup>7</sup>.

---

<sup>7</sup><https://www.cti.co.tz/articles/executive-summary-of-draft-report-study-on-delays-in-tax-refunds>

**90. Mheshimiwa Spika**, ucheleweshaji wa malipo ya madai ya Kodi ya Ongezeko la Thamani – VAT pamoja na madai ya asilimia 15 ya ushuru wa forodha unaolipwa kabla kwa ajili ya uagizaji wa sukari ya viwandani umekuwa na athari kubwa sana kwa wazalishaji wa viwandani na kwenye uchumi kwa jumla. Athari hizo ni pamoja na kama vile kuongezeka kwa madeni ya viwanda na uzalishaji, kuongezeka kwa riba, kutokana na mikopo toka kwenye mabenki kwani viwanda vinalazimika kukopa tena ili kulipa kodi ambazo zinatakiwa kulipwa. Matokeo yake ni kwamba viwanda vingi vinashindwa kufanya uwekezaji katika uzalishaji, jambo ambalo linasababisha kupunguza wafanyakazi, uzalishaji unashuka na hivyo badala ya uchumi kushamiri unaanza kusinyaa.

**91. Mheshimiwa Spika**, ni kutokana na sababu hizo ambapo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaishauri Serikali kuchukua na kutekeleza mapendekezo ya CTI,ili kunusuru anguko la viwanda vya uzalishaji na makampuni ya uuzaji na uagizaji wa bidhaa na huduma njeya nchi. Mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ilipe malimbikizo madai ya kodi (VAT na asilimia 15 ya ushuru wa forodha unaolipwa kabla) pamoja na riba kama iliyoelekezwa kwenye mwongozo wa marejesho ya madai hayo.

(b) Serikali iufute mara moja mfumo wa kulipa kabla asilimia 15 ya ushuru wa forodha kwa uagizaji wa sukari ya viwandani. Licha ya mfumo huo kuwa kikwazo kwa uzalishaji wa viwandani na kandamizi kwa makampuni yanayoagiza sukurari ya viwandani kutoka nje; mfumo huo hauna uhalali wa kisheria kwa kuwa haujatajwa popote katika sheria za Tanzania na kwa maana hiyo unakiuka taratibu na kanuni za kiforodha za Afrika Mashariki na pia unaongeza gharama za uzalishaji na kufanya mazingira ya biashara nchini kuwa magumu.

(c) Serikali ifungue Akaunti Maalum ya Akiba kwa ajili ya Kuweka Fedha za Kulipa madai ya Kodi kwa wafanyakabiashara.

**92. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba; Serikali ikirejesha kwa wafanyabiashara kiasi cha shilingi triliuni 2.3 ambacho ni madai ya kodi; uzalishaji wa viwandani utaongezeka; biashara zitaimarika hasa katika kipindi hiki ambacho biashara nydingi zimefungwa na wafanyakazi wamesimamishwa kazi kutokana na madhara Corona. Hivyo basi badala ya kutoa fedha taslimu kwa ajili ya kusaidia sekta ya viwanda na biashara (STIMULUS PACKAGE) Serikali iwarejeshee wafanyabiashara fedha zao za madai ya kodi ili wazitumie kuimarisha biashara zao na hivyo kuurudisha uchumi katika hali yake ya kawaida.

**ii. Serikali ilipe Madeni ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili Wastaifu waweze kulipwa Mafao yao na pia Kuiwezesha Mifuko ya Hifadhi Kujientesha**

**93. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ya CAG ya 2018/19 kuhusu Utendaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni kwamba Mfuko mpya wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) haujafanya tathmini ya hali ya mali na madeni (actuarial valuation); na pia kumekuwepo madai ya muda mrefu ya shilingi bilioni 171.91 ya michango katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

**94. Mheshimiwa Spika**, ukaguzi wa CAG ulibaini kuwa kuna hatari ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma kutolipwa kiasi cha shilingi bilioni 111.8 kilichowekezwa katika Benki ya Uwekezaji Tanzania kutokana na matatizo ya ukwasi yanayoikabili Benki hiyo.

**95. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa miaka mingi sasa imekuwa ikiitaka Serikali kulipa madeni ya mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili mosi, mifuko hiyo iweze kulipa mafao ya wastaifu kwa wakati lakini pia ili iweze kujientesha. Serikali kuendelea kutolipa madeni hayo ni kuwahujumu wastaifu na pia ni kuihujumu mifuko ya hifadhi ya jamii.

**i. Serikali ilipe Fao la Kukosa Ajira kwa Wafanyakazi wote ambao wamekidhi vigezo vya kisheria.** Tangu kuingia kwa janga la Corona nchini taasisi binafsi, zikiwemo shule binafsi zilisimamisha ajira. Kwa mujibu wa taarifa kutoka Chama cha Walimu wa Shule Binafsi (Tanzania Private Schools Teachers' Union); ni kwamba janga la Corona limesababisha walimu 89,475 kusimamishwa kazi na hivyo hawalipwi mishahara. Kwa hiyo, Serikali itumie Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi kuwalipa watumishi wote waliokosa ajira ana ambao wamekidhi vigezo vya kisheria fao la kukosa ajira ili waweze kumudu maisha yao.

#### **F. MFUKO MKUU WA HAZINA YA SERIKALI**

**96. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa ibara ya 135 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, makusanyo yote ya Serikali yanatakiwa kuwekwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Hata hivyo, licha ya maelekezo hayo ya kikatiba; imebainika kuwa utaratibu huo haufuatwi. Kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka wa fedha 2018/19 kati ya shilingi bilioni 659 ambazo ni makusanyo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, ni shilingi bilioni 105 tu ndizo zilithibitika kupokelewa na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

**97. Mheshimiwa Spika**, sambamba na hilo, kati ya shilingi trilioni 3.4 ambazo ni makusanyo yote ya mikopo ya nje ni shilingi trilioni 2.17 tu ambazo ziliripotiwa na Mfuko Mkuu wa Hazina. Hii ina maana kwamba, kiasi ambacho hakiripotiwa hakijulikani kilikwenda wapi na kwa kazi gani jambo ambalo linatoa taswira kwamba kuna uwezekano mkubwa wa uwepo wa ubadhirifu na ujisadi unaofanyika kwa kutopeleka makusanyo yote katika Mfuko Mkuu wa Hazina kama Katiba ya nchi inavyoelekeza. Na hii inadhihirishwa na uhalisia kwamba, jumla ya fedha zilizoripotiwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ni shilingi trilioni 24.2 lakini jumla ya fedha zilizotumika ni shilingi trilioni 26.6, na hivyo kuwa na nyongeza ya matumizi ya shilingi trilioni 2.3 ambayo hayakupita katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

**98. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili, ni kwanini haipeleki makusanyo yote kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina na ni kwanini inafanya matumizi ya fedha ambazo hazijapita katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

**G. DENI LA TAIFA NA HATMA YA UCHUMI WA NCHI**

**F1. Deni la Serikali**

**99. Mheshimiwa Spika**, Deni la Taifa, limeendelea kuwa kubwa kila mwaka jambo ambalo limekuwa na athari kubwa katika bajeti ya Serikali na hivyo kuathiri uchumi wetu na maisha ya wananchi kwa jumla.

**100. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2018/19; ni kwamba hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2019, deni la Serikali lilikuwa limefikia Shillingi **trillioni 53.1**. Kati ya fedha hizo, **shilingi trillioni 14.9** zilikuwa ni deni la ndani na **shilingi trillioni 38.2** zilikuwa ni deni la nje. Kwa mujibu wa ripoti hiyo, deni la Serikali limeongezeka kwa **shilingi trillioni 2.2** sawa na **asilimia 4.3** ikililinganishwa na deni la **Shilingi trillioni 50.9** liliropotiwa tarehe 30 Juni, 2018.

**101. Mheshimiwa Spika**, sababu zilizotolewa na CAG kuhusu ongezeko hili la deni la Serikali, ni mikopo kwa ajili ya kulipa mitaji na riba ya dhamana za Serikali za muda mfupi pamoja na mikopo kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

**102. Mheshimiwa Spika**, jedwali Na. 1 hapo chini linaonyesha mwenendo wa ukuaji wa deni kwa miaka minne iliyopita:-  
*Jedwali Na. 1. Mwenendo wa Ukuaji wa Deni la Serikali kwa miaka minne iliyopita*

	2015/16	2016/17	2017/18	2018/2019
<b>Shilingi Bilioni</b>				
Jumla ya Deni	41,039	46,081	50,927	53,105
Deni la Nje	29,846	32,746	36,194	38,241
Deni la Ndani	11,193	13,335	14,732.45	14,863

**Chanzo: CAG 2017/18 ; 2018/19**

**103. Mheshimiwa Spika**, ukiangalia mwenendo huo wa ukuaji wa deni utaona kwamba Serikali hii ya awamu ya tano inayojigamba kwamba haikopi nje, na kwamba inatumia fedha zake za ndani kuendesha miradi yake ya maendeleo, ilikuta deni la Serikali likiwa **shilingi triliioni 41.039** ilipoingia madarakani; ikaongeza deni hilo kwa **shilingi triliioni 5** hadi kufikia **shilingi triliioni 46.081** kwa mwaka wake wa kwanza tu madarakani. Aidha, katika mwaka wake wa pili madarakani, Serikali hii imeliongeza deni kwa shilingi kwa takribani **shilingi triliioni 5** nyingine hadi kufikia **shilingi triliioni 50.927**.

**104. Mheshimiwa Spika**, kana kwamba kuwa na madeni mengi ni sifa; Serikali hii, licha ya kuonywa na kupewa maanganizo mengi juu ya athari za kukopa kwingi kuliko uwezo wa kulipa; bado imeendelea kuongeza deni kwa takriban **shilingi triliioni 2** zaidi na sasa limefikia **shilingi triliioni 53 .105**.

**105. Mheshimiwa Spika**, deni la shilingi triliioni 53.105 ni sawa na asilimia 38.9 ya Pato la Taifa ambalo kwa sasa ni Dola za Kimarekani bilioni 59<sup>8</sup> ambazo ni sawa na **shilingi triliioni 136.504** kwa kiwango cha ubadilishaji fedha cha dola moja kwa **shilingi 2,313.63<sup>9</sup>**cha tarehe 14 Mei, 2020. Kiwango hiki cha deni ni kikubwa mno na kina mwelekeo wa kuiweka nchi rehani kwa kuwa kinakaribia kufikia nusu ya pato letu.

**106. Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameshaeleza kuwa sababu kubwa ya deni la taifa kuongezeka kwa kasi ni kuongezeka kwa mikopo ya ndani na nje – ambapo mikopo peke yake inachangia ukuaji wa deni kwa asilimia 77; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarejea tena ushauri wake ambao imekuwa ikiutoa

---

<sup>8</sup> Pato la Taifa kwa mwaka 2019 kama lilivyorekodiwa kwenye tovuti <https://tradingeconomics.com/tanzania/gdp> iliyosomwa tarehe 14 Mei, 2020.

<sup>9</sup> Hicho ni kiwango cha ubadilishaji fedha (exchange rate) cha dola moja ya marekani kwa shilingi ya Tanzania kwa tarehe 14 Mei, 2020 kama kilivyorekodiwa kwenye tovuti:

<https://www.xe.com/currencyconverter/convert/?Amount=1&From=USD&To=TZS>

miaka yote kuwa; mikopo yote ya Serikali iwe inaidhinishwa na Bunge kabla ya kukopa.

#### **F2. Deni la Sekta Binafsi**

**107. Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu sasa, Serikali imekuwa ikikwepa kuonyesha takwimu za Deni la Taifa kwa ujumla wake kwa maana ya Deni la Serikali na Deni la Sekta Binafsi ambalo hudhaminiwa na Serikali. Badala yake, Serikali imekuwa ikitoa takwimu za deni la Serikali pekee na kuuaminisha umma kuwa deni hilo ni himilivu.

**108. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwezi Aprili, 2020, jumla ya deni la nje kwa maana ya Deni la Serikali na Deni la Sekta Binafsi, liliifikia Dola za Kimarekani milioni 22,386.7 kwa rekodi ya mwezi Machi, 2020. Kiasi hicho ni sawa na **shilingi 51,825,210,500,000** (kwa kiwango cha kubadilsha fedha cha shillingi 2,315, kwa dola moja ya kimarekani) kama kilivyorekodiwa tarehe 10 Juni, 2020. Ukiondoa deni la Serikali la nje ambalo kwa mujibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni shilingi trilioni 38.241; deni la sekta binafsi la nje (ambalo ndilo lenye dhamana ya Serikali) litabaki kuwa **shilingi 13,584,210,500,000**

**109. Mheshimiwa Spika**, ili kupata takwimu halisi za deni la Taifa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imechukua jumla ya deni la Serikali (la nje na ndani) ambalo kwa sasa ni **shilingi trilioni 53.105** na kujumlisha na deni la sekta binafsi ambalo limefikia **shilingi trilioni 13.584** na kupata jumla ya Deni la Taifa kuwa **shilingi trilioni 66.689**

#### **F3. Uhimilivu wa Deni la Taifa**

**110. Mheshimiwa Spika**, ukifanya tathmini ya wastani wa makusanyo halisi ya mapato kwa miaka minne iliypita na fedha inayotengwa kila mwaka kulipa Deni la Taifa na mishahara ya wafanyakazi, utagundua kuwa Deni la Taifa si himilivu tena! Hii ni kwa sababu wastani wa makusanyo kwa miaka minne ilivopita ni shilingi trilioni 15<sup>10</sup>; ilihali fedha

---

<sup>10</sup>Vitabu nya makusanya ya Mapato ( Revenue Books – Volume I) kwa miaka ya fedha 2016/17; 2017/18; 2018/19 na 2018/2020

inayokwenda kulipa deni la taifa ni wastani wa triliion 9 kila mwaka na fedha ya mishahara ni wastani wa triliion 7 kila mwaka.

**111. Mheshimiwa Spika**, tafsiri ya takwimu hizo ni kwamba nchi inaendeshwa kwa mikopo na sio mapato ya ndani jambo ambalo ni hatari sana kwa ustawi wa uchumi wa nchi yetu.

#### **H. MASLAHI YA WAFANYAKAZI NA HIFADHI YA JAMII**

**112. Mheshimiwa Spika**, Serikali hii ya CCM ya awamu ya tano inamaliza mhula wake wa uongozi, ikiwa haijaongeza mishahara ya wafanyakazi kwa muda wote wa miaka mitano iliyokaa madarakani. Licha ya kutotekeleza wajibu huo wa kisheria; imekwenda mbali zaidi na kuingilia mafao ya wafanyakazi kwa lengo la kuyapunguza ili wafanyakazi walishi maisha ya dhiki baada ya kustaafu utumishi wao Serikalini.

**113. Mheshimiwa Spika**, hakuna asiyefahamu sakata la marekebisho ya kikokotoo cha mafao ya wastaafu baada ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuunganishwa. Kimsingi sheria ile ya kikokotoo bado hijafanyiwa marekebisho. Alichokifanya Mheshimiwa Rais, ni kuahirisha matumizi ya sheria hiyo kwa kuisogeza mbele hadi mwaka 2023 ndipo kikokotoo kipyka kianze kufanya kazi. Kambi Rasmi ya Upinzani inatafsiri kitendo hicho kama hadaa na danganya toto kwa wafanyakazi ili waichague Serikali ya CCM kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, lakini baada ya hapo tatizo liko palepale.

**114. Mheshimiwa Spika**, athari za kutofanya marekebisho ya kikokotoo cha mafao ya wastaafu katika sheria kimekuwa na athari kubwa katika utumishi wa umma. Kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali watumishi wengi wanaomba kustaafu mapema kabla ya umri wa kisheria wa miaka 60 ili wanufaike na kikokotoo cha zamani cha mafao yao, ambacho kinatumika sasa kwenye kipindi cha mpito; kabla kikokotoo kipyka kinacholalamikiwa hakijaanza kutumika mwaka 2023.

**115. Mheshimiwa Spika**, sambamba na kutopandisha mishahara na kuminya haki ya wafanyakazi kupata mafao mazuri wanapostaafu ajira; Serikali imefumbia macho utekelezaji wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wanaokosa ajira kwa sababu mbalimbali tofauti na kufukuzwa isipokuwa kuacha kazi kwa hiari (resignation).

**116. Msheshimiwa Spika**, kifungu cha 35 cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ya mwaka 2018 (Public Service Social Security Fund Act, 2018) kinaeleza kama ifuatavyo; naomba kunukuu:-

*35.-(1) A member of a pension scheme who ceases to be employed shall, subject to the provisions of subsection (2), be entitled to unemployment benefit.*

*(2) Unemployment benefit shall not be paid unless the applicant-*

- (a) has been a contributing member for a period not less than eighteen months;*
- (b) is terminated or ceased to be employed in the circumstances other than resignation;*
- (c) is a citizen of the United Republic of Tanzania;*
- (d) is not qualified for pension, gratuity or any other long-term benefits payable under this Act.*
- (e) proves to the Director General that he has not secured another employment;*
- (f) is below fifty five year old.*

*(3) Unemployment benefit shall be payable in a manner and at the rate to be prescribed in the regulations.*

**117. Msheshimiwa Spika**, kifungu hiki kinatoa ulinzi kwa wafanyakazi watakaokosa ajira kutohana na sababu mbalimbali isipokuwa kufukuzwa kazi au kuachishwa kazi kwa sababu nyingine tofauti na kuacha kazi kwa hiari, ilimradi wawe wamechangia katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa muda wa usiopungua miezi 18; wawe ni raia wa Jamhuri ya Muungano; hawana mafao mengine chini ya sheria hii;

wamethibitisha kwa Mkurugenzi Mkuu kuwa hawajapata ajira nyingine; na wako chini ya umri wa miaka 55 ya kuzaliwa.

**118. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitarajia kwamba kipindi hiki cha janga la Corona ambapo taasisi nyingi zikiwemo hoteli, shule na vyuo vya elimu, viwanda na makampuni mbalimbali ya biashara zimepunguza wafanya kazi; sheria hii ingetumika ili wafanyakazi ambao wanakidhi vigezo vilivyowekwa na sheria hii walipwe stahili zao kama ambavyo imeanishwa kwenye kanuni za utekelezaji wa sheria hii.

#### **I. SURA YA BAJETI NA SEKTA ZA KIPAUMBELE**

**119. Mheshimiwa Spika**, bajeti mbadala ya mwaka 2020/21 imejikita katika uhalisia wa uchumi wa ndani na pia katika uchumi wa Dunia. Kwa muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imefanya rejea ya makusanyo halisi ya mapato ya ndani na kufanya tathmini ya utekelezaji halisi wa bajeti za Serikali kwa miaka minne iliyopita na kufikia uamuzi wa kupanga bajeti mbadala kwa kuzingatia uhalisia huo.

**120. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imezingatia pia madhara ya janga la Corona ambalo limetikisa uchumi wa dunia; na hivyo kufikia uamuzi kushusha makisio yake ya bajeti kwa kuwa janga hili limefanya mwelekeo wa uchumi kuwa na mserereko wa kushuka badala ya kupanda. Mbali na mlipuko wa ugonjwa wa Corona kulitokea pia mafuriko makubwa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu katika kipindi cha mvua za masika, jambo ambalo limesababisha maafa na athari kubwa katika sekta mbalimbali za uchumi hususani sekta ya kilimo, na uchukuzi (kutokana na uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara na reli). Matukio yote hayo kwa vyovyote vile yameathiri upangaji wa bajeti ya Serikali kwa kuwa yalitokea bajeti hiyo ikiwa imeshapangwa.

**121. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa wastani wa makusanyo halisi ya mapato kwa miaka minne iliyopita ni shilingi trilioni

26.273; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepunguza kiasi hicho kwa asilimi 10 na kufikia kiwango cha bajeti ya shilingi trillioni 23.646 ili kuzingatia madhara ya COVID -19.,

**122.** Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarejea ushauri wake kuwa Serikali kufanya marekebisho ya bajeti yake ili iendane na uhalsia huo. Vinginevyo utekelezaji wa bajeti utakuwa mgumu kwa kuwa msingi wake hauna uhalsia kama ilivyoelezwa katika hotuba hii.

**Jedwali Na. 1: Sura ya Bajeti Mbadala kwa mwaka wa Fedha 2020/21<sup>11</sup>**

MAELEZO	MAPATO (TZS)	
JUMLA YA MAPATO YA KODI <sup>12</sup>	15,125,250,000,000.00?	
MAPATO YASIYO YA KODI	1,774,683,333,333.33	
MAPATO YA HALMASHAURI <sup>13</sup>	517,798,229,763.60	
JUMLA YA MAKUSANYO YANDAN	17,417,731,563,096.90	
MSAADYA KIBAJETI TOKANJE	935,622,133,119.60	
Mkopo ya ndani na nje	5,292,913,303,783.50	
JUMLA YA MAPATO		23,646,267,000,000
<b>MATUMIZI YA KAWAIDA</b>		
Deri la Taifa	7,004,480,000,000.00	
Mishahara ni 25%ya bajeti mbadala	5,911,566,750,000.00	
Matumizi mengineyo 15% ya bajeti Mbadala	3,546,940,050,000.00	
JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA	16,462,986,800,000.00	
<b>MATUMIZI YA MAENDELEO</b>		
Fedha za ndani + Nje	7,183,280,200,000.00	
<b>JUMLA YA FEDHAZA MATUMIZI</b>		23,646,267,000,000

<sup>11</sup> Taarifa ya CAG Serikali Kuu- Utekelezaji halisi wa bajeti- 2016/17, 2017/18,2018/19

<sup>12</sup> Taarifa ya CAG Serikali Kuu-Makusanyo halisi ya kodi kwa miaka ya 2016/17, 2017/18,2018/19

<sup>13</sup> Taarifa ya CAG Serikali za mitaa- Makusanyo halisi kwa miaka 2016/17, 2017/18 na 2018/19

**Jedwali Na. 2 : Mgawanyo wa Fedha katika Sekta za Kipaumbele**

Na.	Sekta	Kiasi (Tshs.)	Asilimia (%)
1.	Elimu	4,729,253,400,000	20
2.	Kilimo	3,546,940,050,000	15
3.	Viwanda	3,546,940,050,000	15
4.	Maji	2,364,626,700,000	10
5.	Afyा	4,729,253,400,000	20
6.	Nyinginezo	4,729,253,400,000	20
7.	JUMLA	23,646,267,000,000	100

**J. HITIMISHO**

**123. Mheshimiwa Spika**, pamoja na Serikali kusitiza kuwa Ugonjwa wa COVID 19 umepungua nchini, lakini kiuhalisia ugonjwa bado upo duniani na kwa maana hiyo milango ya shughuli za kiuchumi duniani bado imefungwa na inaendelea kuwa na athari kwa uchumi wetu. Kwa sababu hiyo, Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 inatakiwa kuelekeza nguvu zake kwenye kunusuru kuanguka kwa uchumi ambao umeathiriwa na janga la mlipuko wa ungonjwa wa COVID - 19 kama ambavyo pia imeainishwa na Ripoti ya Benki Kuu ya Tanzania ya Aprili, 2020 na kama ambavyo Waziri wa Fedha amekiri katika hotuba yake ya Hali ya Uchumi. Ili kuweza kufikia lengo hilo, ni lazima Serikali ihakikishe kuwa kuna mzunguko wa kutosha wa fedha katika sekta mbalimbali za uchumi ili kuwapa wananchi nguvu ya kununua (purchasing power).

**124. Mheshimiwa Spika**, uhakika wa mzunguko wa fedha utakuwepo tu pale ambapo Serikali itapunguza kodi katika biashara mbalimbli ili kuhamasisha uzalishaji kwa gharama nafuu na kukuza soko la ndani; kulipa madeni ya kodi (tax refunds) ili kuwezesha viwanda kuendelea kuzalisha bila vikwazo na pia kuyawezesha makampuni ya biashara kuendelea na biashara za manunzi na mauzo nje ya nchi bila vikwazo vyaa uhaba wa fedha.

**125. Mheshimiwa Spika**, tatizo kubwa ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imelibaini katika upangaji wa bajeti ya Serikali kwa miaka yote, ni kwamba Serikali imekuwa ikifanya makisio makubwa ya bajeti bila kuzingatia vyanzo halisi nya mapato na uwezo wa ukusanyaji mapato. Matokeo yake kila mwaka wa bajeti Serikali imekuwa ikishindwa kufikia malengo ya makusanyo kwa wastani wa takribani asilimia 20 mpaka 30. Kutofikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kumesababisha Serikali kushindwa kutekeleza Mpango wa Taifa wa Maendeleo na pia kulazimika kukopa kwa masharti ya kibashara ili kuziba pengo la nakisi ya bajeti jambo ambalo limepelekea Deni la Taifa kuwa kubwa.

**126. Mheshimiwa Spika**, napenda kumalizia hotuba yangu kwa kwa kurejea tena ushauri ambao Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeutoa kwa miaka yote mitano ya Serikali hili ya awamu ya tano kwamba; Serikali ipange makisio ya bajeti kwa kuzingatia vyanzo nya mapato vilivyopo na uwezo wa kukusanya; pili iwe na utaratibu wa kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo, na mikopo yote ya Serikali iwe inaidhinishwa na Bunge ili kudhibiti ukopaji usio na tija.

**127. Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Halima James Mdee  
**WAZIRI KIVULI NA MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI  
YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA  
YAFEDHA NA MIPANGO**  
12 Juni, 2020

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaingia sasa kwenye awamu ya mjadala kama tulivyosema leo na kesho ambapo Waheshimiwa Wabunge wengi sana mtapata nafasi. Sasa nikuita hapa ukawa haupo basi utashuka chini kama utapata nafasi hiyo, baadaye labda utapata hiyo nafasi, vinginevyo ni vizuri sote tukawepo. Unakwenda

kwenye chai mara moja unarudi, tunaendelea na shughuli zetu.

Sasa nitaanza na orodha kadri nilivyoandikiwa hapa na *Chief Whips* lakini muwe *ready*, usiseme mimi niko mbali sana ukakaa mbali, hapana. Kila mtu awe tayari tayari. Mchangiaji wa kwanza ni Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda. (*Makofi*)

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia bajeti yetu ya mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, nikupongeze sana wewe kwa kazi nzri unayolifanyia Bunge na Taifa hili, unafanya kazi nzuri na maazimio ya kukupongeza tumeyapitisha kwa hiyo na mimi nayaunga mkono Mungu akupe uhai mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niendelee vilevile kupongeza Chama changu cha Mapinduzi, Chama cha Mapinduzi ndicho chama chenye dira, mweleko sahihi katika uchumi uliochangamka. Kwa hiyo, mimi nakipongeza sana na nawapongeza viongozi wetu wa chama kwa kazi zao nzuri wanazozifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kipekee nimpongeze Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli amefanya kazi kubwa katika nchi hii na nishukuru sana kwenye azimio lile la kumpongeza namna alivyoshughulikia Covid-19, jambo lile ni kubwa kwa hiyo na sisi tunapongeza kweli kwa kazi nzuri aliyofanya. Lakini niendelee kupongeza Wizara kwa kazi nzuri ya kusimamia bajeti ya Serikali yetu kama ilivyowasilishwa jana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kwenda mbali naomba niseme jambo moja, wiki moja iliopita kulikuwa na *clip* moja inayosema TAKUKURU wananiangalia, wananicbunguza mimi. Niliiiona kwenye mtandao, kwa hiyo naomba niseme tu kwa kifupi kwamba na nitumie nafasi hii kumshukuru

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU Brigedia John Julius Mbungo kwa kuliweka sawa na kusema Obama yuko *clean*, msimchafue yuko ndani ya bajeti. Kulikuwa na watu wanaonihofu mimi kwenda kutumia vyombo wakifikiri kwamba Obama atachafuka, Obama nina maadili, niko safi kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukija kwenye hali ya uchumi naomba niipongeze Serikali kwa sababu mwaka 2015 ukuaji wa pato la Taifa ulikuwa ni asilimia 2.2 lakini sasa Aprili, 2020 tunaongelea ukuaji wa asilimia 6.9; hii ni kazi kubwa ambayo Mawaziri na Mheshimiwa Rais naomba mijipongeze kwa kazi nzuri sana. Ukuaji unakuaje? Huwezi kukua bila kuwa na miradi, tuna ujenzi mkubwa, mambo ya uchukuzi, mambo ya nishati, afya, elimu na mambo ya maji. Kwa hiyo, hiyo miradi yote mikubwa ambayo inazunguka ndani ya nchi yetu katika maeneo mbalimbali ndiyo yamefanya kwamba uchumi uonekane ni mkubwa. Kwa hiyo, ni jambo kubwa, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kusimamia uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nipongeze tena kwenye Sera za Fedha na Bajeti; mfumuko wetu umeendelea kuwa himili, umeendelea kuwa mzuri wa 3.4 mwaka 2019 ukilinganisha na mfumoko wa bei wa 4.4 wa mwaka 2015. Kwa hiyo, nalo hili ni jambo kubwa ambalo inabidi tujisifie kwamba uchumi wetu unaenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho kabla sijaingia ya Jimboni, niseme akiba ya fedha. Mpaka mwezi Aprili, 2020 Tanzania ina bilioni 5.5 kama fedha ya akiba ambayo inatosheleza sasa kununua bidhaa kwa miezi 6.1 ukilinganisha na lengo letu la miezi minne. Kwa hiyo, hili ni jambo kubwa ambalo pamoja na miradi tunayoifanya mikubwa, lakini Serikali inayo *reserve* ya kutosha ya kuweza kuhimili mtikisiko wowote katika uchumi, lolote likitokea. Kwa hiyo, hilo nalo naomba nilipongeze sana kwa hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Obama na John Pombe Magufuli 2020 wanapewa kura? Lakini kabla ya kwenda huko,

nimpungeze Dkt. Mpango, amesema hivi anatuombea Wabunge wa CCM wote wa Kamati ya Bajeti wapite kwa kishindo, kwa hiyo Dkt. Mpango nakushukuru sana, umesema vizuri kabisa na mimi nipo Kamati ya Bajeti, tupite bila kupingwa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, narudi sasa kwenye bajeti, tulieni msikilize mambo.

Mheshimiwa Spika, Wilaya yetu ya Buhigwe inaishukuru sana Serikali kwa sababu mimi mwaka 2010 nili pochaguliwa kuwa Mbunge nilikuwa ndani ya Wilaya ya Kasulu, mwaka 2010 tukaanza mchakato wa kuomba Wilaya mpya na wakati tunaomba Wilaya mpya mimi nilikuwa kwenye Wilaya mama ya Kasulu, nawashukuru Kasulu walitulea vizuri, lakini hatimaye Serikali ikatupatia Wilaya yetu ya Buhigwe na muasisi namba moja wa kutafuta Wilaya hii si mwingine ni Obama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulivyoendelea kutaunda Halmashauri mpaka sasa hivi Halmashari inaenda vizuri kabisa mambo yako vizuri, lakini tumefanya nini ndani ya Wilaya hiyo mpya? Kuwa na Wilaya mpya haishangazi, ziko hata mpya, lakini tumefanya nini kwenye afya?

Mheshimiwa Spika, naomba niutangazie umma kwamba Wilaya yangu ya Buhigwe ambayo tulianza ni changa kabisa tunaitoa kwenye ngazi ya kijiji kuwa Wilaya, sasa Hospitali yetu ya Wilaya imeanza kazi, kwa hiyo Mheshimiwa Jafo ambaye mara ya mwisho ulikuwa Kigoma kuhimiza uanzishwaji wa hospitali hii, naomba nitamke na Mheshimiwa Rais anajua, ajue kwamba Hospitali ya Wilaya ya Buhigwe inaanza kufanya kazi na wanaanza kutibiwa. Kwa hiyo ni jambo kubwa ambalo ni zuri sana, lakini tumetengeneza vituo vingi vya afya, mambo yako vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, upande wa barabara naomba niendelee kuishukuru Serikali, lami inayoenda kuanzishwa tumeanza mchakato wa kuiomba tangu mwaka 2010

mpaka sasa wameanza kulipwa fidia, kwa hiyo lami kutoka Manyovu kwenda Kasulu inaanza kutengenezwa. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Rais ndiyo maana nikasema Rais atapata kura nydingi Buhigwe na mimi nitakuwa pale kunyanya mkono wake kumuambia kura zote hizo ni za kwake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile tuna barabara ambazo tumezipandisha kwakweli. Zimeenda vizuri kwa hiyo nashukuru kwamba Serikali hii imefanya vizuri, mambo yanaenda vizuri. Kwa upande wa maji, kwenye Wilaya yangu kuna miradi mingi ya maji, tuna miradi ya maji ya vijiji 17 inaendelea na mpaka sasa vijiji vyote vya Muzeze, Kirungu, Mbanga, Kigogwe, Nyamugali, Kasumo, Mgera, Songambele, Nyegera, Migongo, Myama na Mwinanila tunaanza sasa hivi na Buhigwe. Mambo yanaendelea kule Kinazi, kwa hiyo miradi ya maji tunayo mingi kwa hiyo, hawana sababu ya kumnyima Mheshimiwa John Pombe Magufuli kura na kumnyima Mheshimiwa Obama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vijiji vyangu vyote vya Buhigwe, umeme unaingia, vyote viko kwenye mpango, wanamalizia na Wakandarasi wako kule, kwa hiyo hatuna kitu kingine cha kuongea, ni kumshukuru sana Waziri wa Nishati kwa kuendelea kufanya kazi nzuri na amefika na Naibu wake kazi nzuri kabisa mnafanya. Kwa hiyo mambo yako vizuri.

Kwa upande wa elimu niishukuru Serikali, John Pombe Magufuli anatupa bilioni moja na milioni 100 kwa kila mwaka kwa elimu bure ya shule ya sekondari na shule ya msingi. Kwa hiyo, ni jambo kubwa na wananchi wangu wa Buhigwe watampa kura kwa sababu hiyo. Lakini iko miradi mingi, tunajenga *high school*/Myama na Buhigwe kwa hiyo, mambo yanaenda vizuri. Niishukuru Wizara ya Elimu, Chuo cha VETA tunaendelea kujenga kinaendelea. Kwa hiyo nikushukuru sana unayeshughulikia elimu, mambo yako vizuri, tuko vizuri.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza mapato kwa sababu Buhigwe ni Wilaya ambayo ni changa na mapato yake ni kidogo, tunajengewa soko la bilioni mbili na milioni 300

ambalo sasa tutaanza kupata ushuru. Kwa hiyo, watu wa Mnanila na Buhigwe wote wanalijua na tunajenga na stendi kubwa, mambo yapo bambam.

Mheshimiwa Spika, upande wa mawasiliano; Jimbo la Buhigwe linasikika kwa asilimia 95, sina shida na wapi husikiki, kwa hiyo, mimi mawasiliano nina asilimia tanolabda nati imelegea tu kwenye mtambo basi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kiti chako kikumbuke mambo yafuatayo; majina yaliyopo inayoitwa Jimboni ukija wewe ukinitembelea utaambiwa huyu anaitwa Obama, jina la pili utakaloambiwa utaambiwa huyu ni mashine ya Jimbo, jina la tatu utakaloambiwa huyu ni mashine ya kusaga na kukoboa, jina la nne utakaloambiwa kwangu ni Simba wa Yuda na la mwisho utakaloambiwa ukiulliza utaambiwa huyu ni *caterpillar*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hayo majina naomba yakae kwenye *Hansard za Bunge* iwe kumbukumbu kwenye kizazi kijacho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa Buhigwe wanajua tulipotoka, tulipo na tunapoelekea, niseme mwaka 2020 Magufuli hapa, Obama hapa. Wamenituma nikwambie neno moja... (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa sentensi ya mwisho, muda haupo upande wako.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** sentensi ya mwisho ni mwaka wa uchaguzi, kila mtu yupo huru na hata kwenye harusi ukaoa na watu maarufu wapo, wewe umekosa nini? Mungu awabariki sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba.

Waheshimiwa Wabunge, tulieni mwaka wa uchaguzi huu. Mheshimiwa Joseph George Kakunda atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ambayo kwa Bunge hili ni ya mwisho kwa upande wangu. Napenda sana nitumie nafasi hii awali ya wote kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Sikonge kwa jinsi walivyonipa ushirikiano mkubwa tangu nilivyoapishwa na wewe kuwa Mbunge hapa mpaka leo wamenipa ushirikiano mkubwa sana katika kusimamia mambo ya maendeleo yanayohusu Jimbo la Sikonge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na leo hapa nasimama nataka nipongeze Serikali kwa dhati kabisa hasahaha nampongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa jinsi anavyoiongoza nchi hii kuipeleka kwenye neema ya maendeleo makubwa sana ambayo hayajawahi kutokea. Ameboresha sana usimamizi wa nidhamu ya mapato na matumizi ya Serikali na ndiyo maana hata Mheshimiwa Waziri wa Fedha alivyosoma bajeti jana hapa ametudokeza jambo moja muhimu sana, *budget performance* imepanda kutoka chini ya asilimia 60 miaka 10 iliyopita mpaka zaidi ya asilimia 95, hilo ni jambo la kuponceza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usimamizi wa uchumi kama ambavyo tulikuwa na mikakati huko nyuma tuna Dira ya Taifa kipindi hiki cha miaka mitano ndiyo tumevunja rekodi ya namna ya kusimamia uchumi vizuri zaidi na mambo yamekwenda vizuri zaidi kuliko miaka mingi iliyopita na ndiyo maana rekodi ambayo imesomwa hapa na Waziri wa Fedha jana amelinganisha mwaka 1970 ilikuwaje na mwaka 2020 ikoje, kitakwimu tupo vizuri zaidi sasa hivi, hilo ni jambo la kupongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika nyanja nne zote ukianzia kuboresha maisha, uje kwenye ulinzi na usalama, kukuza uchumi, utawala bora; katika nyanja zote nne kwa mujibu

wa takwimu tunazopewa tupo vizuri zaidi sasa kuliko tulivyokuwa huko nyuma, hilo ni jambo la kupongeza sana.

Mheshimiwa Spika, natolea mfano kwenye Jimbo langu la Sikunge katika kuboresha maisha, huduma za jamii, elimu tumepata maendeleo makubwa hatujawahi kupata maendeleo ya aina hiyo tangu Jimbo lianzishwe, hilo ni jambo kubwa sana ambalo Mheshimiwa Rais tunahitaji sisi Wana Sikunge kumpongeza kwa dhati.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na malengo ya kupata *high school* zaidi ya miaka 20 iliyopita katika kipindi cha miaka mitano hiki kuitia maombi ambayo niliyapeleka mimi kwakwe kuitia Mawaziri ameyapokea vizuri na ndiyo tumepata *high school* mbili; *Kamagi High School* na *Kiwele High School*, hilo ni jambo kubwa na tumejengewa shule mbili mpya kabisa za sekondari na shule za msingi 12 mpya kabisa, hilo ni jambo ambalo ni kubwa sana na kwa kweli nampongeza sana na namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa niaba ya watu wa Sikunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwenye afya napo tumepata maendeleo makubwa sana, tumejengewa Hospitali ya Wilaya, lakini tumeboreshewa kituo kimoja cha afya na kujengewa vituo viwili vipyta kabisa vya afya na zahanati nne ambazo ni za mfano wa kuigwa daraja la kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwenye maji mambo yanaendelea vizuri na mimi nataka nikwambie katika suala la usimamizi wa miradi ya maji nampongeza sana Waziri wa Maji amekuwa mkali katika kusimamia miradi ya maji kuliko kipindi chochote ambacho mimi nimewahi kuona na kukisikia katika utawala wa nchi hii. Nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Mbarawa kwa kazi hiyo anayoifanya kwa niaba ya Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la utawala bora; kipindi hiki tumeshuhudia maamuzi makubwa ambayo yanakwenda kuwapa huduma na nafuu Watanzania walio wengi, hilo ni jambo ambalo ni la kupongeza sana.

Mheshimiwa Spika, kwenye ulinzi na usalama, matukio ya uhalifu ambayo tuliyazoea huko nyuma yamepungua sana kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho ambalo ningependa kulizungumzia ni eneo la miundombinu/kukuza uchumi. Nyanja hii ya kukuza uchumi napenda kuileza kama ifuatavyo kwa kulinganisha na miaka ile ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1967 ni mwaka ambao ultangazwa Azimio la Arusha kwa ajili ya kuonesha kwamba njia kuu za uchumi zinamilikiwa na wananchi kipitia Serikali, lakini kwa sasa hivi Azimio la Arusha Mheshimiwa Rais amelirudisha kipitia sheria mbili zile za kumiliki rasilimali za nchi hii zimilikiwe na wananchi kipitia Serikali. Kwa hiyo, ina maana kwamba tayari tumerudi kwenye misingi ya Azimio la Arusha katika suala la kumiliki rasilimali za nchi, hilo ni jambo la kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye miundombinu, barabara tumepata rekodi kipindi hiki. Reli ya kati ambayo ilijengwa zaidi ya miaka 110 iliyopita leo hii tunajengewa reli ya kati ambayo ni ya viwango vya kimataifa kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 110. Historia hii haitakuja kusahaulika kwa kipindi cha miaka 100 ijayo, jina la Mheshimiwa Magufuli litatajwa ndani na nje ya nchi kwa kipindi cha miaka 100 ijayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, viwanja vya ndege, kufufua *ATCL*, kuboresha bandari, madaraja ya chini barabarani, madaraja ya ghorofa kwenye maeneo ya miji kama Dar es Salaam, madaraja yanayovuka mito, maziwa na bahari kipindi hiki kimekuwa ni kipindi cha rekodi. Umeme tumeongoza Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza masuala haya ya miundombinu wana Sikonge, Tabora na wananchi wa Tanzania wote na dunia nzima inajua kwamba Mheshimiwa Magufuli ameweza kufanya rekodi. Kwenye mawasiliano pia vilevile tumepata rekodi kubwa sana. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hatuna mfano wa Mheshimiwa Magufuli kwa jinsi alivyosimamia masuala yanayohusu gonywa hili la homa ya mapafu (Corona), dunia nzima imemjua Mheshimiwa Magufuli ni nani. Msimamo wa Rais wetu umeturudishia uhai wetu wa kuwa na sifa dunia nzima. Mimi nina ndugu zangu walikuwa China juzi, kila wakiingia sehemu wanaulizwa hivi Mheshimiwa Magufuli anaendeleaje yaani wanamfahamu Mheshimiwa Magufuli wananchi wa kawaida wa China, ina maana kwamba tumepata sifa kubwa sana sasa hivi kipindi cha miaka mitano hiki kuliko miaka mingi iliyopita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na hata Uingereza, Marekani, Canada na kila nchi ukienda anatajwa Mheshimiwa Magufuli, lakini yeye hajawahi kwenda huko, hapo ndiyo mjue kwamba umaarufu na sifa ya mtu jinsi anavyowapenda wananchi wake na jinsi anavyowahudumia sio lazima usafiri, unaweza ukakufuata hapo hapo ulipo na ndiyo maana hata mimi umaarufu wangu wa Sikunge siyo lazima mpaka niende Dar es Salaam, umaarufu wangu wa Sikunge naupata Sikunge huko huko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, haya tunayoyasema hapa yanamfanya Dkt. John Pombe Magufuli apite tu mwezi wa kumi akipunga mkono, siyo lazima apige kampeni kubwa, kampeni ameshaipiga kipindi cha miaka mitano; apite akipunga mkono na Sikunge atapita anapunga mkono na hata asipokuja tutampa kura zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kuwashukuru tena ndugu zangu wa Sikunge, najua kuna vijana wangu na wengine wazee wanapitapita huko wanataka Jimbo, mimi kama mtu muungwana ambaye nililelewa vizuri nawakaribisha wapite Jimboni lakini wasifanye vurugu, sisi tunataka tumalize uchaguzi wetu vizuri bila kupigana ngumi. Wale ni Wana CCM ndugu zangu wapokelewe, mtu anakwenda kusalimia mjomba au shangazi yake huwezi kumkataza. Ninaomba sisi tuwe na uchaguzi wa amani ambaao utakuwa ni mfano kwa Mkoa wa Tabora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa nafasi hii na napenda nikupongeze wewe mwenyewe binafsi kwa jinsi ambavyo umekuwa mahiri katika kuliongoza Bunge hili, kweli nimejua kwamba kumbe mtani Mgogo anaweza akafanya mambo mazuri sana kwa ajili ya nchi hii, ahsante sana ndugu yangu. Nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph George Kakunda kwa mchango wako na hasa jinsi ulivyomalizia kwa kumsifu mtani wako. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji, lakini niwaambie tu kwamba kwa utaratibu uleule na juzi mmepitisha Azimio la kunipongeza na mimi basi niwahakikishie mambo ya kuhusu utaratibu niachieni jamani, tatizo lenu mdomo, mmenielewa? Niachieni mdomo funga. (*Makof*)

Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo hoja iliyo mbele yetu. Naomba nianze kwa kumpongeza sana Waziri wa Fedha kwa ajili ya bajeti hii, *speech* yake ni nzuri sana inayohitimisha miaka mitano. Pongezi sana Mheshimiwa Waziri endelea kuchapa kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi nzuri ambazo amezifanya kwa miaka mitano. Aliyoyafanya siyo ya kusema, yanaonekana na Wabunge wengi wamesema kwa kweli hatuna cha kumpa ila kumshukuru yeye kwa kazi yake hiyo nzuri pamoja na Mwenyezi Mungu ambaye alitupa mtu kama huyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nipende tu kuzungumza kidogo kuhusu ujenzi wa viwanda ambao unategemewa kutokea

kwa ajili ya kuiweka nchi yetu katika uchumi wa kati. Hili jambo Mheshimiwa Rais amelifanya vizuri, tumekuwa na miradi ya kielelezo mingi na tunaendelea vizuri, miundombinu imejengwa vizuri, tutafika kwenye nchi ya ahadi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda niseme changamoto kidogo zilizobaki kwenye jambo hili ambazo zinaweza kutusaidia tukizitekeleza. Niseme ili ujenge nchi ya viwanda ni lazima uhamasishe viwanda vinavyohamasisha viwanda, maana yangu ni kwamba viwanda mama ni muhimu uvijenge na nitazungumzia sekta moja tu ambayo mimi naijua, zipo sekta nyingi ambazo zina viwanda vinavyohamasisha viwanda vingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya madini inaweza kuwa mhamasishaji mzuri sana wa viwanda na hasa madini ya viwanda ambayo tunayo katika nchi yetu. Tukihamasisha uchimbaji wa chuma, tunesema miaka mitano kwamba Mchuchuma Liganga kwa kweli ni kiwanda ambacho tukikianzisha kitatusaidia sana na kwenye Mpango wa Miaka Mitano jambo hili limesemwa vizuri, lakini tumechelewachelewa kidogo. Naomba niihamasishe Serikali tena msiliache hili jambo nyuma. Japokuwa sijalisikia sana kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri naona ni vizuri kwa kweli tuendelee nalo kwa sababu litatusaidia sana siku za usoni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna madini kama ya *graphite* sasa hivi kuna watafutaji wengi tu wamepata *graphite* katika nchi yetu, tunaweza kutengeneza betri, saa na hata simu zetu hizi hapa hapa Tanzania ajira ikawa kubwa. Naiomba sana Serikali ijitahidi kuhamasisha utafutaji wa madini haya na kuanzisha migodi hii, kwa kweli viwanda vitafufuka, tuna miaka mitano kufika mwaka 2025 tutakuwa nchi ya viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze tena Mheshimiwa Rais kwenye kusimamia sekta hii ya madini, amefanya vizuri sana kwa sababu ametupeleka mahali ambapo Sera ya Madini hii ambayo nimeishika hapa tulioitunga mwaka 2009

ilitaka Serikali irudi kuwa mwekezaji tena. Baada ya sera hii tulitunga sheria na sheria ninayo hapa ya mwaka 2010 ambayo illitaka Serikali wananchi wake washiriki sana kwenye Sekta ya Madini lakini Serikali nayo ishiriki kama mwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati nikiwa Serikalini pale tulianza kushauriana na makampuni ili kulingana na Sheria ya Madini ya mwaka 2010 kifungu 12(2) kwamba lazima Serikali iwe na hisa kwenye kila kampuni, *free carried interest*. Wakati huo hatukusema kiasi gani, tukiacha nafasi kwamba tunaweza kushauriana na makampuni tukachukua hata hisa asilimia zaidi ya 20 hata 30 na tulishauriana na baadhi ya makampuni kwa mfano Mradi wa Makaa ya Mawe Ngaka tulipata asilimia 20, Mradi wa Uchimbaji wa Dhahabu-Bacliff tulipata asilimia 45 na tulianza kuzungumza na makampuni Barrick na wenzake ili watoe hisa. Bahati nzuri mwaka 2012 mimi na mwenzangu Mheshimiwa Waziri Ngeleja tukawa tumeondoka kwenye Serikali.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuendelea kuyashauri makampuni haya ukasimama kidogo, lakini Mheshimiwa Rais huyu alivyokuja akaanza palepale na alianza kwa *speed* kubwa zaidi, wengi hatukumuelewa inaitwa *speed* ya kijeshi, unawakamata unawaleta kwenye meza ya majadiliano. Wamekuja na bahati nzuri zaidi badala ya kuwa na hisa tu asilimia 16 tumekuwa wawekezaji kama Sera ya Madini inavyosema. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais ametekeleza vizuri na anatupeleka kuzuri sana, naomba nimpongeze na tuendeleee. Sasa hivi makampuni yaliyobaki haya *GGM* na wenzake tushauriane nao watupe hisa kama walivyotuba watu wa Barrick. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nipende kusema kwamba niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Igunga, tumekuwa nao kwa miaka mitano na kwa kweli tumefanya mambo mengi ambayo Mheshimiwa Rais katuletea maji kutoka Ziwa Victoria, umeme tumebakiza kata tano tu, afya ipo vizuri

sana. Kwa kweli tumefanya vizuri na Mungu atubariki sana na Mheshimiwa Rais abarikiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kusema bado kuna changamoto kwenye barabara na jambo hili nalisema na Mbunge atakayekuja mwaka 2020 mwezi wa kumi natarajia niwe mimi, lakini ayachukue haya ninayoyasema hapa. Barabara Jimbo la Igunga nilishasema tupo mbugani, ziwani, udongo ni mweusi Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu hauwezi ukajenga barabara kwa kukwangua, asilimia 80 ya Jimbo letu ni mbuga ya Ziwa Victoria liliokauka. Kwa hiyo, barabara zetu, tuna barabara moja tu inayokatisha Igunga zingine zote ni mbovu hazipitiki kabisa wakati wa masika. Naiomba sana Serikali hebu iangalieni Igunga kwa jicho tofauti ili mtupe barabara awamu inayokuja basi tuwe na barabara hata mbili/tatu. Ningependa kutaja barabara ya kutoka Igunga kwenda Itumba mpaka Loya kwa Mheshimiwa Ntimizi ni mbugani kabisa ikifika masika hamna kupita barabara ya kutoka Igunga kwenda Igurubi nayo iko mbugani hamna barabara.

Mheshimiwa Spika, pia barabara ya kutoka Mbutu kwenda Sakamaliwa barabara mbaya; Mbutu kwenda Kinyinginila hakuna barabara, barabara ya kutoka Bukoko kwenda Mtungulu hakuna barabara; barabara ya kutoka Itunduru kwenda Kagongwa hakuna barabara, barabara ya kutoka Igogo kwenda Isugilo hakuna barabara na barabara ya kutoka Itumba kwenda Mirumbi hakuna barabara. Nataja hizi barabara nikiomba kwa kweli Mheshimiwa Waziri safari ijayo hata barabara moja basi mtutengenezee ili wananchi hawa waweze kupata mahali pa kupita na nchi maendeleo yaweze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema tumefanyakazi nzuri tunategemea kufanyakazi nzuri na naomba sana kama walivyosema Wabunge wengine, Mheshimiwa Rais wanasema Wasukuma *damalaise*, mgombea wetu ni mmoja na tumuunge mkono, watakaojitekeza tu sijui tufanyeje tuwapatilize kwa sababu tunataka nini zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii Mungu awabariki tutaonana mwaka huu mwezi wa 11 kuendelea na shughuli ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Dkt. Dalaly Peter Kafumu, tunakushukuru sana kwa maneno ya matumaini, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond atafuatiwa na Mheshimiwa Lathifah Chande, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Kishoa.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii, lakini kipekee namshukuru Mungu kwa kuniweka hapa salama na urafiki na Wabunge wote na sasa natimiza kipindi changu cha miaka mitano, nawashukuru sana Waheshimiwa wenzangu wote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninakila sababu ya kukushukuru wewe kipekee kwa jinsi ambavyo umetuongoza vizuri na jinsi ambavyo umetupanga katika Kamati ambazo kila mmoja aliweza kutoa utaalamu wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nianze kupongeza bajeti hii na niiunge mkono siyo tu kwa vile mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, lakini kwa vile bajeti hii imesisimua wote wananchi wa Tanzania kwa kuona kwamba leo wameamka kila kitu kikiwa katika bei ilivyokuwa jana.

Mheshimiwa Spika, jana mimi mwenyewe nilienda kwenye kituo cha mafuta tayari walikuwa hawana mafuta wamezuia eti wanangoja bajeti isomwe yatapanda bei. Kumbe siku hizi *EWURA* inapandisha au inapunguza kila mwezi mara moja mwanzo wa mwezi na akaja Mheshimiwa Mpango na mipango yake, wala hajagusa mafuta, wala hajagusa sigara, wala hajagusa soda, wala hajagusa *wine*, watu waendelee maisha kama kawaida ni nani huyo kama Dkt. Mpango? Amekuja na vionjo tofauti vyatya bajeti. Watu walikuwa wanaficha maboksi ya sigara ndani wakijua bajeti ikishasomwa kila bei juu hakuna hiyo, naomba tusisitize na kuwaelimisha wananchi wetu maisha yanaendelea kama kawaida. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Covid-19 ni ugonjwa umesumbua sana, hatuwezi kutamka ni nani amekwenda, nani amerudi au ni nini itakuwaje au hata mimi labda ni vipi, lakini kila mahali penye shida pia kuna jambo lake zuri. Kunawa mikono ilikuwa ni shida siyo Tanzania tu ilikuwa ni shida dunia nzima ndiyo maana tarehe 15 Oktoba kuna *Global Washing Day* watu wanawana mikono wanafundishwa kunawa mikono na Tanzania hii inasimamiwa kabisa ni siku ya kunawa mikono, leo imekuwa rasmi, kizazi hiki kinachokwuwa sasa na hata baadaye wamejua umuhimu wa kunawa mikono kwa maji tiririka, lakini elimu hiyo imepelekewa kueleweka kwa ajili ya Covid-19 ambayo mmeiweka ni Corona.

Mheshimiwa Spika, ni jambo jema nani jema na naomba liendele, lakini Watanzania tunapendana mno ziada, hatutaki ku-observe au ku-exercise *social distance*, unakuta watu unaona kwenye runinga mtu kuliko ampite mwenzie bila kumgusa wanapeana pale wanapokoholea Corona mtu anampa mwenzie kipepsi, ya nini jamani?

Mimi nawaomba tusikilize anachosema mwenzetu Waziri wa Afya Dkt. Ummy Mwalimu amekuwa mwalimu sana, nampongeza sana huyo dada, ni Mheshimiwa ambaye ametufundisha tukaelewa wote. Hakuna haja ya kugusana gusana, wewe kama umemfurahia sana mwenzio mpe *body language, just smile* na ye ye mwenyewe atajua kwamba umemfurahia mara mgusane vikwapa, mara mgusane miguu, *what for?* Hilo nimeona nilitoe hapa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa nirudi kwenye bajeti baada ya uzuri wa bajeti hiyo ina mambo kadhaa ambayo ni mazuri. Nitaanza na lile la benki zetu nichukue nafasi hii nimpongeze sana Gavana wa Benki Kuu...

## TAARIFA

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa.

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR:** Mheshimiwa Spika, inatakiwa kwanza sisi Wabunge tujifunze katika kujikinga na maradhi ya Corona, tumemuona juzi Mheshimiwa Jenista na Waziri Mkuu wamepeana mikono kwa hivyo Corona bado ipo pamoja na Mheshimiwa Silinde, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jenista ultaka kutajwa tuameona umetulia sana Mheshimiwa Jenista siku za karibuni. Mheshimiwa Shally Raymond pokea taarifa hiyo.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, unajua tuliambiwa na Rais aliyejita ukiambiwa changanya na lako, sasa niishie hapo hapo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nazungumzia lile la benki, baada ya nafuu iliyotolewa na Benki Kuu kwenye ile amana ambayo mabenki yanaweka Benki Kuu, *statutory minimum reserve*, lakini pia kwa kupunguza *discount rates* sasa mabenki yana hela za kukopesha, jibu lake ni nini? Jibu lake sasa ni watu waende benki kukopa rasmi. Lakini mabenki hayo ni machache tumeyasikia kwamba yameshusha *interest rate*. Mimi kumbukumbu zangu nilisoma kwenye gazeti *CRDB* wameshusha kutoka asilimia 17 mpaka 14, lakini hiyo ni kwa *commercial loans*.

Mimi naiomba *CRDB* hiyo hiyo na mabenki mengine yafikirie sasa *personal loans* za watu kama wafanyakazi, watu kama ninyi wenyewe hapa tunachukua na wengine ambao wako mahali ambapo haitumiki gharama yoyote, kwa kweli napongeza sana hiyo hatua yao ya kupunguza *rates*.

Mheshimiwa Spika, lakini nilikuwa naomba kama *commercial rates* imepungua *by 2%* basi na *personal loans* zipungue *by 4%*. Kwa nini nasema hivyo? Wengi wafanyakazi ili waweze kufanyakazi zao kwa utulivu mambo yao lazima yaendelee na kwa hiyo wawe waaminifu kwa benki ni pamoja na hizo *rates* kuwa nzuri. Tumeona haya yakifanyika na *BoT* mara nyingi, lakini hayafiki chini matokeo yake ni kwamba wafanyakazi na watu wa kawaida wanaenda kwenye *VICOBA*, wanakwenda kwenye *microfinance*,

wanakwenda kule kwinge kuna taasisi mbalimbali za kukopesha. Lakini kule wanapigwa sana 30%. Sasa mimi nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Dkt. Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango elimu itolewe, watu warudi kule rasmi kwa kukopeshana, kule wanakopigwa waachane nako. Ninasema hivyo nikiwa na akili timamu kwamba pamoja na watu wengi kupenda kujiendeleza, lakini wakiona kule rasmi siyo kawaida wanakwenda ambako siyo. Lakini siyo hiyo tu tulipitisha hapa sheria ya kutoza kodi kwenye hao, tulipitisha kanuni ya kwenye hizo *savings* na *microfinances*, sasa kama hawatazingatia itakuwa ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo la benki na kupongeza, nilikuwa naomba sasa nizungumzie miradi mikubwa. Waziri wa Fedha alitueleza jana kwa uhakika kabisa hela za maendeleo zinaenda kutoka, miradi ambayo hajjamalizika inaenda kumalizikia, mimi naomba nitamke rasmi nitokako mimi kaskazini tuna kilio cha mradi wa maji kutoka Bwawa la Nyumba ya Mungu kwenda Mwanga, Same na Korogwe. Huu mradi ni shida, tunamaliza hapa hatujui tunaenda kusemaje, lakini mengi yameelezwa, tunaomba sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha ule mradi umalizike, umenieleza mwenyewe kwenye Kamati ya Bajeti una nia nzuri umalizike sasa sijui shida ni wakandarasi, sijui shida ni kitu gani, matenki tumeyaona lakini asilimia iliyokwisha kamiliaka ni 43 tu, haitoshi, sisi tulijua akija bwana mkubwa sasa kutupungia anachukua zile kura tuseme na mradi tayari na watu wanawawa maji tiririka kwenye maeneo hote hayo.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wale wanashida na mimi ni mmojawapo ni shida kubwa lakini pamoja na mradi huo wa Nyumba ya Mungu mpaka Korogwe kuna Mradi wa Maji ya Chala kila akizungumza Mbunge wa Rombo amekuwa akiomba sana na mimi nasisitiza tunaomba sasa yale maji yasitumiwe upande wa Kenya tu na sisi Tanzania tuyafaidi, ni maji masafi, matamu na yana kina kirefu, tunaomba ule Mradi wa Maji ya Chala sasa umalizike.

Mheshimiwa Spika, tunampongeza Rais kwa mambo mengi lakini wanawake wa Kilimanjaro wamenituma

nimpongeze sana kwa vile vibali vya wajasiriamali vimetoka, amekizungumzia Mwenyekiti wangu vinakwenda kuboreshwa viliwasaidia sana, tunaomba sana hiyo iendelee na kila siku wasisumbuliwe tena hata siku moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niseme nini ambalo hajasema Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Ndaki, naomba nimpongeze Mheshimiwa Ndaki nampongeza Mwenyekiti wa Bajeti kwa sababu mengi aliyyoyazungumza ni yale yote tuliyokuwa tumeyasemea.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kipekee niseme tena wewe ni mtu mstaarabu sana, wewe ni mtu mnyoofu, umetuongoza hapa, kiti chako akiweko Naibu Spika mmepata mangumi ya ukutani wanakwambia ngumi zinashindiliwa, lakini mmetoka imara na Dkt. Tulia na Wenyeviti wako wote umetuliza, tunawaombea wote muende salama na kurejea salama. (*Makof*)

Nawatachia wote uchaguzi mwema ndugu zangu, ikimpendeza mungu na ikiwapendeza walioitulo ambao sasa nawashukuru rasmi wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro walioniona kwamba naweza kuwasemea, nawatachia afya njema na hii bajeti ni rafiki hata kwao, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, nakushukuru sana, ahsante sana. Mheshimiwa Jesca Kishoa, Mheshimiwa Lathifah ajiandae.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Nitajikita zaidi kuonesha tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017 mpaka 2020/2021. Nafikiri ni wakati muafaka ambapo Serikali kuitia Waziri wake wa Fedha Mheshimiwa Mpango mnapaswa kuwaomba msamaha wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ina kila sababu ya kuomba wananchi msamaha kwa sababu mmeefeli

kuteketeleza Mpango wa Miaka Mitano wa Pili ambao mlikuwa mmeuandaa. Nitagusia maeneo machache kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni eneo la wastani wa ukuaji wa uchumi. Wakati wa Mpango wa Kwanza wa Miaka Mitano ambao ndiyo unamalizia muda wake, nchi yetu ilikuwa na wastani wa ukuaji wa uchumi Mpango wa Miaka Mitano ambao ulikuwa unaishia mwaka 2015, nchi yetu ilikuwa ina wastani wa uchumi wa 7%; lakini Mpango wa Pili wa Miaka Mitano ambao ndiyo unaoweka malengo ya ukuaji wa uchumi inasikitisha sana kwamba tuliweka malengo ya ukuaji wa uchumi kwa 10% lakini mpaka hivi ninavyozungumza sasa mwaka 2017 mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano tuli-*drop* kwa 0.2% kutoka 7% mpaka 6.8%.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo mwaka 2018/2019 tukarudi kwenye wastani wa kawaida ambao ni wa 7% kama tungekuwa tuko darasani leo *pass mark* ya Mheshimiwa Mpango ingekuwa ni sifuri. Ingekuwa ni sifuri kwa sababu hatukufika lengo la 10% na wala hatukuondoka kwenye 7% ambayo tulikuwepo mwaka 2015 na inasikitisha sana kuwa na Serikali ambayo inapanga mipango na haitekelezeki.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

## TAARIFA

**SPIKA:** Subiri kidogo kuna taarifa toka kwa Mheshimiwa Mlinga

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Jesca Kishoa, shemeji yetu wa nguvu kuwa anaposema Serikali hii iwaombe Watanzania msamaha ni pamoja na Mkoa wa Songwe ambao unaongozwa na RAS kaka yetu ambaye ni mume wake ambao katika huo mkoa Serikali imejenga

uwanja wa ndege, imejenga vituo vya afya, imejenga Hospitali za Wilaya. Ahsante sana.

**SPIKA:** Pokea taarifa hiyo Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, mimi nazungumza *facts*, naomba nijibiwe kwa *facts* na *the good thing* ni kwamba *facts* ninazozitumia ni za Serikalini huko huko. Naomba niendelee twende kwenye kiwango cha umaskini Mpango wa Maendeleo ya Kwanza...

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

## TAARIFA

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Jesca kutoka kwa Mheshimiwa...

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mchangiaji anayechangia sasa kwamba badala ya kusema kwamba Serikali hii iwaombe msamaha wananchi, angeanza kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumpa ajira mume wake ambaye ni RAS wa Mkoa wa kule Songwe, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca, taarifa hizi anapewa Jesca, sasa inabidi mwenye taarifa yake apokee kwanza kama kuna lingine baadae wanachosema Jesca watoto wako wanakula mnyepe mnyepe. Taarifa hiyo wanakupa Jesca. (*Kicheko/Vigelegele*)

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, *I am doing my job*, mimi ni Mbunge na ninalipwa kwa kazi ya Ubunge, nawakilisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ya Kwanza uliacha kiwango cha umaskini mwaka 2015 kilikuwa ni asilimia 28.2 lakini Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wenyewe ulikusudia kupunguza kiwango

hicho mpaka kufikia 16.7% mwaka 2021, lakini badala yake mpaka ninavyozungumza taarifa ya mwaka 2018 inaonesha kwamba kiwango hicho kilipungua kutoka 28.2% mpaka 26.4% ambalo ni sawa na punguzo la 1.8% kama tungekuwa darasani leo Mheshimiwa Mpango angekuwa ana-failure ya 84.4%. Ni vema mkaomba radhi kwa Watanzania.

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

## TAARIFA

**SPIKA:** Jesca subiri upokee taarifa

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Spika, nataka Mheshimiwa mwenzangu hapa...

**SPIKA:** Ndiyo Mheshimiwa Masele endelea.

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** ...kwamba ndugu Mheshimiwa Philip Isidori Mpango ni *Ph.Dna* Mkufunzi Mstaafu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, sasa anapozungumza kwamba angepata sifuri nataka nimpe taarifa kwamba ni mmoja wa wachumi wabobezi katika nchi yetu. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca anachosema Mheshimiwa ni kwamba unapomwambia Mheshimiwa Mpango ni zero *Ph.D holder* anataka tu kusikia *cv* yako ili ajue *basis* ya *assessment* yako. Unapokea taarifa?

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, napotezewa muda tu kwa sababu mimi naangalia hasa kwenye suala la utekelezaji na matendo ndiyo yanayomtafsiri mtu.

Mheshimiwa Spika, naendelea na tathimini kwenye suala umeme mwaka 2015 uzalishaji wa umeme ulikuwa wa *megawatts* 1,501 Mpango wa Pili ukaweka malengo kufikia mwaka 2020 iwe imezalisha *megawatts* 4,915. Mwaka 2020 ambaao ndio tunao sasa ambaao ni mwisho wa utekelezaji kuna ongezeko la *megawatts* 102.38 ambaao inaepelekea

kuwa na jumla *megawatts* 1,603 yaani mpango unatakiwa kuwe na *megawatts* 4,915 lakini mkaishia *megawatts* 1,603.38. (*Makofii*)

**WAZIRI WA NISHATI:** Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca taarifa uwekwe sawa. Mheshimiwa Waziri wa Nishati nimekuona.

## TAARIFA

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge na ningependa taarifa hizi zinaingia kwenye jamii zinalenga kupotosha, ambazo sio nia njema.

Mheshimiwa Spika, nimpe taarifa zifuatazo; mwaka 2016 tulilingiza kwenye Gridi ya Taifa *megawatts* kutoka Kinyerezi I, mwaka 2017 tukaingiza kwenye Gridi ya Taifa *megawatts* 248 kutoka Kinyerezi. Kwa hiyo, anachosema Mheshimiwa Mbunge ana lengo la kupotosha umma. Tumeingiza *megawatts* zaidi 448 ndani ya miaka mitatu iliyopita na bado tunaendelea, ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca amerekebisha hizo taarifa kama ulikuwa umezipata vibaya. Endelea.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikwambie tu kwamba nasikitika sana kuona Serikali inakuwa na *double standard*. Serikali imepeleka taarifa kwenye Kamati Bajeti *figure* hizi ambazo nazingumza hapa na taarifa anayoisema Mheshimiwa Waziri nafikiri anafanya *politics* tu, lakini ninachokosoma hapa nina uwezo wa kukuletea ushahidi hapa ulipo kama unauhitaji.

Mheshimiwa Spika, ili mpango utimie ilitakatiwa ongezeko la *megawatts* 3,414 tafsiri yake ni kwamba Mheshimiwa Mpango kama leo tungekuwa darasani angekuwa amefeli kwa asilimia 97.1.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**SPIKA:** Subiri kidogo Mheshimiwa Jesca. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

### **KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu natumia Kanuni ya 68(1) naongelea utaratibu.

Mheshimiwa Spika, la kwanza muongeaji anaeyeongea anasema Serikali inapotosha, nilitaka hilo niliweke wazi kwamba Serikali haipotoshi. Lakini ninachoombea utaratibu Mbunge anayeongea amepewa taarifa nydingi mno ndani ya dakika hizo hizo anazoongea na ni dhahiri anaonekana kupotosha, sasa nikataka nipate mwongozo wako inaruhusiwa Mbunge ambaye anapotosha kuendelea kupewa ruhusa ya kuendelea kuongea ni dhahiri anaendelea kupotosha Mbunge?

**SPIKA:** Taarifa hiyo Mheshimiwa Jesca kwamba uache kupotosha.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, mimi namsihi Mheshimiwa Mwigulu anisubiri jimboni Iramba Oktoba, 2020. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninaitaka Serikali iwaombe radhi Watanzania, sasa niwashauri tu nini kifanyike ili msirudie makosa kama haya. Hakuna sheria ya kusimamia Mpango wa Maendeleo ambayo matakwa ya Katiba ukifungua Katiba yetu Ibara ya 63(3)(c) Katiba inaweka masharti ya kutunga sheria ambayo inasimamia utekelezaji wa mpango wowote ambao unakusudiwa kutekeleza kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama ushauri wetu mngekuwa mnauchukua kwa kipindi chote ambacho tumekuwa humu

ndani haya yasingejitokeza. Ni jambo baya kwa Serikali ambayo inajita ni Serikali makini, kwa miaka mitano mna-*plan ku-fail* mna-set *plans halafu mna-fail. Shame.*

**MHE. DKT. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca pokea taarifa nyingine Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya.

## TAARIFA

**MHE. DKT. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani na pengine mchangiaji anayeendelea kuchangia ameangalia hiyo hoja yake, lakini unapoweka malengo maana yake unatengeneza *model* ambayo ndani yake ina *factors* nyingi ili kufikia yale malengo. Katika Mpango wa Maendeleo umeenda na *research* ambazo zimefanyika na *models* ambazo zimetengenezwa kulingana na *factors, time, mazingira ya kufanyakazi yana matter* katika kufikia yale malengo.

Mheshimiwa Spika, inawezekana anataka kufikia *targetya* kuishauri Serikali kutunga sheria, lakini katika jambo ambalo huwezi kutulitungia sheria ni pamoja na *models* ambazo zinategemea mazingira mengi kufikia hiyo *objective*, hicho unachokizungumza ni kwamba inawezekana unawaoondosha Watanzania kutoka katika jambo la uhalisia na kulipeleka katika jambo la *theory* ambalo si lazima tufikie huko tunakotaka kufikia. Cha msingi hapa nadhani kama Wabunge tuna-*task* ya kuendelea kufanya utafiti kwa namna gani tunaweza kufikia huko au ni sababu gani zitufanya tusifike huko. Kwa hiyo, nadhani tu aendeleee, lakini ajue kwamba kuna *factors* nyingi ambazo zinasababisha malengo mengi yasiwe yanafikiwa ukienda katika mrengu wa *research* na *development*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca pokea taarifa hizo.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, huyu Mbunge *in a way* amekubali kwamba kuna uwezekano mkubwa Serikali imeshindwa kufanya utekelezaji wa mpango na sababu aliyoitao ni kwa sababu kuna mambo ya *strategies* na nini ku-fail, *I think you can understand. (Makof/ Kicheko)*

*(Hapa baadhi Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)*

**MHE. DKT. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa kwa nini...

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa jamani.

## T A A R I F A

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, taarifa.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, mimi ni shahidi tulivyotengeneza Mpango huu tulifanya utafiti wa kutosha na nimekuwa nikiufuatilia kwa karibu sana na nilikuwa na Dkt. Mpango alivyokuwa Mkuu wa Tume ya Mipango na ye ye anautekeleza na sisi ni mashahidi kwamba hakuna mpango uliotekelzeza kama huu wa sasa utakoisha.

Mheshimiwa Spika, naomba mwanangu akubali kwamba asiseme mambo ya *rumours* aende akaangalia *statistics* kama Dkt. Mpango alivyoangalia. (*Makof/*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca taarifa nyngi namna hii maana yake *there is something wrong with you somewhere.*

Ukisema kwamba kumekuwa na kushuka kwa ukua ji wa uchumi kutoka malengo ya asilimia saba *into six point something*, angalia Afrika nzima ni nchi gani ambayo ina percentage ya uchumi wa kiwango hicho? Ndio maana jana

ukaambiwa hivi sasa Tanzania ni moja ya nchi kumi ambazo ni *powerful economics* katika Afrika nzima. (*Makofi*)

Kwa hiyo utaona hizi *factors*, tena asilimia tulizonazo tena utakuta nchi kubwa, hazina hata asilimia hizo za ukuaji wa uchumi kama tulionao. Kwa hiyo wanakupa taarifa kukuelimisha tu katika mambo haya. Malizia Mheshimiwa.

Katibu bado dakika zake? Malizia, malizia bado dakika yako moja hapa. (*Kicheko*)

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia narudia tena ni vyema tu kwa kuzingatia kile ambacho mlikuwa mmekipanga, mkakiri kwa Watanzania kwamba kwenye hili na hili na hili Watanzania hatujatekeleza malengo na mkaomba msamaha sio dhambi. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante ni kengele ya pili.

**MHE JACQUELINE N. MSONGOZI:** Muda, muda, muda.

**SPIKA:** Ahsante ni kengele ya pili, ahsante sana Mheshimiwa Jesca Kishoa ahsante sana.

Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande Kigwalilo atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii ya kuweza kuchangia, najua ni kwa ajili ya utaratibu wako umeniwezesha leo hii pia kuweza kuchangia kwa mara nyingine, ahsante sana kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, nimepitia hotuba ya Waziri wa Mipango Mheshimiwa Dkt. Mpango juu ya bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 na nimegundua ya kwamba katika hotuba yake kati ya maneno 25,631 yaliyokuwemo katika hii hotuba yake neno wanawake limetajwa mara tatu tu na

neno vijana limetajwa mara nne, huku neno wazee likitajwa mara moja tu na neno la watu wenyewe ulemavu likitajwa mara moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wazee na watu wenyewe ulemavu kutajwa mara moja inawezekana ikawa haina maana ya kwamba Taifa letu haliwachukulii hawa wazee kwa uzito wake. Lakini pia inawezekana ikawa haina maana Taifa letu halichukulii hawa watu wenyewe ulemavu kwa umuhimu wake. Lakini hii inaashiria kwa namna moja au nyingine kwamba Mpango wetu wa Taifa hauzingatii mahitaji ya watu hawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ili bajeti iweze kuwa na tija inapaswa kuhakikisha inagusa wananchi wa hali ya kawaida na ili Serikali iweze kutimiza wajibu wake wa kuweza kusimamia ustawi wa wananchi wake basi inapaswa kule bajeti ambayo inaendana moja kwa moja na mahitaji ya watu wake na watu hawa ni wanawake, vijana, wazee pamoa na...

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa ipo upande gani endelea mtoa taarifa.

## TAARIFA

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Spika, nimepende kumpa taarifa mzunguzaji anaendelea anatoa takwimu kwamba Mpango huu hajagusa wanawake, vijana, watu wenyewe ulemavu. Wananchi wa Tanzania ni jumuifu ndani ya wananchi hao ndio hao tunao vijana, tunao kina mama, tunao wazee, tunao walemaavu.

Mheshimiwa Spika, sasa ajikite kwamba mpango huu umewatosheleza makundi yote ambayo ameyasema hayo bila ya kungalia jinsi ambavyo yeye ameangalia, ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Lathifah ni taarifa tu.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante siipokei hiyo taarifa kwa sababu kiuhalisia hata takwimu zinaonesha katika watu waliopo hapa nchini wanawake ndiyo wanaongoza, lakini pia na vijana lakini pia na wazee wakiwemo na watu wenye ulemavu wapo katika kundi la watu maalum. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo basi bajeti inapaswa ihakikishe inatekeleza mahitaji ya hawa watu moja kwa moja. Kwa mantiki hiyo basi naishauri Serikali ieweze kuhakikisha bajeti hii ili iweze kuwa na tija kwamba inaenda kugusa na kutekeleza mahitaji ya watu hawa moja kwa moja kwa ajili ya kuwashakikishi wananchi wake matumaini. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Magufuli katika sekta mbalimbali katika mikoa mbalimbali ikiwepo na Mkoa wa Lindi, lakini Wilaya ya Liwale imeonekana kuwa nyuma kwenye Mipango ya Maendeleo ya Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Liwale wanakabiliwa na changamoto nyingi ambazo Mpango wa Maendeleo unapaswa kuzitatua. Katika changamoto walizonazo wananchi wa Liwale changamoto kubwa iliyopo ni juu ya barabara ya Nangurlukulu – Liwale. Naomba nikiri wazi barabara hii ya Nangurukulu – Liwale yenye urefu wa Km 230 ilijengwa kwa kiwango cha changalawe alikuwa kwa juhudzi za Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kipindi ambacho alikuwa Waziri wa Ujenzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, endapo Waziri wa Miundombinu sasa hivi aliopo angetilia umuhimu barabara hii kwa kutaka kujengwa kwa kiwango lami ni uhakika Serikali ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli asingesita kuleta mpango huo hapa Bungeni kwa ajili ya kuhakikisha hii barabara inaenda kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, tungependa kumuomba Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli itakapofika wakati wa kampeni wa Uchaguzi Mkuu mwaka huu awaze kupita kwenye hii barabara ya Nangurukulu – Liwale ili aweze

kuona ni kwa namna gani wasaidizi wake wameshindwa kumsaidia katika kutatua changamoto hii kwa kipindi cha miaka mitano ya Urais wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja kuhitimisha wiki ijayo, aweze kuja kuitolea maelezo juu ya ujenzi wa barabara hii ya Liwale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo yote nakushukuru, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande Kigwalilo. Nilishakutaja Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka na utafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, nakushukuru sana kwa sababu kama nilivyokwisha kukuarifu nasimama hapa kuwajulisha wenzangu na Bunge lako tukufu kwamba nina majonzi makubwa sana naomba niwape taarifa kwamba leo asubuhi hii katika Hospitali ya Bugando, Halmashari ya Wilaya ya Muleba tumempoteza Mwenyekiti wetu, amefariki baada ya ajali ya pikipiki na kinachosikitika zaidi na kaka yake Mzee Aloyce kwa mshtuko naye akafariki.

**MBUNGE FULANI:** Ooh, pole sana.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Kwa hiyo, naomba mniunge mkono katika kuwaombea na kuona kwamba ni pigo kubwa sana. Mheshimiwa Chrisant Kamugisha alikuwa ni mmojawapo wa Madiwani mahiri na ameendesha Halmashuri ya Muleba kwa ufanisi mkubwa sana. Tunapojadili bajeti hapa mafanikio makubwa ambayo tumeyapata na ye ye amekuwa ni mmojawapo, amekuwa ni kiuongo kikubwa sana katika utekelezaji wa programu yetu ya kazi katika Halmashauri ya Muleba na Mkoa wa Kagera kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango na Wizara kwa ujumla kwa kazi nzuri walioifanya. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti na Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Mashimba Ndaki amewashawasilisha mawazo yetu ambayo tumeona kwamba yanawakilisha, tunapongeza Serikali. Sina budi ninaposimama hapa leo kupongeza sana utekelezaji wa programu katika Wilaya ya Muleba, kwa kuwa historia inaandikwa kwa Wilaya yetu siku ya leo naweza kusema kwamba Mheshimiwa Dkt. Rais John Pombe Magufuli ambaye pia ni jirani yetu kutoka hapa Chato amefanya mambo mkubwa katika kipindi cha Serikali yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Muleba na hasa kwa ukaribu zaidi Mwenyekiti wangu ambaye ametangulia mbele ya haki sasa niseme kwamba sisi tuna matokeo ambayo yanaonekana, ninapozungumza hapa Muleba barabara zinajengwa kwa lami, yote hiyo ni kazi ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli na Serikali yake, naomba mniunge mkono tuwapongeze. Ninavyoongea sasa hivi kwa mara ya kwanza katika historia Hospitali yetu Teule ya Rubya lami karibu inakamilika, kazi kubwa imefanyika; na ninapoongea sasa hivi kwa Wizara ya Elimu Shule ya Sekondari ya Profesa Joyce Ndalichako ambayo tulipewa na Mheshimiwa Rais kwa zawadi kabisa kwa upendeleo na ikapewa jina maalum mnaweza mkafikiria yatayotoka pale. Naomba kusema hiyo ni hatua kubwa katika sekta ya elimu, sekondari Muleba zimeendelea vizuri na mojawapo imepewa jina Waziri wetu huyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niombe basi nichukue nafasi hii Dkt. Mpango kusema kwamba sekta ya elimu ukiingalia kwa mtazamo wa uchumi ina idara mbili; kuna idara ya Serikali (*public sector*), lakini pia kuna *private education sector*.

Naomba kabisa katika bajeti hii tutambue mchango wa shule binafsi na sekta binafsi ya elimu, kwa sababu bajeti jambo hili haikulizingatia katika kuweka masharti nafuu, katika mipango maalum kusaidia sekta ya elimu tusizisahau shule binafsi. Najua Bunge hili lilijadili lakini nadhani mapendekezo

yalipotea hayapo kwenye bajeti. Shule binafsi nikiwapa mfano zinaajiri walimu takribani 90,000.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza hapa walimu 90,000 wengi mishahara yao iko mashakani. Wengi shule haziko katika *position* ya kuwalipa siyo kwa uzembe wa shule kama wengi wanavyofikiria sheria yenyewe ya elimu na Mheshimiwa Waziri wa Elimu anajua inazuia shule hizi kuwa na ziada, zinachangisha karo kufuatana na mahitaji. Kwa hiyo hazina *reserve all endowment fund*. Nadhani ni wakati wa kujifunza hapo kwa Dkt. Mpango kwamba labda shule hizi sasa zitakiwe kuwa na *endowment funds* kuhakikisha kwamba zina kuwa endelevu katika matatizo kama haya yanayotukabili.

Mheshimiwa Spika, ninaposimama hapa pia naomba niseme kwamba nishukuru maendeleo ni makubwa na leo kwa mara nyine tena unanipa nafasi kuagana na wenzangu na niwatakie kila la kheri kila mmoja wenu ambao mnakwenda kwenye kinyang'anyiro, huo utani wa jadi, mipasho isiwakatishe tamaa kwa sababu mwisho wa siku wananchi watawasikiliza naamini wengi wenu mtarejea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa katika sekta ya afya, sina budi kuwapongezeni, kumpungeza Waziri Ummy, lakini hasa kumpungeza pia Rais Magufuli kwa nguvu aliyoweka kwenye hizi tiba asilia, nadhani ni wazi wazi kwamba baada ya Rais kuweka nguvu sasa hivi Tanzania imekuwa mfano wa kuigwa katika sehemu mbalimbali. Niyoyasema pale awali nimefurahi kuona kwamba tumefika hapa tulipofika na kwamba Rais aliweza kuweka nguvu zake katika mpango huo. Pia kumpungeza rasmi kama mchumi, nadhani Waziri Mpango pia amesema katika *speech* yake kwamba aliona kwamba *lockdown* isingewezekana.

Kwa hiyo, nataka kusema kwamba mambo ni mengi lakini kwangu leo nashukuru sana na ninaomba nadhani wewe ndiyo mamlaka hayo kwamba angalau kwa dadika moja Bunge hili lingesimama kuniunga mkono katika kuwapa

pole wanafamilia wa *Mrs. Chrisant Kamugisha* na wana Muleba kwa sababu tumepata pigo kubwa sana mnaona hata na kuongea kwangu ni kwa wasiwasi, lakini ni uchungu mkubwa tuliokuwa nao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofj*)

**SPIKA:** Ahsante sana Profesa Tibaijuka tunakushukuru sana, tunatoa pole sana, kwa niaba ya Wabunge wote na Bunge zima kwa msiba wa Mwenyeekiti wetu huyu wa Halmashauri, aliyefanya kazi nzuri sana na kwa niaba ya wenzangu wote niseme tunamuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu pahali pema peponi, utufikishie pia salamu zetu kwa wafiwa.

Mhesimiwa Magdalena Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye Bajeti Kuu ya Serikali ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nichukue dakika chache kwenye muda wangu huu kuwashukuru sana kwa kuwa inaweza ikawa ni mara yangu ya mwisho kuchangia kwenye Bunge hili la Bajeti, Bunge hili la miaka mitano, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wote wa Jimbo langu la Kaliua, lakini pia niwashukuru sana viongozi wote wa Kaliua kwa ushirikiano mkubwa kwa nafasi mbalimbali kwa kuwa maendeleo mengi ya Kaliua yameletwa na kila mmoja ku-*play role* kwenye nafasi yake.

Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa ushirikiano walionipa tumefanya mengi Kaliua, leo Kaliua katika Mkoa wa Tabora ni Wilaya ambayo inaongoza katika nyanja mbalimbali ni kutokana na ushirikiano mkubwa wa viongozi wenzangu, wananchi kufanya kazi bila kuchoka, lakini pia kwa ushirikiano wa pamoja *as a timework* ndani ya Jimbo la Kaliua nawashukuru sana Mungu awabariki sana. (*Makofj*)

Pia naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru Chama changu cha Wananchi (*CUF*) kwa kunipa heshima kiliniteua kuweza kubeba bendera ya chama na hapo hapo ndiyo wananchi wakaniona kwamba ninafaa kuweza kuwa Mbunge wao naomba kwamba nitakapoenda kurudi tena kwa ajili ya kuomba radhaa waone yale tuliyoyafanya kwa pomoja tuweze kuyaendeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye bajeti sasa. Ukienda kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri, kwenye taarifa ya fedha ukiangalia bidhaa ambazo tume-*export* thamani ya bidhaa ambazo zimeuzwa nje ya nchi mwaka 2019 ni dola za Kimarekani milioni 5,954.2; ukiangalia thamani ya bidhaa zillizoingizwa ndani ya nchi mwaka huo huo ni dola za Kimarekanimilioni 8600.

Kwa hiyo ninachokiona hapa ni kwamba tuna *export* kidogo sana na tuna *import* kikubwa sana, matokeo yake kama nchi tunatumia fedha nyingi za nje kwenda kununua bidhaa nje, lakini tunapeleka kidogo sana kwa ajili ya kwenda kupata fedha za nje. Kwa hiyo, liko tatizo na tatizo kubwa ni kwamba sekta mbili muhimu sekta ya kilimo na sekta mifugo hatujawekeza vya kutosha ambayo ni sekta ambayo inaweza ikaongoza kwa ajili ya *ku-export*.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia taarifa ya Mheshimiwa Waziri utaona kwamba kwenye mazao ya mifugo tumepeleka nje kidogo sana. Nikianza na zao la ng'ombe, kwetu tuna mifugo mingi sana ukiangalia kama tungeweza *ku-export* tu ngozi za mifugo tume-*export* kidogo sana na imekuwa inashuka mwaka baada ya mwaka. Ukiangalia kuanzia mwaka 2015 ukija mpaka kwenye mwaka 2019 unawenza kushangaa kwamba mwaka 2015 tume-*export* asilimia 4.4, lakini mwaka 2015 tulikuwa ni asilimia 75.4. Kwa hiyo, ni kidogo sana na ile ngozi ambayo imepewa thamani, imefanyiwa thamani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ukija kwenye mazao, ukiangalia kwenye mazao mengi, kwa mfano mazao ya biashara, zao la pamba, zao la korosho, zao la tumbaku, zao

la chai, bado tume-export kidogo na hata pia thamani ya fedha ambayo imeuzwa ni kidogo, hii ni kutokana na kwamba hatujawekeza kwenye utafiti wa masoko.

Mheshimiwa Spika, kiukweli mazao mengi bei zake ni kidogo sana na hata wananchi wanashindwa kunufaika kwa sababu hatujawekeza vizuri kwenye utafiti wa masoko. Naomba kwenye Wizara sekta hizi mbili muhimu tuwekeze vya kutosha, viwanda, leo ukiangali akinamama wanatembea mitaani wanaauza maziwa, ukiona watu wanatembea na baiskeli wanaauza maziwa, viwanda visto ndiyo, lakini havijatosheleza bado. Kwa hiyo naomba kwenye sekta hizi mbili muhimu sana tuhakikishe kwamba tuwekeza vya kutosha ili tuhakikishe kwamba tuna-export sana, tuna *import* kidogo.

Mheshimiwa Spika, tulikubaliana kuna baadhi ya vitu ambavyo hatuhitaji ku-*import* kwa mfano samani za maofisi, tuna mbao nzuri Tanzania, tuna vijana wenye uwezo wa kutengeza samani nzuri, lakini leo ukiangalia ofisi zote za Serikali zinachukua mbao za China na Mchina ndiyo anaingoza kwa *import* bidhaa nyingi Tanzania kuliko nchi nyingine zote ni kwa sababu kwamba tumeshindwa kutumia hata kile tulichokuwa nacho sisi wenyewe kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunakitumia sisi wenyewe. Serikali ingeweka utaratibu kwamba samani za maofisi zitumika kwa ajili ya vijana wetu wapate ajira, lakini pia viwanda vya ndani vifanye kazi, leo tuna *import* kila kitu, meza, mpaka stuli, vitu ambavyo vimetengenezwa kwa *material* ambayo ni *very weak*, lakini sisi tunapeleka mbao nzuri, mninga, mkongo tunaletewa vitu ambavyo ni *very weak* ambavyo vinakaa siku mbili vimepotea. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hilo ni tatizo naomba kwa vitu ambavyo tunavyoenda nchi yetu tuweze kuvipa soko la kutosha tupunguze ku-*import material* ambapo ni dhaifu tuweze ku-*export* vitu ambavyo vinathamani kubwa.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, jana ametuambia hapa kwamba Serikali

imeamua sasa labda ni mapendekezo kwamba kuamua mapato ya hifadhi zote kwa maana ya hifadhi zote za Tanzania kwa maana ya Hifadhi za *TANAPA*, za Ngorongoro pamoja na *TAWA* mapato yake yote yakusanywe na *TRA*.

Mheshimiwa Spika, kwa jicho la uhifadhi aliyependekeza hiki kitu hana jicho la hifadhi hata kidogo, tunakwenda kuua hifadhi zote Tanzania hii ni wazi kabisa na tumeona kwa mfano mdogo namna ambavyo imekuja Covid miezi miwili leo *TANAPA* katikati ya mwezi hakuna mtumishi aliyepewa hata mshahara.

Mheshimiwa Spika, nilisema hapa, lakini leo haiwezekani walinzi wanaolinda wanyamaporI wanakutana na nyoka wapambane na majagili wenyе sihala nzito, wanafanya kazi mazingira magumu sana, leo aje mtu wa *TRA*, shati lake jeupe akusanye tu wapeleke kwenye Hazina halafu hifadhi ziendeshwe kwa *OC*. (*Makof*)

Mheshimiwa Waziri kiukweli na bahati nzuri wengine sisi uhifadhi ni damu zetu, tunakwenda kuua hifadhi zote kwa sababu ninajua Serikali ikikusanya kama hakuna *retention* wakati wanahitaji hizo fedha kwa ajili ya maendeleo ya hifadhi zile haitakuwepo hilo hela na mfano mdogo tumeuona mimi kwa kweli nasema kwamba hili pendekezo halitekelezeki na kiukweli halitakiwi kupitishwa ndani ya Bunge hili, kama tunataka hizi hifadhi ziwepo, hapa Tanzania ni nchi pekee Barani Afrika na duniani pia ambapo hifadhi za taifa zinajiendesa kwa mapato yenyewe, pia zinalipa kodi zote zinazotakiwa, pia zinatoa ruzuku gawio kwa Serikali peke yake, maeneo mengine wanapewa ruzuku. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana, leo watumishi wa hifadhi mbalimbali wanakaa wanafanya kazi kwa moyo wakijua kwamba angalau maslahi yao yanaboreshwa, leo ukaseme kwamba wategemee *OC*, wapewe fedha ambayo au mishahara ambayo inalingana na watu ambao wanafanya kazi mijini, hizi hifadhi zinakwenda kuteketea, nguvu ilitunza miaka yote inakwenda kuharibika na ndani ya heshima ambayo tuliyokuwa nayo kama Taifa kutunza

hifadhi, rasilimali zetu, vivutio vyetu itakuwa ni hadithi, itakuwa ni historia.

Mimi naomba na namuambia Mheshimiwa Waziri kabisa *TANAPA* na Ngorongoro wamekuwa ni muhimili mkubwa kwenye utalii na tunajua kwamba utalii wetu unategemea wanyamapori, ndiyo muhimili mkubwa, pia kwa kutumia mashirika haya vyuo mbalimbali vinaendeshwa kuna Chuo cha Mweka, Tosamaganda, kuna Chuo cha Likuyu, Sekamaganga ambavyo vyuo vyote hivi vinaendeshwa na mapato, pia ziko Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori, pia kuna Taasisi ya *Tanzania Wildlife Protection Fund* pia wanasaidia wanapata fedha kutoka kwenye hifadhi hizi, leo taasisi hizi zitakufa, vyuo hivi vitakufa hakuna uhifadhi tunakwenda wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba angalia mara mbili wazo hili kama kweli mnataka kuwepo na uhifadhi nchi hii acheni kwamba kunakuwepo na *retention* ya kutosha kwenye maeneo ya hifadhi ili hifadhi ziendelee kuwepo, barabara leo hazipo, leo wanyamapori tunaotunza wote watapotea. Tunaheshima kubwa kama Taifa, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri angalia suala hili kwa umakini mkubwa tuhakikishe kwamba hifadhi zetu zimepewa nafasi ya kukusanya mapato, Serikali ichukue kile ambacho inachukua kama sasa hivi. Ni pekee ambapo, unafanya kazi kwa moyo kwa kuwa wanajua kabisa kwamba wanajaliwa na watumishi wao wanafanya kazi mpaka kwa sababu wanajua kwamba hata mishahara yao inazidi kidogo watu ambao wanafanya kazi mijini.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ongezeko la kodi kwenye vifaa vya ujenzi. Tumeongeza kodi kwenye mabati, tumeongeza kwenye marumaru, *tiles* tumeongeza kwenye nondo, tumeongeza kwenye kila kitu. Tunakwenda kuwafanya watu wameendelee kuishi kwenye tembe, nyumba za udongo, nyumba za makuti na wajibu wa Serikali kwa kwanza kuhakikisha wananchi wake anakaa kwenye mazingira mazuri, kwenye nyumba nzuri, leo unavyoongeza kodi kwenye vifaa vya ujenzi, kwanza hata nyumba za kodi

za kupanga mapango yatakuwa na gharama kubwa. Kwa hiyo, hata watumishi wa kawaida kama walimu, manesi mishahara yao ni midogo watashindwa kukaa kwenye nyumba nzuri za kupanga. Pia hata wananchi wa kawaida alikuwa na mpango wa kujenga hawezi kujenga. Kwa hiyo, mwisho wa yote kwamba tunazidi kuoleta umaskini kwa watu ambaa wangeweza kujikomboa kwa sababu hatujapata angalau makazi ya kukaa unakuwa umejhakikishia kwamba angalau kwa upande wa kukaa una mahali pa kukaa.. (*Makof*)

**SPIKA:** Kuna taarifa Mheshimiwa kutoka kwa Waziri. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara tafadhali.

## TAARIFA

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, Serikali tunachukua ushauri wa Mheshimiwa Sakaya, lakini kwenye upande wa kulinda viwanda vyta ndani kwa mfano, saruji, *tiles* kwa maana ya vigae na nondo, mkakati wa Serikali tuliwasikiliza Waheshimiwa Wabunge hapa kulikuwa kuna mapendekezo kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge kwamba tulinde viwanda hivi na Serikali timesikia, tumeongeza *duties* ili kulinda viwanda hivi viweze kuzalisha hapa hapa nchini, tuwaajiri Watanzania na viwanda hivi vinazalisha zaidi na ziada tunauza nje ili kupata fedha za kigeni.

Kwa hiyo, ningependa kumpa Mheshimiwa Sakaya hiyo taarifa lakini nilitaka nitoe hiyo *clarification* kwa sababu mkakati wa Serikali na kipaumbele ni kutengeneza ajira nchini kupitilia viwanda vyetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sakaya taarifa hiyo?

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa ya Mheshimiwa Waziri kwa maana ya kwanza kama nikuongeza kodi kwa mali zinazotoka nje ya nchi, lakini kwa taarifa ya Mheshimiwa Waziri imeongezwa

mabati yameongezwa, nondo zimeongewa. Naomba niendelee.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunaomba miaka mingi hapa Bungeni kuona kwamba Serikali inapunguza Viat kwenye shilika la *National Housing Cooperation*.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Ndiyo Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika,

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kutokana mchango wa Mheshimiwa Sakaya ni dhahiri hiki kipengele hajakisoma vizuri kwa sababu *import duty* ni kwa bidhaa ambazo zinatoka nje siyo bidhaa za ndani, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ndiyo ameshaendelea na mambo mengine, endelee tu Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante tumekuwa tunaomba miaka yote Kamati yetu ya Maliasili hapa Bungeni kuhakikisha kwamba Serikali inapunguza *VAT* kwenye vifaa vya ujenzi kwa Shirika la Nyumba la Taifa ambalo lina jukumu kuhakikisha kwamba wananchi wanapata nyumba bora, nyumba nzuri lakini *affordable price*.

Sasa nilikuwa nategemea pia bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri ingekuja na hilo na siyo kuongeza tena. Kwa hiyo, niikuwa nategemea tunaomba wakati Mheshimiwa ana *windup* atuambie, ni lini sasa au Serikali ina mpango gani sasa kupunguza ongezeko la kodi ya thamani kwenye vifaa vya *National Housing Cooperation*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:**...ili nyumba zinazojengwa na Shirika la Nyumba ziweze kununuliwa na wananchi wa hali ya chini, wananchi wa *standard* na wa kada zote kuliko ambavyo ilivyo sasahivi kwamba nyumba za *National Housing* mtu wa kawaida hawezি kununua wananunu matajiri wanakuja kuwapangisha maskini.

Mheshimiwa Spika, naomba nimwachie Mhehimiwa Waziri anijibu, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya, kwenye mchango wako umegusia suala la hifadhi, ukaniusa na mimi nikawa nawaza labda baadae Mheshimiwa Waziri atatufahamisha vizuri, kuwapeleka *TRA* sijui wanaenda kufanya nini, kwa sababu siku hizi mambo ni ya kisasa ni elektroniki, hakuna mtalii anayefika kwenye geti la *national park* yoyote akiwa na *cash* hakuna hata mmoja, fedha mtalii anakuwa alishalipa tangu yuko Ulaya hata ajapanda ndege na kunakuwa na kampuni ambazo zina *moderate* hiyo safari yake. (*Makofii*)

Kwa hiyo, zinalipwa tayari akifika Tanzania zile kampuni, wanalipa benki tayari, pale benki anachukua tu ile kadi ile. Kwa hiyo, yule anakwenda na watalii wake kama ni kumi na ngapi na kadi ambayo tayari ilikwashilipa fedha ilishaingia Serikalini tayari kuititia *TANAPA*. Kwa hiyo pale getini wana *swap* tu, sasa *unless TRA* anakwenda kuangalia jinsi wanavyo-*swap* pale au yeye ndiye anaye-*swap*, lakin *already the money is in the bank*. Kwa hiyo watalii wanaingia hamna *cash*, *cash* kama ni katika geti la Ngorongoro, Serengeti labda wawe wasafiri wa mabasi, lori, sasa hiyo inahitajia malori ni mangapi, inahitajia *TRA* kwenda kukaa getini pale? Haihitajii.

Pili inatoa *implication* gani, yaani mashirika yote yameshakuwa ya kijeshi yale, watumishi wote mpaka mfagizi, halafu anaenda mtu ana shati nyeupe na tai nyekundu anaenda kufanya nini pale katikati ya wanajeshi wale na

vituo vingine viko maporini ambako *TRA* hawezi kukaa, atakosa ushirikiano yaani ni la kulifirkiria vizuri, yaani wanaenda kufanya nini hasa na je, kuna shida gani? Kuna tatizo gani, lakini kubwa zaidi siyo *TRA* kwenda, wanaweza wakaenda japo najua watapata shida sana kwa sababu ya mazingira, kwingine ni porini sana, unajua *nature* ya kazi inamfanya mtu anaona kukaa porini *is okey*, mwingine hawezi kabisa, *TRA* wamezoea mijini na nini na nini, ukim-*post* huko ni taabu.

Lakini kubwa zaidi kuchukua mapato yote yakaenda *centrally* tulikuwa na utaratibu huo miaka ya 1990, ndio tulifika huku si hifadhi zilikuwa zinafutika, misitu ilikuwa inaondoka kwa sababu ya vipaumbele. Hakuna siku tutakaa hapa kipaumbele kiwe wanyapori wala misitu haiwezekani.

Kwa hiyo, ni la kuliangalia kidogo lle *retention scheme* siyo lazima iwe ilivyokuwa, lakini ni muhimu sana huyo ng'ombe anayetoa maziwa akabakiziwa kamashudu kidogo cha ku-*retain operations*, haiwezekani majangili wameingia Kigoma huko unasubiri Hazina watoe sijui nini haiwezekani huwezi ku-*run* namna hiyo.

Kwa hiyo, iko kila sababu ya kuangalia eneo hilo nimeona hata Kamati ya bajeti na ninyi mme-*doubt* tu vizuri ni vyema *retention scheme* haikuwa mbaya kihivyo, ni vyema akaachiwa hata kama ni *twenty percent* chukua *eighthalafu baadae* utajalilizia baadae kadri unavyoona inafaa, lakini kuchukua zote zote, halafu wanabaki hamna kitu leo huko wewe Waziri Mpango utahakikisha unafuatilia kesho atakuwepo mtu mwingine ambaye ye ye wala hangalii hiyo biashara hifadhi zitakufa. Sasa hapa tunajenga *systems*, tunapojenga *systems* tujenge *systems* ambazo ni *workable, whether your there or your not*.

Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo. (*Makofi*)

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya mwisho ya bajeti katika Serikali ya

Awamu ya Kwanza ya Rais John Pombe Magufuli na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa.

Vilevile naomba kumshukuru *Allah* kwa kunipa uhai na kunitia nguvu mimi kuweza kutimiza majukumu yangu kama Mbunge, pia namshukuru *Allah* kwa kumtia nguvu Rais wetu, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu kwa kukutia nguvu wewe Spika na viongozi wengine wote nchini na kuweza kutekeleza majukumu yao kwa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka wa uchaguzi, tumetimiza miaka mitano ya kuwakilisha wananchi. Lakini vilevile Serikali imetimiza dhamira yake ya miaka mitano ya kuwaleta wananchi maendeleo. Mchangwo wangu wa leo utaonesha ni nini tumefanya kwa miaka mitano ili tunapokwenda kuwaomba wananchi watupigie kura kwa miaka mitano mingine, sisi Wabunge wa CCM tumekuwa tukiishauri Serikali yetu mambo mengi, mambo mbalimbali, lakini vilevile Serikali ilikuwa ikitekeleza llani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri wameeleza kwa kina kabisa katika hotuba zao za makadirio ya mapato na matumizi, utekelezaji wa llani ya Uchaguzi katika kila sekta. Na nitumie fursa hii kuwapongeza Mawaziri wetu wote kwa kazi kubwa mliyoifanya kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 22 Novemba, 2015 Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli alihutubia Bunge, alilifungua na akatoa mwongozo wa Serikali yake katika miaka mitano. Kwa bahati mbaya sana ndugu zetu wa upinzani walikimbia hotuba ile. Lakini nataka kuwaambia kwamba hotuba ile ndio iliyotoa mikakati ya Serikali ya Awamu ya Tano katika kuwaleta wananchi maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na kwa uchache sana nitajitahidi kuonesha kwa ushahidi mambo yaliyofanywa kwa kutumia mizania ile ya hotuba ya Mheshimiwa Rais ya Novemba, 2015.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu mpendwa ndani ya Bunge hili alisema mambo yaliyolalamikiwa wakati wa kampeni na wananchi. Nitakuomba uniongezee dakika moja ama mbili naomba kumnukuu Mheshimiwa Rais; "Mheshimiwa Spika, wakati wa kampeni yapo maeneo yaliyojitokeza kwa kulalamikiwa sana na wananchi, ningependa niyataje baadhi ya maeneo yaliyolalamikiwa maeneo haya ni pamoja na rushwa, suala la rushwa limelalamikiwa sana takribani katika maeneo yote yanayogusa wananchi. TAMISEMI, upotetu wa mapato kushindwa kukusanya kodi, ubadhirifu, matumizi mabaya ya fedha na utekelezaji wa baadhi ya miradi chini ya viwango, wizi, uzembe na kadhalika. Ardhi; migogoro ya wakulima na wafugaji, viwanja, kuhodhi maeneo bila kuyaendeleza. Mipango miji kujenga maeneo ya wazi na kadhalika. Bandari – rushwa, wizi, ubadhirifu na urasimu. Maji – kiwango cha chini cha upatikanaji wa maji safi na salama. Huduma ya maji kupatikana kwa mbali na makazi na kadhalika. TRA – ukwepajji wa kodi, rushwa, ubadhirifu, urasimu na upotetu wa mapato kwa kushindwa kukusanya kodi hasa kodi zinazotakiwa kulipwa na wafanyabiashara wakubwa. TANESCO – kukatika kwa umeme mara kwa mara na uwepo wa umeme wa mgao.

Maliasili na Utalii – ujangili ambao lazima Idara husika inashiriki, migogoro ya mipaka kati ya vijiji na hifadhi, upotetu wa mapato na kadhalika. Huduma za afya – hospitali, huduma kuwa mbali na wahitaji, ukosefu wa madawa, hujuma kwenye vifaa vya vipimo, msongamano wa wagonjwa, tozo zisizostahili, lugha mbaya za watumishi kwa wagonjwa, uhaba wa majengo, vitendea kazi, rasilimali watu na fedha kushindwa kukusanya mapato yanayowahusu."

"Uhamiaji na ajira – kutoa hovyo hati za uraia, vibali vya kuishi nchini kwa wageni, kushindwa kusimamia ajira za wageni hususan kwa kazi zinazoweza kufanywa na wazawa. Elimu – uhaba wa vifaa vya kujifunzia, kujifundishia, michango mingi isiyo ya lazima, malalamiko ya walimu yasiyoisha, mazingira ya kusomea ikiwa ni pamoja na majengo, madawati, ukosefu wa nyumba za walimu. Polisi – malalamiko

ya wananchi kubambikiwa kesi, upendeleo, madai ya askari, ukosefu wa nyumba za askari, ukosefu wa vitendea kazi vyatika. Zimamoto – kuchelewa kufika kwenye matukio, kufika kwenye matukio bila vitendea kazi kama maji na kadhalika. Mizani - kuchelewa kwa magari yanayosafirishwa, wafanyakazi wasanii na wanamichezo, mzigo wa kodi kwa wafanyakazi, haki na maslahi yao na kadhalika. Kero hizi tutazishughulikia kwa nguvu zetu zote. Wizara, Ofisi na Taasisi husika zijipange ipasavyo kutatua kero hizi. Nimetaja baadhi ya kero hizi ili nanyi Waheshimiwa Wabunge mztambue na mshirikiane na Serikali na wadau wengine kuzitatua kwa haraka." Mwisho wa kunukuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naendelea na mchango wangu, Bunge linajua Tanzania inajua na dunia inajua kwamba Serikalii ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli imetatua kero hizi kwa vitendo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikianza na rushwa; rushwa imeshughulikiwa kwa kiwango hakijawahi kupata kutokea. Tanzania sasa hivi katika Bara la Afrika ni kinara wa kupambana na rushwa na hii yote ni kwa sababu ya kazi ya Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli. Kulikuwa kuna taarifa za *transparency international*/huko nyumba zilionesha namna gani Tanzania ilikuwa inanuka kwa rushwa. Lakini Taarifa hii sasa hivi inaonesha Tanzania ni kinara wa kupambana na rushwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza PCCB kwa niaba ya Mkurugenzi wao kwa kazi kubwa wanayofanya kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais na sisi wote ni mashahidi kwamba Mheshimiwa Rais Magufuli hana msalia Mtume na rushwa. Tanzania inajua, dunia inajua uchapakazi wa Mheshimiwa Rais Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye ardhi sisi wote ni mashahidi, kero za ardhi zinatatuliwa. Waziri wa Ardhi Mheshimiwa Lukuvi amekuwa mstari wa mbele kumsaidia Rais kuhakikisha watu hawaporwi ardhi, amehakikisha kwamba wale wote kila mtu anapata ardhi yake kwa wakati na

amehakikisha tumeona wazee, wanawake wajane ambao walikuwa wakiporwa ardhii zao wanarejeshewa, yale maeneo yaliyokuwa yakihodhiwa na wafanyabiashara wakubwa yakiwa hayaendelei, sasa hivi yanafanyiwa kazi yanaendelezwa. Mbali na hapo mapato katika Wizara ya Ardhii yamepanda maradufu. Rais ametatua kero hii kwa vitendo. Tanzania inajua na dunia inajua uchapakazi wa Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima Bulembo maneno haya mazuri sana kwa nini humuelimishi Mheshimiwa Zitto Kabwe? Endelea kuchangia Mheshimiwa Halima. (*Makofii/ Kicheko*)

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Spika, *TANESCO*; kero mojawapo iliyolalamikiwa sana ni kukatika kwa umeme mara kwa mara na umeme wa mgao. Leo hii kukatika kwa umeme imekuwa ni historia. Wananchi wengi wamekuwa na umeme kuliko mwaka 2015. Vijiji 2,300 tu ndio vilikuwa vina umeme wakati Rais anahutubia Bunge 2015. Leo hii vijiji 9,000 vina umeme hili ni sawa na ongezeko la asilimia 400 na Rais hajaishia hapo tu akaona kwamba sasa hivi ndoto ya Hayati Baba wa Taifa ya kujenga Mradi wa *Stigler's Gorge* uendelee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, juzi tumemuona Waziri Mkuu akikagua maendeleo ya mradi na mradi huu naomba kuwaambia Watanzania, huu mradi utazalisha umeme, utakuza uchumi na utapunguza gharama ya umeme kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naenda kwenye madini; kama kuna sekta imefanyiwa mapinduzi makubwa ni madini, sisi wote ni mashahidi. Malalamiko ya wachimbaji wadogo wadogo kutopewa mikopo na sehemu za uchimbaji imekuwa ni historia. Wanapewa maeneo, wanapewa mikopo, tumemuona Waziri wa Madini, kila kona ya nchi tunafungua masoko ya madini sasa hivi. Lakini mbali na hapo tumeingia mkataba ambao utainufaisha Tanzania na Barrick na hivi karibuni tumeona Barrick imetoa dola milioni moja za

Kimarekani kati ya dola milioni 300 sawa sawa na bilioni 250 za Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, haya ndio maendeleo sisi Wabunge wa CCM tunatakiwa kuyatambia, tunatakiwa kutembea kifua mbele, huu ni muda wetu Mheshimiwa Rais, ame-solve malalamiko haya kwa vitendo. Tanzania inajua na dunia inajua uchapakazi wa Mheshimiwa Rais Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye maliasili na utalii, ujangili umekwisha, tembo wanaongezeka, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Maliasili na Utalii najua kazi kubwa inafanywa. Mwaka 2015 Mheshimiwa Rais alipokuwa analihutubia Bunge utalii ulikuwa unaiongezea Tanzania dola za Kimarekani bilioni 2.2. Iakini hivi sasa ninavyoongea utalii unaiongezea nchi yetu dola za Kimarekani billioni 2.5. Haya ni maendeleo makubwa na wanachana wa Chama cha Mapinduzi narudia kusema, huu ndio muda wetu wa kuwaambia wananchi mambo mazuri yanayofanywa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hivi niwalize leo hii nani anasikia ujangili? Hapo nyuma kabla sijawa Mbunge likiwa ni suala zima la Maliasili na Utalii ni ujangili. Leo hii hakuna ujangili, uhifadhi umeongezeka, migogoro kati ya vijiji na wahifadhi imekwisha na sasa hivi vijiji wanapewa maeneo wanaweza kulima na mbali na yote Wizara imeweza kuongeza hifadhi ili kuipa sekta ya utalii nguvu nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye elimu; elimu pia ilikuwa ni moja ya malalamiko ambayo Mheshimiwa Rais aliyazungumzia humu. Serikali ya Awamu ya Tano ilivyoingia madarakani moja kwa moja ikaanzisha elimu bure kuanzia shule ya msingi mpaka kidato cha nne. Tumesikia jana kwa Mheshimiwa Waziri Mpango takribani shilingi bilioni 20 zimekuwa zikipelekwa kila mwaka kwenye elimu bure. Uhaba wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia imekuwa ni historia. Michango isiyokuwa ya lazima imefutiliwa mbali, malalamiko ya walimu yamepungua kwa kiasi kikubwa. Majengo, madarasa, madawati yote imekuwa ni historia na mbali ya

yote Wanafunzi wa Vyuo Vikuu sasa hivi wanapata mikopo yao bila migomo nani kasikia migomo? Hii yote ni malalamiko ambayo Mheshimiwa Rais ameweza kuyatatua kwa vitendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye suala zima la reli; reli ni moja ya tatizo ambalo Mheshimiwa Rais alilalamikia...

*(Hapa kengele iililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Spika, naomba dakika moja nimalizie.

Mheshimiwa Rais, alizungumzia kuhusu pia Shirika la Ndege la Taifa (*ATCL*); Shirika la Ndege la Taifa limeboreshwa kwa hali ya juu. Mheshimiwa Rais alipokuwa akilihitubia Bunge, Shirika la Ndege lilikuwa lina ndege moja na wafanyakazi 200. Leo hii tunavyoongea Shirika la Ndege la Taifa lina ndege nane na ninaomba kuzitaja tuna *Bombardier* nne, *Dreamliner* mbili, *Airbus* mbili na Mheshimiwa Rais atakapokuwa anahutubia Bunge la Kumi na Mbili mwezi Novemba, 2020 tutakuwa tayari tuna ndege kumi. Mheshimiwa Rais ameweza kutatua malalamiko ya wananchi yote kwa vitendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kwa kumalizia kwa kusema Mheshimiwa Rais anarudi kwa wananchi akiwa na majibu yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ili waendelee kufanya kazi za wananchi na ninaomba kuwashukuru vijana wa Mkoa wa Kagera na ninawaambia kwa kunipa fursa hii nawashukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, muda haupo upande wako nakushukuru sana. (*Makofi*)

Nakushukuru sana Mheshimiwa Halima, ila hujajibu swali langu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe na Mheshimiwa Raphael Japhary Michael ajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie hoja iliyopo mbele yangu. Nikianza kumpongeza Waziri wa Fedha na wasaidizi wake kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuandaa bajeti na kutuletea mapendekezo mazuri ambayo kimsingi Serikali imefanya kazi kubwa katika miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kwa dhati ya moyo wangu nimpongeze Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa na nzuri alioifanya kuiongoza Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika Awamu ya Tano akiwa amechukua maamuzi magumu kwa nyakati tofauti kwa lengo la kuleta tija, kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nishukuru kwa miradi mikubwa iliyotekelawa katika Mkoa wa Simiyu, baadhi yake ikiwa Hospitali ya Mkoa. Tumejengewa hospitali ya kisasa binafsi sijalona katika mikoa mingine mimi binafsi. Wananchi wa Mkoa wa Simiyu walikuwa wakitembea umbali mrefu kupata rufaa. Na wengine walikuwa wanafariki kabla hata hawajaanza kupatiwa huduma kwa ajili ya kutembea umbali mrefu. Ni miradi mingi ikiwemo ya barabara, ya maji, barabara nzuri za changarawe zimetekelawa kuititia Mfuko wa Barabara wa Mkoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nishukuru kwa ajili ya Daraja la Sibiti ambalo limekuwa mkombozi na kiungo kwa ajili ya Mkoa wa Singida, Mkoa wa Simiyu na hata Mkoa wa Mara. Wananchi wengi sasa wa Mara wamekuwa wakipitia katika Daraja la Sibiti na sisi Simiyu limetupunguzia gharama kubwa tuliyokuwa tunaitumia kwa kuititia Shinyanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ilikuwa inakulazimu uende Shinyanga kwa nauli ya shilingi 10,000 ulale, ule na kesho yake uanze safari ya kwenda Dodoma mpaka Dar es Salaam. Lakini kwa kupitia daraja hili unaondokea Simiyu na kufika Dar es Salaam ndani ya siku moja. Utakuwa umeokoa muda, umeokoa gharama kubwa ambayo umeipitia kwa kuzunguka Shinyanga. Lakini pia imeleta urahisishaji kwa wananchi kwa kufanya shughuli zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi Mkoa wa Simiyu tunashukuru kwa fedha nyangi sana zilizoletwa za ukamilishaji wa maboma, kwa ajili ya vyumba vya madarasa vya sekondari na shule ya msingi, kwa ajili ya nyumba za walimu. Tumeleteewa fedha nyangi kwa hivyo nguvu za Wananchi hazijapotea bure. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini Mkoa wetu wa Simiyu tushukuru kumekuwepo na ongezeko la maeneo ya malisho na uhifadhi wa mazingira kutokana na Mheshimiwa Rais kuamua sasa wananchi wasibughudhiwe walio kando kando ya uhifadhi. Mkoa wa Simiyu tungeathirika kwa kiwango kikubwa viji vingi sana vingeondoka kwa mfano Wilaya ya Meatu tu viji 31 vingeondoka. Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Simiyu nalishukuru hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini nikiongelea bajeti, unapoongelea pato la taifa huwezi kuacha kuongelea pamba. Nikiongelea pamba naongelea pamba inategemewa kiuchumi na ni mhimili wa uchumi katika Mikoa 17 na Wilaya 56. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niishukuru Serikali kwa mageuzi makubwa iliyoyafanya katika zao la pamba katika miaka hii mitano. Serikali ilipoingia tu madarakani Awamu ya Tano, tatizo la kupunjwa kwa mizani kwa wakulima wa pamba limekwisha mpaka leo imebakia ni historia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa ajili ya Mfuko wa Wakfu (*CDTF*) ambaa uliondolewa mikononi mwa wachache waliokuwa wakiumiliki kwa manufaa yao binafsi na kuupeleka

katika Bodi ya Pamba kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa mapato yanayokusanywa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zilikuwa zinatumwiwa vibaya kwa sababu hakukuwa na maendeleo yoyote katika zao la Pamba, mbegu zilikuwa zinaletwa hafifu, zilikuwa hazioti, madawa yalikuwa yanaletwa hafifu, hayaui wadudu, lakini sasa hivi nashukuru kupitia mfuko huu unasimamiwa vizuri wananchi wanaletewa viuadudu ambavyo vinaua wadudu. Lakini changamoto iliyopo katika msimu huu wa pamba unaoendelea dawa hizi ziliuja chache kwa mara ya kwanza kwa hiyo pale katikati wakati ndio wadudu wanashambulia kukawa hakuna dawa. Iliwalazimu baadhi ya wananchi wakanunue dawa lakini tukikumbuka wananchi mpaka leo hii wakulima wa pamba takribani shilingi bilioni 4.6 hazijalipwa kwa ajili ya wakulima wote wa pamba. Kwa hiyo hii ilikuwa ni changamoto kwa wakulima ambao hawakuwa na fedha.

Mheshimiwa Spika, hii inasababisha sasa kuwasababisha wakulima hawa Pamba yao inunuliwe shambani kabla ya msimu. Kwa kuwa itabidi wakope hela zenye riba ili waweze kununua dawa. Lakini bei hii pia ilikuwa juu kuliko iliyokuwa inanunuliwa *cashshilingi* 22,000 kwa chupa badala ya shilingi 15,000 zaidi ya asilimia 46 faida ndani ya miezi minne. Serikali iangalie pale, bei ni kubwa kuliko ile inayonunuliwa na fedha taslimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nipongeze kwa ajili ya uanzishwaji wa mbegu mpya ya *M08* ambayo imeleta ubora na kuongeza kwa kilo za pamba katika hekari moja ya pamba. Lakini tunapoelekea msimu wa pamba wa kuanza kununua 2020/2021 Serikali imetangaza kujitoa katika kusimamia bei elekezi.

Mheshimiwa Spika, jambo hili halijawahi kutokea, Serikali kuwaachia wanunuzi bila kusimamia bei. Tunaenda kuwarudisha wakulima wetu walipotoka, wakati awamu hii inaanza pamba ilikuwa inanunuliwa kwa shilingi 600 lakini Mheshimiwa Dkt. John Magufuli amepambana pamba ikanunuliwa mpaka shilingi 1,000. Kwa kuwaachia wanunuzi

hawa ndio waelekeze bei itakavyokuwa wakulima wetu tunaenda kuwarudisha nyuma. (*Makofi*)

Ninaomba Serikali iingilie kati kuhakikisha inasimamia bei elekezi, tunajua wanunuzi wanafunga mikataba kwa wakati tofauti, kuna wengine mikataba yenyé faida mingine hasara. Lakini wanunuzi hawa katika kupata faida huwa wanakuwa kitu kimoja. Mimi naamini wanakuwa kitu kimoja kwa sababu gani wana nia ya kupata faida kwa hiyo wenyewe watang'ang'ania katika bei ambayo inawapa faida. Naomba Serikali isiwaacie wakulima maana yake wanaenda kuumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, najua matatizo yamejitokeza katika msimu uliopita kutokana na bei iliyokuwepo, Serikali imefanya makubwa. Kulikuwa kuna kilo zenyé thamani zillzonunuliwa za shillingi billioni 419 lakini Serikali imesimamia fedha nyingi zimelipwa hadi imebaki billioni nne. Tunaomba Serikali sasa iwasaidie wakulima kwa kuweza kutoa chochote ili wakulima wale kulipwa madeni yao ili waweze kuendelea na msimu unaoendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Leah Jeremia Komanya. Mheshimiwa Munde Tambwe.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia bajeti yetu iliyopo mbele yetu. Awali ya yote nianze kukupongeza wewe binafsi kwa kazi kubwa ulioifanya kwenye Bunge letu hili, kwa upendo wako mkubwa ulioonyesha Waheshimiwa Wabunge umefanya nao kazi kwa ukaribu, umekuwa mshauri mzuri lakini pia umekuwa pale kwenye matatizo ukiwaita na kukaa nao na kuwashauri hatimaye tumeweza kufikia tamati ya Bunge letu. Tunakupongeza sana wewe binafsi kwa kazi zako nzuri ulizozifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania kwa kazi kuwaba alioifanya ndani ya miaka mitano. Nimpongeze kama yangu Mheshimiwa Mpango na Naibu wake kwa kazi kubwa lakini nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha kaka yangu Dotto James pamoja na Menejimenti nzima ya Wizara hiyo ya Fedha kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kipindi hiki cha miaka mitano. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia bajeti niombe niongee kidogo kuhusu Jimbo la Ulyankulu. Jimbo la Ulyankulu lina wakimbizi, wakimbizi wale wameandikwa kwenye daftari ya kupiga kura, wakimbizi wale wanaruhusiwa kumchagua Rais, wakimbizi wale wanaruhusiwa na sio wakimbizi sasa hivi ni raia wanaruhusiwa kumchagua Mbunge lakini hawaruhusiwi kumchagua Diwani katika kata wanazoishi kata tatu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niwaombe akiwepo Mheshimiwa Waziri Mkuu au Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI watu hawa wana haki sasa ya kuchagua Madiwani wao wao wenyewe kwa sababu kama wanamchagua Mbunge wao, wanamchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa nini wasipate nafasi ya kuchagua Madiwani. Kwa hiyo, mpaka tunavyoongea Ulyankulu kuna kata 15 lakini kuna kata tatu hazima Madiwani. Niombе Serikali kuititia Bunge hili wapate fursa ya kuchagua Madiwani wa kata hizo tatu tumeshawakubali, wameshakuwa Watanzania sioni sababu tena ya kuendelea kuwanyima haki zao za msingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie bajeti; kwanza nitoe pongezi zangu za dhati kwa Serikali na Wizara nzima ya Fedha kwa kuweza kukuta makusanyo ya bilioni 800 lakini wameendelea kukusanya mpaka tukakaribia trillioni mbili, tulishawahidi kufika trillioni 1.9 kwa hiyo ni pongezi kubwa na ni jambo la kujivunia. Lakini uchumi wetu ulikuwa 6.2% lakini sasa tunaongelea 6.9%, hili ni jambo kubwa na jambo la kujivunia. Lakini kubwa kabisa ni udhibiti wa pesa hizo zilizokusanywa kwa wingi, wamekuwa wadhibiti wazuri wa pesa na hakuna kitu kigumu kama kudhibiti pesa, siku zote tumekuwa tumekusanya huko nyuma, maendeleo hayakuwepo kwa sababu kulikuwa hakuna udhibiti wa pesa. Tuliona kuwa na

mamilioni ya JK, yale mamilioni ya JK yalipotea hivi hatujui yako wapi kwa sababu ya kutokuwa na udhibiti. Kwa hiyo niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kusimamia udhibiti mkubwa wa fedha za Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, udhibiti huu ndio wametusababishia tumepata miradi mikubwa ya kihistoria, Napata taabu kumsikia mtu anasema Serikali iombe msamaha kwa sababu hajatekeleza chochote, huu ni wendawazimu. (*Makofi*)

Mimi niseme hivi ng'ombe anapoanza kukata roho, ng'ombe anapokufa lazima arushe miguu na mikono, ndugu zangu hawa wamekufa, wameshaanza kufa wanarusha miguu, wanarusha mikono, hakuna Mtanzania yeyote utakayemwabia Serikali ya Awamu ya Tano hajafanya chochote iombe msamaha huu ni ujinga na utoto, yaani anaongea vitu ambavyo havi-*apply* kwenye jamii, havi-*apply* kwa Watanzania. Leo hata ukienda kijijini Watanzania wanajua Serikali imefanya kitu gani na kila siku nimekuwa nawaambia hapa tukiwa ndani ya Bunge ....(*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Munde nilitaka tu kukwambia msamahe bure wifi yako. Endelea kuchangia Mheshimiwa. (*Kicheko*)

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Spika, ni wifi yangu na ndio maana katika kutekeleza tukamujiri na mume wake anapata mshahara na anasomesha na watoto wake yeeye, ahsante. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika udhibiti wa hizo pesa ndio maana tumeweza kutekeleza miradi mikubwa ikiwemo *Stigler's, SGR* lakini mradi mkubwa wa kuhamia Dodoma. Katika udhibiti wa hizo hela tumeweza kujenga vituo vya afya, tumeweza kujenga zahanati 1,148 karibu na 1,150, tumeweza kujenga vituo vya afya 482, tumejenga hospitali za Rufaa kumi, tumejenga hospitali za kanda tatu, lakini tumetoa bajeti ya shilingi bilioni 30 kwenye Wizara ya Afya mpaka shilingi

bilioni 270, yote hii ni udhibiti na ukusanyaji mzuri wa mapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumeona mradi mkubwa wa reli ambao sasa hivi umekamilika kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro, tumetumia pesa zetu wenyewe za makusanyo yetu, hili ni jambo la kihistoria ni jambo ambalo halitasahaulika, tumetumia shilingi bilioni 170 lakini tumetumia USD milioni 1.5 pesa zetu wenyewe Watanzania yaani mradi kama huu ni lazima tungkuwa tumekopeshwa, lakini kwa juhudii za Mheshimiwa Rais na Mawaziri wake leo tumeweza kutekeleza miradi mikubwa kwa pesa zetu za ndani. Tumenunua ndege 11 kwa shilingi triliioni 1.27 haya yote ni mambo makubwa ya kihistoria hizi ni *legacy atakaziozachaa* Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli hazitasahaulika kamwe, zitabakia kuwa historia na zitabakia kuwa alama yake kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumetekeleza miradi mikubwa ya maji kwa muda siwezi kuitaja. tumewagusa wananchi wa chini kiuchumi TAMISEMI imekuwa ikitoa asilimia 10 kwenye mapato yote ya Halmashauri kila bajeti yao ya mwaka hela zinatoka kila mapato yanapopatikana asilimia nne kwa vijana, asilimia nne kwa akinamama na asilimia mbili kwa walemavu.

Mheshimiwa Spika, elimu bure tumeshatoa shilingi triliioni 1.03 mpaka sasa hivi ni pesa zetu za ndani ni pesa za kihistoria. Yaani unapata shida mtu anaposimama na kusema hatujatekeleza kitu chochote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi vibaraka wa mabeberu walikuwa wanaita *press conference*, wanasema Tanzania haikopesheki, Tanzania inanuka mikopo, Tanzania imepita yaani haina uwezo tena wa kukopeshwa lakini *IMF* wameweza kutupa *relief* ya dola milioni 25 na wakati wa Corona sisi Tanzania hatukwenda kuomba mkopo, wenzetu waliomba mikopo, lakini vibaraka hawa waliita *press* wakasema tumenyimwa mikopo, hatukuomba mkopo na mpaka hibi ambapo hatukuomba mkopo lakini tulikuwa

tunaendelea kulipa mikopo kama kawaida juu ya janga kubwa la Corona, lakini kwa sababu uchumi wetu uko imara, uchumi wetu ume-stabilize dunia sasa inajua, dunia sasa inaelewa ndio maana wamekubali kutupa *relief* ya dola milioni 25 hii ni sifa kubwa kwa Mheshimiwa Rais wetu, lakini ni sifa kubwa kwa nchi yetu ya Tanzania na tumeonesha kabisa kwamba Tanzania kuna dume moja linatawala ambalo halitaki mzaa wala halitaki masihara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kusema haya naona kengele zimeshanililia niwaombe sasa Watanzania wote wanaonisikiliza hapa Bungeni, lakini walioshuhudia miradi iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano twendeni tukampe Mheshimiwa Magufuli kura za heshima, twendeni tukampe Mheshimiwa Magufuli kura za kumuonesha kwamba tumeona kazi nzuri aliyoifanya, hatuna malipo yoyote ya kumlipa zaidi ya kumuombea kwa Mungu na kumpa kura za heshima. (*Makofi*)

Lakini niwaombe wenzenetu Wapinzani wa upande wa pili najua wanajua kwamba Mheshimiwa Rais amefanya mambo makubwa wakae wajitafakari nafasi ya Urais tumpitishe Mheshimiwa Rais wetu bila kupingwa, twendeni tukagombee kwenye majimbo, twendeni tukagombee kwenye kata lakini kwenye nafasi ya Urais tumpe mzee huyu aliyeleta historia Tanzania apite bila kupingwa ili watu wajue kwamba tunawa-appreciate na tunakubali kazi zake nzuri anazozifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hayo machache niwatakie Waheshimiwa Wabunge wote uchaguzi mwema na Mwenyezi Mungu akipenda tuweze kurejea mjengoni hasa wewe tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu upite bila kupingwa kwa kazi nzuri uliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile tunamuombea Mheshimiwa Rais wetu apite bila kupingwa na Waheshimiwa wote Wabunge mpite bila kupingwa nikiwemo mimi Mheshimiwa Munde ikiwezekana nipite bila kupingwa, ahsanteni sana. (*Makofi/Vigelegele*)

**SPIKA:** Huyo ni Mheshimiwa Mundwe Tambwe Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa ujatuambia upite bila kupingwa wapi? Wanataka kusikia Wanyamwezi.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Spika, saa hizi watanishughulikia maana mambo yangu mazuri. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jumanne Selemani Zedi atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Saada Salum Mkuya na Mheshimiwa Frank Mwakajoka ajiandae.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti kuu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya uya kuweza kusimama hapa na kuweza kutoa mchango huu, lakini pili nimshukuru sana Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika kipindi hiki cha miaka mitano, lakini na wewe pia nikupongeze sana kwa namna ambavyo umekuwa ukiliendesha Bunge letu kwa kipindi chote ambacho tuko hapa, nakupongeza sana mtani wangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la kwanza ambalo ningependa kuliogelea na kuliunga mkono ni mapendekezo ya mabadiliko kwenye Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura 290 ambayo Mheshimiwa Waziri Mpango ameyapendekeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo haya ambayo yanahu ushuru wa huduma wa minara ya simu katika mapendekezo haya Serikali inapendekeza kwamba kuanzia sasa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI ndiye kwa niaba ya Halmashauri atakuwa anasimamia/anakusanya ushuru wa huduma kutoka makampuni yote ya simu halafu anaugawa kwa Halmashauri zote nchini, hili jambo naliunga mkono kwa asilimia 100 kwa

sababu kwa kipindi kirefu Halmashauri zilikuwa zinakosa haya mapato kwa namna ya utaratibu ulivyokuwa. Ilivyokuwa ni kwamba mnara wa simu ambao upo pale Kongwa wa Airtel unazalisha mapato Kongwa, wananchi wa Kongwa ndio wananaunua vocha *airtime* wanapiga simu lakini yale mapato ambayo kampuni ya Airtel inayapata ule ushuru wa huduma badala ya kulipa Kongwa walikuwa wanaulipa yalipo makao makuu yao ambayo ni Manispaa ya Kinondoni, kwa hiyo Manispaa ya Kinondoni ilikuwa inalipwa fedha zote za nchi nzima za minara Halmashauri zote wakati fedha kwenye minara hiyo zinazalishwa ziliko kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, unakuta mnara wa Airtel uko Nzega unazalisha mapato Nzega, lakini kampuni ya Airtel badala ya kuilipa Halmashauri ya Nzega wanailipi Manispaa ya Kinondoni, kwa hiyo haikuwa *fairsana*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa mapendekezo haya yanakoja sasa ni kwamba sasa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ndie atakusanya ushuru wa huduma wote kutoka Airtel, kutoka Voda, kutoka Zantel makampuni yote ya simu halafu utatengeneza utaratibu ambapo sasa fedha hizo zitagawanywa kwa Halmashauri zote nchini na wala sio Manispaa ya Kinondoni peke yake. Kwa hiyo, hili linakwenda kuongeza mapato katika Halmashauri zetu ambazo kwa muda mrefu sana zilikuwa zinakosa haya mapato ambayo minara ipo kwenye Halmashauri inazalisha mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni-*declare interest* nilikuwa nafanya kazi Airtel kabla ya kuwa Mbunge nilikuwa Meneja mauzo wa Airtel Makao Makuu, kwa hiyo unakuta kwamba mwisho wa mwaka inaandikwa cheque moja ya ushuru wa huduma kwa sababu Makao Makuu yako Manispaa ya Kinondoni tunapelekea Manispaa ya Kinondoni *billions* za hela, lakini kumbe hela hizi zilipaswa zisambae nchi nzima kwa sababu minara iko nchi nzima na ina nani kule. Kwa hiyo, mapendekezo haya ninayaunga mkono asilimia 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni hotuba ya Kamati ya Bajeti, imezungumza kwamba Kamati ya Bajeti walikaa

pamoja na *TARURA* ili kutathmini uharibifu wa miundombinu hasa barabara za maeneo ya vijiji ambazo uliletwa na mvua kubwa zilizokuja. Ni kwamba mvua kubwa zilizonesha nchini kwetu zillikuwa na *effectmbili* upande wa kwanza kwa mfano kwetu sisi tulipata maji mengi sisi ni wakulima wa mpunga tukalima mpunga tumevuna vizuri, lakini upande wa pili *effectnyingine* ni uharibifu wa miundombinu, barabara ziliharibika kwa kiwango kikubwa sana. Sasa Kamati ya Bajeti walikaa na *TARURA* wakatathmini uharibifu huo na ikaonekana kwamba inahitajika shilingi bilioni 132 ili kuweza kuzirudisha barabara zote hasa za vijiji nchi nzima ziweze kurudi katika hali yake ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, naungana na Kamati ya Bajeti kuiomba Serikali hizi shilingi bilioni 132 zote zitoke ziende *TARURA* ili *TARURA* waweze kurekebisha miundombinu ya barabara hasa maeneo ya vijiji ambapo barabara illikuwa imeharibika sana, kwa sababu *effectya* barabara kuharibika hasa maeneo ya vijiji moja kwa moja inawaathiri wakulima kwa sababu hata kama wamevuna vizuri kwa mfano kwetu kule tumevuna vizuri sana mpunga mwaka huu lakini kutokana na hali ya barabara ilivyo wanunuzi wa mpunga ili waje mpaka wafike kijiji na hali ya barabara wanafika kule wanaununua mpunga kwa hali ya chini sana na kwa bei ya chini sana.

Kwa hiyo unakuta kwamba pamoja na kwamba mkulima amelima amepata mazao mengi lakini hanufaiki sana kwa sababu ya bei kwa sababu na bei hiyo mnunuzi analazimika kuiweka katika kiwango hicho kwa sababu ya hali ya barabara ilivyo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzo naunga mkoно bajeti hii asilimia 100 kwa sababu ninaridhika na mambo ambayo ni ya kimaendeleo ambayo yanatekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tano. Kule katika Jimbo langu bado ninahitaji fedha kwa ajili ya kuendelea kutekeleza miradi ya umeme vijiji kwa mpango huu wa *REA*. Hali ilivyo sasa hivi ni kwamba mpango unatekeleza vizuri, vijiji vinaendelea kupata umeme na kwa namna ya kipekee

nimpongeze sana Mheshimiwa Kalemani - Waziri wa Nishati na Naibu wake Mheshimiwa Subira Mgusu ambao mara kadhaa wametembelea *physically* Jimboni na kujiona hali ilivyo na kusukuma kwa kasi utekelezaji wa miradi ya REA. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Kalemani sasa ni mwenyeji sana katika vijiji vya Kayombo kule Mwamala kwa sababu amefika mara kadhaa na kuhimiza jambo hilo. Cha msingi ni kwamba fedha za REA zitoke na ushauri wangu mwingine ni kwamba kwa bahati mbaya Mkao wa Tabora tulipewa mkandarasi ambaye katika awamu iliyopita hakuwa na *speed*sana. Mapendekezo yangu ni kwamba *next round* tubadilishiwe tupewe mkandarasi ambaye ame-*prove* kuwa na *speed*nzuri na uwezo mkubwa ili miradi ya vijiji vingi viweze kupata umeme.

Lakini niipongeze sana Serikali kwa Mradi mkubwa wa Maji ya Ziwa Victoria, Mkao wa Tabora sasa kwa kweli tumepependelewa tulipata zaidi ya bilioni 500/600 kuyatoa maji Kahama mpaka Tabora Mjini, lakini kwa namna ya kipekee baada ya maji kufika Nzega mimi pia nimepata karibu bilioni sita kuyatoa Nzega kuyapeleka Bukene sasa ambako zaidi ya vijiji 20 na vitongoji zaidi ya 100, kwa hiyo, naunga mkono bajeti hii kwa sababu nahitaji hizi fedha ili maji yafike Bukene na vijiji 20 na vitongoji 100 viweze kunufaika na huduma muhimu ya maji.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, lakini naunga mkono asilimia 100 bajeti hii na nimalizie kwa kupongeza Mheshimiwa Rais Magufuli kwa namna ambavyo anafanya kazi kwa kasi ya ajabu na nimhakikishie kura kutoka Jimbo la Bukene ni za kumwaga na kama alivyosema Mheshimiwa Obama na Bukene pia huku Mheshimiwa Magufuli huku Zedi, ahsante sana. (*Makofii/Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Saada Mkuya subiri kidogo Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, Mheshimiwa Frank Mwakajoka halafu Mheshimiwa Saada Mkuya.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hotuba hii ya Bajeti Kuu ya Serikali na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu itakuwa ni nafasi yangu ya mwisho ya kuchangia katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hasa katika hoja hii muhimu sana kwa ajili ya *projection* ya namna ya kuweza kulipeleka Taifa mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la kwanza nishukuru sana kwa Serikali kufanikisha ujenzi wa reli ya kutoka Dar es Salaam mpaka Moshi kwenda Arusha kwa sababu itakuwa ni jambo ambalo linakwenda kusaldia sana wananchi wa Moshi na maeneo jirani na Moshi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, wakati Mheshimiwa Waziri anamalizia hotuba yake alisema kwamba anaomba Waziri atakayekuja baada yake kwa Serikali ijayo awe na uwezo wa kuwa mwadilifu na kuwa na uwezo mkubwa wa kuikataa rushwa kwa vitendo na amuogope Mwenyezi Mungu na maneno mengine aliyozungumza katika eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maneno ya Waziri yalikuwa ya msingi sana na yaliyoibeba hotuba yake kwa ujumla wake, lakini inawezekana pia yakaakisi namna ambavyo aliweza kuitumia Wizara ya Fedha kwa kipindi cha miaka mitano. Lakini hoja yangu ni kwamba muda mwingi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na mimi binafsi nimekuwa nikisisitiza umuhimu wa kuwa na mifumo ya taasisi imara katika nchi yetu, kwa sababu tunapokuwa na mifumo ya Taasisi imara hatutatekeleza kwa utashi wa mtu, bali tutatekeleza kwa utashi wa sheria na misngi tuliojiwekea. Kwa maneno haya ya Mheshimiwa Waziri yanatuongoza pale pale kwamba hatuna uhakika kwamba kipindi kijacho tutampata Waziri Mpango. Sasa inawezekana akaja mwingine yoyote yule na

bahati mbaya hakuna anayejua moyo wa mtu umebeba nini na hasa anapokutana na pesa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ukitaka kujua uwezo wa mtu mpe madaraka au mpe fedha. Sasa unawenza ukamuangalia mtu kwa kumtazama tu wakati hana chochote lakini akiwa na chochote ndiyo utakapoju tabia yake vizuri. Sasa unapompeleka Waziri wa Fedha kwenye fedha, halafu hunu misingi uliyomuwekea ya kumlinda ili asiwe mbovu maana yake ni kwamba unapeleka fisi kwenye *butchery* la nyama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hoja yangu mimi hapa ninachosema ni kwamba maneno ya Waziri haya yangetafsiriwa kwamba ni lazima twende kwenye kujenga mifumo imara ya kitaasisi itakayosimamiwa vizuri na Bunge, itakayosimamiwa vizuri na Serikali, itakayosimamiwa vizuri na mihimili yote tuliyonayo ili tuhakikishe kwamba Waziri anapochanguliwa anasimamia misingi ile na hasimamii utashi wake peke yake. Maana yake hatuwezi kuwapata akina Mpango kila siku, hatuwezi kuwapata hao watu ambaeo ni waadilifu kila siku ambaeo watakuwa ni waadilifu kwa utashi wao na siyo kwa utashi wa misingi tulijojiwekea. Kwa hiyo nilikuwa najaribu kuliona hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, niliongea tangu mwanzo wakati tunaamua kuchukua vyanzo vya Halmashauri kupeleka Serikali Kuu, nikasema *tuta-paralyse* Halmashauri, lakini kukawa hakuna usukivu mzuri wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, leo kwa hali hiyo hiyo, tunadhani kwa kuifanya *TANAPA* na mamlaka zingine za hifadhi zifanye kazi vziuri tuchukue tena vyanzo vile vya maduhuli yao tupeleke Serikali Kuu. Nimerudia mara nyingi kusema, kazi *TRA* walizonazo kwa sasa hivi ni nyingi, wala *TRA* hawana *manpower* ya kutosha kukabiliana hata na kazi walizonazo kwa sasa hivi, bado wigo wetu wa kodi ni mdogo, Watanzania wanaolipa kodi ni wachache. Kwa sababu ya *manpower* ya *TRA* tunahitaji kuongeza *manpower* ya *TRA* kwa kazi tu walizonazo. (*Makofi*)

Sasa kwa nini tuendelee kuwaongezea majukumu mengine ambayo tayari yanafanyakazi na yanaendeshwa vizuri? Muhimu kwenye taasisi hizi kama tunahisi kwamba kuna mapungufu ni kuimarisha usimamizi na uratibu, siyo kuwanyang'anya vyanzo hivyo. Ni kusimamia vizuri uratibu kama ambavyo ingekuwa sawa sawa kama mngefanya hivyo kwenye Halmashauri, leo msingepata taabu hii mnayoipata. Leo hapa tayari tunaanza kufikiri Waziri akakusanye *service levy* katika sekta ya mawasiliano ndiyo azirudishe katika hali kama hiyo ni kwa sababu mliamua kuzi-paralyse Halmashauri leo mnakwenda ku-paralyse sekta hii ya utalii na mauzo ya mazoa ya misitu. (*Makof!*)

Kwa hiyo, ni vizuri tuhakikishe tunasimamia vizuri misingi yetu ya mifumo imara ya taasisi ili tuiamrishe usimamizi katika Serikali yetu. Kwa hiyo lilikuwa naomba la kwanza hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ni suala la marekebisho ya viwango vya tozo; Serikali imefanya vizuri sana katika bajeti hii, imerekebisha viwango vingi vya tozo, imefuta viango vingi vya tozo ni jambo jema na hata bajeti iliyopita walifanya hivyo. Ni jambo jema na la kupongezwa sana. Lakini bado tatizo kubwa tulilonalo katika nchi hii ni viwango vya kodi vya VAT na *Corporate Tax* ndiyo tatizo kubwa tulilonalo. Viwango hivyo vinalipika kwa shida ama havilipiki, matokeo yake vimikuwa ni mzigo kwa wafanyabiashara. Wafanyabiashara hawesi kufanya biashara zao vizuri kwa sababu kodi ni kubwa mno ukiongeza na *penalties*, ukiongeza na *interest* hali inakuwa ni mbaya zaidi, Wabunge mvae hili vazi. Mfanyabiashara analetwa kodi ya billioni mbili, billioni tatu analipaje hiyo kodi na ni *auditing* ya miaka mitatu mpaka mitano, analipaje hiyo kodi? Anawezaje kuendesha biashara? Matokeo yake kodi haiwi tena ni *incentives* imikuwa ni sehemu ya kuwa-discourage wafanya biashara.

Sasa ni vizuri tufikiri pamoja na kazi hii kubwa ambayo serikali inafanya ya kupunguza na kufuta baadhi ya tozo ambazo ni kero, lakini lazima ifikiri ni kwa namna gani na ni kwa nini tusifikiri kupunguza VAT kuwa asilimia labda 12 au

11, ni kwa nini tusifikiri kurekebisha *corporate tax* ili wafanyabiashara wetu walipe kwa sababu tukiweza kuongeza wigo wa *tax base* yetu vizuri maana yake ni kwamba hao watu wataweza watakuwa wanaweza kulipa wenyewe bila kusumbuliwa. Kwa hiyo, ni vizuri tuwafanya watu wasukumwe na kulipa kodi, waone kodi inalipika, wasione kodi ni mahali pa kukimbia. Ukimuona Afisa wa *TRA* anakuja dukani kwako unapata kichaa kuliko kumuona simba anakuja maana yake utampiga bunduki. (*Makofi*)

Sasa ni kwa nini tufikie hapo ambapo leo Maafisa wa *TRA* wanaogopeka na bahati mbaya na wao hawana ile lugha ya kibinadamu, ya kikazi, wana lugha ya kifedhuli. Sasa wanapokuja badala yake wanawakatisha tamaa wafanya biashara.

Kwa hiyo, ni vizuri Bunge llijalo tufikiri sana namna gani tutaweza kurekebisha viwango vya tozo za *VAT* na viwango vya tozo za *Corporate Tax* ili sasa tuwasaidie wafanyabiashara kwa ujumla wake. Mheshimiwa Rais ameshakaa na wafanyabiashara, ameshajaribu kuongea nao, akawapa moyo...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niwaambie tu kwamba Mheshimiwa Raphael alishasema maneno hapa kwamba huenda akafikiri vinginevyo kuhusu kurudi au kutokurudi, lakini mnaona mchango wa mtu ambae anaipenda nchi yake, yuko *objective*, hata kama hukubaliani na mawazo yake, lakini unaona anatoa moyoni yale ambayo anayaona. Nakupongeza sana kwa *ku-remain objective* siku zote. Malizia tu mchango wako. (*Makofi*)

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilichokuwa najaribu ni kwamba lazima tuone kwa sababu *after all* sehemu kubwa ya mapato yetu yanatoka kwa wafanyabiashara ni lazima tuwalinde kwa vivu mkubwa sana, mapato yetu makubwa yanatoka kwa wawekezaji lazima tuwalinde kwa vivu

mkubwa sana sasa tutakwenda kwenye kilimo, tutakwenda kwingeine lakini lazima tuone kuwa tutapata katika eneo hilo, kwa hiyo lazima tuwalinde kwa vivu mkubwa sana tusiwabughudhi. Walipe kodi na wasipolipa kodi waadhibiwe lakini tuhakikishe kwamba tunawatengenezea mfumo ambao ni rafiki kama vile ng'ombe wetu wa maziwa kwa hiyo, nilikuwa naomba sana tuliangalie hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni suala la *service levy* kama nilivyosema ya kutoka 0.3 kutoka sekta ya mawasiliano; ni jambo jema sana, katika eneo ambalo Halmashauri zimekuwa zikiathirika ni upande huu wa hii *service levy* ya sekta za mawasiliano kwa sababu Halmashauri zimekuwa haziwezi kutoza hi kodi. Kwa muda wote nilikuwa kwenye Halmashauri, nimekuwa Meya, imekuwa ni vigumu sana kutoza hii kodi na ukweli inawezekana ikaonekana hiyo kodi inakwenda kwenye eneo moja labda la Dar es Salaam siyo kweli pia kwa kiwango cha kutosha kwa sababu inawezekana hata kiwango wanacholipa ni kidogo sana. Kwa hiyo, ni vizuri hili wazi liliiletwa leo kwenye Bunge lako lipitishwe kwa nguvu zote ili sasa hivi *service levy* itozwe na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa halafu ai-disburse kwenye Halmashauri, Halmashauri zitakuwa zimepata mapato ya kujitegemea na kuweza kujidesha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Raphael Japhary Michael. Mheshimiwa Frank Mwakajoka sasa iga mfano sasa, halafu Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kushukuru kwa nafasi hii, lakini niwashukuru pia wananchi wangu wa Mji wa Tunduma kwa jinsi ambavyo wameendelea kuniunga mkono na bado wananihitaji sana na niko imara sana. Inawezekana niko imara kuliko hata Kongwa pale. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa tunakuja Tunduma. (*Kicheko*)

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wale wote ambao wanajiandaa andaa, wajipitisha pitisha...

**SPIKA:** Tunakuja.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:**...nafikiri watakulua walikopeleka mboga, lakini nilikopeleka fedha za mboga mimi uhakika ni mkubwa na najua kabisa nitashinda kwa kishindo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nikishukuru sana chama changu, nimshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Chama, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbewe kwa uongozo wake bora na kuhakikisha kwamba chama kinakuwa imara na najua kabisa Chama cha Mapinduzi pamoja na Serikali hawalali kwa sababu chama kinaendelea kustawi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba upinzani imara katika nchi yoyote kutakuwa na maendeleo imara, lakini kama kutakuwa na upinzani ambao ni dhaifu kama ambavyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi inahitaji upinzani dhaifu na kuendelea kuona wale wote ambao wanaondoka kwenye chama hiki wanastahili kuliko wanaobakia watakuwa anapoteza muda wao. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka hiyo ni ukurasa wa ngapi wa hotuba ya Waziri?

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ni utangulizi, ni utangulizi kama Munde. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mimi niseme tu kwamba nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Mpango na natarajia kuichangia vizuri kama ambavyo nimejipanga na kama ambavyo nimeona na muda wote ambao Serikali ya Awamu ya Tano imekuwepo madarakani imeweza kufanya, nataka na mimi nizungumze na ikiwezekana niwakosoe na kuwalekeza maeneo yote ambayo hamjafanya vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ukweli tu tunakwenda kwenye Uchaguzi Mkuu mwaka huu na kama tunakwenda kwenye Uchaguzi Mkuu mwaka huu matarajio yetu makubwa sana ni kuona kwamba Taifa letu linabaki kuwa imara na Taifa letu linabaki na amani ya kutosha. Ili kuwe na amani ya kutosha ni lazima haki isimame na itendeke kweli kweli. Wananchi wamejiandaa vizuri kupiga kura, tunaomba Serikali pia ihakikishe kwamba inatumia nafasi ya wananchi ambao tayari wamejiandikisha na wanatakiwa kupiga kura waweze kupiga kura zilizo huru na zilizo na haki. Haya ambayo tunayasililiza kwamba watakimbia na fomu, Wakurugenzi hawatakuwepo maofisini nafikiri tunatoa tahadhari kwa mapenzi mazuri ya Taifa letu; tunahitaji amani, tunahitaji nchi yetu iendelee kuwa salama kabisa. (*Makofi*)

Ninaamini kabisa kwamba trumefanyakazi kubwa sana kama Upinzani tangu kipindi ambacho wananchi wametuamini mpaka sasa hivi kwahiyo tunatarajia kurudi wote na tutaongezeka zaidi kama ambavyo wananchi wameendelea kutuamini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na ulisema kwamba tutakuwa wawili, naamini kabisa hatutakuwa wawili, tutakuwa wengi na Mungu akijaalia kwa kweli tulikuwa tunafikiri hicho kitin sisi tukikalie siku moja kuhakikisha kwamba Watanzania waone mawazo yetu na ni namna gani tutaongoza Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nafikiri nakwenda sasa kwenye mchango wangu; nataka nianze na hotuba ya Mheshimiwa Mpango. Nilikuwa naangalia vipaumbele vya Serikali hii ya Awamu ya Tano ambayo muda wote imesema kwamba ni Serikali ya wanyonge.

Nimejaribu kuitia kwenye Wizara ambayo inahudumia Watanzania karibuni asilimia 65 mpaka 70, Wizara ya Kilimo siyo kipaumbele kabisa katika Serikali ya Awamu ya Tano na hii imekuwa ni tatizo miaka yote. Miaka yote tunashauri, tunajaribu kuelekeza ni namna gani kilimo kwa nini inakuwa siyo kipaumbele katika Serikali hii, lakini hakuna

hata simu moja tumepesta majibu ya kutosha kwanini Serikali hii haionti kilimo kinahitaji kuwa kipaumbele katika nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunajua kabisa kwenye chakula, asilimia 65 mpaka 70 kilimo kinachangia, lakini ukienda kwenye ajira kinachangia kwa asilimia kubwa kabisa na tunajua kabisa katika nchi yetu, watu wanaohitimu kwenye vyuo vikuu mbalimbali kwenye nchi hii ni karibuni watu 800,000 hizo ni takwimu za Serikali, lakini kati ya watu 800,000 wanaokwenda kupata ajira rasmi hawazidi 40,000. Wale watu wote wanaobakia wanakwenda kujiajiri kwenye kilimo, ufugaji na uvuvi, lakini Serikali haionti kama ni eneo muhimu sana la kupeleka fedha kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata huduma na mmekuwa mnasema sana ndani ya Bunge kwamba Watanzania wanatakiwa kijiajiri, wanajiajiri namna gani wakati maeneo muhimu ambayo wangeweza kujiajiri kama kwenye kilimo, ufugaji na uvuvi hampeleki fedha kule? Kwa hiyo, tulikuwa tunafikiri...

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, tulikuwa tunafikiri ni vizuri sana...

**SPIKA:** Pokea taarifa Mheshimiwa Frank.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, si uliwaambia kwamba watapata dakika tatu/tatu hawa vipi tena?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

## TAARIFA

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kumpa taarifa Mheshimiwa Mwakajoka kwamba bajeti hii imejikita sana kwenye kuwezesaha viwanda vya ndani kuwa na uhitaji mkubwa wa malighafi

ambazo zinatoka kwenye sekta ya kilimo, kwa hiyo, anavyosema kwamba hatujawekeza kwenye kuendeleza kilimo ningependa kwanza asome bajeti vizuri aone namna Serikali ilivyojipanga vizuri katika kufungamanisha kilimo na ujenzi wa uchumi wa viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba apokee taarifa hiyo. (*Makofii*)

**SPIKA:** Anachokwambia ni kwamba ukiangalie kilimo katika mapana yake, usiangalie kilimo kwa jicho *very narrow*, uliangalie katika mapana yake na mawanda yake utaona bajeti *ime-cover* ndiyo hoja yake sasa na wewe njoo na ushahidi wako sasa.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, mimi nasema na nina ushahidi wa kutosha na imekuwa ni mara zote kwenye bajeti hizi na ndiyo maana ukiangalia mwaka 2016/2017 tulitenga tu shilingi bilioni 101 tukatoa shilingi bilioni tatu kwenye kilimo. Mwaka 2017/2018 tulitenga shilingi bilioni 150 tukatoa shilingi bilioni 16 kwenye kilimo, mwaka 2018/2019 tulitenga shilingi bilioni 95 tukatoa shilingi bilioni 45 tu kwenye kilimo. (*Makofii*)

Kwa hiyo, haya ninayoyazungumza nayazungumza ni mambo ambayo yako wazi, lakini pia ukienda kuangalia kwenye vipaumbele katika bajeti hii utaona kabisa ni Bwawa la Mwalimu Nyerere, *Standard Gauge*, utaona ndege na mambo mengine. Kwa hiyo, ninachokizungumza mimi mazungumza namaanisha, sizungumzi tu kwamba labda nazungumza tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini tunakumbuka kabisa katika miaka iliyopita, mwaka 2017/2018 mchango wa kilimo kwenye Pato la Taifa ilikuwa ni asilimia karibuni 30 mpaka 31 leo mchango wa Taifa kwenye pato la Taifa unaotokana na kilimo umeshuka mpaka asilimia 26 kwahiyio inaonyesha jinsi gani ambavyo Serikali haioni umuhimu wa sekta ya kilimo kuhakikisha kwamba inachangia pato kubwa la Taifa katika nchi yetu. Kwa hiyo, haya yote...

**SPIKA:** Hata hizo ndege ambazo zinaagizwa na umesema ukweli vizuri tu, nazo pia zinaboresha kilimo, yaani kweli kabisa ametuambia Waziri kuna ndege tunasubiri *Boeing 787-8 Dreamliner* halafu inakuja na nyingine *Haveland 8-400*.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika,...

**SPIKA:** Nilitaka kukuunga mkono ulisema ndege zinaagizwa nikataka kusisitiza tu. Endelea kuchangia.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, nilichotaka kusema ni kwamba tukiboresha kilimo tutakuwa na uhakika hata wananchi wetu hawa wakiwa na uwezo watakuja kupanda ndege, lakini sasa hivi tukiwa tunasubiri tu kwamba watu watoke Jamaica, watoke Italy, watoke maeneo mengine na nchi zote ambazo tayari zimekuwa na ndege nyingi wanajitahid kupata hata asilimia 50 au 45 ya wananchi wao kupanda ndege. Sasa kama tutaendelea kuwaona wananchi wetu wanaendelea kuwa masikini ila tunasubiri tu wageni watakaokuja au tutakapoisafirisha mazoa yetu hilo jambo ni lazima tufike mahali tulitazame kwa jicho lingine.

Mheshimiwa Spika, wako wananchi ambao wali-supply pembejeo mwaka 2014/2015, mwaka 2015/2016; unaona taarifa hii hapa ni barua mbalimbali zilizokwenda kwa Waziri Mkuu, zimekwenda kwa Waziri wa Fedha na majibu yake kwamba mawakala ambao walisambaza pembejeo za kilimo kwa wananchi hasa Mkoa wa Rukwa na Mikoa mingine ya Mbeya, Songwe na maeneo mengine hawa wananchi walikaa na Waziri Mkuu na Waziri Mkuu akatoa barua kwamba hao watu ndani ya mwezi mmoja walipwe mwaka 2017 leo mawakala hawa hawajalipowa fedha zao na Wizara ya Fedha ilishafanya uhakiki. (*Makofii*)

Kwa hiyo, wakati Waziri anakuja kutoa ufafnuzi ajaribu kutueleza ni namna gani ameweza kukiuka maagizo ya Waziri Mkuu aliyetoe maagizo ya kwamba wananchi hawa walipwe ndani ya mwezi mmoja baada ya kuhakikisha kwamba

wamegawa mbolea kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini. Kwa hiyo, wananchi hawa ambao ni mawakala wameuziwa nyumba zao na mabenki, wamefilisiwa na wengine wamekufa kwasababu wanaidai Serikali fedha nyingi na Serikali haitaki kuhakikisha kwamba fedha hizo zinatolewa ili...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Naambiwa ni kengele ya pili Mheshimiwa.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, niongezee hata mbili si unajua tena umeniingilia ingilia sana? *(Makof)*

**SPIKA:** Haya nakuongeza dakika mbili za kuaga. *(Kicheko)*

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, nilichotaka kuzungumza hapa ni kwamba tulikuwa tunaomba Serikali sasa iwalipe wananchi hawa fedha zao, wanadai mabilioni ya fedha. Leo ukiangalia kwenye taarifa ya Waziri anasema amelipa madeni, lakini nimejaribu kuititia madeni walioipa hakuna wakala hata mmoja aliyelipwa fedha hizi. *(Makof)*

Kwa hiyo, tunaomba hawa mawakala walitoa huduma kwa wananchi waweze kulipwa fedha zao ili waendeshe maisha yao na ikiwezekana walipe mikopo ilioko benki, lakini kama tutaendelea kufanya hivi na kesho mnakwenda kwenye uchaguzi hawa mtawakuta, watakwenda kuwahuliza kwamba kwa nini hamjatulipa fedha zetu na hawa ndiyo ambao wanawapigia kura na walipeleka pembejeo kwa wapiga kura. Kwa hiyo ninaomba mlipe mapema ili msikilizwe hata kidogo kwa sababu hamtasikilizwa kabisa. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine wafanyakazi/ajira, miaka mitano ya Serikali ya Awamu yetu ya Tano hakuna

ajira kabisa zimefanyika, ajira ambazo zimefanyika, Waziri anatakiwa anatakiwa atueleze hapa anatakiwa atupe takwimu kwamba Awamu ya Nne kila mwaka walajiri watu wangapi? Lakini awamu hii kwa nini watu wanalamika hawaajiriwi tatizo ni nini? Kwa nini hatuoni ajira ambazo zinakuwa ni rasmi watu wanaajiriwa, vijana wetu wanakwenda shule wanamaliza shule hampeleki fedha kwenye maeneo mengine ambayo ni kilimo na ufugaji ... (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Frank.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Halafu bado hamtaki kuajiri. (*Makof!*)

**SPIKA:** Dakika mbili zimeisha ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya sasa na Mheshimiwa na Dkt. Charles John Tizeba ajiandae.

**MHE. DKT. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hoja, kabla sijaenda kwenye hoja nataka nikuombe jambo moja, tunakutarajia utakuwa Spika hata katika Bunge Ijalo *Inshallah*. Sasa unakazi kubwa sana ya kutoa elimu kwa Wabunge kabla ya kuanza mjadala wa bajeti hizi shida ndogo ndogo tunazozisikia zitaondoka *it simply* kwa sababu tuna shindwa ku-connect baina ya mambo yalivyo katika bajeti. Leo ukizungumzia kwamba kilimo hahijapewa kipaumbele, lakini fedha hizo za vijana wanaotaka kwenda kusomea kilimo zinapitishwa Wizara ya Elimu kama mikopo.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile kuna masuala ya kuimarisha afya za watu ambao wana-*engage* kwenye kilimo zinapitishwa Wizara ya Afya. Lakini vilevile kuna masuala ya sayansi na teknolojia ambayo mifumo hiyo itatumika kwenye kilimo inapitishwa katika Wizara ya Elimu, tunazungumzia masuala ya maji, maji ni kilimo fedha zinakwenda katika Wizara ya Maji. Kwa hiyo, unajukumu kubwa sana ili tuone kwamba majadala wetu wa bajeti unakuwa una tija zaidi huko tunakokwenda. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine nilikuwa nataka kuongezea kidogo pale ambapo nilikuwa nimempa taarifa mzungumzaji yule, lakini akajaribu kupotosha, shida yetu ndiyo, shida yetu kubwa ndiyo hii kwamba tunaangalia mambo kama kitu kimoja na tuna-stick hapo hapo. Katika ulimwengu wetu huu wa leo Mabunge yetu, ambao wananchi wanatutegemea tuje kuwasema hatuwezi tukaangalia mambo kwa *so narrow minded* tunaweza tukasema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, unajuwa mtu unaposoma sema mwaka 2010 kulikuwa hivi, mwaka elfu kumi na ngapi kulikuwa hivi bila ya kuangalia *underlined measures* inakuwa unapotosha tu na tunazungumzia siasa *rather than scientific thought towards issues*.

## TAARIFA

**SPIKA:** Mheshimiwa Saada tusubiri Taarifa

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, nampa taarifa Mheshimiwa Saada anasema ananipa taarifa wakati anachangia kwamba...

**SPIKA:** Hapana haikuwa ya kwako hiyo.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ameniambia amesema ananipa taarifa kwa sababu..

**SPIKA:** Hapana siyo ya kwako hiyo.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Ya kilimo, nakuomba Mheshimiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoja hakuongelei wewe, kabisa kaa utulie.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, kanipa ..nilitaka nimjibu Mheshimiwa.

**SPIKA:** Hapana hajakupa wewe, mimi ndio nakataa. Tuendelee Mheshimiwa Saada endelea.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Spika, tumerudi pale pale.

Mheshimiwa Spika, nataka nimpongeze sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na mafanikio makubwa ambayo yamepatikana katika kipindi cha miaka mitano, hakika hili ni jambo la kupigiwa mfano, jambo la kupigiwa mfano Tanzania, jambo la kupigiwa mfano Afrika Mashariki, lakini mambo ya kupigiwa mfano katika dunia, hakika uongozi wa Rais ambao amekuja na *approach* mpya kabisa ya uongozi, ni kitu kipyaa na kinapaswa kuigwa, ni lazima tuwe tunamtazamo mpya na kwa nini nasema hivi?

Mheshimiwa Spika, unajua mara nydingine tunaweza tukaona mambo yanakuwa yanakwenda sawa, lakini anapokuja mtu mwingine akaona kwamba twende huko tunakotaka kwenda, lakini katika mtazamo mwingine na tunaona mambo yanakwenda *speed* kabisa hayo ndiyo maendeleo ambayo tunayatafuta. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maendeleo siyo kitu tunasema leo halafu kesho ndiyo tumefika, maendeleo *is the process*, yaani ni mchakato mrefu, lakini tunashukuru kwamba katika kipindi cha miaka mitano tumekuja na mtazamo mpya kabisa wa jinsi gani tunaweza tukaendesha mambo. Pongezi hizo kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini vilevile pongezi hizo ziende kwa wasaidizi wake Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Waziri Mkuu na Serikali yote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Naibu wake na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kufanikisha hili ambalo leo tunaendelea kulijadili. Nina hoja mbili tatu ambazo naomba tu, tuziangalie tunajuwa kwamba tuko katika bajeti ya mwisho lakini siyo vibaya kwa sababu Serikali yetu itaendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, tuangalie suala la Corona limekuja kama ni changamoto ya kiuchumi na ya kiafya, lakini *actually* imetupa nafasi ya kuweza kuji-*engage* katika utafiti zaidi hususani kwenye taasisi yetu ambayo imesimama *COSTECH* lazima ingalie ni jinsi gani itaweza ku-*engage* watu zaidi ya kuweza kufanya utafiti kwenye hili namuomba Mheshimiwa Waziri kupitia kwako Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa ofisi yetu ya *COSTECH* iliyopo Zanzibar ile ndiyo ofisi inayosimamia masuala yote ya *Research and Development* kwa upande wa Zanzibar ipo lakini bado tunashukuru kwa hatua ilipofikia tunajengo nzuri pale Maruhubi, lakini suala la watumishi bado ni changamoto.

Lakini vilevile hata ukiangalia *organigram* ya *COSTECH* kwa hatuoni ofisi ya Zanzibar ina-fit wapi, kwa hiyo tunaomba kwamba kipaumbele vilevile katika masuala hayo ya sayansi na teknolojia ni pamoja na kuimarisha ofisi yetu ya *COSTECH*. Nampongeza sana Dkt. Afua anafanya kazi kubwa sana na nzuri kule Zanzibar, lakini sasa ili tumuongezee nguvu anahitaji kuangaliwa katika mtazamo mpana zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la utalii nilikuwa na mimi nina mtazamo kama ambao uliokuwa umeuona kwamba kwa mfano hizi taasisi zetu za *TANAPA* siyo taasisi ambazo tunaweza tukasema mapato yote yaende katika *approach* ile ya Hazina kwa maana kwamba *TRA* ikusanye, halafu irudishe ndiyo iendelee, unajuwa *tourism* ni jambo ambalo linahitaji *innovation* *creativities*. *Tourism* siyo kitu ambacho siyo *destination* inawezekana na bahati nzuri Afrika utalii wetu unafanana kwa hiyo ili wewe kuwa bora zaidi kuliko mwenzako ina maana lazima utafute *innovation*, *uwe innovating* zaidi. Kwa hiyo haya mashirika yetu ni lazima yawe yanapata *muscles* kuwa na *innovation* na *creativities*, wenzetu wa Kenya jana wametangaza bajeti yao na katika jambo moja ambalo tunakuwa tuna *stick competition between* yaani hizi katika nchi za Afrika ni sisi na Kenya.

Mheshimiwa Spika, jana wao katika kuangalia mambo kwa mapana yake wame-*abolish landing fees*, na

*parking fees za ndege, hiyo ni kwa sababu ya kuvutia ndege zinazokuja pale zisiwe zina-*incar cost* na kwa maana hiyo watalii wanapokuja maana yake watakuwa wanapata *ticket* za ndege bure kabisa. Nadhani katika nchi zetu tunajaribu kutafuta kila aina ya mambo ili tuweze kuwavutia watalii wanapokuja.* (Makofi)

Kwa hiyo, tunapochukuwa hii *approach* kwa mashirika yetu kama *TANAPA* na mengineyo tunawanyima fursa ya kuwa *innovation* kwa sababu mchakato wa *TRA* kukusanya hiyo kodi, kodi inakwenda katika Mfuko Mkuu kutoka sasa kuanza kuwa na harakati za kiutalii inakuwa ni ngumu. Kwa hiyo, naomuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha utalii ni jambo ambalo ni very *fragile*, lakini very *competitive*, tuangalie haya mashirika yetu katika jicho lingine rather than kuiachia katika huu mlolongo wa Hazina. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika jambo lingine Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametengeneza vizuri mfumo huu wa kodi na amefanya mabadiliko mengi katika Kodi hii ya Ongezeko la Thamani. Nilidhani Mheshimiwa Waziri toka mwaka wa mwanzo tumekuwa tukizungumza angalau upate fursa ya kuangalia *VAT* ya *goods* ambazo zinanunuliwa kutoka Tanzania Bara zinakwenda kutumika Zanzibar *destination principle*, tunajua kwamba unaweza uka-create matatizo, lakini kwa sababu sasa hivi tumetengeneza mifumo bora ya usimamizi wa fedha, mimi nadhani hili jambo linawezekana. (Makofi)

Mheshimiwa Waziri hebu angalia kwa mapana yake unanunua bidhaa Tanzaniza Bara unakwenda unatumia bidhaa hiyo Zanzibar; Tanzania Bara, unatozwa *VAT*, Zanzibar unatozwa *VAT*bado kunakuwa kuna ugumu wa husuani wa maisha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahante sana Dkt. Saada.

**MHE. DKT. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Spika, dakika moja naomba ili la Nishati Mheshimiwa najua kwamba Mheshimiwa Waziri atakuja kunijibu.

Mheshimiaw Spika, tumefanikiwa katika VAT, lakini kwenye gharama bado na mlolongo wa mazungumzo, mlolongo wa mazungumzo ni mrefu, hauishi wananchi wanaumia. Tunaomba walichukuwe kwa mtazamo mpana zaidi kwa ajili ya kuweka unafuu wa maisha kwa upande wa wananchi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninaipongeza sana Serikali kwa ajili ya *speech* hii. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Dkt Saada Mkuya. Mheshimiwa Dkt. Charles John Tizeba, hayupo. Basi Mheshimiwa John Peter Kadutu.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi ili kuzungumza katika mjadala wa bajeti. Kabla sijasema nimpongeze na kumshukuru dada yangu Mheshimiwa Munde, Mjumbe wa Kamati Kuu kwa kuwasemea watu ya Ulyankulu, nina imani tutaelewana tu mbele ya safari. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii nikushukuru wewe binafsi na uongozi wako pamoja na Naibu Spika, pamoja na Katibu wa Bunge na Wabunge wote kwa ujumla. Azma yangu ya kutokugombea Ubunge mwaka huu niliisema kabla hata Jimbo halijapatikana. Nikaja kusema ndani ya Bunge miaka mitatu iliyopita.

Namshukuru sana Mwenyezi Mungu sasa tumbakiza siku chache jambo hili litakaa vizuri. Kwetu sisi Unyamwezini mtu anaheshimika kwa kufuata yale aliyokwisha kuyasema na mimi ninafuata mle mle, lazima kufika mahali unatelekeza yale uliyokwisha kuyasema. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, na ndio maana pamoja na maombi mbalimbali nimeshika msimamo wangu kwamba...

**MBUNGE FULANI:** Umebadilisha maamuzi.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Acha bwana.

Mheshimiwa Spika, kuna watu hapa wanataka kunichanganya maneno. Sijabadiilisha uamuzi, nitaendelea kuwa na uamuzi huo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Magufuli, kwa maendeleo mbalimbali tuliyoyapata kama nchi, lakini kama Jimbo la Ulyankulu, pia nichukue fursa hii nimshukuru Rais wa Awamu ya Nne Mheshimiwa Jakaya Kikwete kuturuhusu kupata hili Jimbo. Wewe Mheshimiwa Spika ulikuwepo hapa Bungeni mwaka 2010, kura za maoni zilikuwa zinaenda kupigwa kesho yake Jimbo likafutwa dakika za mwisho kabisa kwamba hawa Wanyamwezi bado, lakini baadae Mheshimiwa Kikwete mwaka 2015 kabla hajaondoka tukapata Jimbo na sasa Kadutu ndio Mbunge wa kwanza wa Jimbo la Ulyankulu. Mama Kikwete tupelekee salamu sana kwa mzee bado tunamkumbuka sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwashukuru wapiga kura wa Ulyankulu kwa kuniamini na kunisikiliza pamoja na changamoto nyingi tulizonazo, lakini nina imani Mbunge atakaekuja atayapigania yote yale ambayo tumekuwa tukiyapigania. Niwashukuru wanangu Rhoda, Peter, Laurent na Didas pamoja na wajukuu zangu kwa kuniunga mkoно toka wakati wa kampeni mwaka 2015. Lakini bila kuwasahau wasaidizi wangu wa Jimboni Mheshimiwa Diwani Lufungija pamoja Ezra Kigati. Kwa kweli wamenisaidia sana kufanya kazi zangu za Ubunge ziwe nyepesi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bila kuwasahau Mawaziri wote wakiongozwa na Waziri Mkuu Mheshimiwa Majaliwa pamoja na wafanyakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumze kidogo sasa kwa nini natoa shukrani hizi. Ulyankulu kama nilivyosema ni Jimbo jipya, Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ni mpya kama ambavyo wamesema Mheshimiwa Sakaya, amesema Mheshimiwa

Munde. Halmashauri ya Kaliua pamoja na upya wake tunafanya vizuri, *performance* yake ni nzuri, hesabu zinakwenda vizuri kila jambo linakwenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Jimboni upande wa afya tulikuwa hatuna hospitali sasa tunazo hospitali tunavyo vituo vya afya karibu maeneo yote na vingine viro kwenye hatua ya ujenzi tunaenda vizuri. Kuhusu nishati nichukue nafasi hii kumshukuru Dkt. Kalemani kwa kutusaidia kupata umeme, tumebakiza kata mbili tu, maeneo mengine yote yatakuwa na umeme na kujazia jazia vijiji ambavyo havijapata umeme. Kwa upande wa elimu tumeongeza sana sekondari na shule za msingi kwa hiyo sasa hivi watu wetu watoto wetu hawaendi mbali kupata elimu. Kuhusu miundumbinu tuna barabara hasa tatu, barabara inayotoka Kahama ambayo tunaisemea kila siku Kahama – Ulyankulu – Kaliua na kwenda Mpanda hiyo bado ipo kwenye mpango tunajua Serikali ni siklu itateleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini tuombe sana juu ya barabara inayotoka Tabora Mjini kwenda Ulyankulu; barabara inayotoka Ulyankulu kwenda Urambo na zile barabara ambazo Mheshimiwa Rais aliahidi na bahati nzuri wiki iliyopita tulikuwa na Mheshimiwa Jafo amekwisha kutuhakikishia kwamba jambo hili litafanyika. Kuhusu maji, baada ya kutengwa na miradi mikubwa ya maji sasa maji tutapata kutohana na ujenzi wa bwawa kubwa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho niruhusu kidogo tu niseme jambo moja nilikuwa na mambo mengi lakini kwa sababu ya shukrani. Liko jambo moja lilitunganisha Waheshimiwa Wabunge, nalo ni michezo. Michezo lilitunganisha bila kujali vyama vyetu bila kujali vyeo vyetu ndani ya Bunge tukawa wamoja na Mheshimiwa Spika nikushukuru sana kutusaidia na hasa kusaidia kazi yangu mimi. Kuna wakati mimi na wewe tulikuwa tunapigiwa simu usiku saa nane na hasa wakati wa mashindano ya Afrika Mashariki na kwa kweli Waheshimiwa Wabunge na wafanyakazi wote mimi nawashukuru kwa kuniheshimu na kunipa ushirikiano mkubwa sana wakati tunaongoza michezo hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ulinisaidia sana unakumbuka kuna wakati, niseme kuna wakati tulileta orodha ya majina ya wanaosafiri utadhani tunaleta jina la Waziri Mkuu Bungeni. Ilikuwa ni siri kubwa kabisa lakini Waheshimiwa Wabunge na wafanyakazi mlitupokea, mlitusikiliza, mltuelewa na kwa kweli nitawa-*miss*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme leo niiteni siku yoyote nitakuja kusaidia kuona timu yetu ya Bunge inafanya vizuri kama nilivyosema juzi kwenye *ma-group* bado tuna deni. Uganda imeendelea kutusumbua kwenye michezo, wanatufunga, wanatupa migogoro. Niwaombe sana mtakaporudi tuweke mikakati ya kushinda kupata ushindi wa jumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi niwatakie heri wote na hasa wa Chama changu cha Mapinduzi. Turudi hapa, lakini mimi nipo tayari nitapanda majukwaani na bahati nzuri jambo moja hamfahamu mimi ni msanii, ni mtunzi wa nyimbo, tutapambana mpaka CCM ipate ushindi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, sana, sana, hakika imekuwa ni vyema umekuwa ni msemaji wetu wa mwisho asubuhi ya leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Kadutu tunakushukuru sana kwa ushirikiano mkubwa ambao umetupatia. Tulikuheshimu sana, ulituongoza sana hasa katika michezo na maeneo mengine yote. Umefanya kazi yako vizuri na hakika ni ndoto ya kila mwanasiasa ufile siku fulani ung'atuke kama Mwalimu Nyerere alivyofanya. (*Makofi*)

Ni heshima sana kuliko unakwenda mpaka unapigwa chini chali, ni heshima sana. Kwa hiyo wote tunaiombea sana siku ya namna hiyo *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatuweka huko mbele lakini tunakutakia kila la heri ukipita Dodoma hapa watani zako Wagogo wapo. Tutakupokea vizuri hutolala njaa, ugali kwa mlenda upo kabisa.

Nimeshangaa tu Mheshimiwa Mwakajoka hakuchukua nafasi hii kuaga vizuri mmeona mfano wa Kadutu, sasa wewe nimekupa dakika zote nimekupa na mbili za nyongeza kwamba utaaga. Maana yake hilo Jimbo la Tunduma hili tumeshali-target tayari, tumeshaliweka katika rada za CCM. (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Hata la Kongwa.

**SPIKA:** Hata la Kongwa eee, ahsante sana. Ndio uzuri wa Bunge walioko nje ya hapa wanafikiri Bungeni hapa tunaishi kwa uadui na nini kumbe ni marafiki wakubwa kabisa. Tunafanya kazi kwa pamoja, tunatofautiana tu mambo fulani fulani ambayo baadhi ya wenzetu wanashindwa kuyaona hasa haya ya Chama cha Mapinduzi mazuri kabisa. (*Makofi*)

Tutaendelea na mchango wetu na unaendelea vizuri tu na wachangiaji wengi wazuri sana. Kwa hiyo tutaendelea jioni Dkt. Kamala utatuanzishia, Mheshimiwa Kitwanga atafuatia, atafuata Mheshimiwa Charles John Mwijage, na upande wa upinzani pia wote ambao majina yenu ninayo nitajitahidi mpate nafasi leo na wengine kesho, nina hakika kabisa kwa sehemu kubwa ya wachangiaji wetu watapata nafasi. Kwa hiyo, tuendelee kujiandaa bila wasi wasi wowote. (*Makofi*)

Basi kwa nafasi hii sasa nisitishe Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 leo jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitisha hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Bunge lilirudia Saa 11.00 Jioni)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaomba tukae.

Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH- KATIBU MEZANI:**

## **HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2019 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 – Wizara ya Fedha na Mipango**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea kama nilivyoahidi asubuhi sasa tunaanza na Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala na atafata Mheshimiwa Charles Kitwanga

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii muhimu ya kuchangia ajenda iliyombele yetu ajenda ya bajeti ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kunukuu hotuba ya Waziri wa Fedha kama alivyoeleza vizuri kwamba uchumi wa dunia kwa sasa inatarajiwa mwaka 2020 utashuka hado hasi tatu (-3), uchumi wa dunia. Pia Mheshimiwa Waziri katueleza uchumi wa nchi za Afrika na Kusini mwa Jangwa la Sahara utashuka hadi asilimia hasi 1.6; lakini Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametueleza pamoja na ukweli kwamba uchumi wa dunia utashuka mpaka hasi tatu (-3) lakini uchumi wan chi za Kusini mwa Afrika utashuka mpaka hasi 1.6; lakini uchumi wa Tanzania utakuwa kwa asilimia 5.5. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa hilo ni jambo kubwa na ni jambo muhimu na jambo la kuuliza inakuwaje wenzetu walotuzunguka, inakuwaje uchumi wa dunia unashuka kwa hasi tatu walotuzunguka asilimia hasi 1.6 lakini wa kwetu unakuwa kwa asilimia 5.5. Hii inatokana na mambo mengi, lakini kubwa ni uongozi thabiti uliotolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha anaongoza Watanzania katika kipindi kigumu, nampongeza sana na namshukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini nadhani Mheshimiwa Rais pia alijua kuna mambo mengine ukiwa Rais unatekeleza kwa kujua sio kila kitu uwaambie Watanzania. Tafti zinazoonekana duniani maeneo mbalimbali, tafiti zinasema unapofungia watu wako kwenye nyumba ukawa-*lockdown* kinachotokea muda wote unaokuwa umewa-*lockdown* wanakuwa wanapoteza *immunity*. Kwa hiyo, siku ukiwaachia wakatoka nje basi watashambuliwa na magonjwa mengine mengi tu. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwamba anaona mbali ametuepusha sio tu na Corona, lakini pia na magonjwa mengine ambayo yangeweza kuwakabili Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vitabu vyta uchumi vinatuambia kwamba inapotokea uchumi ukadorora ziko njia nyingi unaweza ukajaribu kufanya kutokana na hali hiyo, lakini njia moja muhimu ni kuhakkisha unaongeza *aggregate demand* na tukisema *aggregate demand* kwa maneno ambayo yanaweza yakaeleweka kwa urahisi ni kwamba uwezeshe watu wako kuwa na *disposable income* kubwa zaidi, uwawezeshe kuwa na kipato zaidi cha kuweza kuongeza matumizi ili uchumi wako uweze kuanza kuchukua hatua na kurejea katika hali yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa leo hii tunapitisha bajeti kwa hiyo maswali ambayo najiuliza ni je, hii bajeti tunayopitisha leo hii imechukua hatua mbalimbali za kusaidia uchumi wetu kuweza kurudi katika hali yake au je, bajeti hii inatusaidia kujenga *aggregate demand*?

Sasa leo nitawapa majibu kwa ufupi niseme bajeti hii inatusaidia kuwawezesha Watanzania kujenga *aggregate demand*, kwa hiyo, itatusaidia kututoa kwenye hali iliyopo. Sasa hatua ziko nyingi siwezi kusema zote lakini nitasema chache tu.

Kwanza Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametueleza kwamba kutokana na ushuru wa bidhaa kwa kweli sheria inaruhusu Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Bunge lako linaweza likaruhusu kubadilisha kulingana na mfumuko wa

bei kuongeza ule ushuru mwaka hadi mwaka. Kwa kweli Mawaziri wengi duniani huwa wanakuwa ni Mawaziri wa kuongeza kodi kwenye sigara, kuongeza kodi kwenye soda, lakini unavyoongeza kodi hizo kwenye sigara, bia maana yake unapunguza uwezo wa watu kuweza kutumia unapunguza *disposable income*, kwa hiyo, hujengi *aggregate demand*, lakini kwa hatua alivyoeleza Mheshimiwa Waziri amesema hakuongeza kodi yoyote na anaomba Bunge tusiongeze kodi yoyote kwenye ushuru wa bidhaa. Kwa hiyo, nakubaliana naye kwa asilimia 100 yuko sahihi na taratibu na falsafa za uchumi zinatutaka tufanye hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili unaelezwa kwamba ukiwa katika hali kama tuliyonayo hii ukitaka kujenga uchumi basi ziangalie *employment taxes* (kodi zinazohusiana na mambo ya ajira). Sasa hii bajeti ambayo tutapitisha kesho inatueleza nini? Inatueleza kwamba *skills development levy* ambayo ilikuwa asilimia 4.5 sasa Mheshimiwa Waziri anapendekeza tupunguze kutoka asilimia 4.5 mpaka asilimia nne; unapofanya hivyo maana yake unajenga *aggregate demand* kwa sababu unaongeza *disposable income* kwa wafanyakazi na waajiriwa, ndio maana nasema hilo naliunga mkono kwa asilimia 100. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia tunaposema uangalie jinsi ya kuongeza *disposable income*, unaangalia na kodi za mapato za wafanyakazi. Mheshimiwa Waziri kama alivyotueleza ni kwamba ule wigo wa kutoza kodi amepandisha kutoka 170,000 hadi 270,000, kwa mwezi. Kwa hiyo, maana yake ni kama unapata 300,000 au 400,000 hizi nyingine zote hautalipa kodi, utalipa kodi kidogo tu kwa maana hiyo umeongezewa *disposable income* na kwa maana hiyo unajenga uchumi. (*Makofii*)

Kwa hiyo nichukue nafasi hii kukubaliana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha alichofanya ni sahihi, lakini hakuishia hapo ametoa na jedwali linajieleza lina-cover wafanyakazi wote katika sekta mbalimbali na kuonesha ni jinsi gani watanufaika na taratibu hizi.

Mheshimiwa Spika, ziko hatua nyingine nyingi tu sitawea kuzieleza zote; moja, tunaona kwamba tumeongeza kwa vyama vyama msingi vimesaidiwa kwamba sasa vyama vyama msingi vile au *SACCOS* kama shughuli zake sio zaidi ya kutoka milioni 50 mpaka milioni 100 tunasema hawa wasilipe kodi, ni jambo kubwa na ni jambo zuri. Pia hotuba hii inatuambia inaondoa tozo na ada 60 kwa hiyo, zinaongezeka tulishasamehe ada na tozo, sasa zinakuwa tozo na ada 274 unapofanya hivyo unajenga mazingira ya biashara na kwa hiyo, unawawezesha watu kutengeneza fedha kupata hela na kwa hivyo *una-stimulate spending* na kujenga uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kubwa alilolisema pia ametoa *limit* ya *dispute* zinapotokea za kodi kwamba sasa isichukue miezi sita Mamlaka ya *TRA* iwe imefanya maamuzi imalize kwa sababu wafanyabiashara wengi walikuwa wanatozwa kodi kubwa wanakuwa *accessed*, unaambiwa lipa asilimia 30 ukishalipa asilimia 30 ile *dispute* inaendelea hata mpaka miaka mitano au sita. Kwa hiyo unakuwa umechukua fedha unazifungia badala ya kuachia fedha hizo kuendelea kwenye shughuli za kiuchumi. Kwa hatua hizo namuunga mkono Mheshimiwa. Sasa ziko nyingi unaweza ukasema ukasema lakini ziko nyingi.

Mheshimiwa Spika, basi nichukue nafasi hii kumshukuru kwanza Mheshimiwa Rais kwa jinsi alivyotuongoza, nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla na niseme namshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu alituahidi mambo mengi pale Misenyi na mengi ameanza kuyatekeleza, ametupa mradi mkubwa wa maji wa shilingi bilioni 40, miradi ya maji iliyokuwa imekwama maji yameanza kutoka. Alituahidi kilometra tatu za barabara pale makao makuu ya Wilaya naona asilimia 70 lami zinawekwa na mambo mengine mengi, naweza nikasema, nikasema, lakini siwezi nikamaliza lakini kwa kuwa sasa tunajandaa kwenda kwenye kipindi cha kampeni tunazo silaha za kutosha, tutatumia vizuri wakati muafaka ukifika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja kwa asilimia 100. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Dkt. Kamala. Sasa anafuata Mheshimiwa Kitwanga

**MHE.CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru na mimi kupata nafasi hii kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wafanyakazi, kwa kweli bajeti ni nzuri sana sana sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nisitumie muda mwingu kuponjeza au kusema mengi bali nitumie muda wa kutosha kutoa ushauri kwenye maeneo ambayo nina uhakika yataboresha bajeti yetu ili tuweze kupata *revenue* zaidi. Nina mambo matatu yanaweza muda usitoshe kwa sababu na mimi huwa naongeaga polepole hivi ndio sababu wakati mwiningine mnasemaga mambo mengine lakini nianze kusema hivi; la kwanza; kuna hii *transit trade* hasa katika eneo la mafuta. Nakumbuka nilishashauri zamani kwamba kuna *flow meter*, tengenezeni *now is four years* haijapatikana. Kama miaka miwili nilizungumzia *single receiving terminal* maana yake ni kwamba meli inapofika na mafuta, mafuta yote yashushwe, yaende sehemu moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama mtakumbuka tulikuwa na *TIPER* tuna kiwanda cha *TIPER* kikavunjiwa kati ya mwaka 1994 na 1996 kwa sababu *South Africa* walipata mkopo wa *World Bank* wa kujenga kiwanda cha mafuta kikubwa sana na sisi pamoja na Kenya ikawa *designed* kama *depot* za kuweza kupokea mafuta hayo. Leo hii *TIPER* ambayo tuna asilimia 50 na mwekezaji ana asilimia 50 inaweza kuwa ikatumika na ninashauri itumike mafuta yote yanayopokelewa yote yashushwe kwenda *TIPER*. *TIPER* wana *flow meter* pale yakishatoka kwenye tipa pale ndio yaweze kusambazwa kwenye sehemu zingine. *TRA* sasa waweze kuwa na *mechanism* ya kuweza *ku-monitor* sasa haya mafuta yaliyoshushwa *TIPER*. Mangapi yanatoka pale kwenda kupelekwa Rwanda, Burundi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hebu hesabu *petrol station* kuanza Chalinze mpaka pale Kibaha ni nyngi na *petrol station* moja ni karibu shilingi milioni mia tatu na kitu, *tank* moja ni shilingi milioni 70 matenki matatu maana *diesel*, *petrol* na *kerosene* unazungumzia shilingi milioni 210. Mtu ana-*invest* kiasi hicho chote lakini kwa siku unaona magari manne au matatu tu yanakwenda kunywesha mafuta pale, jilize kuna nini.

Mheshimiwa Spika, kinachotokea kwa sababu mafuta yanayoshushwa kuna kitu kimoja kule Kigamboni kunaitwa *manfold* ya Kigamboni ilikuwa ya mtu binafsi. Juzi from nowhere imehamishiwa *TPA*, hivi wewe kweli unaweza ukafanya *investment* ya kutoa mafuta kwenye meli kuja kwenye *manfold* halafu ukazigawanya kwenda kwenye *depots* halafu baadaye ukaigawa tu. Kinachotokea ni kwamba yale mafuta yanakuja kwa mfano lita milioni 50, milioni 40 ni za *lock*, milioni 20 zinazobaki ni *transit*. Sasa wanapotoa pale wanabeba kwenye matenka yale matenka yana *compartments*, yanapofika hapa katikati katika labda tuseme *tanker* limebeba lita 60,000, lita 20,000 zinashushwa njiani 40,000 zinakwenda zinapita mpakani. Panapogongwa pale mpakani zimepita lita 60,000 zile zile kumbe zingine zimeachwa hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hata kama magari hayatakuja kujaza mafuta hapo itakuwaje? Si nitafaidika tu kwa sababu nimekwepa ushuru. Sasa tukishakuwa tumeweka *single receiving terminal*, *TRA* na uwezo wao yule Kamishna Jenerali kijana yule ni *very good upstairs*, tumtumie aweke *system* ya *ku-monitor* mafuta yatakayoshushwa pale *TIPER* na kama tuna matenki mengine Tanga na penyewe *it doesn't matter* kuwaza ya Serikali wala ya nini kinachotakiwa yale matenki yawe *monitored* na *TRA*. *TRA* mafuta yanapokuja pale kila yanayotoka pale wao ndio wana-*monitor*. Leo hii *depots* ambazo zinatumia hiyo *manfold* ya Kigamboni acha *KOJ* ile Kigamboni kila mahali kuna *TRA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa weka sehemu moja, weka *system* nzuri, weka *control*/mpakani na kuhakikisha kwamba

kila mafuta yanayopita pale ni yale yaliyotoka pale, utaona.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilizungumza *issue* ya TTMS wakati nazungumzia simu hizi ilituchukua miaka sijui mingapi. Naomba niseme wakati nikiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini nilitembelea TIPER katika *resolution* tulizoziweka ni kuwa na *single receiving terminal* pamoja na ile *bulk procurement institution* ilikuwa chini ya *privatekuwa agency*. Leo hii nawashukuruni sana imeshakuwa *agency* ya Serikali, mnashindwa nini hii *single receiving terminal*? Mpaka sasa hivi Kalemani anazungumzia atumie TPDC, *we are going back where we were*. TPDC wa-concentrate na core business yao, core functions zao TIPER ipo na ina *infrastructure* tayari na mimi niliwaeleza TIPER wakati huu jengeni matenki mwaka 2013 leo ni 2020 halafu tunazungushazungusha tu hata hapa nitazungumza natwanga kama vile natwanga maji kwenye kinu.

Mheshimiwa Spika, lakini mpaka inafikia wakati naona *there is sabotage the same government* Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi wanassema TPA wajenge matenki Kalemani hapa anasema TPDC wajenge matenki wakati tuna TIPER ambayo tuna 50% na Mwenyekiti wake anateuliwa na Rais. Halafu tuna Puma Energyna penyewe tuna 50 na wana *infrastructure why don't you use those and you start immediately from tarahe 1 Julai muanze kupanga hapo mwezi wa tisa mnaanza ku-implement*. Mimi nadhani hili mllichukue seriously...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE.CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Spika, hebu niongezee moja tu niseme hili.

Mheshimiwa Spika, unajua mimi mpaka wakati mwingine juzi nilipokuwa namsikiliza Mheshimiwa Keissy naona

kwamba anasababu ya kuzungumza alichozungumza. Maana mimi wakati nataka kuwasilisha ile hoja wewe ulikataa kata kata, urafiki wetu na wewe ukafa, ukawa hutaki kuniona lakini nikakuona wewe sasa unanikwamisha, nikakuacha nikaenda kwa Kagaigai tukafanya mambo yetu na wenyewe wakakataa baadhi ya mambo kuyaingiza kwenye hiyo, lakini *at the end of that we are achieved what we wanted. (Makof)*

Mimi nimwambie tu Keissy aendelee na wewe si utakuwa umerudi utakuwa umekaa hapo hapo tuendelee, hivyo hivyo na wazo lake japokuwa nilikuwa silipendi. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makof)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles Kitwanga. Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Ridhiwan ajandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipatia fursa ya kuweza kuhutubia bajeti kuu ya Serikali. Awali ya yote nikushukuru wewe kwa kunipatia fursa lakini kwa uongozi wako wote tulioCAA wote miaka hii mitano. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, nisje nikasahau, naunga mkono bajeti hii aliowasilisha Mheshimiwa Mpango.

Mheshimiwa Spika, ninazo *point* nne hii bajeti ni muhimu kwa sababu ni bajeti ya kuimarisha uchumi wa Taifa wakati uchumi wa dunia unaanguka, ni bajeti ya kukaribisha Mpango wa Tatu wa miaka mitano.

Pili ni bajeti ya kuandaa dira mpya ya taifa kuioboresha sasa hivi tulipo dira ya taifa inatuambia mwaka 2020/2025 lakini ukisoma bajeti ya Wizara ya Fedha waliowasilisha tunaingia kwenye maandalizi ya dira ya taifa yaani pale tulipo tuangalie tunakwenda wapi, kumbe safari ya Taifa hili sio uchumi wa katika safari ya Taifa hili ni kwenda kwenye uchumi mkubwa kwenye ustawi ndio *point* yangu ya tatu. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, sababu ya nne, hii ni bajeti ya kukamilisha utekelezaji wa Ilani ya Chama, yaani Ilani ya Chama kwa miaka mitano hii ndiyo funga kazili, yaani ndiyo tumemaliza mambo yote na nitoe taarifa, nilikuwa nazungumza na rafiki yangu mmoja akaniambia kama hiyo Ilani ya Chama ninyi Ilani ya Chama mlishtaimaliza mwezi Septemba mwaka jana, yaani hapa mnaongeza kwamba mmetekeleza zaidi ya tulivyotegemea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa kabla sijatoa mapendekezo yangu naomba nizungumze mambo mawili kutokana na yale waliyozungumza wenzangu. Moja, nianze na Mheshimiwa Waziri wa Fedha; Mheshimiwa Waziri wa Fedha nimeoma sana ripoti yako, umempungeza Mheshimiwa Rais, mimi nataka nimshukuru. Umempungeza Mheshimiwa Rais alivyokwenda Uwanja wa Taifa mnyama akachomwa mkuki, lakini umeshindwa kumshukuru kwa sababu Mheshimiwa Rais kama angeamua kama watu wa Ulaya waliosimamisha ligi yaani mtu wa kwanza wa kupata kombe na wa pili huyo aliyefunga goli asingekuwemo, sasa umpongeze Mheshimiwa Rais, lakini sasa kama angesimamisha kama watu wa Ulaya mshindi wa kwanza asingekuwemo na wa pili asingekuwepo. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine hili ni la kitaalam, kuna mtu amezungumzia suala la nishati umeme na kama unavyojua ndiyo taaluma yangu ya miaka 30. Unapopima ufanisi wa Serikali hii kwa umeme usipime kwa megawati, upime ni vijiji vingapi vimepewa umeme.

Mwaka 2015 vilikuwa 2,000 sasa viko 9,000. Lakini megawati 1,500 za mwaka 2015 nilikuwa Naibu Waziri wa Nishati tulikuwa na *megawatt number*, lakini Mtera ilikuwa haizalishi *maximum*, Kihansi ilikuwa haizalishi *maximum*, ndiyo maana tulikuwa na megawati 1,500 kwenye karatasi lakini umeme ulikuwa unakatika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo tuna umeme umeongezeka, megawati 100 zinazobezwa, lakini hakuna kukatika. Lakini ninataka niwaeleze jambo moja la kitaalam....

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** ...ni kwamba kwa sasa tunaweza kuwasha umeme tukitaka wakati wowote kwa sababu nishati ya gesi ipo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage, kuna taarifa, kijana anataka kukuparua ndevu kidogo.

## TAARIFA

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji, ndugu yangu, baba yangu Mheshimiwa Mwijage kuhusu hili suala la kukatika umeme. Kwa mfano Mkoa wangu wa Songwe mimi umeme unakatika mara nane kwa siku na siyo hapo tu yaani umeunguza hadi vyombo vinavyotumia umeme.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba mzungumzaji achukue muda wake kutowapotosha Watanzania kuhusu suala la umeme kutokukatika katika, ni taizo kubwa na ni janga kubwa sana. (*Makofî*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage, pokea taarifa hiyo.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nakubali taarifa ya mwanangu na ndiyo ujue maana ya uwakilishi, kabla sijaja Bungeni hapa nimejibu hoja za wapiga kura wangu wanaosema hapa kuna tatizo, hapa nguzo imeanguka, hapa kuna nini, ni kazi yako wewe kuwasikiliza wananchi na ukamwabia Waziri, ndiyo maana ya wewe kuwa hapa mwanangu. Kwa hiyo ni kazi yako hiyo, ulipaswa kuchukua hoja na kuwaeleza watu wako. (*Makofî*)

**SPIKA:** Kwa hiyo Mheshimiwa Mwijage unachosema ni kwamba hajawajibika?

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, niseme nini zaidi ya hapo? (*Makofî/Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, mwanangu ameharibu muda wangu, nataka niwaeleze suala lingine la umeme. Uchumi wa nchi yetu si wa kutengeneza umeme na kuuacha. Mataifa yaliyoendelea wana kitu kinaitwa *idle capacity*, unatengeneza megawati unaaziacha tu, lakini ukiwekeza lazima ulipe. Sasa sisi hatuna haja ya kuweka *idle capacity*, lakini tuna mipango yetu kadiri tunavyohitaji umeme tutaendelea kujenga. Ilibidi nilzungumzie hilo.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo suala la Covid-19 na hapa nataka kumshukuru Mheshimiwa Rais. Napenda nikiri mimi nilianza kuratibu suala la madawa ya asili tarehe 18 Machi ndiyo tulanza kuratibu haya madawa na nillipowaslliana na mama yangu tarehe 18 Machi nillipoona mambo yanakuwa mazito nikamwambia mama yangu ambaye na ye ye ni Mbunge wa Muleba Kusini akasema mimi nakwenda Serikalini, akaandika barua Serikalini na akaja akahutubia Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa madawa tuliyoratibu wametibiwa wazungu kutoka hukohuko na nina vielelezo hata vya sauti, wanashukuru. Nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutuletea utaratibu wa kurasimisha dawa za asili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye uchambuzi wangu kwa haraka; ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri, ili tuweze kuchangamsha uchumi kama nilivyozungumza kwenye bajeti yako, nakuomba ufungulie tena *re-export*, ukianzisha *re-export* tunayo fursa ya *re-export* kwenye mafuta.

Lakini niipongeze Serikali kwa kuanzisha utaratibu wa kipeleka mbogamboga na matunda Ulaya. Kwa kufanya hivyo ina maana hizi bidhaa ambazo siyo *traditional* zitaweza kwenda kwenye soko la Ulaya haraka sana na kuweza kupata pesa ina maana wannachi zitaweza kuwaletea pesa. (*Makofi*)

Lakini Mheshimiwa Waziri naomba kitu kimoja, wewe na Waziri wa Mambo ya Nje mkajadiliane na nchi zilizotuzunguka zipunguze vikwazo kwenye biashara ya kusafirisha mizigo. Bado Rwanda hajaonesha utamaduni mzuri, muweze kuhakikisha mizigo yetu inakwenda. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala la bajeti; naipongeza Serikali kwa niaba ya mkoa wangu. Ujenzi wa Meli ya Victoria umkamilika, tuna imani Victoria itafika Bukoba na kwa kweli ikifika Bukoba suala la maboksi ya kura ni kwenda usihesabu tu ni mia mia kwa Mheshimiwa Rais, kwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini nipongeze namna mlivyowekeza au tulivyowekeza kwenye suala la elimu. Kwanza mlivyouunga mkono Mkoa wa Kagera katika ujenzi wa Sekondari za Ihungo na Nyakato, lakini kwenye mtiririko wa vyuo vya elimu ikwemo Gera, Katoke na madarasa. Nitakuwa mwivi wa fadhila nisipozungumza ujenzi wa barabara za lami na hususani katika Wilaya ya Muleba; barabara ya Muhutwe kuja mpaka Machumu na nishukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuwa na wazo la kupeleka umeme barabara ya lami pale Kamachumu na kwenda mpaka Buganguzi lakini na barabara ya kutoka Muleba kuja Kanyambugo mpaka Rubya. Tunawashukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niishukuru Serikali kuititia Wizara ya Mifugo kwa kumaliza migogoro ya ranchi Mkoa wa Kagera. Sasa tunatoka kwenye migogoro tunakwenda kufuga kisasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie kidogo tunapokwenda kwenye Mpango wa Tatu wa Miaka Mitano, wale wanaopitia tena mpango na kuangalia dira lazima muwekeze/tuvekeze nguvu, tutakuwa wote, tuwekeze nguvu kutoka kwenye mazao ya bei twende kwenye mazao ya tija yaani tuisiwazoeshe watu kahawa kilo ngapi, tuwafundishe na kuwawezesha wananchi kwenye ekari moja utapata kilo ngapi, kwenye ekari moja ya pamba utapata kilo ngapi badala ya kukimbia bei, kwenye shamba moja,

ekari moja ya korosho utapata ekari ngapi. Uchumi shindani tunaokwenda unalenga kwenye tija kuliko kulenga kwenye bei. Nina imani kama nilivyosema hii ni bajeti muhimu, kwa vidondozo hivyo sina muda wa kutosha, tunakwenda kuvuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri una maotoe ya asilimia 5.5 utaishangaza dunia, tunaweza kukua kukaribia hiyo saba, lakini nakuhakikishia muda si mrefu tutakwenda hiyo kumi tunayoitamani ili twende kwenye uchumi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, tuonane mwezi Novemba. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwijage. (*Makofi*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge mnisaidie tutoke kwenye *dilemma* moja; kwa kweli wachangiaji nillionao ni wengi na kesho wale ambao ni nje ya orodha niliyonayo leo ya wengi, kesho peke yake nina wachangiaji 50. Leo hapa yaani bado wengi kweli. Mnaonaje tukienda dakika tano kila mmoja?

**WABUNGE GULANI:** Dakika saba.

**SPIKA:** Saba bado wengi watabaki.

Nchi za jirani wanafanya dakika tatu kila mmoja, sisitano je? Tano sawa? Haya, kengele italia mara moja tu na nidakika tano. Tunaanza tu-*practise*, tuanze kidogo niangalie na Upinzani nimepiga sana upande wa Chama Tawala; aanze Mheshimiwa Yosepher Komba, atafuata Mheshimiwa Aida Khenani, dakika tano kila mmoja.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi nianze kwa kumshukuru Mungu, lakini pia niwashukuru viongozi wangu wa chama kuanzia ngazi ya Taifa mpaka kwenye msingi wangu. (*Makofi*)

Kwa namna ya pekee nampa pole Mwenyekiti wetu wa chama kwa madhila aliyoyapata, naamini Serikali itachukua hatua stahiki kwa waliofanya jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, nawapa pole wafanyabiashara wa Wilaya ya Muheza ambao leo wamepata adha ya kuunguliwa maduka yao kwa sababu ya changamoto ya kukatikakatika kwa umeme, kwa hiyo ninawapa pole sana na ninaiomba Serikali suala la vifaa kwa ajili ya zimamoto lichukuliwe utaratibu wake ili Wilaya ya Muheza iweze kupata gari la zimamoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nina jambo kuu moja tu ambalo linahusu Wilaya ya Muheza, lakini limegusa pia maeneo ya Pangani na Tanga Mjini lakini Muheza ni zaidi. Serikali inajinasibu kuhakikisha inawapa unafuu wa maisha wananchi wake, lakini kumetokea katika Wilaya ya Muheza mwaka 2017 mwezi Desemba, amekuja mtu anaitwa Alphonse Mkama, Mwenyekiti wa *Fisheries Cooperative Society* ametumwa na Serikali kwa maana alikuwa na barua kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, alikuwa na barua ya kutoka Tume ya Ushirika ya Taifa, amekuja Wilaya ya Muheza akaanzia kwenye mkoa, akapata kibali kwa Mkuu wa Mkoa, akaja kwenye Wilaya akapata kibali kwa Mkuu wa Wilaya, akaja kwa Mkurugenzi akapata kibali, akaenda kwa Afisa Ushirika wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, alichokisema ni kwamba Serikali imepata ufadhili wa kupata mikopo kwa wananchi, hivyo wananchi wajunge kwenye vikundi waweze kuchanga ili waweze kupatiwa mikopo hiyo. Kuna vikundi vya vijana, vikundi vya wakulima na vikundi vya wafugaji, wananchi walijiunga. Hivi ninavyoongea wananchi takribani 9,600 walijiunga kufanya hili zoezi, tangu mwaka 2017 wananchi hao hawajui hatma nini inaendelea.

Mheshimiwa Spika, wananchi hawa walikuwa wanatakiwa wasajili wawe na kadi za *NMB*. *NMB*tunafahamu Serikali inamiliki hisa zaidi ya asilimia 31. Waliambiwa wawe na kadi za *NMB* wakawa wanalipia shilingi 10,000, wakawa

wanalipia shilingi 15,000 kwa ajili ya bima ya mkopo. Mkopo huo ni kuanzia milioni mbili mpaka milioni nne.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza, baada ya kuona hili suala halieleweki kwenye Baraza la Madiwani tuliuliza tukaambiwa halina majibu linafuatiliwa, lakini ni suala ambalo lilikuwa linafanyika kwenye Ofisi za Serikali, lilikuwa linafanyika na watendaji wa Serikali. Kwa hiyo hivi ninavyoongea wannachi 9,600 hawa hawajui suala hili maana yake litafikia wapi, waliambiwa miezi mitatu tangu 2017.

Mheshimiwa Spika, fikiria tu kwa kiwango cha chini kama kila mwananchi alitoa shilingi 45,000 kwa wananchi 9,600 ni shilingi ngapi? Mimi ninavyoongea hapa wananchi wa Muheza wamenituma. Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango nafahamu utakuwa unafahamu hilo suala kwa sababu liko kwenye Wizara ya Fedha, nafahamu Mheshimiwa Waziri Mkuu Ofisi yake itakuwa inalifahamu, nafahamu Ofisi ya TAMISEMI ambayo ndio ilitoa kibali wananchi wapatiwe kadi za benki kupitia *NMB*inafahamu.

Naomba Mheshimiwa Dkt. Mpango utakapokuja kesho utujibu hapa wananchi wa Muheza 9,600 wanapataje mikopo? Kama mikopo imeshindikana ya milioni mbili mpaka nne kila mmoja, wanapataje fedha zao ambazo walichanga, wengine kwa kukopa, wengine kwa kuazima ili waweze kupata mikopo ya Serikali. Tofauti na hapo tutajua Serikali mmeamua sasa kuiba fedha za wananchi kwenye mifuko yao. (*Makofii*)

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Meshimiwa Yosepher, Mbunge wa Muheza anataka kutoa taarifa. Mheshimiwa Balozi Adadi.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Spika, suala ambalo analiongelea Mheshimiwa Mbunge ni suala ambalo tumelishughulikia na ni suala ambalo liko mahakamani sasa hivi na sasa hivi Mkuu wa Wilaya pamoja

na Halmashauri ya Wilaya wanafanya mpango wa kuweza kuanza kurudisha hizo fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yosepher, kwa taarifa hiyo usiendelee kulijadili.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee.

**SPIKA:** *Unless una uhakika haliko mahakamani unaweza ukaendelea, kama liko mahakamani basi tuheshimu tu hilo.*

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, ninachotajka tu kumwambia kaka yangu Mheshimiwa Balozi Adadi ni kwamba ye ye aliwahi kushindwa kujibu hili suala kwenye mkutano wa hadhara, sasa sijui hapa inakuaje anatoa hayo anayoyatoa. Wananchi walimuuliza akashindwa kujibu.

Kwa hiyo, mimi sitaendelea nalo lakini Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpago akilifuatilia leo na kesho atakuja kujua nini kinaendelea Wilaya ya Muheza na Muheza tunasubiri. (*Makofii*)

**SPIKA:** Sasa angelijibuje wakati liko mahakamani?

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, kabla, ilikuwa kabla, tangu mwaka 2017 mpaka leo, angesema mahakamani limeenda lini kama limeenda mahakamani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia suala la vifo vya akina mama wajawazito. Mheshimiwa Waziri amejinasibu sana jana kwa makofii na vigelegele na nyimbo nyingi. Bado vifo vya akina mama na watoto vinaendelea...

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Yosepher. Mheshimiwa Aida Khenani, mkumbuke ni dakika tano kila mmoja. Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na kwa sababu zimekuwa dakika tano ntazungumzia mambo mawili ambayo yanawahu su wananchi wa Mkoa wa Rukwa ambayo ni uvuvi pamoja na kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mkoa wa Rukwa walitegemea bajeti hii ingewagusa moja kwa moja ama kwa kuboresha yale makosa yaliyotokea miaka minne iliyopita au kuwadidimiza moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha amezungumzia ni namna gani suala la uvuvi limeweza kuwa na faida kubwa na kwenye makusanyo wamekusanya zaidi, lakini hivi ninavyozungumza hawajatuambia mpaka leo wamefanya tafiti kiasi gani kuhusu hizo nyavu zinazoitwa haramu, matokeo yake wanawaingiza wananchi kwenye umaskini mkubwa wanapokwenda kuchoma hizo nyavu kila siku. Ninapozungumzia Ziwa Tanganyika tuna-share na nchi mbalimbali zikiwemo Burundi, Kongo na Zambia, kwa nini wameshindwa kufanya tafiti hizo nchi nyingine wanafanyaje badala yake wanakuwa na suluhu ndogo sana ya kwenda kuwadidimiza Watanzania?

Mheshimiwa Spika, wakati tunazungumzia Ziwa hilo hilo la Tanganyika ni miaka mitano ambayo Mbunge wa Nkasi Kaskazini anasema Rais aongezewe muda. Miaka mitano bado wananchi wa Mkoa wa Rukwa tunalia na usafiri wa Ziwa Tanganyika kwa maana ya MV Liemba, mpaka leo hakuna majibu. Wananchi wa Nkasi wanataka kujua suala hilo limefikia wapi kwa sababu miaka mitano ndiyo hii inakwenda kuisha na hii ndiyo bajeti ya mwisho. (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

## T A A R I F A

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Aida Khenani kwamba uvuvi ni sayansi, *number one; number two*, hatufanyi maamuzi katika kutengeneza sheria za uvuvi mpaka tufanye utafiti. Ndiyo maana tuna Shirika la Utafiti la Taifa ambalo linahusika na kuangalia zana hii inayokwenda kutumika, je, ni sahihi?

Mhesmiwa Spika, nataka nimpe taarifa kwamba sisi hatuendi kuchoma nyavu kinyume na sheria na sheria zetu zote zinakwenda sambamba na utafiti unaotokana na wananchi wenyewe wavuvi na sisi wataalam. Kwa hiyo, asipotoshe. (*Makofii*)

Mhesimiwa Spika, na ninataka nimhakikishie kwamba katika Ziwa Tanganyika wananchi wamelelewa na ndiyo maana Wabunge wanaotoka katika Ziwa Tanganyika akiwemo Mheshimiwa Mbunge Hasna Mwilima, Mheshimiwa Kakoso, Mheshimiwa Keissy na wengineo walitupongeza, akiwemo na Naibu Waziri Mheshimiwa Kandege, kwa sababu wananchi wamelelewa na sasa wana-complyna sheria yetu. Kwa hiyo asipotoshe na ndiyo maana migebunga sasa inapatikana kwa wingi baada ya *control* iliyo fanyika na Serikali. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi nimwambie Naibu Waziri kwamba nashukuru kwa sababu mmekubali kwamba hamjafanya tafiti, bado mnakwenda kufanya tafiti. Mimi sipotoshi na ushauri wangu kwenu nataka kuwaambia hawa Watanzania ambaao ni wavuvi leo ndio wanaotakiwa kusomesha watoto, hao ndio ambaao tunategemea leo watoto wasipoenda shule tukawakamate, wanategemea uvuvi huo huo.

Nategemea pesa na makusanya mliyokusanya mtumie kutoa elimu kwa wavuvi hao. Lakini leo tulitegemea kwenye bajeti hii mtuambie mmetenga kiasi gani kwa ajili ya kuwakopesha wavuvi hao ili wafanye uvuvi bora.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, taarifa tena.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi hii...

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kwa sabau Naibu Waziri alikuwa na muda wa kujieleza katika miaka minne...

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** ...Serikali ya Awamu ya Tano...

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida, umechokoza mwenyewe, pokea taarifa.

## TAARIFA

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu Serikali ya Awamu ya Tano ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli tumefanikiwa kwanza kutoka katika Ibara ya 25 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inaelekeza Serikali kuunda vikundi vya ushirika vya wavuvi, tumeunda vikundi vya ushirika vya wavuvi. (*Makofî*)

Ilani inaelekeza kwamba tuvikopeshe vikundi hivyo, Benki ya *TADB* imeanza kutoa mikopo kwa wavuvi. Kule Ukerewe wamepata shilingi milioni 200, pale Sengerema wamepata shilingi milioni 100 na sasa tunaelekeea Ziwa Tanganyika. Yes.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Aida mambo ya uvuvi na nini, kuna mwanamke *Lake Tanganyika* anavua?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mimi hapa navua.

**SPIKA:** Wewe unaingia uwanja ambao siyo wako ndio shida, kama unavua unaajiri watu huingii Ziwanu kule. Endelea Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, unaweza ukakaa hapo kwenye kitu, lakini unafanya kilimo si kwamba unakwenda wewe shambani, kwa hiyo mvuvi siyo yule anayeingia ziwani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nataka nimwambie tu Naibu Waziri, nilitegemea angesema huko unakozungumzia Nkasi, wapi, vimekopeshwa vikundi kadhaa, lakini naona anachoendelea hapo ni habari ya ilani, ilani, ilani hiyo ndio imeshindwa kutekeleza hayo mambo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la kilimo; kwa upande wa kilimo mpaka leo, ndani ya miaka mitano mawakala hawajalipwa mpaka leo. Mlikaa kwenye kigezo cha kwamba mnafanya utafiti, utafiti kwenye Serikali ya Chama cha Mapinduzi miaka mitano mnafanya utafiti, mmeshindwa kuwalipa mawakala, wale mawakala wana watoto, wale mawakala wanafamilia, wale mawakala wanategemewa, leo wamekopa kwenye mabenki Serikali ya Chama cha Mapinduzi imewapa umaskini Watanzania. (*Makof!*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida dakika tano zako zimeisha. Kama ulitumwa na mawakala kwamba watakukatia basi ndio umeliwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Shamsa Mtamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Sonia Magogo.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia katika bajeti hii, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya nzuri na leo hii nikaweza kusimama katika Bunge hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nikushukuru kwa ushirikiano mkubwa ambao umenipa kipindi chote ambacho nipo katika Bunge hili na niwashukuru Wabunge wenzangu wote kwa ushirikiano mkubwa ambao mmenipa kipindi chote ambacho nipo katika Bunge hili. Ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu Wabunge wote muweze kurudi katika Bunge hili, ili tuendelee kuwatetea Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitaanza kuzungumzia sekta ya maji; kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maji pamoja na Naibu wake kwa kutekeleza kero ya maji katika maeneo mengi ya Mtwara Mjini, lakini bado kumekuwa na changamoto ya maji katika maeneo mengi ya Mtwara Vijiji kama maeneo ya Lipwidi, Mango, Pacha Nne, Nanguruwe pamoja na Mbawala Juu. Maeneo haya yamekuwa na changamoto ya maji kwa muda mrefu sana kutokana na vyanzo vyake vya maji kutokuwa vya uhakika. Hivyo, niombi Serikali ipeleke fedha kwa ajili ya kuboresha vyanzo hivi vya maji ili wananchi wa maeneo haya waweze kufurahia huduma hii muhimu ya maji safi na salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kujenga hospitali za mkoa na hospitali za rufaa, lakini bado kumekuwa na changamoto, kwa mfano Hospitali yetu ya Mkoa wa Mtwara, Hospitali ya Ligula, changamoto zilizopo ni nyingi, changamoto ya kwanza ni utaratibu unaotumika sasa unachelewesha manunuzi ya dawa pamoja na vitendanishi hali inayosababisha kutopatikana kwa wakati, hivyo utaratibu huo ubadilishwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna uhaba wa watumishi, madaktari bingwa pamoja na wauguzi, lakini miundombinu ya Hospitali hii ya Ligula ni chakavu, kwa mfano jengo la *OPD* limeharibika na ni chakavu mno, tuliahidiwa

fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la *OPD*, lakini mpaka sasa ninavyozungumza fedha hizo hazijapatikana na kuna maboma yaliyojengwa zamani kwa ajili ya upasuaji, *ICU* pamoja na *mortuary*, maboma haya mpaka sasa hayajakamilika. Hivyo niombe Serikali ipeleke fedha kwa ajili ya kumalizia majengo haya muhimu ili wananchi wa maeneo haya waweze kufurahia huduma bora ya afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kuboresha katika sekta hii ya elimu, lakini bado kumekuwa na changamoto katika sekta hii hasa katika maeneo mengi ya Mtwara Vijijini, kama Shule ya Msingi Ziwanini ina upungufu wa madarasa pamoja na madawati. Madarasa yaliyopo ni chakavu na yanavuja, ofisi za walimu nazo ni chakavu na zinavuja, hali inayosababisha walimu kuhama ofisi na kuna uhaba wa nyumba za walimu, hali inayosababisha walimu kuishi mbali na maeneo yao ya kazi. Hivyo niombe Serikali ipeleke fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarsa pamoja na nyumba za walimu ili walimu hawa waweze kuishi karibu na maeneo yao ya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nije kuongelea sekta ya barabara; pamoja na Serikali kufanya vizuri katika sekta hii ya barabara, lakini bado kumekuwa na changamoto katika sekta hii hasa katika maeneo ya Mtwara Vijijini. Kama barabara inayoanzia Ziwanini kuelekea Msanga Mkuu, barabara hii ni mbovu na haipitiki, hasa kipindi cha masika, hivyo niombe Serikali iwe inachonga barabara hii mara kwa mara na ichongwe kwa kiwango cha changarawe ili wananchi wa maeneo haya waweze kutumia barabara hii. Wananchi wa Msanga Mkuu, wananchi wa Nalingu, waweze kutumia barabara hii. (*Makofii*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Shamsia, ahsante sana. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Sonia. Mheshimiwa Sonia atafuatiwa na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete. (*Makofii*)

**MHE. SONIA J. MAGOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye bajeti hii.

Kwanza kabisa nianze kwa kuishukuru Serikali kwa namna ambavyo imekuwa ikikarabati bandari yetu ya Mkoa wa Tanga na binafsi nimetembelea pale na kuona kazi inavyoendelea. Tuna imani kubwa sana kwamba baada ya ukarabati huu shughuli nydingi ambazo zinaelekezwa Dar es Salaam zitahamia pia na Tanga ili kuweza kuchochea uchumi wa Mkoa wa Tanga pamoja na mikoa mingine jirani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na ukarabati wa bandari ningeomba pia Serikali ituangalie kwa upande wa viwanda. Mkoa wa Tanga una viwanda vingi sana na mara nydingi nimekuwa nikisimama hapa kuelezea tatizo ambalo tunalo Mkoa wa Tanga. Viwanda vingi sasahivi vimekuwa Mkoa wa Tanga, hivyo nniombe Serikali itusaidie kuvihuisha hivi viwanda ili hata ile bandari itakapokamilika iweze kupata mizigo mingine kutika kwenye hivi viwanda vyetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni tatizo la maji na niongelee *specific* katika Wilaya ya Handeni. Wilaya hii imekuwa na tatizo kubwa sana la maji, tuna Mradi wa HTM ambaao umekuwa ukiendelea kwa muda mrefu sana bila kukamilika, wananchi wa Wilaya ya Handeni wamekuwa wakiteseka kwa muda mrefu sana kwa kukosa maji. Niombe sana Mheshimiwa Waziri utupie jicho kwenye huu mradi ili uweze kukamilika wananchi hawa waondokane na hii changamoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nije upande wa miundombinu; miundombinu na yenyewe ni tatizo sana. Narudi palepale kwenye Wilaya ya Handeni, kuna barabara inayoanzia Kwa Mkono – Mzundu mpaka Kabuku, hii barabara imeharibika kwa muda mrefu sana na ni kiungo

kikubwa sana cha kupitishia mazao, hivyo nikuombe sana Mheshimiwa Waziri katika bajeti yako uangalie uwezekano wa kuirekebisha hii barabara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nigusie kwenye upande wa elimu. Tunashuhudia walimu wengi ambao wanapelekwa kwenda kufundisha kwenye shule za vijiji ni wanakuwa hawako *comfortable* na wengine wanaondoka na kusababisha ubaba mkubwa sana wa walimu, lakini nina imani kama Serikali itakuja na mpango wa kuhakikisha inawapa *incentive* hawa walimu ambazo zitawafanya waone kukaa kule vijiji ni sehemu salama na pengine kuwe na utofauti kwa mwalimu ambaye anafundisha mjini na vijiji hata katika kipato, ili mwalimu anapopangiwa kwenda kufundisha vijiji aweze kutulia na kufanya kazi zake vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia, nigusie suala la vifaa vyatya ujenzi vyatya nje kuongezewa kodi. Hili ni wazo zuri sana Mheshimiwa Waziri, lakini ningeishauri Serikali pia iangalie ni namna gani wanavisimamia hivi viwanda vyetu vyatya ndani ili kuongeza ubora kwenye vile vifaa, kwa sababu unakuta unanunua bati leo mtu anaazeke, lakini baada ya muda mfupi limeshabadilika rangi ama yanatoboka, *tiles* zinakuwa zinachubuka, misumari inaota kutu. Kwa hiyo, ni muhimu sana wakati tunaweka kodi kwenye hivi vifaa vyatya nje tuweke msisitizo kwenye ubora wa vifaa vyetu vyatya ndani. (*Makof*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ndio dakika tano hizo, ahsante sana. Inabidi uwe na mambo machache. Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete atafuatiwa na Mheshimiwa Stephen Masele na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi ajindae.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, nami nishukuru kwa kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia bajeti hii ambayo tunasema ndio tunamalizia katika Bunge lako hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi kawaida huwa sina utaratibu wa kujibu watu wanapotoa hoja zao, lakini liko jambo limezungumzwa na Mheshimiwa Dada Sonia hapa, nadhani ni wajibu wangu niweke vizuri, Wilaya ya Handeni inapata maji yake toka Chalinze kwenye Mradi wa Wami – Chalinze.

Mheshimiwa Spika, mradi ule ulikuwa umekwama katika kipindi kisichopungua mwaka mmoja, lakini Serikali imetoa fedha shilingi bilioni sita kwa ajili ya kukarabati na kuweka sawa miundombinu, ili mradi wa maji sasa uweze kufika Manga na kutoka Manga uende mpaka Handeni na mradi huu sio tu utaenda ku-serve Handeni Mjini, lakini pia hata Handeni Vijijini kwa Mheshimiwa Dada yangu Mboni. Kwa hiyo, nataka nimtoe wasiwasi kama anataka kuwazungumzia watu wa Handeni basi ajue Dkt. John Joseph Pombe Magufuli amekwishalifanya hilo jambo kwa vitendo na sasa hivi watu wa Handeni wasubiri maji kwa sababu Chalinze mambo ni mazuri sana upande wa maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na mambo yote haya nataka niipongeze sana Serikali yangu kwa kazi kubwa ambayo imefanyika kwenye eneo la viwanda, unaweza kuwa shuhuda mwenyewe unapopita katika eneo la Chalinze, viwanda vikubwa hasa vile vya marumaru, viwanda vya matunda vimetapakaa katika eneo lile na mimi niseme tu kwa kifupi kwamba namshukuru sana mjomba wangu Mheshimiwa Waziri Mpango, sina hakika sana wakati wanaandika bajeti kama walikuwa wanaangalia Chalinze, lakini kwa kweli naweza kusema katika eneo la viwanda wameangalia Chalinze kwa jicho la karibu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, umezungumzia ndani ya bajeti hii suala la marumaru kupunguzwa bei ili kusaidia viwanda vya ndani viweze kupata nguvu ya kuzalisha, lakini pia umeongeza bei kwa zile *importationza* marumaru kutoka nje, hili ni jambo zuri na kwa kweli mimi nataka niwambie Watanzania kwa utaratibu huu, maana yake bei za marumaru zinaenda kushuka na marumaru zitatengenezwa kwa wingi kwa sababu, tutakuwa na uwezo mkubwa na hivyo, wananchi sasa wataweza kupata marumaru kwa ajili

ya nyumba zao. Nataka niwahakikishie Watanzania leo hii ukienda Chalinze mpaka Ofisi zetu za Serikali za Vijiji zimewekwa marumaru, ni kwa sababu ya bei nzuri na mambo yako mazuri sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini sio chalinze tu, Mheshimiwa Waziri umeiangalia na Mkuranga pia kwa ndugu yangu Mheshimiwa Ulega kule kwa sababu kule Mkuu *materials* zinazotoka nazo ni *materials* za kisasa. Hii inafungua sio tu kwa upande wa viwanda, lakini pia hata kwa wenzetu ambaao wamewekeza kwa upande wa madini yale yanayotumika kwa ajili ya kuzalisha *materials* zinazoenda kutumika kwa ajili ya kutengeneza marumaru hizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini sio hilo tu Mheshimiwa Waziri, umeliangalia jambo pia la mifugo. Mheshimiwa Waziri kwa kweli watu wa Chalinze wanaendelea kumpenda Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, lakini pia wanaendelea kukushukuru wewe kwa kuangalia hivi. Kwangu mimi ambaye nina sehemu kubwa ya jamii ya kifugaji, kwa kweli nataka nikwambie tunataka kwenda kubadilisha maisha ya wafugaji, ule ufugaji wa kwamba nchi nzima iwe ni sehemu ya malisho unaondoka, sasa hivi tunataka wafugaji wetu kupitia tafsiri ya bajeti hii kwamba sasa waende wakawekeze katika kupata bidhaa zinazotokana na mifugo yao, kwamba tuchinje ng'ombe, tuuze nyama nje, tufanye mambo ambayo yanaweza kubadilisha maisha yetu na kwamba sasa hata wafugaji wangu wale wa kimasai walio katika eneo la Chalinze waweze kubadiliaka nao. Twende Umasaini kule tukute mtu ana nyumba nzuri na anafuga na manbo yanakwenda vizuri sana. Kwa kweli, hongera sana Mheshimiwa Waziri, lakini kipekee kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hilo pia Mheshimiwa Waziri liko jambo ambalo nataka nikupongeze, lakini pia nina ushauri nalo, hili jambo la mazao ya magunia. Mheshimiwa Waziri nimeona mmeweka nafikiri asilimia 20 kwa magunia yanayotoka nje, lakini pia mmeweka sifuri kwa

vibebeo vya ndani. Sasa mimi mswahili ninayetokea Bagamoyo kule wakati mwingine napata shida sana, tofauti ya magunia na vibebeo? (*Makof!*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, imekwisha?

**SPIKA:** Dakika moja, malizia.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi naomba tu atoe ufanuzi kidogo tofauti ya vibebeo na magunia kwa sababu kwa mswahili mimi wa Bagamoyo hivi vyote ni vibebeo. Sasa nataka niweke vizuri hapo, ili tuweze kuona kwa pamoja tunalenga vipli kuwasaidia wakulima wa korosho, wakulima wa kahawa, wakulima wa pamba, ambao wanategemea vibebeo hivi na binanii kwa ajili ya...

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa nairuhusu.

## TAARIFA

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Pamoja na mchango mzuri wa Mheshimiwa Mbunge anaoutoa, lakini nataka nimpe Taarifa kwamba tunaposema vibebeo ni vile vifungashio vya kuwekea korosho zilizobanguliwa. Tunaposema magunia ni magunia ya kuwekea korosho zisizobanguliwa.

Mheshimiwa Spika, na tunamtoa wasiwasi kwa sababu haya magunia ambayo yanazalishwa hapa nchini, tuna viwanda viwili, lakini kiwanda kinachofanya kazi ni kimoja tu. Sasa tumeweka ushuru huo ili kama Serikali kwamba

kuinua na kuvilinda viwanda nya ndani ili kwamba magunia ya kutoka nje yawe na bei kubwa yalingane na viwanda vyetu hapa nya ndani. Vilevile kwamba, yale magunia yanayotoka nje kama yanatumika kwa ajili ya *export* yenye we yana *exemption* na hayalipiwi kodi kwa sababu ya kushusha hiyo gharama ili tuweze kuwa na ushindani katika soko la dunia.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa Taarifa hiyo, Taarifa ya ufananzi.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, nimalizie. Kwa kweli, kwa majibu haya ya Mheshimiwa Waziri kwa hakika kwa kweli mwaka 2020 mambo yetu yatakwenda mazuri sana hasa katika Mkoa wa Mtwara na maeneo mengine ambayo tunalima korosho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ridhiwani. Mheshimiwa Stephen Julius Masele kwanza, halafu Jaqueline Msongozi.

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu ya Bajeti Kuu ya Serikali.

Awali ya yote na mimi nianze kwa kuwashukuru viongozi wangu wakuu, wakiongozwa na Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu pamoja na Chama changu cha Mapinduzi kwa kazi nzuri ya kusimamia llani ya Chama cha Mapinduzi katika kipindi hiki cha miaka mitano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Shinyanga hususan Jimbo langu la Shinyanga Mjini tumefanya kazi kubwa ya maendeleo na ninapenda nichukue nafasi hii kuishukuru sana Wizara ya Fedha na wakati wote ambapo nimekuwa nikiomba fedha kwa ajili ya Halmashauri ya

Manispaa ya Shinyanga tumekuwa tukipewa fedha. Tumekamilisha ujenzi wa barabara kilometra 16 za lami na tumeziwekea taa na Shinyanga sasa ni mji wa kisasa kabisa, lakini tumekamilisha ujenzi wa machinjio ya kisasa, tumekamilisha miradi ya maji ambayo inaendelea vizuri na Waziri wa Maji aliweza kutembelea kuzindua mradi huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaendelea na Miradi ya *REA* ambayo inafanya vizuri. Yamebaki maeneo machache ambayo Waziri wa Nishati ametembelea na ametuahidi kwamba katika Kata ya Chibe pamoja na Mwamalili na Mwawaza, zote zitapata huduma hii ya Miradi ya *REA*, lakini tunajenga Hospitali ya Rufaa ya Mkoa na kila mwaka Waziri amekuwa akitutengea fedha kwa kweli, namshukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siwezi nikamaliza mchango wangu bila kumshukuru pacha wangu, Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Lucy Mayenga ambaye tumekuwa tukishirikiana naye sana katika kutekeleza majukumu yetu katika Jimbo la Shinyanga na Mkoa wa Shinyanga kwa ujumla. Aliweza kutoa msaada mkubwa katika Kituo cha Afya cha Kambarage ambacho kinatoa huduma nyingi kwa wananchi wa Manispaa ya Shinyanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda nimuombe tu Waziri wakati mwininge awe anatumia muda kutupa elimu kidogo ya uchumi, maana leo nimesikia hapa michango watu wengine wakibeza kazi nzuri ambayo inafanywa na Serikali ya CCM chini ya Rais John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Spika, nataka tu niseme kwamba duniani kote *theory* za uchumi zinajulikana na chama chetu Chama cha Mapinduzi ni chama ambacho kinafuata mlengo wa ujamaa na kujitegemea na hivyo, ukiangalia vyama vingine ambavyo viko hapa nchini mlengo wao ni mlengo wa ubepari, lakini jamii ambayo tunaiongoza ni jamii ya watu wa chini, lazima kutafuta namna ambayo tunaweza kuwasaidia watu wa jamii ya chini ili kupunguza umaskini na

*gape la umasikini kati ya walionacho na wasionacho na hiki ndicho anachokifanya Rais Magufuli. (Makof)*

Mheshimiwa Spika, ukitazama miradi ambayo inatekelezwa inalenga kwenda kumsaidia mtu wa hali ya chini kuweza kujikwamua kiuchumi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mpango saa nyingine utumie muda wako utufundishe kidogo mambo ya uchumi, hasa masuala haya ambayo mnayasimamia ili Wabunge waweze kupata kuelewa na kuweza kusaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Fedha. Mimi nimekuwa Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, tumeshirikiana kwa miaka mitano, tumeshirikiana vizuri sana timu nzima ya Wizara ya Fedha, wanafanya kazi nzuri sana ya kusimamia matumizi ya fedha. (Makof)

Mheshimiwa Spika, unaweza kutazama kipindi hiki cha Corona nchi nyingi zimeyumba, lakini nchi yetu imeweza kuwa imara, imesimama imara wala hatukuyumba. Mimi binafsi nilikuwa sio muumini wa kufungia nchi yetu, kwa maana ya *lockdown*, niliamini kabisa *lockdown* haina muendelezo, hiwezi kuwa kitu cha kuendelea na Rais wetu kwa kweli ameweza kusimamia hilo na watu wengi ambaa walikuwa na mashaka na Tanzania sasa wanajifunza kutoka Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nimesoma leo nimeona Rais wa Uganda na yeye anasema kwamba maabara za Uganda kule na zenyewe zimetoa vipimo ambavyo sio sahihi na Rais wetu aliposema wengine walipinga, lakini wameanza kujifunza kutoka kwetu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie kwamba nchi nyingine za Afrika zinaniuliza ninyi mnafanyaje? Mnawezaje kuendelea na kazi na huku mmeweza kudhibiti gonjwa hili la Corona? Kwa hiyo nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake na

timu nzima ya Wizara ya Fedha ikiongozwa na Waziri wa Fedha Dkt. Mpango.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii.  
*(Makof)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa fursa hii uliyonipa. Naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa mafanikio ya maendeleo makubwa katika kipindi hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa maendeleo ambayo ametupelekea Mkoa wa Ruvuma katika huduma za jamii pamoja na miundombinu ya barabara, maji umeme wa *REA*, afya na elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kuwapongeza Wakuu wa Vyombo vyta Ulinzi na Usalama vyote nchini Tanzania, lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Kamishina Mkuu wa *TRA* pamoja na Waziri wa Fedha, ndugu yangu Dkt. Mpango pamoja na viongozi wengine katika taasisi hiyo ambao wamewzesha makusanyo makubwa sana hata kuweza kufikia malengo haya ambayo tuliyakusudia tunapoelekea uchumi huu wa viwanda kwa maana ya mwaka 2020 - 2025 tuwe tumefikia uchumi wa kati.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie suala la Msajili wa Vyama vyta Siasa; mimi naomba tu niulize kama imetokea hapa katikati tumemsikia Mheshimiwa Lijualikali, tumemsikia Mheshiiwa Mwita Waiatara akizungumza kwenye vyombo vyta habari. Lakini pia tumewasikia Wabunge wawili wa Viti Maalum kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo ambao walikuwa wakilalamikia michango mbalimbali ambayo imekuwa ikikusanywa wakikatwa katika mishahara yao na kwamba hawatambui hiyo michango fedha hizo zinapelekwa wapi. Wakati huo huo ajenda hiyo imekuwa ikibagua wengine wanakatwa michango hiyo, lakini wengine pia hawakatwi.

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi wamesikika Wabunge hawa wawili wakilalamikia jambo ambalo limesikitisha sana. Sisi kama wanawake inabidi tusimame kuwatetea wanawake wenzetu kwamba wanawake hao wamelalamika kwamba wamekuwa wakidhalilishwa hasa katika masuala ya ngono katika chama chao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline utaendelea tu baada ya sekunde mbili, na mimi nimshangae Mheshimiwa Waziri wa Fedha; hivi baadhi ya vyama kuweka masharti ndani ya Katiba zao na Kanuni na nini za kuwa ni *TRA*. Wanakusanya mapato, wanakusanya kodi, ni ukusanyaji wa kodi vinakusanya kodi kwa kuweka kabisa masharti kila unachopata (*Pay As You Earn*) wanaweka mule, kila unachopata asilimia 30 unaleta hapa, kila unachopata *10 percent* unaweka hapa, msibishe ninyi, tunazungumza vitu vya msingi sana. Huwezi kuweka katika taratibu zako ukusanyaji wa kodi kwamba kila huyu anachokipata asilimia fulani unaleta hapa, haiwezekani, inawezekanaje hivi vitu? Asilimia 30, mimi nahangaika hapa Jumanne watu kidogo kuhusu utaratibu halafu asilimia 30 ya hiyo wanadaiwa na chama fulani kweli hiyo *is that fair?*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha hebu huko mbele ya safari vyama vya namna hii viangaliwe. Huwezi kukigeuza chama cha siasa kuwa mkusanya kodi haiwezekani na ndiyo maana *TRA* inabidi ifuatilie hii kodi iliokusanywa huko maana yake ni kodi ya Serikali hii. Endelea Mheshimiwa Jackline ulinikumbusha jambo muhimu sana.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kukazia hapo.

Mheshimiwa Spika, mimi nimesikitishwa sana kwa sababu hiki ni Chama cha Demokrasia na Maendeleo wamejitokeza Wabunge wao wanawake kulalamika. Hakuna kiongozi wao yoyote hata kiongozi wa wanawake wa chama hicho hajachukua hatua yoyote ya kuwaita, kuwasikiliza hoja zao, lakini imeendelea kuwa hivyo hivyo kimya. Mimi najiuliza tu, Mwenyekiti wa Chama hicho yuko wapi? Je, hajasikia hizo

habari? Na ni nani anayefanyakazi ya kuwadhalilisha kingono? Hiyo tunahitaji kujua. Na kama yuko mtu ambaye anawadhalilisha kingono basi mimi naomba Msajili wa Vyama vya Siasa akae na kufuatilia chama hicho, akafanye upembuzi yakinifu huko, awahoji wanawake hao ambaao ni Wabunge ambaao wamekuwa wakidhalilishwa wameshindwa kuvumilia mpaka wamejitokeza nje. Maana yake haya mambo ni ridhaa. Kama unakwenda kushughulikiwa bila ridhaa yako maana yake ni tatizo na ndiyo maana sasa wameamua kujitokeza hadharani wakilalamikia hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingineniwaombe pia TWPG hawajafanyakazi yao ipasavyo katika eneo hilo.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Yosepher Komba

## TAARIFA

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa dada yangu Jacqueline kwamba anachokifanya ni kuzidi kuwadhalilisha hawa wanawake, lakini nimuombe pia awashauri kama kweli wamefanyiwa hivyo viko vyombo vya dola vinaweza kushughulikia hayo mambo awashauri waende huko. Ahsante. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ndicho anachokifanya.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, awashauri, asiongelee kuhusu...

**SPIKA:** Ndicho anachokifanya, kwa hiyo kaa chini afanye hiyo shughuli. Ushauri huo unapewa Mheshimiwa Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, huyo anayeongea na yeche pia aliwahi kunifuata kama dada

yake anatoka pia Mkoa wa Ruvuma akaniambia na yeze ana tatizo hilo hilo, kwa hiyo naomba nikwambie kabisa kwamba katika hilo...

*(Hapa baadhi ya Wabunge Walishangilia)*

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:**...wenzetu wamekuwa wakiteseka sana, wanateseka sana. Mimi naomba...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** ...Msajili wa Vyama vya Siasa aingilie kati, kwanza aifahamishe...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka mambo ya akina mama hayakuhusu.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Hayo waacie wenyewe. Mheshimiwa Msongozi malizia hoja yako. Mambo ya unyago hayakuhusu Mwakajoka. (*Kicheko*)

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ifahamike hizo fedha zilizokatwa zimekwenda wapi na zimefanya kazi gani na kama ingekuwa halali hawa wasingelalamika.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine...

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Kwa nini wamekuwa...

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Kwa nini katika chama hicho...

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika,...

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, siko tayari kudhalilishwa, Kuhusu Utaratibu.

**SPIKA:** Naomba...

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Kwa nini wamekuwa na tabia...

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:**...ya Wabunge wa Viti Maalum kwa ajili...

**SPIKA:** Yosepher usilete fujo. Yosepher usilete fujo.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Sileti fujo.

**SPIKA:** Hujaruhusiwa kusema nani amekuruhusu kusema?

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nilindiwe dakika zangu, dakika nne bado sijazitumia

**SPIKA:** Kaa chini.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**SPIKA:** Nimekwambia ukae chini kwa sababu unaleta fujo, kaa chini. Nakwambia kaa chini mara ya mwisho.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, Benki ya Kilimo; Mkoa wangu wa Ruvuma ni Mkoa ambao...

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, nitashughulika naye nje ya hapa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Msongozi naomba ukae.

Mheshimiwa Yosepher umekuwa ukiwash *microphone*, kila ukielekezwa hutaki kusikia sasa.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Ananidhalilisha.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Hebu msinipigie kelele ninapotaka kufanya mamauzi yangu. Mheshimiwa Yosepher kwa salama na amani naomba utupishe. *Sergeant At Arms* akichelewa dakika mbili mumuoneshe njia iliko kwa sababu ananichukulia muda wangu.

*(Hapa Mhe. Yosepher F. Komba alitoka nje ya Ukumbi)*

**SPIKA:** Naangalia tu na mwingine anayetaka kuelekea huko huko. Ukiniletea fujo hapa nakwambia urudi Jumatano ijayo tu kwani mbona rahisi na simnaelewa maana ya hilo neno? Malizia dakika yako moja Mheshimiwa Jackline. *(Kicheko)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, vyama vyaa aina hii tunamuomba Msajili wa Vyama vyaa Siasa

viondolewe mbaya zaidi hata Mwenyekiti wake juzi amefanya vitu vyahovyo kabisa. Amekwenda kustarehe, kunywa pombe zake halafu anasingizia kwamba amekamatwa, amepigwa na watu wasiojulikana, watu gani? Wakati sisi tunaishi pale Medeli tumemsikia kabisa akipandisha ngazi kwenda kwa nyumba ndogo yake.

Mheshimiwa Spika, lazima tuwe wawazi katika mambo haya...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:**...ili Serikali isiendelee kuchafuliwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba niombe Benki ya Kilimo; Waziri Mpango ninaomba Benki ya Kilimo iende Mkoani Ruvuma kwa sababu wakulima wa Mkoa wa Ruvuma wanalima sana. Hata mwaka jana tumepata kushika nafasi ya kwanza kwa uzalishaji wa mazao ya nafaka. Tunaomba Benki ya Kilimo iende kule kwa sababu wale ndiyo walengwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo machache nimshukuru sana Mungu, ninakushukuru wewe, namshukuru Mheshimiwa Rais, ninawashukuru Wabunge wote kwa ushirikiano mazuri na wananchi wa Mkoa wa Ruvuma hususani Wanawake wa Mkoa wa Ruvuma. Ahsanteni sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jacqueline Msongozi. Nilishakutaja Mheshimiwa Esther Alexander Mahawe na atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Lulida. Mheshimiwa Riziki ajiandae.

**MHE. ESTHER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza kabisa nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa kibali cha kuhudumu katika nyumba hii takatifu hapa duniani kwa miaka mitano sasa. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais

wangu Dkt. John Pombe Magufuli kwa mambo makubwa aliyoitendea Tanzania. Amekuwa Rais wa mfano duniani. Niumbee Rais wangu Mungu aendelee kumuongezea umri, amkinge na majanga yote na hatimaye aendelee kushinda kwa kishindo katika uchaguzi ujao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wetu wa Manyara tumefanyiwa mambo makubwa sana na Serikali ya Awamu ya Tano. Ukitungumzia suala zima la elimu, maboma mengi yalimaliziwa, matundu mengi ya vyoo yalijengwa, shule nyingi zilikarabatiwa na walimu madai na manung'uniko yao yamepunguzwa kwa kiwango kikubwa sana katika Mkoa wa Manyara. Niipongeze sana Serikali ya Awamu ya Tano. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukisogea kwenye suala zima la afya, vifo vyta akina mama na watoto vimepungua kwa sababu ya upatikanaji wa hospitali za kutosha, zahanati, vituo vyta afya kama ambavyo ninaweza kuvisema kwa haraka haraka. Tumepata zahanati 1,198, vituo vyta afya 487 kabla ya Awamu ya Tano kuingia madarakani. Kuanzia Uhuru mpaka 2015 tulikuwa tuna vituo vyta afya 65 nchi nzima, leo tunavyo 487. Juhudi hizi sio za kubeza hata kidogo! Kwa hiyo niipongeze sana Seriakli yangu ya Chama cha Mapinduzi, tumepata hospitali za Wilaya, kwa mfano Mkoa wa Manyara, wilaya tatu zimepata hospitali za Wilaya ambako ni Simanjiro, Mbulu pamoja na Babati Vijijiini. Hivi vitu havikuwepo, ninaomba sana niipongeze Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, tumepata Hospitali za Rufaa kumi na za kanda, tatu. Lakini sio hivyo tu, magonjwa mengi yalikuwa yanatibiwa nje ya nchi, Serikali imeweza kuokoa fedha nyingi zaidi ya shilingi bilioni 20 kwa sababu wagonjwa wa magonjwa haya ya moyo, figo na magonjwa mengine tatanishi kutibiwa ndani ya nchi yetu. Hii ni hatua kubwa. Mungu ambariki sana Mheshimiwa Rais. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tulikuja na ajenda ya kumtua mama ndoo kichwani, sasa hivi *at least* akina mama wana uwezo wa kwenda *salon*, nywele zimeota. Maeneo mengi

yamepata maji safi na salama kwa asilimia zaidi ya 85 katika maeneo mengi ya Mkoa wa Manyara na Tanzania kwa ujumla. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hili, ameweza kuwasaidia akina mama sasa wana uwezo wa kwenda kufanya kazi zao za ujasiriamali kwenda kutafuta fedha kwa ajili ya familia zao. Muda mwingu walikuwa wanapoteza mabombani na mitoni kutafuta maji. Jambo hili sasa linaanza kuwa hadithi katika Mkoa wetu wa Manyara na maeneo mengine ya nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie masuala mazima ya miundombinu; mambo mengi yamefanyika, barabara za lami, Makao yetu Makuu yaliyoko Wilaya ya Babati yamepata lami kilometra 35, taa zinawaka utasema ni Toronto. Nipongeze sana juhudhi hizi. Tumesikia kujengwa kwa viwanja vya ndege. Kujengwa kwa meli katika maeneo mbalimbali, tunawezaje kupuza juhudhi zote hizi? Hata kama huoni, basi na masikio hayasikii? Kule kwetu Mbulu wanasesma *life is so hard to a blind person*. Niwaombe tu wale ambao mpaka sasa basi ni vipofu, haidhuru, nina hakika masikio yao yanasiakia na yanaona juhudhi kubwa iliyofanyika katika nyanja tofauti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukianza kuelezea mambo yaliyofanyika katika Serikali hii ya Awamu ya Tano hata ungepewa kutwa nzima bado hayawezi kuisha lakini itoshe kusema Mheshimiwa Rais na Serikali yake, Mheshimiwa Dkt. Mpango na Wizara yako ya Fedha na watendaji wote, Mungu aendelee kuwabariki na aendelee kuwakinga na majanga yote ili kwamba ndoto zenu zikaendelee kutimia kila iitwapo leo ya kuendelea kuwahudumia Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninajua dakika hizi hazitoshi, ni dakika tano tu, lakini niweze kusema tu kwamba niipongeze pia Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuongeza Pato la Taifa kutoka asilimia 6.2 kwa miaka mitano kwenda asilimia 6.9 ongezeko la asilimia saba, ni ongezeko kubwa na limeingia katika historia katika nchi zetu za Afrika. Hili ni jambo kubwa na si jambo dogo. Serikali pia imejitahidi sana kukusanya mapato kwa njia ya kielektroniki na upotevu mwingu wa fedha

umeweza kuepukika. Hii imesababisha miradi mingi kufanywa kwa fedha zetu za ndani, niipongeze sana Serikali. (*Makofii*)

Mwisho, niwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Manyara kwa kunipa ridhaa ya kuja kuwawakilisha katika Bunge lako tukufu, Mungu awabariki sana na Mungu akubariki wewe pia pamoja na Naibu Spika wetu na Wenyeviti wote walioantuongoza katika kipindi chote cha miaka mitano. Mungu awabariki sana na naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Mahawe. Mheshimiwa Riziki Lulida atafuatiwa na Mheshimiwa Hongoli na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ajlandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nikushukuru sana kwa kunipatia na kuniona. Nimshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema allyenijaalia kunipa afya njema na niwaombee Wabunge wenzangu wote kwa pamoja Mungu awape afya njema ili Mungu awajaalie na muweze kurudi tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru wewe binafsi, nimshukuru Naibu Spika, nimshukuru Katibu wa Bunge, nimshukuru Mwenyezeki wetu wa Kamati ya Bajeti na Wajumbe wote, kwa kweli mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Ndaki Mashimba amefanya kazi nzuri ya kutuunganisha sisi Wajumbe wa Kamati ya Bajeti na kazi aliyofanya nasema nampongeza. (*Makofii*)

Nampongeza Mheshimiwa Ndaki kwa sababu akishirikiana na Wizara mbalimbali alishirikisha wadau mbalimbali wa maeneo mbalimbali kuja pale, wale ambao wana kero zao. Kwa mfano, wadau wa Wizara ya Maliasili walikuwa wanakuja kuleta kero zao, anawaita timu ya Maliasili wanasikiliza, hivyo mambo yote yalikuwa mezani yakiwa yanamalizika mezani, kila mtu anatoka pale akiwa na furaha. Wanakuja wadau kutoka mafuta wanauza petroli na kadhalika, wanakuja ndani ya Kamati, wadau wauza maziwa, wanakuja pale katiak Kamati, kwa kweli ushirikishwaji imekuwa ni kitu kizuri sana. Ni timu nzuri ambayo imefanya

kazi vizuri na nimshukuru vilevile mjomba wangu Mheshimiwa Mpango, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niishukuru vilevile Serikali yangu kwa kazi inayofanya. Leo tulikuwa tunaona tunategemea kupitia hii Covid-19 tuneteremka kiuchumi na walitegemea katika *World Economic Forum Outlook* walisema kwamba nchi za Kiafrika zitateremka mpaka zitakuwa na asilimia 2.0 lakini cha kushukuru Tanzania sasahivi tuko asilimia 6.9. Haya ni maendeleo makubwa ambayo hatukuyategemea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi, humu ni ndani walitulemaza wakatudumaza na porojo za uongo wa kusema kuwa Barrick hawatailipa Tanzania na Barrick wanaidai Tanzania kwa mikataba yetu mibovu, lakini wao wanakula vitu ambavyo havina maana yoyote. Leo Barrick wameji-feel kabisa kwamba walichoitendea Tanzania haikuwa haki, wameweza kulipa kwa awamu ya kwanza, dola milioni 600 za fedha ya Kitanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli haya ni maendeleo makubwa ambayo hatukuyatarajia. Jiulize uongo waliokuwa wanauchonga ulikuwa na faida gani kwa nchi yao? Nchi ni yako, umezaliwa hapa, mama yako amezaliwa hapa, baba yako amezaliwa hapa na wewe utakufa hapa, lakini bado unataka kuleta uongo na kuwa karibu na wao ili Watanzania wenzako wasifanikiwe. Kwa kweli hii ni aibu kubwa sana. Hawa Watanzania wenye roho kama hizi Mwenyezi Mungu tuwaombee maana tusilaani. Tuwaombee, warudi, wapate uzalendo wa nchi yao ili nchi yao iweze kuzidi kuneemeka. Tuwasamehe kwa kila jambo bovu wanadolifanya. Kwa kweli tumepeata hizi bilioni 600 na tunategemea kupata hela zingine kwa kweli mimi nasema Mheshimiwa Mpango, Mheshimiwa Kabudi na wote mlioshirikiana katika hili Mwenyezi Mungu awabariki sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni mpenzi sana wa kusoma hizi taarifa mbalimbali za kidunia, nikaona siku hiyo

wananiambia *Tanzania Executive Board* ya IMFimeisamehe Tanzania dola milioni 14. Na hii wamesamehe kama *relief* tu lakini humu ndani walitaka nchi zote za dunia zisiisaidie Tanzania na walitegemea sisi kwa kutuingiza katika mkenge tuchukue mkopo kwa ajili ya Covid-19 lakini tumekataa kuchukua mkopo, lakini wao wenyewe wame-*feel guilty conscious* wametupa sisi *relief* ya katuondolea madola hayo yote, hivi tunataka nini kwa Mwenyezi Mungu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ujasiri mkubwa na kipaji kikubwa alichopata Mheshimiwa Rais lazima tumpongeze, dunia yote inampongeza; mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Mnataka nini hata mtu unaweza kuzaa watoto kumi, ndiyo, lakini akatokea mtoto mmoja ana kipaji, kwa nini kipaji hiki tunataka kukidumaza? Haikubaliki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nampongeza kwa dhati kwa kazi anayoifanya na mimi nasema sina la kufanya na wala sina la kusema zaidi ya kusema Mwenyezi Mungu azidi kumbariki na Watanzania wote tuendelee kumuombea ili aendelee kutufanya mambo mazuri sana. Mengi tunayaona, shule, madarasa, hospitali, reli na barabara tunaziona, mnataka nini madaraja mnayaona katika kipindi kifupi, hivi tunategemea baada ya miaka mitano atayaleta mabadiliko makubwa sana, Mwenyezi Mungu ambariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nimekaa katika Bunge lako hili na wewe ni shahidi ulikuwa Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Maliasili mwaka 2005, kwa kweli ulinionesha huruma kubwa leo nataka nitoe ushuhuda na unipe dakika tatu niongeze ushuhuda wako.

Mheshimiwa Spika, ushuhuda wa kwanza ulikuwa Mwenyekiti wangu, mimi nimeshapata ajali, tukiteremka K/A basi Wabunge wanaelekeea *VIP* yeye alikuwa hakubali mpaka tufuatane taratibu mpaka niingine *VIP*. Yote ile alinionesha huruma kuwa huyu Mheshimiwa Riziki lazima nimuhurumie, siwezi nikamuacha nyuma lazima niende naye, Mwenyezi Mungu huruma yako na wewe utapata watu wa

kukuhurumia. Mimi nakupongeza sana na Mwenyezi Mungu...  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitataja baadhi ya Wabunge ambao walinionesha kunipenda na kunihurumia, wa kwanza, Mheshimiwa William Lukuvi, huyu ni mtani wangu lakini alihakikisha katika Bunge hili amenifaraji sana, hakunipa kiburi na alikuwa akiniona ananinyang'anya magongo na mimi namwambia wewe kama unaninyang'anya magongo nitaenda kukushitakia kwa Rais kwa vile unaninyang'anya magongo lakini ile yote ni kuonesha yeye kwangu alikuwa anipenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ngeleja, huyu alikuwa akiniona aniambia aah Osama Bin Laden upo nikamwambia nipo ndani wala sina wasiwas. Mheshimiwa Chenge amenifundisha mambo mazuri, mimi siyo mwanasheria, mimi ni mhasibu *by profession*, lakini kwa busara za Mheshimiwa Chenge nimejifunza mengi sasa hivi mimi ni mwalimu mkubwa ndani ya Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwinyi; Mheshimiwa Mwinyi anatoka Zanzibar lakini hana kiburi na ndio maana nataka niwaambie Wabunge wenzangu ishini mkijua dunia hii tuachane na kiburi, siku moja tutaondoka tutarudi kwa Mwenyezi Mungu mwenye kiburi peke yake Mwenyezi Mungu. Vilevile niwaase vijana, haifai kuwa na tabia mbovu, ujeuri, lugha mbaya itakusaidia nini? Siku moja utakuja kupata tatizo hawahawa ndio watakaokufariji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwamoto; Mheshimiwa Mwamoto huyu mimi ni kibajaji fulani pamoja na Mheshimiwa Lusinde (Kibajaji) humu ndani ni marafiki zangu wakubwa.

Vilevile niwapongeze wanawake fulani mmoja wapo Mama Sitta ameiendesha *TWPG* kwa njia nzuri, leo tumejenga shule ya sekondari ni mfano wa wanawake kuwa tumewajengea wanawake wenzetu/watoto wa kike shule ya sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza mdogo wangu Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Mboni Mhita, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Mheshimiwa Mariam Kisangi na Mheshimiwa Shamsia Tamba. Vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Shally Raymond, nikiwa katika kamati yeye ndiyo ananibebea begi langu kutoka nje, hii yote ni dalili ya upendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo siku tatu kabla ulinipa nafasi ya kuchangia humu ndani, sasa hivi nitatulia. Ulinipa nafasi ya kuchangia, maana ya kunipa ile nafasi kwangu nimejuliza maswali mengi sana, nilikuwa ni mtu wa kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais na nilipompongeza Mheshimiwa Rais kwa mazuri yote ambayo alikuwa anayafanya katika kipindi chake cha miaka mitano na nikarudia nyuma katika bajeti zake za nyuma ilikuwa inapita bila kusumbuliwa, hili yote ni dalili kuwa allkuwa na uwezo mkubwa na kipaji yeye na Mheshimiwa Mwinyi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hilo nimevumilia nimeshindwa, leo natangaza rasmi kama utaridhia na wataridhia mimi ninarudi katika Chama cha Mapinduzi, nimerudi nyumbani kumenoga. Nimerudi nyumbani... (*Makofi/Vigelegele*)

**MBUNGE FULANI:** CCM kunogile.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, nimelelewa na Chama cha Mapinduzi, Iakini yaliyojitokeza naomba mnisamehe na kama niliwakwaza na wale walionifanyia maovu dhidi yangu mpaka nikafikia hapa naomba Mwenyezi Mungu niwasamehe sana na nasema tena nimerudi kwa sababu nydingi, sababu ya kwanza nimemuona Mheshimiwa Rais ni msikivu na hoja yangu atakaposikiliza atakuwa ni msikivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini namwambia ni msikivu, naomba mnisikilize, naomba masikio yenu; mwaka 2015 Mheshimiwa Rais alinikuta hapo nje akaniambia Mheshimiwa Riziki unafanya nini hapo? Nikamwambia nipo nataka kwenda nyumbani kufuturu, sasa mimi ndiyo baba watoto

twende nikamwambia *okay* twende, akanichukua mpaka nyumbani kwangu, tukafuturu naye, tuliongea kama ni ndugu yangu kabisa. Hivyo kukaa upande wa pili mimi nadhalilika sana, lakini siyo kwa kusudi yangu ni maovu niliyotendewa, nilishinda lakini nikakatwa bila sababu ya msingi, lakini nasema tena naomba msamaha, naomba msamaha. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana Bi Riziki, nakushukuru sana

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** ...mwenye kusamehe yupo karibu na Mwenyezi Mungu na wote walionifanyia maovu nawasamehe kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naomba unisamehe, Wabunge wenzangu naomba mnisamehe, lakini yejote ambaye nitakuwa nimemkwaza naomba vlelevile msamaha. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Riziki.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sina mengine nasema tena kwa idhini yako upo katika Kamati Kuu na wote Wajumbe wa Kamati Kuu naomba msamaha kuwa nimerudi nyumbani kumenoga. *Asalaam Aleykum Wamalaturulah Wabarakatuh.* (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana Bi Riziki Lulida, tunakushukuru sana yote ni mapito na sisi ni ndugu zako tupo pamoja Bi. Riziki; ni historia ya maisha, maisha ni mapito. Ndiyo maana wapo rafiki zangu kina Mheshimiwa Haonga na wengine huwa nawaeleza muwe na kiasi kuna kesho, siasa ni shule kubwa na katika *universities* kubwa Bunge hili, hili Bunge ni chuo kikuu cha nchi, utawaona watu wakienda kushoto, wakirudi kulia, wanakuja kati na kadhalika. Kwa hiyo, tunakushukuru sana Bi. Lulida, dada yetu wa siku nyingi, tumekuwa na wewe na tupo na wewe mpaka mwisho wa dahali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Hongoli atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Musukuma na Mheshimiwa Ally Keissy atafuata.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye bajeti hii ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia zawadi ya uhai mpaka nikawa salama mahali hapa siku ya leo na kuweza kusimama katika Bunge lako tukufu, nashukuru sana, nasema ahsante sana kwa Mwenyezi Mungu kwa yote anayonijaalia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, nimpongeze Waziri Mkuu na Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kazi kubwa ambazo wamekuwa wakizifanya za kuhakikisha kwamba wanamsaidia Mheshimiwa Rais na hatimaye nchi yetu imeweza kupata mafanikio makubwa sana. Miradi mingi mikubwa ambayo imetekelozwa hapa nchini kama miradi mikubwa ya sekta ya afya, sekta ya maji, miundombinu na miradi mingine ya umeme imeweza kutekelezwa na tumeweza kufanikiwa kwa sababu ya ushirikiano mzuri na kazi kubwa ambayo wanaifanya Mawaziri na Naibu Mawaziri wote wakishirikiana na Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu na watendaji wengine wote wa Serikali.

Kwa hiyo, napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru sana kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kwanza kuishukuru Serikali kwa kazi kubwa ambayo imefanya hasa kuhakikisha kwamba inajenga miundombinu ya barabara yenye urefu wa kilometra 2624.27 kwa nchi nzima, hii ni kazi kubwa haijawahi pata kutokea, lakini imeweza kutokea katika awamu hii ya tano. Kwa hiyo, niombe sana wakati bajeti tunaenda nayo, niombe sana kuna baadhi ya maeneo kuna barabara zile ambazo zinaunganisha mkoa mmoja na mkoa mwingine au Wilaya na Wilaya bado hazijakamilika basi nazo hizo ziweze kuingia kwenye mpango ili nazo ziweze kukamilika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika Jimbo langu la Lupembe, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe tuna barabara yetu ile ya Kibena – Lupembe – Madeke na hatimaye Milimba inaunganisha mikoa miwili kati ya Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Morogoro. Barabara hii tumekuwa tukiipangia bajeti toka mwaka wa kwanza 2016 mpaka leo bajeti ya tano tumeipangia fedha lakini bado haijaanza kujengwa kwa kiwango cha lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niombe sana Serikali na Mheshimiwa Dkt. Mpango hebu barabara hii iweze kupata fedha ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami. Barabara hii inaunganisha kwanza Mkoa wa Njombe na Morogoro kama nilivyoeleza, lakini pia inapita kwenye eneo kubwa sana ambalo kuna uzalishaji mkubwa, uzalishaji wa miti ambayo ni ya mbao, miti ya kutengenezea nguzo na miti ya mirunda ambayo tunaitumia katika ujenzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pili kwenye eneo hili pia ambalo tunapita, eneo la Lupembe ni eneo ambalo linazalisha zao la chai na mazao kama ya kahawa na mazao mengine ya matunda. Kwa hiyo, ni eneo muhimu sana kiasi kwamba tukipitisha tukiwa na barabara ya lami katika eneo hili, kwa hiyo, eneo hili kwa maana ya Mkoa wa Njombe kimapato utaweza kuongezeka sana kwa sababu ni eneo la kiuchumi, uzalishaji mkubwa. Kwa hiyo, inapofika wakati wa mvua nydingi, mazao haya ambayo nimeyataja kwa mfano mbao, nguzo za umeme, matunda mbalimbali ambayo yanazalishwa katika maeneo haya huwa hayawezi kufikia soko kwa sababu barabara hii inakuwa haipitiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kumbe basi tukiweza kujenga hii barabara kwa kiwango cha lami, mazao haya ambayo nimeyataja yataweza kufikia soko kwa wakati na hatimaye uchumi wa Mkoa wa Njombe utapanda, lakini pia uchumi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ambayo inategemea sana hii barabara kwa asilimia kubwa itaweza kuongezeka. Kwa hiyo, ni fursa kubwa sana kwetu sisi wana Njombe kwa hii barabara ikijengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe sana Serikali hii ya Awamu ya Tano ambapo inaendelea sasa hivi katika bajeti hii kwa kuwa tumeipangia fedha basi hii barabara ipate mkandarasi na ianze kujengwa kwa kiwango cha lami kwa sababu kila kitu kimeshakamilika, upembuzi na usanifu wa kina umeshafanyika lakini pia makabrasha yameshaandaliwa, bado tu kutangazwa ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali iweze kujenga hii barabara kwa kiwango cha lami ili hatimaye uchumi wa maeneo hayo uweze kukua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine niipongeze sana Serikali katika kukua kwa mapato imeweza pia kupitia miradi mbalimbali ambayo imeanzishwa imeelezwa taarifa kwamba imeweza kuhakikisha kwamba katika kipindi hiki kifupi miaka mitano, jumla ya ajira milioni 12 zimeweza kuanzishwa/ kutokea kutokana na shughuli hizi za kiuchumi ambazo zinaendelea mahali hapa. Katika hizi shughuli, asilimia kubwa ni shughuli/ajira ambazo zimetokana na kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kumbe basi tukiwekeza vizuri kwenye kilimo, tukipanua fursa nyingi za kilimo kwa kutengeneza hii miundombinu, kuwekeza viwanda vidogo vidogo na kuviiwezesha basi ajira zitaongezeka haraka sana kama inavyoonesha kwenye taarifa kwamba kilimo kumbe ndio kimefungua ajira nyingi zaidi ikifuatiwa na Wizara ya TAMISEMI nayo imefungua ajira zaidi ya 2,473,000. Kwa hiyo, kumbe basi tukifungua hizi fursa za kilimo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ismail Joram Hongoli, tunakushukuru sana kwa mchango wako. Nilishakutaja Mheshimiwa Kasheku.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kumteua Dkt. Mpango kuwa Waziri wa Wizara hii na nimekuwa Bungeni hapa kwa miaka mitano, kwa mara ya kwanza nimemuona Mheshimiwa Mpango amecheka jana wakati anawasilisha kwenye lile neno alilomalizia la mshale wa Uwanja wa Taifa, lakini siku zote sijawahi kumuona Mheshimiwa Mpango anacheka hapa, kila siku ni mawazo. Nimpongeze sana Mheshimiwa Mpango pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara yake, mmeefanya kazi kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kumuona mtu mmoja hapa, Dkt. Mpango kwa historia yake tunajua alkhuwa Mhadhiri wa Chuo Kikuu. Amesimama msomi mdogo mdogo tu kama mimi hapa anaanza kusema Dkt. Mpango amefeli, ana zero, lakini nikiangalia hii zero ya Mheshimiwa Mpango naona kama ni nzuri ambayo Watanzania imetufikisha hapa.

Mheshimiwa Spika, anayesema mwenzie ana zero, keshokutwa Jumatano anatarajia kufuatwa na gari iliyonunuliwa na mwenye zero, sasa sijui mwenye zero atakuwa nani. Nimuombe ajirekebishe mambo mengine yanaudhi lakini hawa ndiyo watoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kiukweli mimi ningekuwa Rais wewe na Katibu Mkuu wako, mimi nikuombe hata mawazo tunayosikiasikia ya kugombea, kaa ushughulike na miradi mikubwa, achana na kwenda Jimboni, hivi tunakutoaje kwenye hiyo nafasi wakati Watanzania wote tunafurahia kazi mnazozifanya. Usije ukatukwepa kwenda kushughulika na Majimbo, kaa kwenye Wizara hiyo usiondolewe na uendelee mpaka hii miradi ufe nayo wewe mwenyewe uliyeianzisha. Nadhani *messageimeenda* na Mheshimiwa Rias anaangalia Bunge amenisikia, ataweza kuchukua huu ushauri wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, nilikuwa naomba kutoa ushauri kwenye mambo mawili/matatu utanivumilia. La kwanza, Mheshimiwa Rais amesema tiba asili, Wizara ya Afya itengeneze miundombinu ambayo na wao wawe na sehemu yao ya kufanya utafiti, sasa kuna changamoto.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Kitengo cha Tiba Asili msimamizi wake mkuu ni daktari wa hospitalini, haya mratibu wake Dkt. Susan naye ni daktari. Upatikanaji wa dawa hizi hata ukimuuliza Mheshimiwa Shekilindi na wataalam wengine una *style* zake, mtu anayetafiti dawa za kienyeji pengine anaota usiku, anaenda kuchimba, akiwa kwenye ndoto halafu unafikisha kule kwa msimamizi anakwambia nieleze ulichochanganya, hii kitu haiwezekani kwa sababu hiyo ni siri/taaluma yangu siwezi kumpa mtu kiuwazi, aniache nichangaye halafu nimpatie yeye aende akafanye uchunguzi wake *NIMR*kama inafaa au haifai, lakin masuala ya kuwahoji watu umechanganya mti gani, wote tutakuwa waganga humu ndani itakuwaje, hiyo kitu haiwezekani. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikuombe kwenye Corona hapa Watanzania walivyochukulia nyungu walikuwa hawaaulizi umechanganya nini, alikuwa tu anataka afukizwe apone. Kwa hiyo, tuwape uhuru watafiti hawa na niishauri Serikali hawa wasimamizi watafutwe wenye taaluma ili wabishane taaluma kwa taaluma, siyo taaluma ya uganga halafu na taaluma ya daktari wa sindano, hiyo kitu haiwezekani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la pili, kuna vitu ambavyo tiba mbadala wanazuiliwa na Wizara ya Afya kwa mfano kipima joto na kipima sukari vitu ambavyo haviitaji *degree* kuvikariri na mmeona hata wakati wa Corona hakuna mtu alikuwa anaulizwa umesoma wakati unapimwa, hata hawa mgambo wanaotupima huku kwenye maofisi wengine hata darasa la saba hawajafika lakini kwa sababu ya *pressure* ya kufa watu walikuwa wanakubali. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri waruhusiwe wawe na hivi vitu kwa sababu ni vitu ambavyo hata watu wenye taaluma akimpa mtu akimuona anajua

huyu ana *temperature* ya kiasi gani, nimtibu kwa kiasi gani.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kumpongeza sana na nakubaliana na Mama Tibaijuka na Dkt. Tiisekwa hawa ni wasomi wakubwa, Mama Tibaijuka amekaa huko WHO, lakini amekuwa wa kwanza kuisemea tiba mbadala lakini humu kuna watu wana ka-degree kamoja tu akikuona na kadawa kakienyeji maneno hayo. kwa hiyo, tuoge mfano kwa hawa wasomi wakubwa kama kina Prof. Tibaijuka na Dkt. Tiisekwa ambao wamekuwa wawazi na ni wasomi wakubwa wallobobe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma ukurasa wa 107, nivumilie dakika moja, kuhusiana na Bodi ya Sukari, maelezo ya Waziri ni mazuri sana kuboresha sijui nini. Ushauri wangu tu mwepesi, ninashauri hii Bodl ya Sukari Serikali kama watanisikia wangeivunja kabisa ikawa haipo, lakini mbadala wake tuwe na shirika kama iliyyo TPDC. Tungekuwa tumeacha watu wanajiagizia mafuta kila siku wangekuwa wana uwezo wa kuamua ku-control/wenyewe bei mnahangaika, lakini Serikali imeweka mfumo mzuri, tunaendelea kupata mafuta kwa bei nafuu. Hata hii Bodi ya Sukari vunjilia mbali halafu tuwe na shirika la kuagiza sukari, sukari iwe mali ya Serikali ambayo hautoona tena biashara za kubadilikabadiika kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, namshukuru sana Mheshimiwa Rais mimi ni Mbunge ambaye ninarudi bila kipingwa kwa sababu yote alioyahidi Mheshimiwa Rais yapo. Kuna Hospitali ya Wilaya, vituo vyatya afya, umeme wa kutosha, barabara nzuri na maji yapo, unanishindaje sasa wakati kulikuwa na wasomi ma-degree yamewashinda miaka yote. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Rais najua unaniangalia kwamba mimi ni Mbunge wako ambaye sipingwi, hata nikipingwa ni kwa sababu watu wanataka uteuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunilea vizuri, niwashukuru Wabunge wenzangu najua nazungumza kwa

mara ya mwisho na wananchi wangu walionichagua wameshaniita Mbunge wa kudumu, nina imani tutarudi pamoa hapa ndani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hata kule pembedi kuna watu ni namna tu wanashindwa kutamka lakini tukikaa kwenye kantini wapo kama saba, kama itafika Jumatano hawajatamka labda ni uoga tu wa kumuogopa mwamba. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho nashukuru taarifa ya Polisi iliyotaja jinsi Mheshimiwa Mbowa alivyoumia. Sasa ninawaangalia huko watu wengine wamejifunika maplasta yaani na akili zenu mnaenda kuumizwa na mlevi na taarifa imetoka sasa tujibishane basi huko mtandaoni ninjy mbishane na wataalamu, mtu ameumia kakifundo mnakodi ndege, humu kuna waganga wa mifupa Kalemani na mimi hapa hebu mrudisheni hapa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, narudia kusema mrudisheni mimi nitamtibu ili kwenye kampeni tuwe naye asisingizie kifundo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru dawa imeingia, ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma. Mbunge lazima ujiamini, Mbunge unalalia utarudije hapa, lazima ujiamini vitu vimefanyika, mambo yamefanyika, nakushukuru sana Mheshimiwa na Wabunge wengine igeni nendeni kifua mbele, ndiyo maana siku moja nikatabiri nikasema wakirudi watatu lakini mna nafasi ya kuweza kurudi Frank Mwakajoka vumilia vumilia kwa sababu ziko sinema nyingine kidogo zinatia aibu kama hii sinema anayoelezea ndugu yetu na kadhalika, ndiyo hivyo tena. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Ally Keissy nilikutaja atafatia Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu atafatia Mheshimiwa Dkt Charles John Tizeba.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi na mimi nizungumze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono bajeti 100%. Bajeti ya mwaka huu kwa kuwa hata mafuta hayakupanda bei, kwa hiyo kusema kweli wananchi wengi wamefurahi bajeti ya mwaka huu ni nzuri kuliko bajeti zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa kantini lakini nikasikia Mbunge mmoja wa CHADEMA ambayo mambo mengi ameshaeleza udhaifu wao na Mheshimiwa Jacqueline haina haja ya kurudia maana yake ni mambo yao namna hiyo hiyo moja.

Mimi nitakwenda kusema kwamba nasema wavuvi wa Ziwa Tanganyika hawajasaidiwa, kusema kweli huyu naona si mwenyeji wa Ziwa Tanganyika anababaika. Mimi mwenyewe nimegawa injini tisa, tena siyo kwa kukopesha kugawa bure injini kwenye vijiji vya mwambao wa Ziwa Tanganyika, kijiji cha Kipili, Manda Uhuru, Itete, Kazobu, Bumanda, Kanchui, Utita na Kalila injini Yamaha mpya kila injini thamani yake shilingi 4,500,000 nimewapa bure wanakijiji bure, anashangaa ati wavuvi hawajasaidiwa anataka wapewe nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bajeti ya jana imepunguzwa leseni imepunguzwa ilikuwa inachajiwa leseni kwa dola dagaa dola 1500; jana wamesema itakuwa dola 250 anakuja anaropoka ropoka tu humu Bungeni kiajabu kiajabu. Migeubuka...

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Tulia wewe nikupashe, tulia hujuj chochote.

## TAARIFA

**SPIKA:** Mheshimiwa Keissy uwe mvumilivu kidogo tu tusikie hiyo taarifa.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na kabla sijampa taarifa nafikiri nataka nimuneshe utofauti wa mimi na yeye kwamba mimi na yeye nani ni mropokaji. Nazungumzia Jimbo la Nkasi Kaskazini ambalo yeye amekuwa Mbunge miaka kumi, baada ya kuwapatia hivyo anavyodai aliwapeleke, ameenda kuwanyang'anya akiamini kwamba Watanzania hawana akili au Wana Nkasi sasa nampa taarifa kama ametoa asitoe povu tukutane kule.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika,...

**SPIKA:** Sasa utulie, usilete fujo kama yule wa mwanzo, Mheshimiwa Keissy taarifa unapokea?

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, aende Milembe akapimwe akili, sijanyang'anya injini hata moja, naona akapimwe akili aliyosema Jacqueline naona yanamwingia sasa, wananchi watamshangaa sijanyang'anya injini hata moja.

Mheshimiwa Spika, wamepunguziwa *license* ya Migeureka toka dola 800 mpaka dola 400 wavuvi bajeti ya mwaka huu aliwahi kuzungumza kwamba Namanyere hamna huduma ya afya, Namanyere kuna hospitali zaidi ya vitanda 250; Hospitali ya DDH Namanyere juzi tumefungua Hospitali ya Wilaya na watumishi 28, tuna kituo cha afya kinafanya mpaka *operation* na tumeongezwa milioni 300 kwenye Hospitali ya Wilaya hajui chochote. (*Makof*)

Leo Jimbo langu la Nkasi nimelikuta halina umeme hata kijiji kimoja mpaka Namanyere, leo hakuna kijiji Wilaya ya Nkasi hakina umeme hata kimoja hakina umeme mpaka napeleka umeme Kisiwa cha Mandakerenge, hajui tuna gari/ *ambulance* mpaka Kabwi na Korongwe, Kirando Namanyere Mjini tuna barabara ambayo yanapitika masika na kipwa, tumepata barabara za lami Namanyere mjini zimeweka kilometra tatu awamu hii, tukakutane naye wapi? Kwa Mbewe? (*Kicheko*)

Leo Wabunge wanahama usiku na mchana Madiwani wanahama tukakutane wapi? Wewe si analala usingizi. Jacqueline kawaambia hapa kawaambia ya kutosha mtu anaumia kwenye ngazi? Hamna mgombea Urais ninyi, hamna mgombea Urais wala Ubunge hamna wagombea Ubunge wala Madiwani, tuliwapiga Serikali za Mitaa 100% hawa. Wilaya ya Nkasi hata kijiji kimoja hawakupata, unakuja unaropoka Bungeni hapa kwamba mashine nimewanyang'anya, acha unafiki, ya Jacqueline hayajakuungia wewe umeachana na mume wako Mbunge ameachana na mume wake. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, basi Mheshimiwa Keissy inatosha, ahsante sana dakika tano zimeisha. (*Makof*)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Baada ya kupata Ubunge umeachana na mume wako. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Keissy dakika tano zimeisha ahsante sana.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**SPIKA:** Ahsante sana muda umeisha, inatosha, mmeyataka wenyewe hayo, sasa mtapambana huko huko, lakini kwa maelezo ya Mheshimiwa Keissy mshindi anajulikana kwa sababu vitu vimefanyika watu wanaviona ndiyo maana ni kazi sana, *politics* ni ngumu mtaelewa somo tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt Charles Tizeba.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nadra kuchangia bajeti hii nzuri sana. Naomba nichukue nafasi hii ya awali ili nisije nikasahau niunge mkono kwa nguvu zangu zote bajeti hii ambayo kwa kweli kila mmoja ameikubali hapa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naendelea kukupongeza wewe Rais wetu, Waziri Mkuu, Mawaziri na viongozi wote pamoja na Wabunge kwa kufanyakazi nzuri kwenye maeneo yetu, nawapongeza mno. Lakini vilevile na mimi niwapongeze wananchi wa Hanang na kuwashukuru sana kwa kushirikiana na mimi katika kuleta maendeleo katika nchi yetu nitazidi kuendelea na wao na ninawashukuru sijui niwashukuru kwa kuniambia niendelee kuwa Mbunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi namshukuru Waziri kwasabu kwa kweli ameisimamia vizuri *TRA*, imeongeza mapato kwa 13.6% na vilevile uchumi wetu wakati wote amekuwepo umekuwa umeongezeka ulifika hata 7% na vile vile napenda kusema kwamba mwaka huu tulikuwa na trillioni 24.85 ambayo zilitumika na Wilaya ya Hanang ikapewa bilioni 3.5. Lakini vilevile na Hanang yenyewe iliongeza mapato yake siyo Wilaya ambayo ina mapato makubwa billioni 2.7 na kwa miaka yote mitano tumeweza kuchangia billioni 11.67 lakini wananchi walifanya kazi kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kuipongeza Benki Kuu kwa ajili ya kushusha *Statutory Minimum Reserve (SMR)* kutoka 7% mpaka 6% kwa ajili ugonjwa wa Corona hili litasaidia sana katika kukabiliana na ugonjwa huu. Lakini vilevile naomba niseme katika hayo mapato mliyotuletea Hanang imeweza kuongeza madarasa mengi ya msingi imeweza kuongeza shule za sekondari na vile vile vyuo vya afya na barabara, lakini nishukuru sana kuwa na *TARURA* ambayo sasa inajenga barabara vijijini. Wilaya ya Hanang ilikuwa haina hata barabara ya kwenda kwenye kata mbalimbali hata tarafa zingine lakini leo kata zote zina barabara na ninaomba *TARURA* iweze kuwezeshwa zaidi jamani ili barabara ziweze kujengwa na barabara kuu zitaweza kutoa mchango mkubwa wa uchumi kama viji vitakuwa na barabara.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana barabara mbili na nilishatoa maombi haya kwa Serikali kutoka Bisambalan kwenda Dareda mpaka Lalaji na Masusuu Katikati. Lakini barabara ya pili kutoka Masaroda kwenda Lambo na kwenda Dareda hospitalini, lakini pamoja na hivyo

naipongeza Serikali na bajeti hii kuweka bajeti ya kuweza kukarabati barabara zilizoharibiwa na mvua na kule Hanang barabara karibu zote zimeharibiwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile suala la maji siyo jambo dogo wilaya ya Hanang iko kwenye eneo kavu na kwa ajili ya *Rift Valley* huwezi ukapata maji kwa kuchimba mita 100 mpaka mita 200 au hata 300. Naomba tuiangalie sana kuna maji ambayo kuna *contracts* ambazo zimeanza lakini hawakufika mahali naomba kama kuna hela zipelekwe ili watu wetu..., tulikuwa na visima vinane awali leo tunavisima 80 na zaidi, lakini hali ya maji ya Hanang siyo nzuri naishukuru Serikali kwa kutupa bilioni 2.5 kwa ajili ya Katesh; bilioni 1.3 kwa ajii ya Endasak na bilioni 1.2 kwa ajili ya Masakta na sehemu zingine ninaomba tuungane kwa pamoja kuweza kumsaidia Waziri wa Fedha kwa miaka inayokuja na Rais wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, namtakia Rais wetu kwa kweli afya njema ametusaidia sana kukabiliana na Corona, ametusaidia sana kujenga uchumi, ametusaidia sana amani na utulivu na upendo kati yetu, tukiendelea kufanya hivyo kwa niaba ya watu wa Hanang, wananchi wa Hanang tunamshukuru Rais, tunamshukuru Waziri Mkuu, Makamu wa Rais, Mawaziri wote, Wabunge wote naomba tuendelee kushirikiana na Mwenyezi Mungu ataendeleza nchi yetu na Corona itapita kando ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana nisingetaka kuchukua zaidi ya dakika ulizonipa kwa sababu umenipendelea na wewe Mungu akupe afya njema, Kongwa wakupe kura zote na asitokee mtu na mimi naomba vijana wangu wajifunze kutoka kwangu muda si mrefu nitakapostaafu watakwendwa kunirithi, lakini kwa muda huu wa miaka mitano iliyobaki nitakuwa na ninyi na nitakuwa nawaelekeza mambo ya kufanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aAhsante sana ninaunga mkono bajeti hii na ninampongeza Waziri tena. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu. Mheshimiwa Dkt Charles John Tizeba atafatiwa na Mheshimiwa Paschal Haonga.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi kushiriki katika kuchangia hoja iliyo mbele yetu, namshukuru na kumpongeza Waziri wa Fedha na timu yake yote kwa hotuba nzuri, bajeti ambayo imegusa Watanzania wote na kama kuna mzalendo hana sababu ya kutilia mashaka utekelezaji wake na hivyo Tanzania itapaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mchango wangu leo ni kutoa ushuhuda, naomba nitoe ushuhuda wa mtu mmoja ninayemjua nianze na mimi mwenyewe; mwaka 2000 nikiwa Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza yalitokea mafuriko pale mjini watu 17 wakafariki Rais Mkapa akawa amemteua Ndugu Joseph John Pombe Magufuli kuwa Waziri wa Ujenzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Ndugu Magufuli alikuja Mwanza kuona jinsi barabara zilivyokuwa zimeharibika na baada ya hapo aliamuru kituo cha mafuta kivunjwe katika barabara ya kuelekea *Airport*. Kituo kilivunjwa nikasimamishwa kazi miaka mitano baada ya hapo tukakutana Bungeni mwaka 2010, mwaka 2015 akachaguliwa kuwa Rais, watu wa Mwanza walidhani hanipendi sana, lakini mwaka 2016 akaniteua kuwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Huyo ndiyo Magufuli ninayemjua mimi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2015 akaanza ujenzi wa reli ya kisasa, kununua ndege, kujenga bwawa kubwa la kufua umeme huko *Stigler's Gauge*, wakosoaji wakapiga makelele kwa nini hakopi? Ananunua ndege kwa pesa taslimu, anajenga reli kwa fedha za ndani, lakini baadaye watu wa mazingira wakaingia wanatetea miti na kadhalika, lakini leo *UNESCO* wamemtambua wamemuelewa, Watanzania wamemuelewa, wakosoaji wamejua madhara ya madeni makubwa makubwa huyo ndiye Magufuli ninayemjua mimi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini si hivyo tu miaka 30 au zaidi wachimbaji wa madini nchini hapa wamekuwa wakipora na wakichukua mchanga wetu wakisema hauna thamani, mwaka juzi hapa akawapiga *stopwakosoji* tena wakaingia akina Tundu Lissu wakasema tutashitakiwa kama Taifa, tutakosa sijui nini, tutalipa madeni makubwa ya kuvunja mikataba, lakini Barrick mwishowe wakaja mezani wakazungumza na Serikali jana nimesikia wameanza kulipa fedha bilioni 600 zimeingia Barrick wamemuelewa, Watanzania wamemuelewa tumekoma kuwa kichwa cha wendawazimu kwenye madini huyo ndiyo Magufuli ninayemjua mimi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama vile haitoshi Corona ikaja, dunia nzima ikapagawa, wanaojua sayansi wakawa hawana majibu, lakini Rais huyu akawaambia Watanzania tulieni huu ni ugonjwa kama ugonjwa mwingine, leo tumo humu ndani barakoa zimepungua, *WHO* walioituambia tujifungie ndani wao wenyewe wameanza kunyooka, lakini siyo hivyo tu kiona mbali cha Rais wetu kikamwambia hebu kapime hata hizo *sample*, akapeleka za mbuzi, akapeleka za *oil*, vile vifaa vikaonekana havitupi maji sawasawa, akina Trump wakazinduka na wao ndiyo wakaanza kurudisha vifaa wanavyonunua akina Macron na wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, dunia akaionesha kwamba yuko Mwfrika anaweza kufikiri nje ya boksi tumetawaliwa *minds* zetu kwa miaka mingi lakini Magufuli ameuonyesha ulimwengu kwamba Waafrika pia wanaweza kufikiri *independently*, huyo ndiyo Magufuli ninayemfahamu mimi. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, lakini siyo upande huo tu aliwatumbua akina Simbachawene hapa, akina Mwigulu Nchemba, akina Tizeba, akina Kangi Lugola, akina Andengenye, akina nani wengi tu, lakini mzee huyu wengi wamerudi kazini, wako wanachapa kazi, hajjalishi walifanya nini huko nyuma, lakini kila alipobaini kwamba bado wanao uwezo wa kuwashudumia Watanzania amewarudisha katika

kazi na leo tunaona wanaendelea kutufanyia kazi, huyo ndiyo Magufuli ninayemjua mimi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa najiuliza swali moja demokrasia katika *definition* maana yake nini; Serikali ya watu kwa ajili ya watu. Hivi Serikali ya watu kwa ajili ya watu Katiba tumeandika ya miaka mitano, 10 sijui ukomo tumeweka lakini mataifa yaliyopiga hatua kwa haraka ya nchi hizi zinazoitwa zinaendelea hayakujiwekea masharti ya ku-copyna ku-paste kama tunavyofanya sisi.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa najiuliza mantiki ya *presidential terms* ni nini; wote wanakiri ni kuzuia *popular presidents* wasibakie kwenye madaraka kwa sababu kama *president* na ni *popular you will be voted out* na hii *popular presidents* eti ndiyo tunaweka masharti wasiendelee kutawala wakati wananchi wao wanawataka waendelee kutawala. (*Makofii*)

Sasa Magufuli ameshatufundisha kufikiri nje ya haya maboksi, rafiki yangu Keissy juzi aliongea yeye alienda hatua mbaya tu ya kusema tumlazimishe, mimi naomba tusilazimishe mtu tubadilishe utaratibu wetu, tutende mambo ambayo yana manufaa kwa nchi yetu bila kujali nani anasema nini wapi. Kwa sababu kama *definition* ya *government by the people for the people*. Sasa kitu gani kigumu hicho cha kutaka mtu anayefanya vizuri aendelee kuongoza *as long as* watu wanataka aendelee kuongoza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Rais Nyerere alikaa miaka 23 Mahakri Mohamed wa Malaysia alikaa miaka 22 sisi wa kwetu akikaa miaka 20 kosa liko wapi? Tumechoka kuwa *colonized in the mind*, kuiga kusikokuwa na kufikiri, hebu tujitendee haki Watanzania kama Rais Magufuli anafanya anavyofanya na ataendelea kufanya anavyofanya Mungu ampe afya sisi tukae humu ndani mwaka kesho tuangalie utaratibu wa kuongeza kipindi, tusiogope *the unknown*, tatizo kubwa la haya mambo ni *fear of the unknown* kwamba je, akiwa hivi, sasa akiwa hivi je si mna *option* ya kupiga kula kumtoa? Kwa nini tunaogopa? Kwa nini tunaogopa?

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba.

**MHE. DKT. CHARLES TIZEBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja Mungu awabariki sana Watanzania wote, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Pascal Haonga atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo na Mheshimiwa Ezekiel Maige ajiandae.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushuru kwa kunipa nafasi naomba, nianze kwa kusema kwamba wakati mwingine sisi tunapokuwa tunaishauri Serikali sio kana kwamba hatuachi akiba ya maeneno au tunakuwa na nia ovu. Lengo letu sisi ni kutaka Serikali iweze kufanya kazi vizuri, ndio hicho, na ndio majukumu ya Mbunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali. Kwa hiyo mimi naomba nianze kwa kusema hivyo wala tusionekane kama sisi sijui tunatukana tunafanya nini. Lengo ni kuikosoa Serikali iweze kufanya kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba niende ukurasa wa sita wa hotuba ya Dkt. Mpango ambayo amezungumzia kulipa madai ya watumishi umma malimbikizo ya watumishi wa umma amezungumza kwenye ukurasa wa sita wa hotuba yake. Watumishi wa umma kwenye nchi sio kwamba wao wanahitaji kulipwa madai yao tu yale ya nyuma, watumishi wa umma wanahitaji kuongezwa mishahara ili waweze kufanya kazi katika mazingira mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ujisoma *standing order* (waraka wa watumishi wa umma) Sheria za Utumishi wa Umma ninayo hapa hii hapa nadhani nitakupatia hapo baadaye ujisoma ile 8(e) inasema kwamba na naomba kunukuu; *8(e)\_ an increment is an increase of salary within salary scales in which the prescribed amount which is granted annually to holder of post on incremental scales of salary until the maximum of*

*the scale is reached. In all cases information obtained through performance appraisal should be used in awarding or withholding increments provided that certain conditions are satisfied."*

Mheshimiwa Spika, ile inayoita *annual increment*, nyongeza ya kila mwaka ya mshahara kwa mtumishi ile sio hisani ni Sheria ya Utumishi wa Umma. Lakini Serikali hii Serikali ya awamu ya tano bajeti kuanzia ya kwanza 2015/2016 haijawahi kuweka nyongeza ya mshahara hata ile ya kila mwisho wa mwaka 2016/2017 haijawahi kuongeza; 2017/2018 haijawahi kuongeza; 2018/2019 haijaongeza 2019/2020; sasa hii ni bajeti ya mwisho 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kwa mazingira kama haya tunawaweka wapi watumishi wa umma wanapata wapi motisha kufanya kazi katika mazingira mazuri? Ndiyo maana umeona kwa mfano maeneo mengi hata shule ya *private* zinafanya vizuri zaidi kuliko shule za Serikali kwa sababu hata ukiangalia watumishi wao kwa mfano hawa walimu kwenye shule za *private* kuna motisha, kuna nyongeza inaonekana kule.

Mheshimiwa Spika, mimi niishauri Serikali kama bajeti hii Dkt. Mpango atakapikuwa anaipitisha siku ya jumatatu atuambie kwa nini Serikali ya Awamu ya Tano inamaliza muda wake haijaongeza mishahara kwa watumishi wa umma? Hali hii ni kwa kweli ni mbaya sana na na kweli naamini na wewe pamoja na majukumu mengine unayofanya utamuungoza vizuri Waziri siku anapo hitimisha atuambie kwa nini Serikali haijaongeza mishahara kwa watumishi wa umma?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo jambo hili ni jambo ambalo watumishi wa umma wamekata tamaa, watumishi wa umma wanaona kama wao kwenye nchi hii ni kama wameshawatupa, hawawajali. Kwa hiyo jambo hili jambo ambalo ni kwanza ambalo nilitaka nilizungumze.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nataka nigosie ni kuhusu suala la kilimo, Serikali ilianzisha utaratibu

wa kununua zao la kahawa kupitia Vyama vya Msingi vya Ushirika. Siku za nyuma kabla ya kuanzisha mfumo huo wa kununua zao la kahawa kupitia Vyama vya Msingi vya Ushirika kuliwa na makampuni mbalimbali ambayo yalikuwa yananunua, kulikuwa na vikundi vya wakulima kwa hiyo kulikuwa na soko huria kwenye zao la kahawa na mwisho wa siku aliyenufaika ni mkulima kwa sababu kulikuwa na ushindani. Leo Serikali imeruhusu...

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):**  
Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa naipokea kutoka kwa Naibu Waziri.

## TAARIFA

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):**  
Mheshimiwa Spika, nashukuru sana pamoja na mchango wa Mbunge ambaye ni Waziri Kivuli wa Kilimo, nataka nimpe taarifa kwamba hayo anayosema yalikuwa ni historia siku tatu zilizopita tumefanya mukutano na wadau tena kwenye Wilaya ya Mbozi anapotoka yeye ambao huo utaratibu tushaweka vizuri sasa hivi tumeshatangaza kwamba sasa hivi kuna mifumo mitatu ya ununuzi wa kahawa. Kwa hiyo, wanunuzi binafsi kwamba wanaruhusiwa waende kununua moja kwa moja kwa wakulima kupitia Vyama vyao vya Msingi vya Ushirika, lakini pia viwanda vyetu vya ndani vinaruhusiwa kwenda kununua moja kwa moja kwa wakulima ila kupitia Vyama vyao vya Ushirika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Pascal unapokea taarifa hiyo?

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa hajanielewa vizuri, kwa sababu utaratibu unaotumika ambao Mheshimiwa Naibu Waziri ameruhusu mifumo yote ifanye kazi *at once*, kwa maana ya Vyama vya Msingi vya Ushirika, Makampuni na kadhalika, walichokifanya sasa hivi ni kwamba yanapokuja makampuni kwa mfano ikija kampuni Mbozi kuja kununua kahawa kwa wakulima ile kampuni hairuhusiwi kwenda

kununua kwa wakulima moja kwa moja, inaenda kununua kupitia kwenye Chama cha Ushirika.

Mheshimiwa Spika, mimi ninachokizungumza hapa waruhusu makampuni haya yakanunue kwa wakulima moja kwa moja, waruhusu pia minada ifanyike, waruhusu pia kuwe na ushindani, utakapo kuruhusu ushindani...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, anayenufanika mwisho wa siku ni mkulima wa kahawa. Kwa hiyo, mimi ubaya wowote kikubwa zaidi waruhusu soko huria illi mwisho wa siku mkulima wa kahawa aweze kunufalka na zao la kahawa. Mkulima analima, Serikali imekaa pemberi, ananunua pembejeo Serikali imekaa pemberi, anapokuja kuuza ndipo Serikali inapokuja kusema kwamba uza kwa utaratibu huu. Jambo hili kwa kweli linawaumiza wakulima wetu sana na Serikali vizuri ikaweka jambo hili. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana dakika zako zimeisha, ahsante sana. Tunaendelea kwa sababu ya muda Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo atafuatiwa na Mheshimiwa Ezekiel Maige na tutaendelea.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Spika, nakushuru sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia bajeti iliyopo mbele yetu. Awali ya yote nimshukuru Mwenyenzi Mungu kwa zawadi ya uhai, lakini nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Fedha na Wizara yake kwa ujumla kwa kazi nzuri anayofanya, kwa kweli Watanzania wengi hatukumwelewa mwanzo, lakini sasa tumemuelewa na nchi yetu imepiga hatua kubwa sana kimaendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kadri

alivyoweza kutusaidia kuiendesha nchi yetu na hapa tulipofikia, maendeleo makubwa tumeyapata nikianza na sekta ya afya, katika sekta ya afya tumejenga zahanati 1,998 lakini katika hizo 17 zipo Njombe Mjini ambalo jimbo ambalo mimi naliwakilisha. Lakini vituo 48 vya afya vimejengwa kimoja kimejengwa Njombe, hospitali 10 zimejengwa moja imejengwa Mkoa wa Njombe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo bajeti ya dawa imeongeza kutoka bilioni 31 na moja mpaka bilioni 269. Sasa hivi tunapata dawa za kutosha na wananchi hawana malalamiko juu ya dawa, niombe tu kwamba katika jimbo letu na Njombe Mjini na sisi badala ya Serikali kutujengea kituo kimoja na sisi tumejenga vya kwetu viwili katika Kijiji ya Makoo, Kata ya Makoo tumejenga kituo cha afya na katika Kijiji cha Kifanya tumejenga kituo kimoja cha afya, tunaiombo Serikali itusaldie kupata vifaa kwa ajili vya vituo hivyo viwili vya afya ambavyo Halmashari ya Miji Njombe ikishirikiana na baadhi ya Madiwani na wananchi wa maeneo hayo wamechangia na mimi Mbunge wao nikishiriki kuhakikisha kwamba vituo hivyo vimejengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pekee ambalo leo katika nafasi hii nilyopata itakuwa ni nafasi yangu ya mwisho mwisho kuchangia katika Bunge kwa maana Bunge la awamu hii nimekuwa nikizungumza sana tatizo la maji katika mji wa Njombe. Miaka mitano mfulululizo nimeomba tupatiwe maji Njombe, lakini hatukufanikiwa, niombe sana mpaka dakika ya mwisho tumeahidiwa kwamba makandarasi atakuja kabla ya mwezi wa kumi kufanya hiyo kazi. Niombe Wizara ya Fedha ijitahidi kuhakikisha kwamba tunapata mkandarasi na tupata maji Njombe kwa sababu Njombe ni Makao Makuu ya Mkoa na hatuna maji yakutosheleza wananchi wa Mji wa Njombe.

Mheshimiwa Spika, elimu ya msingi na elimu ya sekondari zaidi ya triliuni moja imetumika katika elimu ya msingi, tunashukuru sana. Lakini fedha hii yote nyingi inaingia dosari pale ambapo panakuwa na upungufu wa walimu. Kuna shida kubwa sana ya walimu wa shule za msingi niombe

sana Serikali ijitahidi sana kuajiri walimu kwa ajili ya shule zetu za msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine la pekee sana katika jimbo la njombe mjini sisi wananchi wa Njombe ni wakulima wa miti ya mbao, mimi ya mbao sisi ni zao la kawaida kabisa kama wengine wanavyolima mkonge, wanavyolima pamba, wanavyolima korosho. Lakini inapofika kwenye mbao kuna tatizo kubwa sana la kodi ya VAT. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha hebu liangalieni tatizo la biashara ya mbao kwa wananchi wa Njombe. Kwa sababu VAT kwa Njombe imekwenda kinyumbe, kinyume VAT inakwenda kwa mkulimka kitu ambavyo sio sahihi kabisa na mkitumia wale Maafisa wa TRA waliopo pale Njombe hawawezi hili jambo kwa sababu wale mmepewa malengo ya kukusanya kodi pia mnataka wawaelemishe wananchi juu ya masula ya kodi ni ngumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri tumeni timu maalumu ikakae na wafanyabiashara wa mbao wa Njombe muangalie ni kwa namna gani kodi ya VAT italipwa, kwa sababu haiwezekani kabisa kodi ya VATiende kinyume kinyume wakati unajua kwamba kodi ya VAT wakati tunajua kwamba kodi ya VAT ni kodi ya mlaji hasa kodi ya VATimerudi nyuma madhala yake mwaka jana miche mingi imelala kwenye vitaru, wananchi hawakupa miti mashambani kwa sababu wameona kabisa kwamba kumbe kupanda miti sasa hakuna maana watu wanapata hasara wakiuza miti yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikuombe sana kwenye mbao kuna biashara endelevu na kuna kodi endelevu. Mheshimiwa Waziri tuma timu maalum ya wataalam wakaangalie mustakabali mzima wa biashara ya mbao wakishirikiana na wafanyabiashara wa Njombe utakuwa umetusaidia sana ili kusudi kodi ipatikane na biashara iweze kuendelea na wale wafanyabiasha wapo tayari kuendelea kulipa kodi tatizo ni kwamba maelekezo wanayopewa na TRA na taratibu zinazotumika haziibebi ile biashara, kwa hiyo ni jambo ambalo linahita na kujadili kukaa kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, tunapoindea kumalizia Bunge letu hili lipo jambo la barabara la Itoni - Lusitu; nashukuru sana kwenye bajeti nimeiona, niombe Serikali itekeleze ifanye utekelezaji wa barabara hii kwa sababu barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa ukanda ule wa njia ya Ludewa kuna kilimo cha chai na kuna kilimo cha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwalongo.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ezekiel Maige atafuatiwa na Ali Salim Khamis.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi, naomba niazé kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, hotuba hii ambayo imewasilishwa jana na Mheshimiwa Waziri kimsingi imetoa taarifa kwa utendaji kazi wa Serikali kwa miaka mitano kwenye maeneo yaliyo mengi na wote tumempsikia Mheshimiwa Waziri kwamba kwa taarifa ambazo ameziwashilisha na wote tunafahamu kwamba Serikali ya Awamu ya Tano katika eneo la uchumi imefanya *wonders* katika *micro economic indicators* zote inaonyesha Serikali yetu imefanya vizuri mno. Sisi wote ni mashahidi na tunafahamu kwamba kwa mfano makusanyo ya Serikali yameongezeka kwa asilimia mia moja kutoka wastani wa bilioni 800 hadi triliuni 1.5 kwa mwezi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia fedha ambazo zimekuwa zikitolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo imeongezaka kutoka wastani wa triliuni nne hadi zaidi ya triliuni kumi na mbili ukiangalia uwezo wa nchi kukopesheka umeongezeka na kwa ujumla nchi inafanya vizuri. (*Makofî*)

Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuyafanya haya ameisaidia nchi kuwa na uchumi imara ambao haujatikisika hata kwenye misukosuko kama hii ya Corona ambayo nchi zingine zenye uchumi mkubwa zimeweza kupata mtikisiko. (*Makof*)

Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais lakini kubwa zaidi nimuombee kwa Mwenyezi Mungu na kwa Watanzania kwamba Mwenyezi Mungu zaidi ampe afya njema na watanzania wenzangu naomba tuone kazi kubwa na nzuri aliyoifanya Mheshimiwa Rais wetu na tumpe zawadi na heshima kubwa ya kutambua kazi hii kwa kumpa anachostahili mwezi kwa kumi mwaka huu kwa kumpa kura zote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nisema katika hayo ambayo yamefanyika hayajawaacha wananchi wa Msalala, niishukuru sana Serikali hii tumeprata zaidi ya bilioni 14 za kutengeneza au kujenga mradi wa maji kutoka Magwa hadi llogi, tumeprata zaidi ya bilioni 23 za kupeleka maji Kango na Isaka na sasa wananchi wanapata maji, tumeprata zaidi ya shilingi milioni 200 kwa ajili ya kuanza mradi wa maji kutoka kijiji cha Ndukwa hadi Busangi na baadaye Ntobo.

Mheshimiwa Spika, tumeprata zaidi ya shilingi bilioni mbili za ujenzi wa wa kituo cha afya Bugalama, tumeprata zaidi ya shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya pale Ntobo, tumeprata zaidi milioni 800 kwa kituo cha afya cha Changaya na kituo cha afya cha Chela, yote haya yamefanyika katika kipindi kifupi zaidi miaka mingi ambayo tumekuwepo katika nafasi hizi. Lakini miaka hii mitano tume-*perform* vizuri niwaombe wananchi wa Msalala tuzidi kumuombea Mheshimiwa Rais wetu ili makubwa haya yaendelee kutokea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninafahamu Serikali inahitaji sana kupata fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mingi mikubwa ya maendeleo kuna eneo moja ambalo mimi nafikiri ni vizuri Mheshimiwa Waziri akalitazama, katika fursa zilizotokana na Covid-19 moja ya eneo ambalo amelizungumza ni kuanguka

kwa bei ya mafuta. Kuanguka kwa bei ya mafuta kumekuwa *reflected* kupunguzwa kwa bei kwenye *pump* au kwenye *retail services*.

Mimi nilikuwa nafikiria kwamba eneo hili pengine Mheshimiwa Waziri akaliangalia vizuri, kwa sababu mwezi wa kumi na mbili mwaka jana bei ya mafuta kwenye soko la dunia ilikuwa wastani wa dola 60 kwa pipa, kufika mwezi wa tatu mwaka huu imeshuka hadi chini ya dola 10 kwa pipa. Lakini athari zake kwenye bei ya soko kwetu sisi imepungua kwenye mwezi wa tano kuja wa sita kutoka wastani wa shilingi 1900 hapa Dodoma kwa petroli hadi wastani wa shilingi 1,600 ukiangalia imepungua kwa wastani wa shilingi 300; sawa.

Mheshimiwa Spika, kakini ukiangalia kwenye maeneo ambayo ni matumizi ya mwisho tumepunguza bei ya mafuta kwa shillingi mia tatu, bei za usafiri hazijashuka hata jana nimesafiri kwa basi kutoka Dar es Salam bei ni zile zile, lakini bei ya bidhaa sokoni iwe ni sukari, iwe ni vitu vyovyote vinavyozalishwa viwandani havijashuka. (*Makofii*)

Mimi nikataka kuishauri Serikali kwamba ni vizuri Serikali ingeangalia namna ya kutengeneza chanzo kwenye eneo hili kwamba kwa kuwa bei ya mafuta imeshuka basi fedha hizo au punguzo hilo badala ya kulipeleka kwa mtumiaji ambaye halifiki kwa mtumiaji wa mwisho Serikali iweke kwenye mfuko maalum ambao utakuja kusaidia kujenga miundombinu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hizi shilingi 300 kwa wastani wa bilioni sita za lita tunazotumia kwa mwaka zinaweza zikawa ni zaidi ya trilioni 1.2 fedha hizi zinaweza zikasaidia kuendeleza uchumi wetu na haitakuwa na athari kubwa kwenye uchumi kwa sababu uchumi wetu ni himillivu na uchumi wetu haujayumba kutokana na mtikisiko wa suala hili Corona.

Kwa hiyo, nilifikiri nimshauri Mheshimiwa Waziri aangalie kwenye hili eneo azingatie kwenye hili eneo kuangalia nini kinachoweza kufanyika badala ya kushusha bei ambayo faida yake hamfikii mtuaji wa mwisho bora bei

ikabaki palepale *stable* ile *potential decrease in price* ikawekwa kwenye eno maalum itakuwa kwa ajili ya maendeleo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba nina muda mfupi kama dakika tano niishauri Serikali kuna wakati tuliwahi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Maige tayari.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, aaaaah nashukuru sana naomba kuunga mkono bajeti hii, naunga mkono juhudhi zinazofanywa na Serikali naniwaombe Watanzania tutambue juhudhi za Serikali yetu kwa kutoa kura za ndiyo kwa Mheshimiwa Rais wetu nashukuru sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Maige. Mheshimiwa Ali Salim Khamis atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Rashid Ntimizi na Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi na Mheshimiwa Almas Maige wajiandae.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia. Awali ya yote namshukuru Mwenyenzi Mungu na mimi kunijalia kuwa sehemu ya kutoa maoni katika bajeti hii ya mwisho ya Bunge hili la Kumi na Moja. (*Makofii*)

Mimi kutokana na muda nataka nizungumze jambo moja tu na hili nataka nimshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni jinsi gani ambavyo anaweza kulisaidia Taifa. Nataka nitoe mfano kidogo ukiangalia katika kitabu cha Waziri wa Ujenzi ameiomba Serikali trilioni 4.7 kwa ajili kuendesha Wizara hii na ukiangalia kwenye mapitio baadhi ya mashirika ambayo yameizunguka Wizara hii kiukweli hayafanyi vizuri jambo ambalo mashirika hayo yangeweza kuisaidia hii Wizara na kuisadia Serikali badala yakuomba fedha za bajeti kutoka Serikalini yakawa haya mashirika yanajientesha yenye.

Mheshimiwa Spika, tukuchukue mfano Shirika la Simu la *TTCL* kwa kitabu hiki cha Waziri mwaka jana walipewa makisio ya bilioni 196 makusanyo yao, lakini wameweza kukusanya bilioni 60 pekee na matumizi yao ni bilioni 66. Kwa hiyo, ni zaidi ya zile fedha ambazo wao wamezikusanya na mwaka 2017 tulibadilisha sheria hapa kwa ajili ya kulifanya Shirika la Posta na Simu kwenda kibiashara na tulishauri kwamba hawataweza kuingia katika ushindani huu na makapuni haya binafsi kwa sababu mashirika haya yanategemea ruzuku kutoka Serikalini. Kwa hiyo, sasa kama ingelikuwa *TTCL* imejielekeza katika ile azma yake ya mwanzo kama Shirika la Taifa la Simu ambalo ukiangalia sasa hivi wateja wa simu za mkononi Tanzania ni karibuni milioni 38.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kama ingekuwa *TTCL* imekwenda kwenye dhamira yake ile ya awali kwamba taasisi za Serikali, za binafsi pamoja na majumbani wakaweza kuwa na hizi *landline* kuitia *TTCL* ambazo kwanza ni *security* kwa ajili ya nchi, pia *TTCL* ingeweza kukusanya mapato zaidi kuliko hivyo walivoingia kwenye ushinfani wa kibiashara na makampuni haya binafsi. Kwa mfano leo kama ingelikuwa *TTCL* kwa sababu inamtandao Tanzania nzima ingeweza kuwa na wateja milioni 10 tu katika Tanzania nzima ambao wateja hawa wanalipa ile *service fee* yao ya mwezi shilingi 10,000; basi *TTCL* ingekuwa na uwezo wa kukusanya bilioni 100 kwa mwezi na hasa ukizingatia *telecommunication* zote nchi unapopiga ndani ya nchi inakuwa ni *free*. Kwa hiyo, mtu anapopiga simu kupiga nje ya mtandao ambao si *TTCL* ndio anatakiwa alipe, nchi zote ukienda duniani inakuwa ni *free* kupiga simu hizi za ndani.

Mheshimiwa Spika, sasa leo ikiwa tunazungumzia watu milioni 10 ambao wangekuwa na simu za *TTCL* yaani ukizingatia maduka, taasisi za Serikali na za binafsi pamoja na majumbani, halafu ukizingatia *TTCL* ina Mkongo wa Taifa ambayo inaweza kupeleka *cable* hii itayokwenda kwenye kupeleka mawasiliano kwenye taasisi hizo mbalimbali pia inanafasi ya kuza *internet* kuitia *cable* hii hii ambayo wameipeleka *either* majumbani au kwenye maofisi na

kusababisha kwamba huduma za simu zikawa nafuu na ikaweza kuijendesha kimapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa ikiwa *TTCL* yenyewe baada ya kuanzisha utaratibu huu miaka mitano inawateja milioni 20, inaweza kutengeneza trilioni 2.4 na ikaisadia hii Wizara na hapa tunazungumzia *TTCL* peke yake hatujazungumzia Posta, hatujazungumzia Bandari, hatujazungumzia Viwanja vya Ndege, hatujazungumzia Madini na hatujazungumzia Utalii. (*Makofii*)

Sasa Mheshimiwa Mpango naomba uliangalie ili kufanya *review* tena upya ya mashirika haya kwa sababu ukizingatia leo hii yameweza kufanya biashara kwa asilimia moja tu, ukiangalia Vodacom wana asilimia 33, Tigo wana asilimia 27, Airtel wana asilimia 18, Halotel wamekuja juzi wana asilimia 10 ya *market* halafu Zantel ana asilimia tatu, *TTCL* ni ya mwisho ni asilimia moja, na kwenye hichi kitabu cha Waziri ameandika kabisa changamoto ambazo wao wanakumbana nazo ambacho kinawafanya kwamba hawawezi kwenda kwenye ushindani.

Mheshimiwa Spika, hakuna sababu ya kuitishwa mzigo Serikali kuyaweka mashirika yakawa yanafanya biashara ambayo hawawezi kwa sababu huwezi kushindana na Tigo au Vodacom wewe ukitegemea pesa ya ruzuku kutoka Serikalini halafu ukaweza kuifanya biashara hiyo ikawa na faida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya kutoa ushauri huo nikushukuru kwa kunipa nafasi, ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Ali Salim Khamis. Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi na baada ya hao atafutiwa Mheshimiwa Zainab Bakar.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa na mimi kwa muda huu mchache niweze

kuchangia katika Mpango wa Serikali na bajeti hii ya Serikali.  
*(Makof)*

Kwanza kabisa kwa sababu ya muda nianze kusema naunga mkono hoja, lakini la pili nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na timu yake yote, nimesema kwa sababu ya muda ziwezi kuwataja wote, kwa kweli mimi nimekuwa kwa miaka yote minne mipango ni mizuri na utekelezaji wa bajeti umekuwa mzuri siku hadi siku, lakini nataka nisisitize kitu kimoja, Mheshimiwa Mpango na timu yake wamekuwa ni wasikivu kwa sababu yale yote tuliyokuwa tunashauri humu ndani yamekuwa yanatekelezwa kwa vitendo katika bajeti zetu zote. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, Mpango unakuwa siyo matumizi kama utekelezaji, utafuatiji wa fedha unakuwa wa hovyo hovyo, nataka niseme Mpango wa mwaka 2015/2020 umekuwa ni matumizi kwa sababu kwanza udhibiti wa fedha umekuwa mkubwa kwa Wizara ya Fedha, ukusanyaji wa fedha ni madhubuti na mwisho wa siku miradi mingi ambayo imepangiwa mnpango mwaka 2015/2020 imetekelezeka kwa asilimia kubwa sana. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, waswahili wana msemo mmoja unasema usione vyaelea vimeundwa. Nataka niseme hata wale wanaosimama na kuepinga mpango na kupinga bajeti ya Serikali ukiangalia katika maeneo yao leo hii wana shule zimejengwa nzuri, wanahuduma za maji ambazo zimeboreshwa, wanapita katika barabara nzuri nakadhalika nakadhalika. *(Makof)*

Mimi nataka niseme sisi Wanyamwezi tuna msemo mmoja wanasesma *funga kalomo* yaani maana yake hii bajeti na hii mipango ambayo inatekelezwa ni kweli *funga kalomo*, ukiwaona wanasisimama kusema kuhusu bajeti wanatapatapa wanatafuta pa kushika kwenye hoja ndogo ndogo. Nataka niseme iko miradi mikubwa ya kimkakati ambayo iliwekewa mipango mizuri, leo kama hajatekelezeka kwa asilimia 100 iko katika hatua za utekelezaji, mwisho wa siku ile miradi *off course* miradi yote inategemeana

unapozungumza tumerekebisha bandari, unapozungumza tunatengeneza *standard gauge*, unapozungumza leo tumerekebisha hii *normal railway* iliyokuwepo sasa tumeirekebisha, unapozungumza tunarekebisha viwanja vya ndege, yote haya kwa ujumuifu wake unajenga uchumi wa nchi, mwisho wa siku tunatekeleza yale ambayo tulikuwa tumeyahaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukizungumzia kwenye miradi mbalimbali ambayo inafanyika katika maeneo yetu mfano mradi wa maji ukizungumzia katika Jimbo langu ya Igala, mimi wakati naingia madarakani kama Mbunge tulikuwa tunapata maji asilimia 40, leo tunapata maji takribani asilimia 70, wananchi wa Igala leo ukiwaambia kwamba mipango mibovu, bajeti mbovu wanaweza wakakupiga mawe na wanaweza wakakuletea matatizo makubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Igala tuna mradi wa Ziwa Victoria wa bilioni 12 lakini tuna miradi mingine midogo midogo ya bilioni 10, kama tungelikuwa hatuna mipango mizuri haya mambo yasingeweza kufanyika, kuna miradi takribani 1,268 vijiji yanafanyika na mingine inafanyika katika watu ambao wanasmama humu ndani wanasema hakuna kilichofanyika, ukizungumzia katika elimu tulisema tutanatoa elimu bure, tumetekeleza, tulisema tutaboresha mazingira ya kufundishia na mazingira ya kusomea tumejenga maboma, tumejenga nyumba za walimu takribani bilioni tisa zimetoka kwenda kujenga mabona na nyumba za walimu. Igala peke yake tumejenga zaidi ya milioni 500 kujenga maboma ya madarasa, kujenga nyumba za walimu, leo madarasa ya Igala yaliyojengwa na hizi fedha za EP4R hata ya Dodoma Mijini hayaingia pale Igala kule vijiji, watu wakiwa na harusi siku hizi badala ya kwenda kwenye *garden* wanakwenda kwenye zile shule, wanapiga picha za ukumbusho kwa jinsi shule zilivo nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukizungumza katika eneo la afya tumejenga hospitali 71 mpya, tumejenga vituo vya afya 487, zahanati, 1,198 haijawahi kutokea na wale wanaobeza

baadhi ya vituo vya afya vimejengwa kwao, zahanati hizi zimejengwa kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilitaka kusisitiza tu kusema kwamba mipango mizuri huleta maisha bora ya wananchi wetu, na mipango hii imepangwa na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Waziri na timu yako imesimamia vizuri nataka niwaambie usione vyaelea vimeundwa, asiyejua maana usimwambia maana, lakini sisi tumeyaona na kazi nzuri imefanyika, kikubwa tutaendelea kuwaunga mkono. (*Makofi*)

Pia nataka niseme kwa kazi hizi zilizofanyika Mheshimiwa Rais wetu atapeta bila matatizo yoyote, Wabunge wa CCM mtarudi bila matatizo yoyote, tutakutana Novemba hapa Mungu akipenda, nashukuru kwa kunipa nafasi hili, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, atafuatiwa na Zainab Bakar, Mheshimiwa Almasi Maige ajiandae. (*Makofi*)

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukushukuru wewe na kumshukuru Mwenyezi Mungu Mungu muweza ya yote aliyenipa nafasi ya kuweza kusimama na kuweza kuchangia katika hoja hii muhimu kwa manufaa ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nimesimama kuwawakilisha wanawake wa nchi hii ambao mimi ndiyo walionileta humu ndani kuwa Mbunge kuitia wanawake. Wanawake wa Tanzania wamenitura nije kuleta shukrani zao kwa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi ambayo si kushangaza Tanzania pekeyake bali na dunia nzima. Wanawake wa Tanzania wanashukuru kwa sababu Rais Magufuli wakati wa kampeni alisema nitumeni mimi mtakaponichagua nitahakikisha wananchi wa Tanzania wanalipa kodi na kodi itakayopatikana itakwenda kuleta matokeo chanya kwa wanawake na Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanawake wa Tanzania wamenituma niye kusema ahsante sana Dkt. John Pombe Magufuli kwa kusimamia yale ambayo uliyahaidi wakati wa kampeni za mwaka 2015, wanawake wa Tanzania wamenituma niye kusema vifo ambavyo vilikuwa vinawasumbua wanawake, watoto wanafariki, wanawake wajawazito wanafia njiani, wanawake wanatembea masafa marefu kwenda kutafuta maji, Dkt. Magufuli umetekeleza, wanasema ahsante na hawa cha kukulipa zaidi ya uchaguzi wa Oktoba mwaka huu wanawake wa Tanzania wanataka ye ye apite bila kupingwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wanawake wa Tanzania wanasema wanamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuwatua ndoo maji kichwani, kiwango cha asilimia 70 upatikanaji wa maji vijijini wanawake wanaoshi vijijini wanasema ahsante na hawana cha kumlipa. Kiwango cha kupatika kwa maji kwa asilimia 84, wanawake sasa mjini wanaoga masaa yote wanashika tu kufungua bomba maji tayari, mfano mji mimi ninaotoka Mji wa Musoma sasa hivi maji yanapasua mabomba wanawake wa Tanzania wanasema hawana cha kumlipa zaidi ya kumpa kura zote za ndiyo itakapofika Oktoba, 2020. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wanawake wa Tanzania ambao mimi ninawawakilisha..

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina kuna taarifa.

## TAARIFA

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru ningependa kumpa taarifa Mheshimiwa Amina ambaye anasema ametumwa na wanawake wa Tanzania kuwasemea kuhusiana na vifo nya mama wajawazito wakati wanajifungua. Mwaka 2014/2015 kulikuwa na vifo 432 kati ya wanawake laki moja, vizazi na vifo, mwaka 2018/2019 kumekuwa na vifo 578 kati ya vizazi laki moja wamama wajawazito. Sasa ukilinganisha mwaka 2014/2015 wanawake 432 walikuwa wanafariki na 2018/2019 wanawake 578

kumeongezeka. Sasa akisema wanawake anaowasemea kwamba vimefungua anakuwa hawatendei haki wanawake wa Tanzania badala yake iitakiwa awasemee ili Serikali sasa iweze kuwekeza zaidi kupunguza hivi vifo vya akinamama, ahsante.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante mdogo wangu, mwanangu Esther Matiko, ni hoja lakini bahati njema niko kwenye Kamati ya Huduma za Jamii, lakini hesabu za kawaida tu hata vifo vikiongeza na watu pia wanaongezeka. Lakini nataka niseme kwamba...

Mheshimiwa Waziri amesimama. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya nimekuona umesimama.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kumpa taarifa mchangiaji Mheshimiwa Amina Makilagi kwamba ni kweli vifo vya wanawake wajawazito vimepungua kwa sababu takwimu anazozitaja Mheshimiwa Esther Matiko ni takwimu utafiti wa mwaka 2015/2016. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, takwimu ambazo zipo Wizarani vifo vya akinamama wajawazito sasahivi havizidi 3,000 na *National Bureau of Statistics* watafanya utafiti mpya. Kwa hiyo, takwimu anazosema Mheshimiwa Esther Matiko zimepitwa na wakati, lakini takwimu anazozisema Mheshimiwa Amina Makilagi ni sahihi na nimuongezee tu vifo vya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano vimepungua kutoka 67 katika kila vizazi hai 1,000 hadi vifo 11 katika kila vizazi hai 1,000. (*Makof*)

Kwa hiyo ndiyo ndiyo kazi ya Magufuli, Mheshimiwa Makilagi taarifa nakupa kwamba ni kweli wanawake wa Tanzania kutokana na kazi kubwa aliyofanya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli wataka apingwe bila kupita, nikuwa natoa taarifa tu kwa heshimiwa Makilagi, ahsante sana. (*Makof*)

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana Mheshimiwa Waziri na mimi naungana na wewe kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati za Huduma na Maendeleo ya Jamii na bahati njema...

**SPIKA:** Alikuwa na maana ya apite bila kupingwa, halafu takwimu haziwezi kuwa hivo kama kweli akinamama ncjhi hii wanakufa 500 kwa kila laki moja, tungeiona hiyo hali, yaani ingeonekana bila hata kwa sababu ni *figure* kubwa sana kwa kila laki moja ya *over hundred* kwa sasa hivi ni kubwa sana. Malizia Mheshimiwa Amina Makilagi.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naendelea kusema tu kwamba sitaki nipoteze muda Mheshimiwa Waziri ameiweka vizuri kwa sababu mimi siongei vitu ambavyo sina uhakika navyo. (*Makofî*)

Lakini nataka niongeze kwamba hata mwenyewe Mheshimiwa Esther Matiko anapozungumza sasa na kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri kama wananchi wanaongezeka na watu wanaongezeka, lakini vifo zinazidi kupungua Dkt. Magufuli apigiwe kura na apite bila kupingwa.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa sababu hospitali zinazozungumzwa za rufaa zinakwenda kuwakomboa wanawake wa nchi hii, mfano ni Mkoa wa Mara Baba wa Taifa aliacha amejenga hospitali Marais wote wamekuja ilishindikana...(*Makofî*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, jamani naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Magufuli oyeee. (*Makofî*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Zainab Bakar na Mheshimiwa Almasi Maige utatufungia.

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na nikatimiza miaka mitano katika Bunge hili lako tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pili niushukuru uongozi wote kuanzia taifa mpaka ngazi ya msingi, tatu naunga mkono maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, la kwanza nitazungumzia kuhusu madeni ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, madeni haya ni makubwa sana, wastaafu wetu wanahangaika wanapomaliza kazi/wanapostaafu wanakuwa hawapati stahiki zao inavyostahiki. Kwa hiyo tunaiomba Serikali Mfuko wa Jamii walipe kwanza haya madeni, pili wawezeshe kuweza kujlendesha wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa CAG madeni ya muda mrefu katika Mfuko wa Hifadhi wa Jamii ni shilingi bilioni 171.91 na vilevile katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Utumushi wa Umma madeni ni shilingi bilioni 111.8. Ukiangalia hali hii ni kwamba wastaafu wetu wanahangaika sana baada ya kustaifu, tukiangalia hao wanafamilia, wana wazee, wana watoto ambao wanawategemea wanahangaishwa kila siku, Serikali ilipe haya madeni ili wastaafu wapate haki zao stahiki kwa muda muafaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo jengine ni kwamba nimejifunza mengi katika miaka hii mitano, nikiwemo katika hili Bunge la Tanzania, nasema niipe pongezi Serikali kwa kuweza kuwalaghai wananchi na kuwatapeli wananchi kwa muda wa miaka yote mitano, iliwaahidi milioni 50 kijiji hadi kwa kijiji mpaka leo haijawapa. (*Makofii*)

Pili...

**SPIKA:** Mheshimiwa Zainab kuna taarifa unapewa. Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

## TAARIFA

### NAIBU WA WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa ufahamu wangu ni kwamba pongezi anapewa aliyefanya vizuri, sasa inakuwaje yeye aipongeze Serikali kwa kulaghai, nadhani ajue matumizi sahihi ya neno pongezi.

**SPIKA:** Unaipokea taarifa hiyo Zainab?

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR:** Mheshimiwa Spika, mimi siipokei kwa sababu wananchi wameelewa kwamba Serikali hii imewalahai na kuwatapeli na mara hii hawatakulabi kulaghaiwa tena, pia iliwalaghai katika ilani yao kuwaambia kwamba miaka hii mitano watashughulikia suala zima la Katiba mpya mpaka tunamaliza hivi sasa hawashughulikia hilo suala la Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika jambo lingine katika Serikali hii ya Awamu ya Tano, wananchi na mimi mwenyewe nimejifunza kwamba uhalifu umeongezeka maradufu, watu wanauawa, watu wanatekwa na kuna watu wasiojulikana ambao katika nchi ya Tanzania hii wameshamiri na ndiyo maana *NIDA* hawatoi vitambulisho wamekatiza kutokana watu wa kwamba wasiojulikana nchi ni wengi hawajui utaifa wao ni wapi.

**SPIKA:** Kuna taarifa unapewa, Mheshimiwa Zainab.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikuombe umpe utaratibu, asiwe anatumia maneno ya kuudhi ambayo hayaruhusiwi kutumika Bungeni.

Lakini la pili asitoe taarifa za uongo, katika nchi hii kabla ya Rais Magufuli hajaingia kila watu wanapotaka kusafiri ilikuwa lazima wasindikizwe na askari ndani ya magari. Lakini si hivyo tu ilikuwa hata vibanda vya Mpesa vilikuwa vinavamia na kila watanzania ni mashahidi, lakini utaona mabenki yalikuwa yanavamiwa, hayo yote yameshapungua na watu wanaendelea kuchapa kazi na yale mengine

aliyokuwa anasemea kuhusu habari ya suala la Katiba, Taifa hili ni Taifa huru, viongozi wote kila eneo walikozunguka hakuna hata mkutano mmoja ambako wananchi wamesimama wakaongelea jambo la Katiba mpya, mahitaji ya Watanzania yanajulikana na Serikali ya Rais Magufuli imeyatekeleza, imezidisha hata ile iliyokuwa llani ya Uchaguzi, kila kijiji kimepata umeme, kila kijiji ni *construction site*, kazi zinaendelea na hata huyo anayeongea ukifuata vizuri kwenye *profile* yake utakuta amepiga picha kwenye majengo yaliyojengwa na Serikali na aka-share na watu wake. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mzungumzaji wa mwisho siku ya leo, Mheshimiwa Ezekiel Maige.

**MBUNGE FULANI:** Ni Mheshimiwa Almas Maige.

**SPIKA:** Mheshimiwa Almas Athuman Maige unajua shida ya Wanyamwezi hawa wote majina yao hayo hayo tu, Mheshimiwa Maige.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kuniruhusu na mimi nichangie bajeti hii, naitwa Almas Maige badala ya Ezekiel Maige nakushukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa dakika tano najaribu kusema kweli kweli kwa haraka, lakini kwanza nikushukuru wewe, pia niwashukuru wananchi wangu wa Uyui walionichangua niwawakilishe hapa Bungeni kwa miaka mitano. Nafikiri nimewatendea haki na kweli nafikiri watafikiria tena kunirudisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na miradi mikubwa iliyojengwa katika nchi hii wakati wa Mheshimiwa Rais Magufuli ningependa kutumia ile methali inayosema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, lakini kabisa kabisa tuibadilishe hii methali iwe mnyonge muoneeni, haki yake mpeni na haki yake ni wakati huu wa uchaguzi tumpe kura zote Mheshimiwa Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi Jimbo langu limefaidika sana na uwepo wa Mheshimiwa Rais Magufuli, moja tumepewa maji ya Ziwa Victoria katika vijiji vyangu vyote 82, vijiji 40 vitapata maji hayo, pia umeme wa REA vijiji vyote 18 tumepewa lakini vile 64 pia vitawekwakatika mpango ujao, tumepewa Hospitali ya Wilaya kwa shilingi bilioni mbili, tumepewa kituo cha VETA shilingi bilioni tano, tumepewa kituo cha afya shilingi milioni 885, pia tumepewa elimu bure Jimbo zima na nchi nzima kwa ujumla. Pia ametusogezea Makao Makuu na kuyajenga hapa kwa Wagogo watani zetu wamekuwa karibu tunatembeleana sasa.

Mheshimiwa Spika, lakini bajeti hii imegusa maeneo muhimu ya waajiri mimi nilipoingia Bungeni hapa *SDL* ilikuwa asilimia sita tumeipunguza kwa kiwango chini kabisa tumeifikia asilimia nne, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais na sisi waajiri tunamuunga mkono sana. Pia wafanyakazi wamepunguziwa kodi tuanze kulipa mishahara wa shilingi 270,000 na zamani tulikuwa tunalipa kuanzia shilingi 170,000, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nina maombi maalum kwa Waziri wangu Mpango na Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara ya Fedha pale kituo cha afya cha Upuge ambacho kimekarabatiwa kwa shilingi milioni 850, kuna *x-ray* mashine mpya na *ultrasound* mpya ndani ya maboksi karibu mwaka sasa hatuna tu jengo la kuifunga hiyo mashine, nawaombeni sana mfikirie ile mashine itaharibika itaoza ndani maboksi tutafutieni milioni mia moja, tujenge jengo tuweke *ultrasound* na *x-ray* mashine ili jengo la mionzi likikamilika watu wafanyie *x-ray* pale.

Mheshimiwa Spika, mwishoni kuna mradi mkubwa wa kujenga hospitali ya Kanda ya Magharibi pale Jimboni kwangu Kata ya Magiri. Mradi huu umesitishwa kwa sababu ya kumalizia mradi wa Hospitali ya Rufaa ya Kusini, naomba tafadhalii Mheshimiwa Mpango uweke hospitali hii katika bajeti inayokuja ili baada ya kumalizia Hospitali ile ya Kanda ya Kusini, Kanda ya Magharibi hospitali ijengwe pale Jimbo kwangu Magiri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mimi pia kwa kweli nichukue nafasi hii kuunga mkono kabisa kwa nia nzuri hoja hii na mimi nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunisaidia kuweka alama Jimboni kwangu haya yoye Jimboni kwangu utaona kama hayakuwezekana huko nyuma leo tuna alama ya kutosha kabisa, maswali kwamba Mbunge ulikuwa wapi, Mbunge umefanya nini Jimboni, umeacha alama gani, yote yamejibiwa na kwa kweli nawashukuru sana wapiga kura wangu na Mheshimiwa Rais kanifanyia, kanitendea haki kuniwekea alama Jimbini kwangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana mzee mzima, Mheshimiwa Almas Maige kwa kuwa mzungumzaji wa mwisho siku ya leo, maana yake umebariki mazungumzo yote ambayo yameenda vizuri, ni mjadala wa Kibunge, ni kawaida kuvutana hapa na pale, vinginevyo nawashukuruni sana ulikuwa ni mjadala ambao umechangamka sana na wale ambao hamjapata nafasi tutaungana na wale ambao wameomba nafasi kesho naamini kabisa karibu kila mmoja wenu atapata nafasi ya kuchangia bajeti hii na tunawashukuru sana Waziri Mpango na Naibu wake wamekuwa na usikivu mkubwa sana kwa kila ambacho tumekizungumza na kuchangia hapa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kwa vile muda sasa hauko upande wetu naomba niahirishe Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 01.50 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumamosi,  
Tarehe 13 Juni, 2020 Saa Tatu Kamili Asubuhi)*